# ‘NYAMUMA ILIYOBAKI’

## Safari ya Kutafuta Haki ya Kuwa na Kwao:

Miaka 18 ya Maumivu, Uvumilivu Kuelekea Ushindi

**WACHAPISHAJI**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
S.L.P 75254, Jengo la Jaji Lugakingira,
Kijitonyama, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 222 2773038/48
Nukushi: +255 22 27773037
Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

**MWANDISHI**
Dkt. Helen Kijo-Bisimba

**WAANDISHI WASAIDIZI**
Victoria Lugendo
Rodrick Maro

**WAHARIRI**
Anna Henga (Wakili)
Fulgence Massawe (Wakili)
Hamis Mayombo (Wakili)
Joanitha Mutayoba (Wakili)
Hamis Mkindi (Wakili)
Michael Mallya

**©LHRC**
Septemba, 2020

ISBN: 978-9987-740-55-0

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| **DIBAJI** | vi |
| **UTANGULIZI** | vi |
| **HAKI YA WANANCHI KUWA NA KWAO NA HAKI YA HIFADHI** | vi |
| **SURA YA KWANZA** | 1 |
| UTAMBUZI WA HAKI YA MWANANCHI KUWA NA KWAO: KISA CHA NYAMUMA ILIYOBAKI | 1 |
| **SURA YA PILI** | 7 |
| CHANZO CHA WANANCHI WA NYAMUMA ILIYOBAKI KUPORWA HAKI YA KUWA NA KWAO | 7 |
| **SURA YA TATU** | 15 |
| WANANCHI WA NYAMUMA ILIYOBAKI WAFUATILIA HAKI YAO YA KUWA NA KWAO | **15** |
| **SURA YA NNE** | 24 |
| TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA: KIMBILIO LA HAKI | 24 |
| **SURA YA TANO** | 130 |
| KUIENDEA MAHAKAMA KATIKA KUZIDI KUITAFUTA HAKI | 130 |
| **SURA YA SITA** | 185 |
| JAKAMOYO KATIKA KUKAZIA HUKUMU | 185 |
| **SURA YA SABA** | 188 |
| MADHARA YA KUIKOSA HAKI YA KUWA NA KWAO NA UGUMU KUIFIKIA HAKI | 188 |
| **SURA YA NANE** | 198 |
| **HITIMISHO** | 198 |

# DIBAJI

Kuvamiwa na kuondolewa kinguvu kwa wakazi wa iliyokuwa Nyamuma ni ukatili na uvunjifu mkubwa wa Haki za Binadamu uliotokea katika Kijiji cha "Nyamuma Iliyobaki". Kijiji hiki kilikuwa kinapakana na pori la akiba la Ikorongo, pembezoni mwa hifadhi ya Serengeti.

Ikumbukwe kuwa, wakazi wa kilichokuwa kijiji cha Nyamuma waliishi maeneo hayo kwa miaka mingi tena bila bughudha yoyote hadi ilipofika mwaka 1994, ambapo uongozi wa Wilaya ya Serengeti uliamua kuongeza mipaka ya pori la akiba la Ikorongo. Matokeo yake ni kuwa sehemu kubwa ya Kijiji cha Nyamuma ilitwaliwa na kujumuishwa katika pori la akiba la Ikorongo na kubaki eneo dogo tu la makazi ya watu, walililoiita "Nyamuma Iliyobaki".

Watu hawa wa "Nyamuma Iliyobaki" waliendelea na maisha kwa amani wakijihusisha na shughuli zao za uzalishaji kama kawaida, hadi mwezi Oktoba, 2001 ambapo lilitolewa tangazo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya (wakati huo akiwa ndugu Thomas Ole Sabaya) kuwataka wakazi wa "Nyamuma Iliyobaki" kuondoka katika makazi hayo haraka iwezekanavyo.

Siku mbili tu baada ya tangazo la Mh. Mkuu wa Wilaya, kilifika kikosi kilichoongozwa na Mkuu wa Wilaya mwenyewe, akiambatana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti (OCD), ndugu Alexander Pantaleo Lyimo na kusimamia zoezi la kuwaondoa wakazi wa "Nyamuma Iliyobaki".

Zoezi hilo lilikuwa la kimabavu na kikatili, kwani watu walipigwa, nyumba zao zilichomwa moto, mifugo na mazao kuteketezwa kwa moto. Watu walikimbia hovyo kujinusuru, familia zilisambaratika kwa kupotezana na wengine wamepotea hadi leo wasijulikane walipo.

Kwa zaidi ya miaka 19 sasa, waathirika hawa wamekuwa na safari ndefu ya kutafuta haki ya kuwa na kwao na haki nyingine za msingi zimpasazo mwanadamu kuwa nazo, bila mafanikio.

Hata hivyo, kupitia juhudi za watu mbalimbali, hususan Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, mwangaza umeanza kujitokeza mwishoni mwa handaki.

Pamoja na jitihada hizi, haki za watu hawa kucheleweshwa kwa muda wote huu, ni haki za watu hawa kunyimwa.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeamua kuweka katika maandishi kisa hiki ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu ya kazi iliyozifanya kwa kipindi kirefu na kwa wakati huu wa kuadhimisha miaka 25 tangu kianzishwe kumbukumbu hii itasaidia kuonyesha umuhimu wakufuatilia haki kwa kila hali na zaidi kuonyesha kuwa haki ikiminywa bila juhudi, kuipata si rahisi. Kwa jamii ya haki na usawa haki ni lazima zifuatiliwe.

# UTANGULIZI

## HAKI YA WANANCHI KUWA NA KWAO NA HAKI YA HIFADHI BINAFSI

Katika vitu vya muhimu ambavyo vinamfanya mtu aweze kuishi ni kwa haki zake kuheshimiwa ikiwemo kuwa na kwake na hifadhi binafsi. Kama tunavyofahamu haki alizo nazo binadamu anazo tu kwa vile yeye ni binadamu na hivyo anatakiwa aweze kufaidi hizo haki na iwapo kwa njia yoyote ile haki zake zimekiukwa au kuporwa ulinzi wa haki hizo ni muhimu sana kwa vile haki zikiminywa au kuondolewa ubinadamu wake huwa umeminywa au umeondolewa. Binadamu ana haki nyingi sana katika kuukamilisha ubinadamu na utu wake. Ipo haki ya kuishi ambayo ndio msingi wa haki nyingine zote. Haki ya kuishi isipokuwepo haki nyingine hazina pa kusimamia. Ili haki ya kuishi iwe na maana zipo haki nyingine nyingi zinazoijenga haki ya kuishi kama haki ya makazi bora, haki ya kuwa na kazi haki ya elimu na haki nyingine nyingi tutakazozizungumzia.

Kwa mtu ambaye ni raia wa nchi, hii haki ya kuishi hujitegemeza katika haki yake ya kuwa na mahali ambapo anaishi akijua hapo ni kwake na anakuwa na uhuru wakuishi hapo na kuweza kwenda popote atakako bila bughudha. Ukiangalia mikataba ya kimataifa inayosimamia haki za binadamu ambayo ni pamoja na Tamko au Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 limeweka haki ya kuishi na haki ya uhuru wa mtu kuishi popote apatakako. Haki hizi zimeshikamana na haki

yakujitambua kujua wewe ni nani na ndiyo maana lipo suala la kuandikishwa mtoto anapozaliwa na baadaye kupatiwa hati au kitambulisho cha uraia. Haki hii pia hufungamana na haki ya kuwa na mali na kuweza kumiliki mali na kutumia mali zako bila bughudha yoyote.

Kwa miaka 25 ambayo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimekuwa kazini, kimekutana na ukiukwaiji mkubwa wa haki za binadamu katika jamii zetu. Upo ukiukwaji uliofanywa kwa kutumia mamlaka za serikali na kuwafanya wananchi wakose mahali pa kuishi au wasiwe na uhakika wa haki ya kuwa na kwao. Kwa mfano Kituo kilipoanza kazi mwaka 1995 kilipokea mashauri yaliyokuwa yakiendelea ya wananchi wa wilaya ya Hanang, ambao maeneo ya ardhi yao yalitwaliwa na serikali bila ridhaa yao na bila kupewa maeneo mbadala na yakafanywa kuwa mashamba makubwa ya ngano. Wananchi hawa walipeleka mashauri mahakamani wakidai maeneo yao ambayo waliyatambua kama haki yao kwani yalikuwa na mambo muhimu katika maisha yao kama visima vya maji, makaburi ya waliowatangulia ambayo mengine yalikuwa sehemu ya ibada zao. Wengine ni wananchi wa Mkomazi wilayani Same ambao nao walihamishwa maeneo yao yakisemekana kuwa ni hifadhi ya taifa ya wanyama pori. Hali kama hizi zimekuwepo sana nchini maeneo kama huko Katavi, Dodoma Njedengwa, wilaya ya Kiteto na hata jijini Dar-es-Salaam ambapo mwezi Mei mwaka 2001 kwa mfano nyumba za wakazi wa Ubungo na Kimara zilivunjwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara. Waliovunjiwa hawakuwa na pakwenda hadi wakahamia ofisi za shirika la wakimbizi duniani [UNHCR] Dar-es-Salaam. Kwa kuangalia jinsi masuala haya yalivyokuwa yanaendelea hali ya heshima ya haki ya mtu/watu kuwa na kwao na haki hii kulindwa kisheria inaonekana haifuatiliwi na hivyo watu kukosa uhakika wa haki hii hasa inaponyakuliwa.

Katika kitabu hiki tunaangalia zaidi jinsi wananchi wa kitongoji kilichojulikana kama Nyamuma Iliyobaki kaya 135 walivyojikuta hawana kwao baada ya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti wakati huo, aliyejulikana kama Thomas Loy Ole Sabaya kuamua kuwaondosha katika makazi yao

kwa nguvu na kuwafukuza kabisa na mali zao kuteketezwa huku nyingine zikiibwa na kisha ardhi yao kugawiwa kwa watu wengine. Huu ulikuwa ni ukiukwaji mkubwa sana wa haki ya hawa wanakitongoji ya kuwa na kwao na kupata ulinzi wa haki yao hii ya kuwa na kwao. Zipo sababu zilizoelezwa ambazo tutaziongelea kitabuni. Sababu alizoeleza mkuu huyo wa wilaya na sababu walizoeleza hawa wananchi zote tutazichambua kuona umuhimu wa watu kuwa na haki hii ya kuwa na kwao na ulinzi wa hii haki.

Kikubwa ni kuwa wananchi hawa wanatambua kuwa pale walipokuwa ni kwao na wanatambua kuwa ilikuwa ni haki kwao kuishi hapo bila bughudha lakini mamlaka ya mkuu wa wilaya kwa kutumia jeshi la polisi iliweza kuwaondoa kinguvu. Wananchi hawa kwa kutambua kuwa wana hiyo haki waliamua kuifuatilia haki yao. Kitabu hiki kitaonyesha njia walizoweza kuzitumia, taasisi mbalimbali walizozifikia kufuatilia haki yao. Wamefuatilia haki hiyo kwa zaidi ya miaka kumi na minane wakishika kila paliposhikika na kuingia kila ofisi waliyoweza kuingia wakitafuta misaada ya kisheria na ya kibinadamu hadi haki yao ilipotambuliwa.

Katika maelezo yanayojadiliwa humu kitu kikubwa kabisa kinachoonyesha umuhimu wa haki ni ile hali ya upatikanaji wa haki. Haki inapokiukwa ni haki ya aliyekiukiwa kuweza kudai na kurejeshewa haki yake. Ipo mifumo ya haki ambayo inapaswa kufanya kazi kwa wepesi ili waliokiukiwa haki wapate nafuu. Hawa wananchi waliweza kuanzia sehemu kuitafuta haki yao hii yakuwa na kwao na kutafuta kulipwa fidia ya mali zao zilizoporwa na usumbufu walioupata. Katika kufanya hivyo walifanikiwa kukifikia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambacho kiliweza kuwasaidia kufuata taratibu za kisheria kuitafuta haki iliyoporwa. Katika kitabu hiki, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kitaelezewa jinsi kilivyoundwa na jinsi kinavyofanya kazi lakini pia jinsi kilivyopokea wana kitongoji hawa na kuweza kuwasaidia.
Katika mifumo iliyopo ya upatikanaji wa haki moja wapo ni Tume ya Haki

za Binadamu na Utawala Bora ambapo Kituo kiliwaelekeza wananchi hao kutafuta haki yao huko. Wakati shauri hili linaanza ndio kwanza Tume ya Haki za Binadamu ilikuwa imeanza tu kazi zake kwani iliundwa mwaka 2001 na ikaanza rasmi 2002. Kazi iliyofanywa na hii Tume katika shauri la Nyamuma Iliyobaki, ikiwa ni kesi yake ya kwanza ilikuwa ni kubwa na adili. Hapa itaonyeshwa jinsi mwenyekiti wa kwanza wa Tume hii marehemu Jaji mstaafu Robert Kisanga alivyotumia kwa weledi fursa hii yakuwasikiliza na kuwawezesha wananchi hawa kuipata haki yao iliyokuwa imeondolewa na kuvunjwa. Katika mjadala wa Tume ilivyofanya kazi yake tutaona pia hali ya Tume hii na umuhimu wake na jinsi ambavyo ikifanya vizuri ni nafuu ya raia na isipofanya vizuri ni kadhia kwa wananchi.

Wananchi hawa waliyokuwa wamejikuta kuwa 'wakimbizi wa ndani,' walifuatilia haki yao hadi mahakamani pale serikali ilipogoma kutekeleza mapendekezo ya Tume. Hapa itaonyeshwa jinsi ambavyo haki inavyotafutwa kwa kuhakikisha kila chombo cha haki kinatumiwa. Huko mahakamani pia kulikuwa na milolongo mirefu hadi hatimaye haki ilitambuliwa na wananchi hawa wakaanza kufuatilia upatikanaji wa haki kwa kukazia Mapendekezo yaliyotolewa na Tume kupitia mahakama.
Haki hutafutwa kwa njia zote ziwezekanazo na kisa hiki cha Nyamuma Iliyobaki ni mfano halisi wa utafutaji wa haki na hasa haki hii ya mtu kuwa na kwao.

SURA YA KWANZA

01

# UTAMBUZI WA HAKI YA MWANANCHI KUWA NA KWAO:

## KISA CHA NYAMUMA ILIYOBAKI

### 1.1 Wananchi katika Nyamuma Iliyobaki wakiwa kwao

Nyamuma Iliyobaki ni kitongoji ambacho kilikuwa sehemu ya kijiji kilichojulikana kama Nyamuma katika kata ya Rwanchanga wilayani Serengeti. Serengeti ni wilaya iliyoko mkoa wa Mara. Wanavyojieleza wengi wa wakazi wa kitongoji hicho walifika katika eneo la Nyamuma miaka ya themanini wakitokea maeneo yaliyokuwa na watu wengi katika wilaya hiyo. Wakati wanahamia hapakuwa na watu wengi walikuwepo watu wachache sana wakaungana nao kuendelea na maisha. Pia wapo watu waliohamia baada ya maeneo yao kugeuzwa hifadhi ya wanyama pori. Wapo wanaosema wao wako hapo miaka mingi kwani waliwakuta wazazi na wazazi waliwakuta wazazi.

Katika mwaka 1986 kijiji cha Nyamuma kilikuwa sehemu ya kijiji cha Rwanchanga hadi mwaka 1993 kiliposajiliwa kuwa kijiji kamili. Watu walioishi katika kijiji hicho wanakumbuka kuwa ilipofika mwaka 1994 Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti iliamua kuongeza mipaka ya hifadhi ya Wanyamapori ya Ikongoro kwa mujibu wa sheria. Mipaka ilipopanuliwa sehemu kubwa ya kijiji cha Nyamuma ilimegwa na kuwa rasmi sehemu ya pori tengefu hilo la Ikorongo na sehemu ndogo iliyokuwa na kaya 135 tu ndiyo iliyoachwa katika kijiji hicho. Wananchi ambao eneo lao lilichukuliwa kuwa sehemu ya pori tengefu la Ikorongo walilipwa fidia za mali zao tarehe 13/8/2000 ili waondoke na kupisha hifadhi hiyo. Baada ya malipo wananchi hao waliondoka na baadhi yao walitafuta maeneo katika kisehemu kilichobaki cha Nyamuma Iliyobaki kwa kununua au kwa kupewa na ndugu waliokuwa katika zile kaya zilizobakia.

Kwa vile Nyamuma Iliyobaki isingetosheleza kuwa kijiji ilibidi halmashauri iamue kuifanya kuwa sehemu ya kijiji cha Bonchugu na kwa hivyo ikawa ni moja ya vitongoji vya kijiji cha Bonchugu. Wananchi hao walikuwa wanaendelea na maisha yao ya kila siku kwa vile wengi ni wakulima, wengi walikuwa na ardhi ambayo waliitumia kwa kazi zao. Wapo wanaoeleza kuwa walikuwa na ekari hadi 20 na wengine ekari 30 za ardhi, ambapo walifanya kazi za ukulima na ufugaji. Mazao waliyokuwa wanalima ni pamoja na migomba, mahindi, maharage na hata ufuta. Mifugo ni pamoja na kuku, mbuzi, ng'ombe na kondoo na hata punda.

Walikuwa na nyumba zao za kudumu walimoishi, na mashamba na hata makaburi ya wapendwa wao waliotangulia mbele za haki. Wengi wameelezea kuwa katika maisha yao katika kitongoji hicho hali ilikuwa nzuri kimaisha kwani walikuwa na mali za kuwatosha kujikimu wao na familia zao. Watoto wao wenye umri wa kwenda shule walikuwa wanakwenda shule kama kawaida, walikuwa na eneo la kanisa walimokuwa wanasali. Watendaji wa kanisa nao walikuwa wanaishi hapo kitongojini kama sehemu ya wana kitongoji. Wenyeji hawa wengi wao

walikuwa na maghala ya chakula kwa vile ardhi ya kitongoji chao ilikuwa nzuri na ilistawisha mazao mengi waliyoweza kuyahifadhi kwa matumizi ya mwaka mzima.

Wana kitongoji hawa waliamua kufuatilia fidia ya shule iliyokuwa imebaki kuwa sehemu ya hifadhi ya Ikorongo. Kwa vile ile shule ilijengwa kwa nguvu ya wananchi waliona ni vyema wafuatilie fedha za fidia ili waweze kujenga shule nyingine kwa ajili ya elimu ya watoto wao ambao wakati huo walikosa shule ya karibu baada ya ile ya mwanzo kuwa sehemu ya hifadhi. Walipokuwa wanafuatilia suala hili katika wilaya inaonekana haikuwafurahisha mamlaka ya wilaya hasa kwa vile walijua wananchi walishalipwa fidia na walikwisha ondoka. Suala la fidia ya shule halikuwa limetegemewa kutoka kwa wananchi hao ambao wao walikuwa si sehemu ya waliokumbwa kuwa sehemu ya hifadhi. Hata hivyo waliona kuna sababu yakufuatilia wakiona ni haki yao kupata fidia ili warejeshe shule katika eneo lao. Wananchi wa hiki kitongoji walikuwa wanaendelea na maisha yao bila kujua pia wapo watu katika hifadhi na hata wilayani waliotamani ardhi yao kwa jinsi ilivyokuwa na rutuba pamoja na kuwa yenyewe haikumegwa kuingia kuwa sehemu ya hifadhi. Wakiwa katika ufuatiliaji wa fidia walijikuta wakitakiwa kuondoka katika eneo lao hilo kama inavyoelezewa sehemu inayofuata.

## 1.2 Wananchi wa Nyamuma Iliyobaki Walivyoondolewa Kwao

Hali ilianza kuwa mbaya kijijini hapo pale ambapo mwezi Agosti tarehe 20, 2001 Mkuu wa Wilaya ya Serengeti Thomas Loy Ole Sabaya akiongozana na mkuu wa jeshi la polisi wa wilaya ya Serengeti pamoja na Katibu Tarafa aliyejulikamsa kama Paulo Shanyangi na askari magereza na askari wanyapori walipovamia Kitongoji hicho cha Nyamuma Iliyobaki nakuwakamata raia wapatao mia tatu (300) wakiwemo wanawake na wanaume na hata watoto wadogo waliokuwa na mama zao. Baada ya kukamatwa waliingizwa kwenye malori na kusafirishwa hadi mpakani mwa Tanzania na Kenya huko Sirari. Walikuwa wanaondoshwa kwa

kusemekana kuwa si watanzania ni wakenya. Hii ilikuwa njia aliyoitumia Mkuu huyo wa Wilaya kuwanyamazisha wananchi hao waliokuwa wanadai haki ya fidia ya shule ya msingi.

Walipofikishwa mpakani, maafisa uhamiaji wa Kenya na wa Tanzania walikagua vitambulisho na hati kwa waliokuwanazo na wakajiridhisha kuwa hao hawakuwa wakenya. Ifahamike kuwa wenzetu wa Kenya wana njia nyepesi sana ya kumtambua mkenya. Kwanza uandikishwaji wa watoto wanapozaliwa upo vizuri na mtoto anapokuwa na umri wa mtu mzima hupatiwa kitambulisho cha Taifa ambacho ndicho humuonyesha utaifa wake. Kwa upande wa Tanzania watoto wengi hasa miaka hiyo ya nyuma walikuwa hawaandikishwi. Walikuwa hawaandikishwi kutokana na umbali wa sehemu za uandikishwaji lakini pia kuna wakati hata vyeti vyenyewe havikuwepo ili watoto waandikishwe hasa sehemu za mkoani yaani nje ya Dar-es-Salaam na hasa vijijini. Kuhusu vitambulisho vya uraia hivyo havikuwepo kabisa miaka hiyo ya nyuma kwa hiyo ndiyo maana ilikuwa rahisi kabisa kwa mkuu wa Wilaya kuwachukua watanzania na kuwapeleka mpakani akiwalazimisha kuwa wa Kenya. Hapa kulikuwa na uvunjifu mkubwa sana wa haki ya uraia ya watu hawa.

Iibidi Mkuu wa Wilaya wa eneo hilo la Sirari ambalo liko wilaya ya Tarime, afike kuangalia kilichojiri. Mkuu huyo wa wilaya wakati huo aliitwa Paschal Mabiti, alipopata maelezo toka kwa maafisa uhamiaji aliwaamuru wale watu warejee Mugumu wilayani Serengeti. Watu hao ilibidi wapande mabasi ya kurudi Serengeti. Inasemekana Mkuu wa Wilaya ya Serengeti alipopata taarifa kuwa wale watu wanarejea wilayani humo kwa mabasi, aliwatuma askari wakawasuburi mto Mara ambapo walishushwa kwenye magari na walipotambulika ni wale watu wa Nyamuma walipelekwa kituo cha polisi Mugumu ambapo walifunguliwa mashtaka na kupelekwa mahakamani, waliopatikana walikuwa 28 tu ambao walihukumiwa miezi sita jela wakiwemo wanawake waliokuwa na watoto wadogo.Mmoja kati wa watu hao Bhoke Mwita Chahe alifiwa na mtoto wake mchanga wakati wa zoezi hili ambapo ilibidi amzike katika kichaka eneo la Nyamwaga Wilayani Tarime kwa kumfunika kwa matawi

ya miti Watu wengine walifanikiwa kurudi kijijini na wakajumuika na wenzao kuendelea na maisha mpaka hali ilipobadilika tena.

Ilikuwa siku ya tarehe 8 ya mwezi wa Oktoba ya mwaka 2001 pale ambapo wananchi wa Nyamuma Iliyobaki walipoona gari la matangazo majira ya mchana likiingia kitongojini mwao na kutoa matangazo kwa sauti kubwa. Tangazo lililokuwa likitolewa na Katibu Tarafa Paulo Shanyangi, lilieleza kuwa mkuu wa wilaya ya Serengeti anawataka wananchi wa Nyamuma Iliyobaki waondoke katika eneo hilo ifikapo tarehe 12 ya mwezi huo wa kumi yaani siku tatu baada ya tangazo. Amri hiyo iliwaarifu waondoke mara moja vinginevyo watatolewa kwa nguvu siku hiyo ikifika na wakawemo kijijini. Aidha amri iliwatahadharisha majirani wa vitongoji vingine kutowakaribisha watu hao kwani wakifanya hivyo watachukuliwa hatua kwa vile waliambiwa watu wa kitongoji hicho ni wabakaji na wezi wa mifugo na wawindaji haramu.

Wananchi hawa hawakuelewa kwa nini wanatakiwa kuondoka, pia hawakuelewa waondoke waende wapi, maana sababu zilizotolewa kwao hawakuziona ni za kweli. Wapo walioogopa wakaanza kuhamisha mifugo kupeleka kwa ndugu katika maeneo ya jirani lakini wengi walishangaa na wakawa wanaendelea na kazi zao na maisha yao.

Ilipofika alfajiri ya siku ya tarehe 12 mwezi huo wa Oktoba, watu wengi wakiwa bado nyumbani na baadhi wakiwa wameshadamka kwenda mashambani wakati wengine wakiwa safarini, yalionekana magari kama manne yaliyoingia kijijini. Walipoyaona walisikia sauti ya Mkuu wa Wilaya hiyo Thomas Ole Sabaya akiwa ameongozana na Mkuu wa Jeshi la Polisi wa wilaya Alexander Pantaleo Lyimo na watu wengine waliokuja kujulikana kuwa ni wana kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya. Alichosema mkuu huyo wa wilaya ambaye aliongozana pia na wananchi wa vijiji vya jirani vya Rwamchanga, Bonchugu, Miseke na Kyebosongo ni kuwa amefika kutimiza azma yake yakuwaondoa kwani alishawapa notisi siku tatu zilizopita.
Wananchi walianza kutaharuki wakati huo mkuu huyo wa wilaya

alisimama pembeni ya nyumba ya mwana kitongoji mmoja aliyejulikana kwa jina moja la Chacha akawasha moto na nyumba ile ikaanza kuteketea kwa moto wakati alioongozana nao, nao wakifanya vivyo hivyo katika nyumba nyingine. Nyumba zilianza kushika moto kwa kasi watu walianza kukimbia huku wakiwa na watoto wadogo na wengine wakiwabeba waliokuwa hawawezi kwa uzee au ugonjwa. Kuna watu waliotakiwa wao wenyewe wawashe moto nyumba zao, na walipokataa kufanya hivyo walipigwa wengine hadi kuzirai.

Wakati hayo yakiendelea mkuu huyo wa Wilaya alikuwa anawafuatilia na akimkuta mtu alimpiga kwa bakora. Alipofika nje ya nyumba ya bibi Ester Jackson, alimkuta akihangaika kutaka achukue chochote. Alimpiga huyo mama pamoja na kumkanyaga kwa mateke sehemu za tumboni na kifuani. Kwa maumivu makali mama huyu ilibidi akimbie ajifiche chini ya kamsitu kadogo jirani. Mama huyu alisota kwa maumivu hadi alifika sehemu alipopata msaada wakupelekwa hosiptali ambapo alisaidiwa kusafisha kizazi kwa vile mimba aliyokuwa nayo ilikua imeharibika.

Wakati huo pia mkuu huyo wa wilaya alikutana na mtu mwenye ulemavu aliyejulikana kama Bugere Mwita akamwambia akimbie alipoona hawezi alichukua magongo aliyokuwa anatumia mtu huyo na akayatupa kwenye moto uliokuwa unawaka kwenye nyumba baada ya kumpiga na gongo begani. Mtu huyo mwenye ulemavu ilibidi ajibidishe kujisogeza ili asiungue kwa vile sasa magongo aliyokuwa anatumia yalitupwa motoni na mkuu huyo wa wilaya alimwambia 'Si unataka kubaki hapa, basi baki'.

Wakati haya yanaendelea watu wakihangaika kukimbia na wegine kukimbiza watoto walioongozana na mkuu huyo wa wilaya wakaanza kupora mali zilizokuwepo na kuondoka nazo wakati nyingi zikiteketea kwa moto.

Ghafla watu waliokuwa na kwao na mali na maisha yao walijikuta hawana kwao na hata uraia wao ulitiliwa shaka na mali zao zilichomwa moto na

nyingine zikiporwa. Wingu nene lilitanda katika maisha yao walipoanza kuhangaika kujaribu kuona watajikimu vipi baada ya mkasa huu. Ukiangalia Katiba ya Jamhuri ya Tanzania pamoja na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia haki za wananchi hawa ziliingiliwa sana na suala la uwepo wa uhakika wa uraia na mtu kuweza kujihakikishia kwao haikutiliwa maanani kabisa. Na hii si kwa hawa wa Nyamuma tu ni kwa Mtanzania yeyote kwani wengi wa watanzania wapo katika hali kama hiyo ambayo wao ndiyo hupaswa kuthibitisha uraia wao na haki ya kuwa na kwao si thabiti kama inavyopaswa kuwa.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti alitoa amri watu hawa wasipokelewe popote na waliokuwa tayari kuwahifadhi walitishwa na wengi waliogopa kuwapokea. Baadhi ya watu waliohojiwa walisema waliona jinsi watu hawa walivyotendewa na hawakuafiki wala kufurahi lakini hawakuweza kuwasaidia kwa hofu ya kuchukuliwa hatua na mkuu wa wilaya.

Watu hawa wa Nyamuma Iliyobaki, walijikuta wamebadilika kimaisha hawajui kwa vipi kwao kumeacha kuwa kwao na sasa wanaweza kusema kwao ni wapi na mali zao nazo zimeibwa na nyingine kuharibiwa. Kwa hakika walipata changamoto kubwa ambayo ilibidi wajizatiti ili waweze kuendelea na maisha.

### 1.3 Wananchi wa Nyamuma Iliyobaki waliijua haki ya kuwa na kwao

Baada ya kupitia kwenye changamoto kubwa hiyo yakufukuzwa na kuchomewa moto nyumba na mali wananchi wa Nyamuma Iliyobaki walianza kutafuta jinsi wanavyoweza kujikimu kwa kutafuta sehemu za kuishi. Walishindwa kuishi katika vijiji vya jirani kwa vile Mkuu wa Wilaya aliwakataza kabisa wenyeji wasiwapokee na wao kwa hofu wengi walishindwa kuwahifadhi. Walioweza kupata hifadhi ni wale waliokuwa na ndugu wa damu katika maeneo hayo. Watu hawa waliamua kwenda mjini Mugumu kwa vile huko si rahisi sana kutambulika na kufuatiliwa

kama huko kijijini. Hata hivyo huko nako walipata shida ya kukamatwa baadhi yao na kufunguliwa mashtaka ya uzururaji na mambo mengine. Wengine walifungwa gerezani kwa hadi miezi sita.

Pamoja na adha zote hizo walitambua hakika walichotendewa hakikuwa sawa na ni ukiukwaji wa haki zao za msingi. Kwa kutambua hivyo walianza kutafuta njia ya kudai haki yao hiyo. Wakiwa Mugumu mjini walianza kufuatilia kujua vipi wanaweza kuifuatilia haki yao? Mmoja wa wahanga alisema yeye alikuwa anajua kabisa hakukuwa na kosa lolote alilolifanya likastahili atendewe alivyotendewa. Alisema iwapo kuna kosa lolote alilolifanya au walilolifanya kitongoji kizima wakiwemo watoto na wazee basi njia sahihi ilikuwa ni kuwafungulia mashtaka na si kuharibu mali zao. Mzee mwingine alisema anafahamu kuwa kuchoma nyumba ya mtu ni kosa la jinai hata kama huyo ni mhalifu suluhisho si kuchoma nyumba yake bali ni kumfungulia mashtaka ya lile kosa.

Walifuatilia wakijua kuwa hawakuwa wameingilia mpaka wa hifadhi kwani hifadhi ilivyoongezwa wao walikuwa nje ya hifadhi ndiyo maana kitongoji chao kikahamishiwa katika kijiji cha Bonchugu. Walisema hata kama walikuwa wahalifu wa jambo jingine lolote hapakuwa na sababu yakuwapiga hasa wanawake hadi wengine wakaharibu mimba. Walisema hawakuwa na sababu yakufukuzwa kama wanyama kiasi kwamba zipo familia zilizopoteana pale ambapo watoto walikimbia kivyao na wazazi wakakimbia kivyao. Na zipo familia hadi leo hawajaweza kukutana wakati wapo wengine waliofariki wakati huo wa kuhangaika kujaribu kutafuta jinsi ya kuishi baada ya mkasa huo.

Waliangalia vigezo vyote wakaona kwa uhakika hawakutendewa haki hata kidogo na kwa hali hiyo pamoja na kuwa hawakuwa na makazi maalum waliwasiliana wale walioweza wakaamua kufuatilia kuipata haki yao.

### 1.3.1 Wananchi wa Nyamuma Iliyobaki Waitetea Haki ya kuwa na Kwao

Kwanza waliwasiliana na wasaidizi wa kisheria waliokuwa wilaya ya Serengeti na wale wa wilaya ya Tarime. Wengine walijaribu kutoa ripoti polisi lakini haikuwa rahisi kwa vile polisi walikuwa sehemu ya waliowatenda kitendo kile. Hatimaye waliwasiliana na mbunge wa jimbo lao aliyejulikana kama James Wanyancha ambaye aliliwasilisha suala hilo Bungeni. Pamoja na kuwa serikali ilimtuma Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo Muhammed Seif Khatibu yeye alisema hakuna watu waliochomewa nyumba kwa vile alipelekwa sehemu nyingine na si huko kulikokuwa kumechomwa.Wananchi hawa wa Nyamuma Iliyobaki, hawakunyamaza wakati mbunge akifuatilia bali walichagua baadhi yao wakaenda mkoani Mwanza kukutana na wanasheria wa serikali kulielezea jambo lile ili kuona wataweza kupatiwa ufumbuzi gani. Safari zote hizi zilifanywa kwa vile walijua kuwa walikiukiwa haki zao walijua walikuwa na haki iliyoondolewa bila sababu.

### 1.3.2 Milango walioipitia kuitetea Haki yao

Tangu walipotoka katika eneo lao kwa kufukuzwa na kupigwa na mateso mengine mengi, hawakunyamaza. Walianza kufuatilia sehemu wanapoweza kupata haki yao. Walichagua wenzao waliokuwa na nguvu na upeo waweze kulifuatilia suala hilo kwa niaba yao. Walianzia kwenye mashirika ya haki katika wilaya yao na mkoani mwao. Walijaribu katika serikali kwa kwenda kwa mwanasheria mkuu wa serikali. Waliwasiliana na mbunge wao. Waliandika barua kwa Waziri Mkuu na kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo. Ifahamike kuwa raia wengi wanaamini sana katika kupeleka matatizo yao serikalini wakijua serikali ina mamlaka na ina uwezo wa kufanya kwa haraka ili haki yao ipatikane. Wachache sana huwa wanakumbuka au wanaamua kufuata mkondo wa mahakama kwani huko wanaona kuna kuhitaji muda mwingi na wakati mwingine gharama nyingi.

Walipokuwa wanahangaika hivyo walikutana na watendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu waliokuwa Tarime kufuatilia ukiukwaji wa haki za binadamu huko. Wananchi hao wa Nyamuma waliwaelezea watendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadadamu tatizo lao na kuwapeleka katika eneo lao walimohamishwa. Na kuanzia hapo ndipo mchakato wakufuatilia haki zao kisheria ulipoanza. Walipotakiwa kuwasilisha malalamiko yao katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora walikuwa tayari na walifuatilia pamoja na umbali na hali ngumu waliyokuwa nayo. Wananchi hawa walikuwa na nia ya dhati yakufuatilia haki yao bila kujali muda wala umbali.

SURA YA PILI

02

# CHANZO CHA WANANCHI YA NYAMUMA ILIYOBAKI KUPORWA HAKI YA KUWA NA KWAO

## 2.1 Kuielewa Wilaya ya Serengeti ilipo Nyamuma Iliyobaki

Wilaya ya Serengeti inapatikana Tanzania katika mkoa wa Mara. Wilaya hii ipo mashariki mwa mkoa wa Mara ikipakana na wilaya ya Tarime katika Mkoa huo wa Mara. Imepakana na nchi ya Kenya kwa upande wa kaskazini. Kwa upande wa Magharibi, wilaya ya Serengeti imepakana na wilaya za Musoma na Bunda, zote za mkoa wa Mara. Kwa upande wa kusini wilaya hii imepakana na mikoa ya Mwanza na Shinyanga, wakati mashariki mwa wilaya hii ni mkoa wa Arusha. Kijiografia Wilaya ya Serengeti iko kati ya latitudi 1° 30 na 2° 45 kusini mwa mstari wa ikweta na longitudi 34 15 na 35 30 mashariki mwa Greenwich. Ukubwa wa eneo la wilaya ya Serengeti ni kilomita za mraba 10,947 zinazokaliwa na watu 249,420 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012.

Watu wanaoishi Serengeti ni wa makabila mbalimbali kwani kwa sasa watu wamehamia kwenye maeneo hasa ya mijini pote nchini. Hata hivyo, mkoa wa Mara ilipo Serengeti ina kaliwa zaidi na watu wa makabila makuu matatu ambayo ni wakurya, wajaluo na wajita. Wajaluo na wakurya wako zaidi wilaya ya Tarime, Wajita wako zaidi wilaya ya Bunda na Musoma wakati, Serengeti wenyeji wake wengi ni wakurya. Katika mkoa wa mara yapo makabila mengine ambayo hayana watu wengi sana lakini wanafahamika kama vile wazanaki, wasuba, waikizu, waisenye, wangoreme na hata wakwaya.

Wilaya ya Serengeti ina wakazi ambao wanafanya shughuli zao za kiuchumi hasa kilimo na ufugaji. Kilimo ni cha mazao ya chakula kama mihogo, mahindi na kunde. Mazao ya biashara ni pamoja na pamba, kahawa na ufuta. Wakazi wa Serengeti wako wachache sana kwenye kila kijiji kwa makadirio ya watu 2400 kwa kila Kijiji, wakati wilaya zingine wapo watu kama 3000 kwa kila kijiji. Hii wilaya ina eneo kubwa zaidi katika mkoa wa Mara lakini sehemu yake kubwa ni eneo la hifadhi ya Serengeti yenye eneo la kilomita za mraba 14,763. Hifadhi hii ina umuhimu katika Wilaya ya Serengeti kwani inatenganisha mifumo ya kiuchumi iliyoko wilayani. Wamasaai ambao ni wafugaji wanaohamahama wapo upande wake wa mashariki, wakati wafugaji wengine wapo upande wa magharibi wakiwa ni wasukuma waliochanganyika na wakulima upande wake wa mashariki. Uwindaji nao ulikuwa sehemu ya shughuli za wakazi wa Wilaya hiyo ila kwa sasa si kwa kiasi kikubwa kwa vile serikali imezuia.

Uwepo wa wanyama pori katika hifadhi hiyo umeleta athari hasi kwa wakazi wa wilaya hiyo kwani huweza kuambukizwa magonjwa toka kwa vyanzo vya wanyama kuingia kwa binadamu na hata kwa mifugo. Kuongezwa kwa mipaka ya hifadhi hii kumepunguza ardhi inayotumiwa na wananchi katika kazi zao za kiuchumi.

## 2.2 Mifumo ya Haki Wilayani Serengeti

Katika wilaya ya Serengeti kuna rasilimali nyingi ambazo nazo huchangia hali halisi ya uwepo wa haki na wakati mwingine ukiukwaji wa haki. Katika wilaya hii ardhi kubwa ni mali asili hasa hifadhi ya wanyama pori, mapori tengefu na migodi ya dhahabu ambapo shughuli za uchimbaji dhahabu hufanyika. Hali hii ya uwepo wa mali asili imechangia uwepo wa uhitaji wa rasilimali hizo kiasi ambacho kuna sheria na sera zinazosimamia rasilimali hizo ambazo wakati mwingine zinachangia uminywaji wa haki wa wananchi wa Serengeti. Makampuni makubwa yamevutika kuwekeza katika wilaya hiyo na hivyo wakati mwingine hupewa kipaumbele zaidi ya wananchi. Wananchi wa wilaya hii wanapoingia kwenye eneo la hifadhi kwa kulisha mifugo au kufanya uwindaji mdogo mdogo inakuwa ni kinyume cha sheria ya wanyama pori na wakati mwingine wakiigia maeneo ya migodini napo wanakuwa wanaingilia eneo lisilo lao kinyume cha sheria ya kanuni ya adhabu.

Sheria ya Ardhi inatoa ruhusa kwa Rais kubadilisha aina za matumizi ya ardhi . Kwa mujibu wa Sheria hii ya ardhi zipo aina tatu  ambazo ni Ardhi ya kijiji, Ardhi ya hifadhi na Ardhi ya Jumla. Rais anaweza kuibadili ardhi kuwa ya hifadhi kutoka Ardhi ya kijiji na Ardhi ya jumla kutoka ardhi ya kijiji kwa manufaa ya umma . Sheria iko wazi kuwa iwapo ipo nia ya Rais kuhawilisha  ardhi ya kijiji kwa matumizi mengine Waziri wa ardhi ataagiza taarifa itolewe kwenye gazeti la serikali na pia taarifa ipelekwe kwa Halmashauri ya kijiji yenye mamlaka juu ya ardhi inayokusudiwa kuhawilishwa . Halmashauri ya Kijiji husika itaitisha mkutano wa kijiji ili mkutano huo uridhie au ukatae uhawilishaji huo . Sheria pia inatoa maelekezo kuwa Ardhi yoyote haitahawilishwa hadi pamefanyika makubaliano kuhusu aina, tathmini, kiasi na wakati mwafaka wa kufanyika malipo ya fidia .

Hata hivyo imetengenezwa kawaida kwa watu kuhamishwa kutokana na uhawilishwaji huo na wakati mwingine hulipwa fidia au kutokulipwa fidia kabisa wala kupewa eneo mbadala.

Iwapo watu katika eneo husika hawajaridhika na kiasi cha fidia au uhawilishwaji wa ardhi yao basi watapeleka shauri Mahakama Kuu ili iidhinishe fidia.  Pia sheria inaelekeza kuwa uhawilishaji wa ardhi ya kijiji kuwa ardhi ya kawaida au ya hifadhi utatolewa taarifa kwenye gazeti la serikali na utaanza kutumika siku thelathini baada ya tangazo la taarifa hiyo.

Sheria ya Wanyama Pori inakataza watu kuingia katika maeneo ya hifadhi kwa nia ya kufanya shughuli kama kilimo, kujenga au hata kufuga. Pia sheria hairuhusu uwindaji bila kibali maalum. Wanaoingia katika hifadhi bila utaratibu uliokubalika huitwa wavamizi au wawindaji haramu na wakikamatwa huchukuliwa hatua ikiwemo mifugo kukamatwa na watu kutakiwa kulipa fidia au kushtakiwa mahakamani.

Katika masuala mengine ya ardhi ipo mifumo ya utoaji haki iliyotolewa kwa mujibu wa sheria hasa pale panapotokea migogoro ya ardhi ambayo nikuanzia ngazi ya kijiji .

a) Baraza la Ardhi la Kijiji;
b) Baraza la Kata;
c) Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya;
d) Makakama Kuu;
e) Mahakama ya Rufaa.

Kwa mashauri mengine yoyote mahakama zipo kuanzia mahakama ya mwanzo, mahakama ya wilaya/mahakama ya hakimu mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

Wananchi kutoka sehemu mbalimbali katika wilaya ya Serengeti, huiendea mahakama ya mwanzo iliyopo mji wa Mugumu na ndipo ilipo Mahakama ya wilaya. Kwa Mahakama Kuu inabidi wananchi wasafiri mpaka Mwanza ambapo ndipo ilipo Mahakama Kuu ya kanda. Kwa sasa mkoa wa Mara umepata Mahakama Kuu ambayo imeanza rasmi mwaka 2019. Na kwa Mahakama ya Rufaa nayo iko moja tu jijini Dar-es-salaam, Mahakama ya Rufaa hufanya vikao maalumu katika kanda hizi ikiwamo Mwanza, japo ni vikao vya kipindi kifupi.

## 2.3 Mifumo ya Utawala katika Wilaya ya Serengeti

Ipo mifumo ya kiutawala katika wilaya ya Serengeti kama ilivyo katika sehemu zote nchini. Katika ngazi ya kitongoji yupo mwenyekiti wa Kitongoji ambaye huweza kuwasaidia watu walio na uhitaji wa usuluhishi au mahitaji ya utambulisho kuwa ni wenyeji au wakazi wa eneo hilo. Mwenyekiti wa Kitongoji huchaguliwa kwa kura na wananchi wa kitongoji husika na huweza kuwa sehemu ya halmashauri ya Kijiji. Katika ngazi ya kijiji yupo mwenyekiti wa Kijiji ambaye ni mwenyekiti wa Halmashauri ya kijiji na katibu wake ni Mtendaji wa Kijiji. Huyu Mtendaji wa kijiji ana kazi kubwa sana katika ngazi ya kijiji kwani huandaa mikutano na mashauri mengi ya wanakijiji huanzia kwake ndipo huweza kuyapeleka katika halmashauri ya kijiji. Iwapo palikuwa na jambo lolote lile kwa wananchi wa kitongoji cha Nyamuma basi mwenyekiti wa kitongoji angeweza kuwa amearifiwa na mwenyekiti wa kijiji na yeye kushirikisha wana kitongoji anaowaongoza.

Katika ngazi ya kata yupo Mtendaji wa kata ambaye mwenyekiti wake ni Diwani wa Kata. Mara nyingi mtendaji wa kata naye hupokea wananchi wenye mashauri pamoja na kuwa lipo baraza la kata lakini watu huzoea kuanzia kwa mtendaji. Katika ngazi ya kata pia iwapo kulikuwa na jambo lolote, ili lifike kwa wananchi, Diwani au mtendaji wa Kata angekuwa amewaeleza mwenyekiti na mtendaji wa kijiji.

Katika ngazi ya wilaya lipo baraza la madiwani, ambalo hushughulika zaidi na masuala ya maendeleo ya wilaya husika na yupo mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya anayechaguliwa na madiwani wote katika wilaya. Mkurugenzi mtendaji wa wilaya ni mtendaji mkuu katika ngazi ya wilaya na ndiye katibu wa baraza la madiwani katika Wilaya, huyu huteuliwa na Rais. Halmashauri ya Wilaya nayo ingeweza kuwa imepokea taarifa ya kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya inayoongozwa na Mkuu wa wilaya iwapo kulikuwa na jambo lolote la kiusalama kutoka katika kitongoji cha Nyamuma. Haya yote hayakufanyika bali mkuu wa wilaya katika ubinafsi

wake alichukua jukumu lakuwaondosha watu katika eneo lao.

Kwenye upande wa utawala wa kisiasa yupo katibu tarafa ambaye ni kiongozi katika ngazi ya tarafa na yupo Mkuu wa Wilaya ambaye naye ni mteule wa Rais. Wilaya ya Serengeti ina Mfumo huu wa utawala kama ilivyo katika wilaya nyingine zote hapa nchini.

## 2.4 Mifumo ya Usalama ya Kimila katika Wilaya ya Serengeti

Wilaya ya Serengeti imekuwa na mifumo ya ulinzi ya kimila jambo ambalo ni karibu lipo kwenye mkoa mzima wa Mara. Mifumo hii ya kimila ya usalama haipo kisheria bali ipo kwa taratibu za kimila na inafanya kazi zake kwa mfumo huo hata kama utakuwa unakosea, wahusika haki hawana mahali pakwenda kukata rufaa. Mkoa huu umekuwa na historia ya wizi wa mifugo unaofanywa na vijana wa kabila moja dhidi ya jingine. Hali hii imezua magomvi makubwa na uvunjifu mkubwa wa amani katika wilaya za mkoa huu wa Mara wilaya Serengeti ikiwemo. Watu wengi wamekufa kutokana na mapigano yanayotokea kati ya jamii mbalimbali za mkoani hapo.

Baada ya vita vya Uganda mwaka 1979 inasemekana wanajeshi wengi waliotoka vitani walirejea mkoani hapo kwani inasadikika kuwa wengi wa wanajeshi ni watu wa mkoa huu wa Mara. Baada ya kurudi kwao ilionekana hali ya usalama katika mkoa imekuwa mbaya kwani maaskari waliotoka vitani na wakastaafishwa, walijielekeza katika wizi wa kutumia silaha. Ripoti inaeleza kuwa hali ya wizi wa mifugo ilibadilika kabisa katika miaka ya 80 na ikawa ni ya hali ya juu kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma. Mauaji nayo yaliongezeka hasa wilaya za Serengeti na Tarime.

Hali hiyo ya wizi wa mifugo na mauaji ulisababisha mkoa kutafuta njia za kuzuia au kupunguza kwa kutaka kufufua mfumo wa ulinzi wa kimila. Ilionekana kuwa hawapo polisi wakuweza kutosha kukabiliana na hilo wimbi jipya la uhalifu. Ilikuwa wazi kuwa mfumo huo wa kimila

ukifufuliwa utakutana na vipingamizi vya kisheria kwa vile umekuwa ukifanya kazi kwa njia zisizofuata haki na wakati mwingine uvunjifu wa sheria.

Hata hivyo kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa ilikutana hasa baada ya kupata nguvu kutoka kwa kauli ya Rais Benjamin Mkapa akiwa kwenye kampeni za urais mwaka 2000 kuwa atawezesha mifumo ya ulinzi ya kijadi kupata nguvu ya kisheria. Mkuu wa mkoa wa Mara aliunda kamati ya watu saba ili ichambue sheria zilizopo zinazolinda kamati za ulinzi za jadi.

Ukweli ni kuwa kamati hizo za jadi zilikuwepo hata kabla ya kamati hiyo kuundwa zikijulikana kama Ritongo, na zilikuwa zikifanya kazi kiasi cha kupongezwa kwa kazi nzuri ya ulinzi na usalama katika mkoa. Uundwaji wa kamati hii ya watu saba ilikuwa ni kujihami kwa mkoa dhidi ya kupata matatizo ya kisheria. Kamati hiyo ilitakiwa ichambue kwa upana sheria zote zinazoweza kuwa kinzani na mfumo huo wa jadi. Kamati hiyo ilipewa mwaka mmoja kukamilisha kazi yake. Mwenyekiti wa hiyo kamati alikuwa mkuu wa wilaya ya Tarime wakati huo Paschal Mabiti akishirikiana na mkuu wa wilaya ya Serengeti wakati huo Thomas Loy ole Sabaya pamoja na wajumbe wengine watano. Ni wazi kuwa uundwaji wa kamati hii ulitokana pia na jinsi ukiukwaji mkubwa wa haki za wananchi wa Nyamuma Iliyobaki ulivyodhihirika kwani iliundwa mara baada ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuanza kusikiliza shauri la watu wa Nyamuma Iliyobaki dhidi ya mkuu wa wilaya ya Serengeti.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati hiyo ya mwaka 2004, kamati ilikuwa imezichambua sheria 14 za nchi ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mara kwa mara.

Hiyo kamati iligundua matatizo mengi yanayozikabili kamati za jadi za ulinzi na usalama na hasa suala la kushtakiwa kwa makosa ya jinai. Mfano ulitolewa wa jinsi viongozi wa kamati hizo za ritongo,

walivyoshashtakiwa na kusimamishwa mahakamani kwa makosa ya jinai na madai. Serikali ya mkoa ilikubali ukweli kuwa hizo kamati za jadi zinakiuka haki za binadamu kama vile kutoa adhabu kubwa kupita kiasi kwa wale wanaopelekwa mbele yao, kuwa inatumia wahalifu katika hizo kamati, inashiriki kuwafanyia vitendo vibaya watu wasiohusika na hata kuingilia uhuru wa faragha wa watu. Wakati mwingine zinaingilia masuala ya watu ambayo yalishahitimishwa na mahakama, mwisho pia ilionekana walikuwa na matumizi mabaya ya fedha ya hizo Kamati.

Kamati ya mkuu wa mkoa ilitoa mapendekezo ya kuachana na hizo kamati za kimila bali ianzishe au kufufua mabaraza ya kata ambayo yameundwa kisheria. Kamati hiyo pia ilionyesha kuwa hizo ritongo hazikuwa na usawa katika kufanya kazi yake, na wakati mwingine maamuzi tofauti kwa mashauri yanayofanana. Walisema pia yalifanya kazi vizuri yakiwa na mkuu wa wilaya jambo ambalo pia si sahihi kabisa kwani katika kuondosha watu wa Nyamuma Iliyobaki mkuu wa wilaya ndiye aliyeendesha hiyo operesheni akisaidiana na polisi na ritongo na huwezi kusema alifanya vizuri.

Polisi waliwaeleza wazi hiyo kamati kuwa hizi ritongo ni kinyume cha sheria na kuwa masuala yote ya jinai inabidi yashughulikiwe na polisi. Kama zina umuhimu sana ni heri zitungiwe sheria na ziwe na mipaka yake.
Uwepo wa hizi Ritongo wilayani Serengeti zilitumiwa na mkuu wa Wilaya kunyanyasa watu kwa sababu alizokuwa anazijua mkuu huyo wa Wilaya kama alivyoshirikiana nao kuwaondoa kinyama wananchi wa Nyamuma Iliyobaki katika maeneo yao.

### 2.5 Sababu ya Serikali ya Wilaya kuwafukuza Wananchi wa Nyamuma Iliyobaki

Ukiangalia jinsi mifumo ya haki na ya kiutawala ilivyo utaona kuwa Kitongoji cha Nyamuma Iliyobaki kilikuwa chini ya kijiji cha Bonchugu

katika kata ya Rwanchanga wilayani Serengeti. Katika wilaya hii tumeona pia kuna mifumo ya kijadi ambayo imekuwa ikitumika sana kuwafanyia watu ukiukwaji wa haki za binadamu. Kabla ya suala la Nyamuma Iliyobaki kulikuwa na tukio jingine katika kata hiyo ya Rwanchanga. Kuna kitongoji katika kijiji cha Rwanchanga ambacho kilijulikana kama Nyanguge. Kitongoji hiki nacho kinapakana na hifadhi ya Ikongoro. Mwaka 2000 wana kitongoji wa Nyanguge, walivamiwa asubuhi mapema na polisi na askari wa nyama pori wa hifadhi ya Ikorongo wakituhumiwa kuwa ni wakenya. Katika wilaya hii inaonekana iwapo watu hawatakiwi ni rahisi sana kuitwa wakenya na hivyo walisafirishwa hadi Sirari mpakani na Kenya na walipofika huko Mamlaka ya uhamiaji ya Nchini Kenya iliwakataa kuwa si wakenya na Mamlaka ya uhamiaji ya Tanzania iliwathibitisha kuwa ni watanzania. Walikuwa wameshaondoshwa kinguvu na eneo lao lilihitajika kuanzisha mapori tengefu mpakani mwa hifadhi yaani 'WMA'.

Baadhi ya watu waliokuwa wakiishi Nyanguge waliamua kutafuta maeneo sehemu nyingine wakati baadhi yao wakihamia Nyamuma.

Tukitaka kuelewa vizuri sababu za kuondolewa wananchi katika maeneo yao inatubidi tuvae miwani ya haki za kijamii na kiuchumi nchini mwetu. Tunaona jinsi wananchi Wanyanguge walivyoondolewa kwa madai kwamba ni raia wa Kenya, lakini hatima yake eneo liligeuzwa kuwa sehemu ya kiutawala ya wanyama pori. Suala la kimaendeleo hapo katika kuhifadhi wanyama pori limesigana na haki za watu ambao wana haki ya kuishi katika maeneo yao. Kwa vile inaonekana kuwa si halali kumuondoa Mtanzania katika eneo lake bila kufuata taratibu za kisheria kama ilivyo katika sheria za ardhi ilikuwa ni rahisi tu kuwaita watu wale raia wa Kenya na haki yao kuchukuliwa.

Bahati mbaya watu Wanyanguge hawakuweza kufuatilia haki yao hii ya kuwa na kwao na haki hiyo kuhifadhiwa hivyo walijitafutia maeneo na wakaendelea na maisha yao. Huo ulikuwa ni mwaka 2000 walipoondolewa Nyanguge. Iwapo hili suala la kimaendeleo lingefuata misingi ya haki za

binadamu watu hawa wangehusishwa na baada ya majadiliano wangekubaliana na wao wangeelekezwa sehemu nyingine au walipwe fidia kama sheria inavyodai badala ya ukatili huo waliofanyiwa.

Waandishi wa kitabu cha **Stones of Hope** walijaribu kulichambua hili suala la Nyamuma Iliyobaki na walijiuliza maswali kuhusu uhusiano wa haki za kiuchumi na kijamii na muendelezo wa mabadiliko ya kijamii na sera za maendeleo. Walitaka kuelewa vipaumbele vya maendeleo ya kiuchumi vinavyoainishwa na sera zinavyotekelezwa. Walitaka kuelewa ni nani hasa huhusika au huhusishwa katika kupanga vipaumbele hivyo na faida zake zinagawanywa vipi. Kweli sera za maendeleo huweza kuwa za manufaa kwa jamii, lakini pia zaweza kuwa maumivu kwa jamii kama ilivyokuwa kwa hawa wa Nyanguge na baadaye kwa hawa wa Nyamuma Iliyobaki, hasa tukiwa na utawala usio wa uwazi kwa wananchi. Hawa waliitwa raia wa Kenya wakaondolewa lakini hatimaye eneo lao lilitumika kwa suala ambalo lingeweza kuelezeka tu nakueleweka.

Mwaka uliofuata 2001 mwezi wa kumi ndipo wananchi wa Nyamuma Iliyobaki nao walipoondolewa kinyama kabisa katika maeneo yao. Katika maelezo yaliyowahi kutolewa na Mkuu wa Wilaya aliyeongoza uchomaji wa nyumba na kuwafukuza wenyeji, alisema watu wale yaani wananchi wa Nyamuma Iliyobaki walikuwa wabakaji, wezi wa mifugo na wawindaji haramu. Ikiwa hii ilikuwa kweli ndio sababu yakuondolewa kwao bado tuna maswali mengi sana. Inawezekanaje kitongoji kizima kiwe ni cha wabakaji? Na iwapo kweli ni wabakaji kosa hilo ni la jinai na zipo sheria za jinai zinazoelekeza njia za kuchukua pale mtu anapokosa kwa njia hiyo.

Kitongoji kile kilikuwa na wakazi karibu elfu moja wakiwemo watoto, vijana, watu wa makamu na hata wazee. Walikuwepo pia watu wenye ulemavu. Sababu aliyoitoa Mkuu wa wilaya haielekei kuwa na usahihi wowote. Hata angesema kijiji hicho kinaficha wahalifu bado haikuwa sahihi kuwaondoa katika maeneo yao na kuwachomea moto nyumba pamoja na mali zao nyingine.

Hapa inabidi tuliangalie tena suala hili katika muktadha wa upatikanaji wa ardhi na utawala mbovu. Wakati tukiwahoji wahanga wa tukio hili wapo waliolihusisha tukio hili na ardhi yao kuwa ilikuwa nzuri na ilitamaniwa na viongozi hasa kwa vile kijiji kizima kilivyochukuliwa walidhani itakuwa rahisi wao kuchukua ardhi ya kitongoji kilichobaki. Hili linaweza kueleweka kiasi kwani wananchi wa Nyamuma Iliyobaki walipoondolewa tu muda haukupita, ardhi yao iligawiwa kwa watu wengine wakiwemo wafanyakazi wa hifadhi ya Ikorongo na wengine watendaji wa wilaya ya Serengeti kwa kuuziwa. Mmoja wa wahanga aliyekuwa na mali nyingi yeye aliweza kuinunua ardhi yake tena, hivyo wakati wengine wakihangaika yeye alirejea katika eneo lake bila kubughudhiwa kwani aliweza kutoa hela yakutosha kununua ardhi yake mwenyewe. Hapa napo tunaona suala la utawala mbovu kuwa mtawala huyu angeweza kutafuta njia halali za kuwaondoa wananchi hawa kama aliihitaji hiyo ardhi kwa manufaa ya umma. Kwa vile alikuwa na hila hakuwa na sababu za msingi hivyo aliwahamisha kwa mabavu akitumia nguvu alizokabidhiwa kihalali kufanya kazi kwa hila.

Wananchi wengine walipohojiwa walisema kuwa kilichosababisha waondolewe ni kero walioiletea mamlaka pale walipoamua kudai fidia ya shule iliyokuwa katika eneo la Nyamuma iliyochukuliwa kuwa sehemu ya hifadhi ya Ikorongo. Wananchi hawa wanadai kuwa waliona wale wenzao waliokuwa na ardhi katika kijiji cha Nyamuma kilichochukuliwa walipewa fidia ya ardhi na mali zao kama sheria inavyoelekeza. Wao wakaikabili mamlaka nakudai fidia ya shule iliyokuwa imejengwa kwa nguvu ya wananchi. Walifahamu kuwa ile shule ingeweza kulipiwa fidia ambayo ingesaidia kuanza ujenzi wa shule nyingine. Walipokuwa wanafuatilia walionywa na mamlaka husika kuacha vinginevyo itakuwa taabu kwao. Wao waliamini kuwa ilikuwa ni haki kulipwa fidia kwa vile fedha za fidia zilikuwepo na ile shule ilistahili ifidiwe. Kwa vile hawakusikia, wengine wao walikamatwa wakatuhumiwa kuwa raia wa Kenya na kupelekwa mpakani, wakati wengine walipewa kesi ambazo kuna waliofungwa mpaka miezi sita. Iliposhindikana kabisa mamlaka ilichoshwa na kero

hiyo na kuamua kuwaondoa moja kwa moja.

Wapo watu waliokuwa na dhana kuwa wananchi wa Nyamuma Iliyobaki walikuwa wakiishi katika mbuga au pori tengefu la Ikorongo, hivyo waliondolewa kupisha hifadhi hiyo. Ukweli ulio dhahiri ni kuwa wananchi hawa waliishi karibu na hifadhi na sehemu ya kijiji chao kilichukuliwa kuwa sehemu ya hifadhi na waliohusika walilipwa nakuondoka. Sehemu ya mgogoro yaani Nyamuma Iliyobaki, haikuwahi kuwa sehemu ya hifadhi ya Ikorongo pamoja na kuwa vinapakana, pia wananchi wake hawakuwahi kulipwa fidia.

Hili tukio la Nyamuma Iliyobaki kama tulivyoona shauri lake lilivyoendeshwa linaonyesha jinsi mamlaka zinavyoweza kutumiwa vibaya na kuumiza watu na kuingilia uhuru wao na haki zao. Hawa wananchi waliondolewa makwao, bila sababu yoyote ya msingi na njia iliyotumika kama tulivyoona ilikuwa ni mbaya sana na hasa ukiangalia kuwa walikuwepo watu wa kila hali katika tukio hilo.

SURA YA TATU

03

# WANANCHI WA NYAMUMA ILIYOBAKI WAFUATILIA HAKI YAO YA KUWA NA KWAO

## 3.1 Hali Halisi ya Upatikanaji wa Haki

Baada ya wananchi wa Nyamuma Iliyobaki kujikuta wameondolewa makwao ilibidi kuanza kuitafuta haki yao. Hii haikuwa rahisi kwa vile Mkuu wa Wilaya alikuwa amedhamiria kuwaondoa na kuhakikisha hawawezi kurejea tena ili kuuficha ukweli wa yaliyotokea. Kwanza, watu katika vijiji vya jirani walionywa wasiwapokee watu hao. Wapo watu wanaoshuhudia kuwa waliogopa kuwakaribisha kwa vile nao waliambiwa watapatwa na kilichowapata hao. Walioweza kukimbilia mjini Mugumu waliishi kwa kujifichaficha huku wakitafuta njia za kujikimu. Hawakuwa na mali yoyote hata nguo zao zilichomwa moto wakati akiba za chakula ziliteketea. Watu waliokuwa wanawapa ajira za vibarua ili waweze kujikimu nao walitishiwa kuwa hawapaswi kuhusiana na hao watu hivyo

walikuwa wanafanya vibarua kwa kificho. Hali kama hiyo haikuwapa wepesi wakujaribu kufuatilia haki yao lakini walijitahidi kufuatilia kila walipoweza.

### 3.1.1 Kukikabili Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu [LHRC]

Wahanga wa tukio la Nyamuma waliokimbilia Tarime ndio waliokutana na Watendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambao walikwenda huko kufuatilia ukiukwaji wa haki za binadamu. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambacho tutakielezea baadaye, kimekuwa na kazi ya ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu tangu kilipoanzishwa mwaka 1995. Kituo hiki pamoja na kuwa makao yake makuu yapo Dar-es-Salaam kimeweza kufanya kazi za ufuatiliaji sehemu mbalimbali nchini. Mwaka 1999 Kituo kilikuwa kikifuatilia taarifa za mauaji yaliyosemekana kutokea huko katika hifadhi ya Serengeti. Taarifa zilizokifikia Kituo kutoka kwa shirika la maendeleo Tarime, zilihusu watu waliouwawa katika hifadhi hiyo kwa kutuhumiwa kuwa wawindaji haramu. Ilikuwa ni ngumu sana kupata uthibitsho kwani wale waliokuwa wamenusurika walikuwa hawapo tayari kutoa ushahidi. Watendaji wa LHRC walifika Tarime ambapo walielekezwa walipo wahanga wa tukio hilo. Haikuwa rahisi kabisa kuweza kupata ushirikiano kutoka kwa kila mmoja wa wahanga hao kwa hofu aliyokuwa nayo.

Wakiwa huko Tarime, ndipo walipopokea taarifa za Serengeti kuwa wapo wanakijiji waliochomewa nyumba zao. Walipopokea taarifa hiyo ilibidi watoe taarifa ofisini kuwa pamoja na kilichowapeleka kuna taarifa mpya za watu waliochomewa nyumba zao na watu hao walikuwa wamejaribu kuwasiliana na Kituo wakawa hawafahamu pakuanzia. Walipokuwa huko Tarime, walipewa ruhusa ya kuelekea Serengeti kufuatilia. Wakati huo huo Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo naye akiwa safarini Musoma alikutana na watendaji wa Kata za wilaya za Serengeti, Bunda na Musoma ambao baadhi yao nao walitoa taarifa hiyo kuwa wapo watu wa kitongoji cha Nyamuma Iliyobaki wamechomewa nyumba zao na mkuu wa wilaya ya Serengeti.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapopokea taarifa kama hii hufanya ufuatiliaji ili kubaini ukweli na pia kuangalia njia zinazoweza kutumika kuwasaidia wahanga.
Maafisa wale watatu wa Kituo ambao walikuwa ni wanasheria watafiti wawili na dereva mmoja walifunga safari toka Tarime kuelekea Serengeti kufanya ufuatiliaji wa taarifa hiyo. Walipewa majina matano ya wahanga waliokuwa Serengeti. Waliwapata ndugu wawili Ibrahim Koroso na Wilson Chacha ambao ndio waliowaelekeza kwa wahanga zaidi. Waliwakuta wakiwa hawana makazi bali wapo waliokuwa wamejishikiza kwa ndugu zao. Wanasheria hawa walianza kumhoji mmoja baada ya mwingine na kuunganisha kila hojaji kuona picha nzima ya tukio lenyewe.

Katika wahanga alikuwepo mtu mmoja ambaye kwa asili si mtu wa mkoa wa Mara bali alikuwa askari mstaafu na alikuwa akiishi Nyamuma Iliyobaki kwa wakati huo tukio lilipotokea.

Baada ya kuwahoji wote walioweza kuwafikia walijipanga kwenda kwenye eneo la tukio. Huko nako walitembelea nyumba hadi nyumba zile zilizokuwa zimechomwa moto. Walipita hadi kufikia mpakani kabisa na hifadhi ya wanyama pori ambapo waliachana na wenyeji waliowapeleka ambao waliamua kurudi mjini kwa miguu na si kwa gari.

### 3.1.2 Yaliyowakuta Watendaji wa LHRC

Watendaji wa LHRC wakiwa wamekwisha shuhudia kwa macho nyumba na ghala zilizokuwa zimechomwa moto walijiandaa kurudi kwenye gari lao ili waweze kurudi mjini. Walikuwa wamesikitika kuwa yale waliyoyasikia wameyaona kwa macho na walikuwa wakaandae taarifa yao ili wakirejea ofisini waweze kupanga mkakati wa kufanya. Aidha walikuwa wamepiga picha mnato ikiwa ni ushahidi kamili wa waliyoyaona. Wakiwa wanatembea kuelekea kwenye gari waliona gari aina ya 'landcruiser' likielekea mbele yao nakuwafuatilia kama linataka

kuwagonga. Ilibidi wakimbie na wakaingia vichakani kwa nia yakujificha. Waliokuwa kwenye lile gari walishuka wakiwa na bunduki na kuwaamuru watoke mafichoni vnginevyo watawapiga risasi. Hapo kwa usalama wao ilibidi watoke wakiwa wamenyoosha mikono juu kuashiria kuwa hawakuwa na nia ovu na wamejisalimisha.

Hapo hapo walitangaziwa kuwa wapo chini ya ulinzi wakavuliwa mashati, wakanyang'anywa hati za kusafiria. Ifahamike kuwa wakati huo ilikuwa watu wakisafiri kuelekea mkoani Mara au Mwanza huchukua hati za kusafiria kwa vile inawezekana wakati mwingine kusafiri kwa kupitia nchini Kenya kwa vile barabara zilikuwa mbaya sana humu nchini. Walinyang'anywa vitambulisho na kupelekwa katika ofisi za hifadhi ya wanyamapori ya Ikorongo. Walikuja kuelewa kuwa eneo hilo lilizuiwa watu wasitembelee na kuna watu walikuwa wamepewa kazi ya kutoa taarifa iwapo watamuona mtu yeyote akiwa kwenye eneo hilo ambalo mkuu wa wilaya aliweka marufuku hiyo. Hivyo wakati wao wakiwa wanazunguka katika hilo eneo watoa taarifa walipeleka taarifa na ndiyo maana waliweza kufuatiliwa na kukamatwa kabla hawajaondoka.

Watendaji hawa wa LHRC walipelekwa polisi mjini Mugumu. Wakiwa polisi walielezwa kuwa suala la kukutwa katika eneo la Nyamuma Iliyobaki ni la mkuu wa wilaya kwa hivyo walipelekwa kwa mkuu wa wilaya. Mkuu wa wilaya aliwahoji kuwa wao ni nani na wamefuata nini katika lile eneo. Walijieleza lakini mkuu huyo wa wilaya hakuamini kuwa wale walikuwa wafanyakazi wa LHRC alidhani kuwa ama ni wa usalama wa taifa au waandishi wa habari wa kimataifa. Mkuu huyo wa wilaya hakutaka kabisa habari hizo zijulikane kimataifa.

Watendaji hawa wa LHRC walieleza kuwa pamoja na kuwa hawakufanyiwa vitendo vya mateso ya mwilini lakini walitishiwa na wakaondolewa kwa mkuu wa wilaya na kukabidhiwa kwa askari polisi. Walitakiwa waende kuwatafuta wale watu waliowapeleka kule Nyamuma. Baada ya siku kwisha bila kuweza kuwaonyesha waliowapeleka waliruhusiwa kwenda

kulala nyumba ya wageni. Hata hivyo haikuwa rahisi kuweza kulala kwani kwa vitisho ambavyo walikuwa wamevipata hadi kuhojiwa na afisa usalama wa wilaya viliwapa hofu sana.

Kwa siku tatu waliendelea kuwatafuta wale watu waliowapeleka Nyamuma Iliyobaki. Asubuhi hufuatwa na askari kisha huzunguka, siku ikiisha hurejea polisi na kesho yake hivyo hivyo. Gari walilokuwa nalo lilipekuliwa sana wakijaribu kutafuta ushahidi wa yale waliyoyapata huko Nyamuma. Baada ya siku hizo Mkurugenzi wa LHRC alipiga simu kwa mkuu wa wilaya nakutaka waachiwe huru au wapelekewe mawakili iwapo wana kosa lakuwapeleka mahakamani. Baada ya hapo mkuu huyo wa wilaya alitoa amri kwa polisi watendaji hawa wapelekwe wilaya ya Tarime wakisindikizwa na polisi. Hili lilifanyika ikiwa ni siku sita tangu walipokamatwa. Hawakufunguliwa mashtaka na mahojiano yalikuwa zaidi na mkuu wa wilaya ya Serengeti na si polisi.

Walipofika Tarime walipokelewa na mkuu wa wilaya hiyo aliyejulikana kama Paschal Mabiti. Alitaka mikanda ya picha walizopiga isafishwe. Pale Tarime hapakuwa na mahali pa kusafishia picha hizo hivyo walilala na kesho yake walikwenda Musoma mjini ambapo walisafisha zile picha. Nyingi ya hizo picha zilikuwa ni za ukeketaji wa watoto wa kike ambazo walizichukua walipokuwa Tarime. Mkuu huyo wa wilaya alipoona hizo picha hakuona zilikuwa na tatizo lolote ila alichukua baadhi na vifaa vingine walivyokuwa navyo vilikuwa vimechukuliwa huko Mugumu Serengeti.

Ilibidi maafisa hawa waruhusiwe kuondoka na walitakiwa waendelee kusindikizwa na askari polisi hadi wawe wametoka kabisa mkoani Mara. Wao waliweza kuongea na wale maaskari wakawakatia tiketi za mabasi, hivyo askari wakarudi kwa mabasi na hawa maafisa wa LHRC wakapitia Musoma hadi Singida na kisha Arusha wakarudi Dar-es-Salaam. Zilikuwa ni siku za wasiwasi na mashaka makuu kwa maafisa hawa hasa walivyokuwa wakipelekwa kwa mkuu wa wilaya na polisi wakitakiwa

wawaonyeshe waliowapeleka jambo ambalo lingeweza kuwaletea taabu zaidi wale wahanga. Bahati nzuri hawakuwafichua na hata askari walisema si rahisi kuwapata hao watu kwani wana usiri mkubwa. Hapa tunaona jinsi haki ya uhuru wa hawa maafisa ilivyoingiliwa kwani iwapo kuwepo katika maeneo waliokuwa ilikuwa ni kosa basi sheria ilitakiwa ichukue mkondo wake na si kuwazuia kwa siku sita.

Ilivyokuwa ni kuwa mkuu wa wilaya ndiye aliyekuwa amri na ndiye aliyekuwa sheria. Walipofikishwa katika ofisi za hifadhi ilisemekana ni mkuu wa wilaya ndiye alikataza watu wasiingie katika eneo lile. Walipofikishwa polisi napo walielezwa hilo ni suala la mkuu wa Wilaya na si suala la kisheria. Mkuu wa wilaya naye alikuwa akiwahoji na kuzuia wasiondoke wilayani. Gari lao pia lilizuiliwa likiwa limekaa polisi kwa siku zote walizokuwa wamezuiwa kuondoka wilaya ya Serengeti.

Mamlaka ya Mkuu wa Wilaya inaonekana kabisa kuwa nje ya utaratibu wa sheria kwani pamoja na kuwa yeye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, yeye si mtekelezaji. Pale wanapopatikana watu na shutuma za kuvunja usalama, polisi ndio wenye kazi ya kusimamia hayo na wao ndio walitakiwa wawahoji katika kituo cha polisi na iwapo kuna hali ya kuonekana walivunja sheria basi wafikishwe mahakamani. Walipotezewa muda kwa kuzuiwa kuondoka bila sababu za kisheria.

### 3.1.3 Maamuzi ya LHRC Kuwasaidia Wahanga wa Nyamuma Iliyobaki

#### 3.1.3.1 Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa Ufupi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambacho kinafahamika sana kama LHRC ikiwa ni kifupi cha jina lake kwa Kiingereza, ni shirika ambalo lilianzishwa na wanasheria waliokuwa wanafanya kazi Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam wakiwa wahadhiri wa Chuo Kitivo cha Sheria. Wahadhiri hawa walishirikiana na wanasheria wenzao waliokuwa wakifanya kazi za

uwakili jijini Dar-es-Salaam wakaanzisha shirika lililojulikana kama TANLET. Shirika lilikuwa limelenga kutoa elimu ya sheria kwa umma na msaada wa kisheria. Katika kazi zake kilianzisha mradi wa haki za binadamu ambao ulistawi ndio ukageuzwa kuwa shirika ambalo ndiyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Kituo kilianzishwa rasmi mwaka 1995 mwezi Septemba baada ya kupata usajili tarehe 26 na kuwa shirika huru nje ya TANLET. Wanaokumbukwa kwa kusajili shirika hili ni pamoja na Dkt. Ringo Tenga, Marehemu Dkt. Sengondo Edmund Mvungi, Dkt. Harrison Mwakyembe, Profesa Costa Mahalu na Dkt. Wil bert Kapinga. Wakati huo aliyekuwa anasimamia mradi huo uliobadilika kuwa shirika alikuwa Profesa Ibrahimu Juma ambaye wa sasa ndiye Jaji Mkuu wa Tanzania wakati huo akiwa mhadhiri kijana katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Baada ya usajili Dkt. Mvungi aliendeleza kazi ya kuwa mkurugenzi wa muda akapokelewa na Evod Mmanda aliyekuwa Mkurugenzi wa muda kabla ya kupokelewa na Dkt. Helen Kijo-Bisimba aliyeliongoza shirika kwa miaka 22 na kuna kipindi cha miaka mitatu katika uongozi wake alikwenda masomoni kwa miaka mitatu ambapo Wakili Francis Kilian Kiwanga alikaimu nafasi hiyo hadi aliporejea na kuendelea kukiongoza Kituo hadi Juni 2018 alipopokelewa na Wakili Anna Henga ambaye wakati kitabu hiki kinaandikwa ndiye Mkurugenzi Mtendaji. Kituo kimekuwa kikiongozwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo ndiyo msimamizi wa Mkurugenzi Mtendaji.

Tangu LHRC ianzishwe hadi wakati huu imekuwa na wenyeviti wa bodi wapatao watatu ambao ni Jaji Kahwa Lugakingira [Marehemu] ambaye wakati akipokea uenyekiti kama Mwenyekiti wa kwanza alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu na aliacha kuendelea kuwa mwenyekiti alipoteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufaa. Alifuatiwa na Askofu Dkt. Elinaza Sendoro aliyekuwa wakati huo mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania. Alimaliza muhula wake wa uenyekiti alioutumikia kwa miaka 13 mwaka 2013 na akapokelewa na Profesa Geoffrey Mmari kuanzia Januari mwaka 2014. Profesa Mmari ni mstaafu wa ukuu wa vyuo mbalimbali kama Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Chuo Kikuu Huria Tanzania ambapo ndiye alikuwa mwanzilishi hadi akastaafu na kujiunga na Chuo Kikuu cha

Tumaini Dar-es-Salaam na kutoka hapo ndiye mwenyekiti hadi kitabu kinapoandikwa.

Kituo kina makao yake makuu jijini Dar-es-Salaam, kilianzia kwenye jengo la Tulyer lililopo barabara ya Barack Obama ambayo ilikuwa ikijulikana kama barabara ya Ocean. Kwa wakati huu makao makuu yapo kwenye Jengo lijulikanalo kama Justice Lugakingira kwa kumuenzi mwenyekiti wa kwanza wa Bodi ya Kituo aliyefariki mwaka 2003 na Kituo kikahamia katika jingo hilo ambalo ni lake mwaka 2004 mwezi Aprili tarehe 23. Kituo kilifungua ofisi Arusha na kwa sasa kinaendesha ofisi hiyo katika jengo lake lililopo eneo la Sakina. Aidha Kituo kina ofisi ya msaada wa sheria ya mfano iliyopo mtaa wa Isere wilaya ya Kinondoni jijini Dar-es-Salam na ofisi nyingine ilifunguliwa mwaka 2019 huko Dodoma ili kuwezesha mawasiliano ya karibu na wizara na taasisi za serikali ambazo karibu zote zimehamia Dodoma.

Baada ya kuanza, Kituo kilipanga kazi kubwa ya kuelimisha umma masuala ya haki za binadamu, kutoa msaada wa kisheria na kufuatilia ukiukwaji wa haki za binadamu, pamoja na kufanya utafiti kisha kufanya utetezi na ushawishi kuhusu uboreshwaji wa sheria, sera na tabia za haki za binadamu nchini. Kituo kimeweza kufikia watu wengi karibu mikoa yote wakiwemo wanasiasa, watendaji wa Kata na vijiji, askari polisi wa ngazi za wilaya na ngazi za kitaifa na Kituo kimeanzisha huduma za usaidizi wa kisheria katika wilaya za mikoa kumi na moja hadi sasa ambayo ni Manyara, Arusha, Morogoro, Mara, Shinyanga, Mwanza, Simiyu, Singida, Ruvuma, Mtwara na Dar-es-Salaam. Kituo pia kimeelimisha wananchi ambao wamekuwa na utayari wakuwa waangalizi wa haki za binadamu katika wilaya zao na hivyo kuwa na waangalizi wa aina hiyo karibu kila wilaya hapa nchini.

Katika ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu Kituo hiki kimekutana na kesi nyingi za ukiukwaji wa haki ambao umefanyiwa watu katika ubinafsi wao na wakati mwingine watu wengi kwa pamoja. Kesi binafsi huweza kuwa kesi za kusingiziwa kama ilivyomkuta mwandishi wa

habari Bwana Adam Mwaibabile (Marehemu) mwaka 1998 huko mkoani Ruvuma ambapo aliandika taarifa kuhusu uwepo wa njaa mkoani huko taarifa iliyomchukiza mkuu wa mkoa huo wakati huo akiwa Nocodemus Banduka. Adam alipata hekaheka kwa kujikuta anafunguliwa kesi ya jinai kwa kuwa alikuwa na barua iliyokuwa ikimkatalia kupata leseni ya biashara. Barua hiyo ikasemekana ni hati ya serikali iliyokuwa siri ambayo hakutakiwa kuwa nayo. Alipatwa na hatia na akafungwa mwaka mmoja ila alitumikia kifungo mwezi mmoja tu kwani Kituo kilifuatilia na jalada lake likaitwa kwa Jaji Kiongozi aliyeanzisha kesi hiyo upya na akakutwa hakuwa na hatia kwani barua ile ilimhusu yeye na ilikuwa ikijibu ombi alilokuwa amepeleka kwa mamlaka ya leseni mkoani.

Kituo kimeweza kufuatilia mauwaji yaliyofanywa katika Mbuga ya Serengeti miaka ya 1997 na 1999 na pia kiliendelea kuwasaidia wananchi wa wilaya ya Hanang ambao ardhi yao ilitwaliwa na serikali wao wakiachwa bila ardhi wala fidia. Kituo kimeendesha kesi za kimkakati ili kujaribu kubadili sheria mbovu au kuhoji kauli zinazokinzana na sheria na haki za binadamu za viongozi. Shauri la kimkakati lililofurahiwa sana ni lile lililofunguliwa mwaka 2005 kupinga mabadiliko ya sheria ya uchaguzi ambayo yaliweka kipengele cha kuruhusu wagombea uchaguzi kuweza kuwapa wapiga kura takrima kama ilivyo desturi ya watanzania. Sheria hii ilipingwa kwani ilionekana ni ya kibaguzi na pia ingechochea rushwa katika uchaguzi. Mahakama ilikubaliana na hoja za Kituo na kuamuru sheria hiyo ibadilishwe.

Kwa miaka 25, LHRC imeweza kufanya kazi nyingi sana nchini na hata nje ya nchi ikiwemo kuwasaidia wananchi binafsi zaidi ya 300,000 waliokuwa na uhitaji wa msaada wa sheria. Pale ambapo Kituo kinafuatilia haki za binadamu kinaweza kuwasaidia wahanga kufungua shauri mahakamani na iwapo hawana uwezo kuwapatia msaada wa kisheria. Mfano ni ufuatiliaji wa kitendo cha kinyama alichofanyiwa kijana aliyejulikana kama Zakayo Salum wa kijiji cha Magugu huko wilaya ya Babati wakati huo ikiwa ni mkoani Arusha, mwaka 1998 ambapo baada ya ufuatiliaji Kituo kilimsaidia kijana huyu kuendelea na kesi dhidi ya

mlalamikiwa aliyekuwa tajiri mkubwa wa shamba la miwa. Pamoja na kuwa kesi ilikuwa inashikiliwa na dola ikiwa ni jinai dhidi ya yule tajiri, lakini kuhakikisha Zakayo na mashahidi wake wanafika mahakamani ilikuwa jukumu ambalo Kituo ililichukua hasa pale mshtakiwa alipoomba kesi ihamishiwe Arusha mjini akijua kuwa mlalamikaji na mashahidi wake wasingeweza kupata uwezo wa kufika Arusha mjini kwa vile walikuwa hawana fedha.

Hivyo haikuwa suala jipya pale watendaji wa Kituo walipofuatilia suala la wahanga wa Nyamuma Iliyobaki mwaka 2002 na kukubali kuwapatia usaidizi wa Kisheria. Baada ya maafisa hao kukamilisha kazi yao huko Serengeti na kuachiwa kurudi Dar-es-Salaam zilipo ofisi za Kituo walitoa taarifa ya tukio zima na hasa tukio la kuchomwa kwa zile nyumba za kitongoji cha Nyamuma Iliyobaki na pia walivyokamatwa na yote yaliyowasibu. Uongozi wa Kituo uliamua kuwapatia msaada wa kisheria wananchi wale zaidi ya mia nane waliokuwa kwenye kaya 135 kutafuta haki yao.

Ilibidi wataalam wa Kituo wakutane na kuichambua ile taarifa ili kuona watakavyoweza kulikabili lile jambo. Waliona kuwa pale kutakuwa na haki ya wale watu ya kuwepo katika ardhi yao ambayo ni haki yao yakuwa na kwao. Hivyo ilikuwa wazi wale watu wa Nyamuma Iliyobaki, walikosewa kwa kuondolewa kwa njia ya nguvu na kuchomewa mali zao katika eneo lao halali. Kuharibiwa kwa mali yao lilikuwa suala jingine ambalo lilihitaji watu wale kudai fidia ya mali zao zilizochomwa kuharibiwa na kuibiwa.

Kwa vile maafisa wale walikuwa wamekwenda pia kufuatilia haki za watu waliouwawa kwenye hifadhi ya Serengeti, ilibidi wakamilishe pia ufuatiliaji huo ili yote yashughulikiwe kwa pamoja. Kuweza kufuatilia masuala haya kuna gharama hivyo masuala ya gharama nayo yaliangaliwa na utafutaji wa fedha ulianza.
Wakati matukio haya yanatokea ndipo nchi yetu kwa mara ya kwanza

(mwaka 2001) ilipata Tume ya Haki za Binadamu inayojulikana kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Ilijadiliwa ndani ya LHRC iwapo suala hili lipelekwe mahakamani au la? Suala hili lingeweza kupelekwa mahakamani lakini kwa kuona kuwa ipo Tume mpya ya Haki za binadamu iliamuliwa kuijaribu Tume kuona itakavyoweza kulitatua suala hili na kuwapa hawa wananchi haki zao kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Tume.

Hivyo, ilibidi kuangalia na kuielewa vizuri sheria ya Tume na njia inayopaswa kufanyika katika kupeleka malalamiko katika hiyo Tume. Wanasheria walijipanga na kuandaa nyaraka zote zilizostahili ili kuikabili Tume hiyo ya Haki za Binadamu. Ilionekana wazi iwapo Tume itafanya kazi yake kama Sheria inavyoitaka itakuwa ni rahisi zaidi kwa wananchi wale kupata haki yao kwani njia ya mahakama ingeweza kuwa ndefu na pia gharama zaidi kutokana na muda ambao ingeweza kuchukua.

Wakati Kituo kinajipanga kuiendea Tume wahanga hawa waliendelea kupata shida na hivyo walijaribu kuandika tena barua kutafuta msaada hasa walipogundua kuwa mkuu wa wilaya alianza kuigawa ile Ardhi yote kwa watu wengine kwa kuwauzia.

S.L.P 115 MUGUMU
SERENGETI
TAR. 27/4/2002.

LEGAL & HUMAN RIGHTS CENTRE
RECEIVED
29 APR 2002
P. O. Box 75254
DAR ES SALAAM

MKURUGENZI MTENDAJI
KITUO CHA SERIA NA HAKI
ZA BINADAMU S.L.P 75254
DAR ES SALAAM.

YAH: MALALAMIKO YETU KUHUSU TUKIO LA TAREHE 12/10/2001 LA MKUU WA (W) SERENGETI NDG THOMAS OLE SABA'IA KUTUCHOMEA MAKAZI YETU NA KUTUPORA MALI ZETU ZOTE. BAADAYE AMEGAWIYA WATU WENGINE WA KIJIJI CHA BONCHUGU KWA KUWAUZIA.

Ndugu mkurugenzi-

Sisi wananchi wa kijiji cha Nyamuma kwa masikitiko makubwa tunaandika tena malalamiko yetu kwako mara ya tatu tena kuhusu mkuu huyo wa wilaya anavyotutesa kwa hali zetu ofisi yako ni shahidi walipofika kwenye tukio walishuhudia juu ya ukatili wake na unyama aliotufanyia ktk kitongoji.

Ndugu mkurugenzi-

Baadaye sasa kitokile tulilokamishwa kwa hira na vizingizio vingi kwa ajili ya madai yetu ya pesa za shule ya msingi BUGUMBE milioni 19 kwa hivi sasa ametoa amri kwa mtendaji kata ya Manchira, Diwani wa kata. Na mtendaji wa kijiji Bonchugu kwa kuwaagiza wananchi wa kijiji cha Bonchugu. Mahame yetu kila mwananchi analipa sh. 315,000 hadi 320,000 kuanzia tarehe 5/9/2002 zoezi hilo limekwisha fanyika na ujenzi unaendelea ktk maeneo yetu ya kitongoji cha CCM Senta nyamuma iliyobaki na kuwaagiza, kubadilisha sura ya awali kwa kukata miti ya kudumu

(1)

*Inaendelea >*

awali walikuwa kaya 54 na [illegible] wa
(W) amewahamisha kutoka Nyamongo kwa kila
zake na kuanzia watu wengine walikuwa kaya
79 - 91 kwa sasa wamehamisha watu 89 wengine kuto-
ka kijiji cha Nyangoto ambao ni wanyabasi
waliondolewa ni koo ya warenchoka. Amamgaza
kiukabila na rushwa kibao anadai kuwa wa-
renchoka ni koo dogo hawana mali eti wanyaba-
si ni koo kubwa na wanayo mali ya kutosha.

Ndugu Mkurugenzi,

tunaomba msaada wako wakishirikiana
ili kufuta utawala huu wa kufuata ukoo tajiri na ma-
sikini tupate haki zetu.

(1) Tunadishiwe haki zetu pamoja na makao yetu
(2) Chakula cha kutumia.
(3) mali yetu iliyoporwa na mkuu wa (W)
(4) Shule ili watoto wetu wapate Elimu.
(5) Na mavazi ya kujisitiri.

Pia taarifa tunaomba malalamiko hatujapata
msaada wowote ule tumepoteza wazee vikongwe
na watoto wadogo kwa ajili ya tapia mlo na
idadi kubwa. Wanawake wetu wamekimbilia
mijini na kutuachia watoto kwa ajili shida
tunazopata. Hii ya malalamiko yetu ya ku-
fungua kesi bado hatujafunguliwa kwa ajili ya
uchunga wetu. Tunaomuona Mwanasheria wa kanda
Mwanza akija tarehe 9/4/2002.

- Kuhusu kesi ya wenzetu wa kitongoji cha
mara Cooper Nyamongo na RM 12/2000.
- Tunakuomba ofisi yako itusikie kilio chetu
na kutusaidia kwa wakati ufao muafaka. Asante
- Wenu kwa niaba wanakitongoji cha CCM
Senta Nyamwaga iliyobaki.

JACKISON MWITA - [signature]

SURA YA NNE

04

# TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA: KIMBILIO LA HAKI

## 4.1 Uwepo wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa ni chombo kipya cha haki wakati wananchi wa Nyamuma Iliyobaki walipopatwa na huo mkasa. Tanzania haikuwa na Tume ya aina hii kabla ya mwaka 2001. Tume za aina hii zimekuwepo katika nchi nyingine za kiafrika kama Ghana, Uganda na Afrika ya Kusini. Wanaharakati wa haki za Binadamu kwa kuona upungufu huu hapa nchini kwetu walifanya kampeni yakutaka uwepo wa Tume ya aina hii. Mwaka 1998 wakati Tamko la Haki za Binadamu kimataifa limefika miaka 50, Azaki zipatazo zaidi ya 50 zilishirikiana na baadhi ya taasisi za serikali kama magereza na jumuiya za kimataifa hapa nchini wakitumia sherehe za miaka 50 ya Tamko kudai uwepo wa Tume huru ya haki za binadamu.

Tanzania kulikuwa na chombo kilichojulikana kama Tume ya kudumu ya Uchunguzi [Permanent Commission of Enquiry] ambacho kilikuwa kikijishughulisha na kupokea malalamiko ya wananchi zaidi yaliyohusu matumizi mabaya ya madaraka kwa watendaji wa chama na serikali wakati huo nchi ikiwa na chama kimoja tu cha siasa. Wengine walidhani kwa uwepo wa Tume hiyo ya uchunguzi kunatosha na hatuhitaji kuwa na Tume ya haki za binadamu. Baada ya madai ya Azaki mchakato ulianza wa kuipata Tume ya Haki za Binadamu. Ilibidi pia kufuatilia kuhakikisha kweli inaundwa Tume itakayoweza kukidhi matakwa ya haki za binadamu nchini. Wakati mswada umepelekwa bungeni wa kuundwa kwa Tume ya haki za binadamu, wana azaki na wasomi walifuatilia wakiwa na mswada mbadala wa jinsi tume inavyopaswa kuwa, kilichogundulika ni kuwa ule mswada uliokuwa umepelekwa bungeni ulikuwa wa ile Tume ya Uchunguzi iliyokuwepo na kilichobadilishwa ni kichwa cha habari tu. Wabunge walivyoonyeshwa waligundua na hivyo mswada mbadala ndiyo ukatumika ili kuunda Tume ya Haki za Binadamu nchini.

Tume ya haki za binadamu iliongezewa jukumu la utawala hivyo ikajulikana kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume hii iliundwa kwa mujibu wa ibara ya 129 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kwa mujibu wa ibara ya 130(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni kama yafuatavyo:

a) Kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi;
b) Kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa ujumla;
c) Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;
d) Kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadau na utawala bora;

e) Kama ikibidi kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu, au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;
f) Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika na masharti ya ibara hii katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi na majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;
g) Kutoa ushauri kwa serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
h) Kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume.

Kwa majukumu haya pia Katiba imetamka kuwa Tume ni idara huru inayojitegemea katika kutekeleza majukumu yake, Tume hailazimiki kufuata maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa au taasisi yoyote ya umma au ya sekta binafsi. Katiba pia imeainisha watakaoiendesha Tume ambapo kutakuwa na Makamishna akiwemo Mwenyekiti anayepaswa kuwa mtu mwenye sifa za kuwa Jaji, Makamu mwenyekiti na makamishna wengine watano pamoja na makamishna wasaidizi .

Kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Katiba, Tume ilipata makamishna wake na Mwenyekiti wake wa kwanza alikuwa ni Jaji Robert Kisanga aliyekuwa Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufaa Tanzania ila kwa sasa ni marehemu. Ili Tume iweze kufanya kazi zake Katiba ilitoa mamlaka kwa Bunge kupitia ibara 131(1) kuweza kutunga sheria ili kuweka masharti kuhusu mamlaka ya Tume na utaratibu wa kuendesha shughuli zake. Bunge lilitunga Sheria hiyo inayojulikana kama Sheria ya Tume ya Haki zaBinadamu na Utawala Bora namba 7 ya mwaka 2001. Baada ya sheria hii kupitishwa na kusainiwa na Rais, Tume ilianza kazi zake rasmi kisheria mwaka 2002. Ilikuwa ni faraja sana kwa watetezi wa haki za binadamu

kuwa Tume ya Haki za Binadamu ipo kisheria na ina nguvu za kusikiliza na kupokea malalamiko ya watu waliovunjiwa haki zao kwa mujibu wa Katiba na sheria. Hapo kama itakavyoelezewa zaidi ilikuwa fursa kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kuweza kuamua kupeleka shauri lile la Nyamuma Iliyobaki pamoja na la watendaji wake na lile la wananchi wa Serengeti waliosemekana wameuwawa katika hifadhi ya Serengeti.

## 4.2 Malalamiko yaifikia Tume ya Haki za Binadamu na Majibu Yake

Baada ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kutafakari njia za kuwasaidia wahanga wa tukio la Nyamuma Iliyobaki na pia njia ya wao kudai haki yao ya kunyang'anywa vifaa vyao vya kazi, waliamua kulipeleka shauri lao katika Tume ya Haki za Binadamu. Maamuzi haya yalifikiwa baada ya kikao cha kamati maalum iliyoundwa ambayo mwenyekiti wake alikuwa ni Dkt. Sengondo A. Mvungi na wajumbe wakiwa ni Bwana Ezekiel Massanja, Bwana John Wallace na Bwana Kaleb Lameck Gamaya. Kamati ilikutana siku ya tarehe 7 Mei mwaka 2002. Waliamua yapelekwe mashauri mawili kwa pamoja. Moja lilihusu Mauaji ya Serengeti ambapo kuna watu waliokuwa wameuwawa katika hifadhi ya Serengeti na ya pili ni hili la Nyamuma Iliyobaki.

Kwa mujibu wa Sheria inayoanzisha Tume kuna maelekezo ya jinsi yakupeleka malalamiko mbele ya Tume. Kwanza ilibidi kushauriana na wahanga na akapatikana mmoja aliyekubali jina lake kuwa la kwanza likiongozana na wenziwe, huyu ni Ibrahim Korosso na wenzake walikuwa 134 hawa walikuwa ndio walalamikaji wa kwanza na mlalamikaji wa pili katika shauri hili akawa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu akilalamikia kukamatwa kwa watendaji wake na kunyang'anywa vifaa vyao vya kazi. Waliokuwa wakilalamikiwa ni Thomas Loy Ole Sabaya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti wa pili akiwa ni Alexander Pantaleo Lyimo Mkuu wa polisi wilaya ya Serengeti na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ilibidi kuwaendea walalamikaji kuwaelezea kuhusu shauri hilo na kwa

nini iliamuliwa lipelekwe kwenye Tume ya Haki za Binadamu. Ilikuwa lazima kufanya hivyo kwa vile Tume ilikuwa mpya na haikuwa inajulikana sana na pia watu wengine walidhani tukipeleka Tume baadaye itabidi irudishwe mahakamani jambo ambalo halikuwa hivyo kisheria.

Pia baada ya kuandaa nyaraka hapo kituoni ilibidi zipitiwe na watu wengine ili kuhakikisha ziko sawa kabisa kwa kuzipeleka Tume na aliyesaidia kuhariri masuala ya kisheria alikuwa Tundu Lissu akisaidiana na Simia Hassan aliyekuwa anafanya kazi kwa kujitolea hapo LHRC.

Mwezi Juni mwaka 2002 ndipo wahanga wa Nyamuma Iliyobaki pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walipopeleka rasmi malalamiko katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Ibrahim Korosso na baadhi ya wahanga walifika Dar-es-Salaam na kwenda ofisi za Tume kuhakikisha malalamiko hayo yamefika na yamepokelewa.

### 4.2.1 Majibu kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Majibu kutoka Tume yaliyoandikwa tarehe 9 Mei 2003 karibu mwaka mzima tangu malalamiko yapelekwe yalifika Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu wakiwa ndio mawakili wa walalamikaji. Barua hiyo pamoja na kuwa ilikuwa imesubiriwa sana lakini ilipokuja ilizua simanzi kubwa sana kwani ilikuwa barua ya kuyakataa madai yaliyopelekwa. Tume ilieleza kuwa imewasiliana na mkuu wa wilaya ya Serengeti ambaye ndiye alikuwa akilalamikiwa naye amesema kuwa malalamiko hayo si ya kweli kama alivyojaribu kufafanua kwenye barua iliyopo hapo chini yenye kurasa 12. Kwa hiyo kwa kauli hiyo ya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti Tume ikapata sababu ya kuamua kuwa hakuna madai. Ukweli ni kuwa Tume ilikuwa bado ni mpya na ilikuwa ikifanya kazi kama ilivyokuwa inafanya wakati wa Tume ya kudumu ya uchunguzi. Haikuzingatia kabisa matakwa ya kisheria kwa sheria iliyoianzisha Tume hiyo. Hata aliyeiandika barua na kuisaini hakuwa mwenyekiti wa Tume na pia haikuonyesha kuwa yale majibu yalikuwa yameamuliwa na kikao halali cha Tume kwa mujibu wa

Sheria. Ukiiangalia hiyo barua ni kuwa Tume ilimwandikia Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na kumpelekea malalamiko. Mkuu huyo alichofanya aliamua kuandika utetezi wake kwa Tume akikanusha yote yaliyosemwa na Tume nayo ikakubaliana naye bila kuwapa walalamikaji fursa ya kusikilizwa. Yaani Tume ilifunga shauri lile kwa kauli ya Mkuu wa Wilaya anayelalamikiwa kama barua yake kwa Mkurugenzi - Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu inavyoonyesha.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

---------------

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Simu: **2110607-10**
Fax: **2111533.**
**Unapojibu tafadhali taja:**
**Kumb.**
Na.HBUB/S/1032/2001/2002/MAR/A/42

S. L. P. 2643,
DAR ES SALAAM,
TANZANIA.

9 Mei, 2003

LEGAL & HUMAN RIGHTS CENTRE
RECEIVED
21 MAY 2003
P. O. Box 75254
DAR ES SALAAM

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu,
S.L.P. 75254,
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: - KUONDOLEWA KWA NGUVU WANANCHI WA KIJIJI CHA NYAMUMA NA KUCHOMWA MOTO NYUMBA ZAO BILA KULIPWA FIDIA.**

**- KUKAMATWA WATAFITI KUTOKA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU TAREHE 1 – 5/1/2002 NA KUNYANG'ANYWA MIKANDA YA PICHA (VIDEO NA KAWAIDA)**

Rejea malalamiko mliyowasilisha mbele ya Tume yanayohusu vichwa vya habari hapo juu.

1:0 1:1 Kimsingi mmelalamika kwamba Mkuu wa Wilaya ya Serengeti alipokuwa akifanya kazi chini ya mamlaka aliyopewa alimwongoza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti kuwaamuru polisi, askari wa wanyama pori kutoka Hifadhi ya Ikorongo, wanakijiji kutoka Bonchungu na Rwamchanga kuwaondoa kwa nguvu wananchi wa Kijiji cha Nyamuma Wilayani Serengeti Vijijini kwa kuchoma moto nyumba zao na maghala ya chakula. Katika tukio hilo mmeeleza kuwa jumla ya kaya 132 na maghala 696 ya chakula yalichomwa moto.

1:2 Kwamba Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti wakitumia nguvu zao na vipaza

*Inaendelea >*

sauti waliwazuia wananchi wa Kijiji cha Nyamuma kupata hifadhi kutoka vijiji vya jirani na kwamba mwanakijiji yeyote akiwa mwathirika wa tukio au jirani atakayekiukia tamko hilo angepata adhabu kali.

1:3 Kwamba tangu tarehe 12/10/2001 hadi malalamiko yalipowasilishwa mbele ya Tume, wananchi wa Kijiji cha Nyamuma wamepata mateso ya kila aina yaliyo kinyume na utu kama vile kuwa wakimbizi ndani ya nchi yao, kuteswa kukamatwa bila kufunguliwa mashtaka, au kufunguliwa mashitaka bila sababu za msingi na kuwazuia kutoa taarifa zozote.

1:4 Kwamba, juhudi mbalimbali za walalamikaji kuomba msaada katika tatizo lao katika mamlaka mbalimbali kama vile kwa Mkuu wa Wilaya mwenyewe, Mkuu wa Mkoa, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hazikufanikiwa.

1:5 Kwamba, vitendo vya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti vimesababisha ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ambao ni pamoja na kuwafanya wananchi wa Kijiji cha Nyamuma kuwa wakimbizi katika nchi yao, kuchoma moto nyumba zao, upotevu wa mali zao, kugawanyika kwa familia, mateso, kunyanyaswa kukamatwa na kunyimwa haki ya watoto wao kupata elimu.

1:6 Kwamba sambamba na tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti waliwahi kuwaondoa na kuwahamisha nchini jumla ya familia 200 mnamo Januari, 2000 bila sababu za msingi kwamba watu hao ni Wakenya.

Baada ya ukaguzi wa kina, watu hao walionekana kuwa ni Watanzania kwa sababu nyaraka zao zote zilionyesha kuwa ni Watanzania. Watu hao wapo wakihifadhiwa na wengine kutangatanga hapo Serengeti Mjini na wengine huko Korotambe na Kubiterere Wilayani Tarime wakiwa na hali mbaya.

*Inaendelea >*

1:7 Kwamba mateso yote dhidi ya wananchi wa Kijiji cha Nyamuma ni kinyume cha Sheria za kimataifa kama vile Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu – 1948, mkataba wa Kiafrika wa Haki za Watu na Haki za Binadamu wa mwaka 1981, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, Mkataba wa Kimataifa wa Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966, na Mkataba wa Kimataifa wa kutokomeza aina zote za Ubaguzi wa Rangi wa 1965.

1:8 Kwamba, mbali na mikataba ya Kimataifa, Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti wamekiuka sheria na katiba ya nchi. Sheria hizo ni pamoja na kanuni ya Adhabu za Jinai Na. Sheria ya Elimu.

1:9 Kwamba, ili kuhakikisha kwamba habari hazipelekwi mahali popote, Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na Mkuu wa Polisi wa wilaya ya Serengeti walifanya kila wawezavyo kuzuia usambazaji wa habari. Hatua hiyo ni pamoja na kukamatwa kwa watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu tarehe 1 Januari, 2002 hadi tarehe 5 Januari, 2002. Mbali na kukamatwa kwao watafiti hao, walinyang'anywa mikanda ya picha (video na ya kawaida). Pia kwamba hivi sasa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti ameshatoa amri ya kuwaweka watu wengine ndani ili kuharibu ushahidi uliokuwepo.

Tume baada ya kupokea malalamiko haya imefanya uchunguzi wa kina ikiwa ni pamoja na kupata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti kama ifuatavyo:-

**KUH: KUONDOLEWA KWA NGUVU WANANCHI WA KIJIJI CHA NYAMUMA NA KUCHOMWA MOTO NYUMBA ZAO BILA KULIPWA FIDIA.**

Ili uweze kufahamu suala hili vizuri na kwa kirefu, nakuletea historia ya tatizo hili kama ifuatavyo:-

2:1 Mwaka 1984 Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti iliiomba Serikali kuwa na eneo la kuwindia na eneo hilo ndilo lipakane na hifadhi.

*Inaendelea >*

2:2 Wakati kibali kikingojewa kutoka kwa Rais kuidhinisha Serengeti kuwa na "game reserve", watu walianza kuingia ndani ya eneo hilo baada ya vita vya kikabila vilivyotokea Ngarawani na Machochwe na kwa hiyo ukoo wa kabila la Warenchoka kukimbilia humo. Watu walioingia humo walianza kuwaita ndugu zao kutoka Kenya baada ya kuona kwamba kuna eneo la bure tofauti na Kenya. Watu mbalimbali walianza kuingia ndani ya "game reserve" na kuvamia eneo la Kijiji cha Rwamchanga kwa nvuvu na kujenga bila idhini ya Kijiji, na vurugu kati ya kijiji hicho na hao wavamizi zilianza.

2:3 Halmashauri ya Wilaya bila kukumbuka kuwa ilishaomba eneo hilo liwe "game reserve", ikaandikisha vijiji vya Nyamuma na Gurumeti ndani ya "game reserve".

2:4 Serikali kwa Gazeti la Serikali Na. 214 la tarehe 10/6/1994 ilitangaza eneo la kilomita za mraba 1867 kuwa eneo la pori la akiba na hivyo ni lazima watu waondoke.

2:5 Wanakijiji wa Rwamchanga baada ya kulalamika kwa viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali kwamba wameingiliwa na kunyang'anywa eneo lao kwa nguvu mwaka 1994, wavamizi hao waliondolewa baada ya mtu mmoja wa Rwamchanga kuuawa. Watu waliongezeka kwa kazi kubwa ndani ya eneo hilo miaka iliyofuata na hasa baada ya kwenda mahakamani.

2:6 Mwaka 1997 Serikali iliunda kamati ya kutathimini mazao na nyumba za watu waliokuwepo humo pamoja na walio kando ya eneo hilo ili walipwe na kuondoka. Tathimini hiyo ilionyesha kuwa watu 878 walikuwepo ndani ya vijiji hivyo na walistahili kulipwa fidia ya Tshs. 114,885,115/=. Wizara ya Maliasili na Utalii ilituma fedha hizo Mkoani na Serikali ikabainisha vijiji vya kuwapeleka watakaoondoka ndani ya pori hilo la akiba. Walidai walipwe gharama za kesi Tshs. 1,500,000/= nazo zikatumwa tena na Wizara. Lakini bado walikataa kuondoka kwa kudai kuwa fidia ya Tshs. 114,885,115/= ni ndogo.

Inaendelea >

2:7 Mwaka 1999 uchaguzi wa vitongoji na vijiji ulipofika, Vijiji vya Nyamuma na Gurumeti na Kitongoji kipya cha Nyanguge vikaamriwa visifanye uchaguzi kwani si vijiji halali. Kwa sababu hiyo, wakaamua kwa nguvu zote kuvamia Kijiji cha Rwamchaga na kujitangazia kijiji chao cha Nyanguge ili waruhusiwe kufanya uchaguzi.

2:8 Mkuu wa Wilaya ya Serengeti aliwaita Mwenyekiti wa muda na Mtendaji wa muda akazungumza nao kwa muda mrefu kwa kuwataka wafuate utaratibu kwa kuomba wahalilishwe kuishi Rwamchanga na wapokelewe kwa utaratibu na siyo kwa nguvu. Aliwaita na uongozi wa Rwamchanga na kuwashauri kuwa kama wangeombwa na utaratibu ukafuatwa wafikiriwe kuhalalishwa na kuwa wanakijiji.

2:9 Badala ya kutekeleza ushauri waliopewa na Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, waliamua kuongeza nyumba na kuchoma nyumba za wananchi wa Rwamchanga. Kwa sababu hiyo, tarehe 6/1/2000 mapigano yalizuka kati ya hao wavamizi na wananchi wa Kijiji cha Rwamchanga/Miseke na kusababisha vifo vya watu wawili.

Serikali iliingilia kati na kubomoa nyumba zote zilizojengwa bila kufuata utaratibu na watu "29" walikamatwa kwa tuhuma za mauaji na kesi zao zinaendelea Mwanza kwa kesi Na. CC.15/2000 Na. CC.16/2000

2:10 Wakati wa ubomoaji wa nyumba vilikamatwa vyeti vya Klinik toka Kenya, vitambulisho vya uraia wa Kenya, bendera za vyama vya upinzani, vibali vya kuwaruhusu kwenda Kenya kuwaona ndugu zao. Hii iliwathibitishia kuwa wengi wa watu hao sio raia wa Tanzania.

2:11 Kabla na baada ya mapigano na operesheni ya Rwamchanga, watu wengi waliondoka wenyewe hasa kutoka Gurumeti kwa kuomba vibali Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Serengeti na wakahamia vijiji vilivyoandaliwa na wilaya kwa kukubaliana na viongozi wa vijiji husika.

Inaendelea >

2:12 Wengine waliendelea kubaki humo na kuongezeka kwa kuingia ndani ya nyumba za waliohama na wakati huo huo kufungua kesi ya madai Na. 12/2000 Mahakama ya Mkoa, Mara, Musoma wakidai mali na kunyanyaswa, na kesi hiyo inasimamiwa na wakili wa Serikali.

2:13 Vikao mbalimbali vilifanyika vya kuwataka hawa ndugu waondoke kwenye eneo hilo na ili walipwe fedha zao, lakini bado hawakuheshimu na kutekeleza maelekezo hayo.

2:14 Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kwa kuzingatia kuwa wamebaini kuwa vitambulisho vilivyookotwa humo watu hao wengi siyo raia na kwa kuzingatia hali ya usalama ilivyo mbaya Ngorongoro ambayo ni jirani na Serengeti na kwa kuzingatia kuwa huko nyuma silaha zilichukuliwa Kenya na kuja kufanya mauaji Serengeti na pia kwa kuzingatia kuwa eneo hilo ni pori tengefu (Game Reserve) na kisheria hawaruhusiwi kuishi watu humo, ilipendekezwa Serikali ni kwa usalama wa wilaya na nchi kuwa:-

- Watu hao wote waondolewe;
- Wahalifu waliohusika na mauaji wasakwe humo na kufikishwa kwenye vyomnbo vya sheria,
- Wale wasio raia waondolewe na kupelekwa makwao; na
- Wale walio raia waende kwenye vijiji vilivyoandaliwa.

Serikali iliyakubali mapendekezo hayo tangu Aprili, 2000 na kuagiza yatekelezwe. Hata hivyo ili kuona kuwa utekelezaji unafanyika vizuri bila kuingiliana na kesi iliyokuwa mahakamani, ilikubalika kuwa kesi hiyo iishe mahakamani ndipo amri ya utekelezaji ifanyike.

Wananchi wa Vijiji vya Nyamuma na Gurumeti waliofungua kesi walikwenda Mwanza kuomba kesi hiyo ifutwe ili waweze

*Inaendelea >*

kulipwa fedha zao na kumaliza mgogoro huu. Baada ya barua hiyo kupatikana, mkataba wa makubaliano ulisainiwa mahakamani na wananchi hao kulipwa fedha zao na gharama ya kesi, na kuonyeshwa maeneo yaliyotajwa kwenye mkataba. Na baada ya kulipwa wawe wameondoka ndani ya siku "30" na waende kwenye vijiji hivyo au vijiji vyao vya asili. (imeambatanishwa) – **Kielelezo "A"**

Amri iliyotolewa na Jaji ilisema kuwa, "wale ambao hawataondoka waondolewe kwa nguvu baada ya kulipwa na baada ya siku "30".

Nakuambatanishia (1) Barua ya Wakili wa Serikali Mkuu Kumb. Na. Civil Case No. 24/97/24 iliyoambatanishwa na Amri ya Judge, (2) Mapatano ya Vijiji vya Nyamuma na Gurumeti na Wakili wa Serikali. (3) Barua ya kuomba kufuta kesi toka Nyamuma na Gurumeti – **Kielelezo "B"**

Tarehe 7/7/2000 Mkuu wa Wilaya ya Serengeti aliitisha vikao vya ndani ya Vijiji vya Nyamuma na Gurumeti kuwaeleza maamuzi hayo na kwamba fedha zao zitalipwa kuanzia tarehe 10/7/2000 na wakishalipwa waondoe nyumba zao na waondoke kwenye vijiji walivyopangiwa au waende kwenye vijiji vyao vya asili walipotoka au waende kwao Kenya kwa wale ambao siyo raia wa Tanzania.

2:15 Malipo yalifanyika bila kujali kuwa wengine ni wa – Kenya kwa matumaini kuwa wangeondoka kwa usalama.

2:16 Baada ya malipo, wengi walitoka kwenye eneo la Ikorongo "game reserve" na kujenga vibanda vya nyasi pembeni mwa "game reserve" kinyume na maagizo ya mahakama ya kwenda kwenye vijiji vilivyotajwa. Hii ilionyesha kuwa nia yao ni kukaa pale kwa muda na baadaye kurudi kwenye nyumba zao za zamani zilizokuwepo ndani ya eneo. Siku "30" zilipita na wakaongezewa siku zingine "10" na kutakiwa kutii amri ya mahakama vinginevyo wataondolewa kwa nguvu. Pia walielezwa kuwa pembeni mwa "game reserve" hawaruhusiwi kubaki kwa sababu hakuna kijiji wala eneo la kulima na wala haikutajwa katika hukumu ya Jaji.

*Inaendelea >*

2:17 Kuanzia tarehe 21/8/2000 Opereshení Hamisha Serengeti ilianza kutekelezwa kwa:-

- Kuteketeza nyumba zote zilizoachwa ndani ya "game reserve";
- Kuondosha vibanda vyote vilivyojengwa pembeni mwa "game reserve";
- Kuwakamata wote waliokaidi amri hiyo na kuwachambua rais na wasio raia;
- Tarehe 23 – 24/8/2000 lilifanyika zoezi la kuwakusanya watu wote waliokuwa kwenye vibanda na jirani zao nje ya eneo, na kazi ya uchambuzi ilifanywa na Maafisa Uhamiaji na Upelelezi.
- Kati ya kaya 419 zilizokamatwa ilibainika kuwa kaya 182 ni raia wa Kenya na 237 ni raia wa Tanzania na waliachiliwa kwa kuagizwa kuondoka kwenye eneo lote pembeni mwa "game reserve" na kwenda kwenye vijiji vilivyotajwa.

2:18 Wale ambao siyo Watanzania walipelekwa mpakani na Kenya. Pamoja na barua hii, ninakufungashia nakala ya barua Kumb. Na. MM/P.1/VOL.1/140 ya tarehe 16/4/2001 kutoka kwa Afisa Uhamiaji wa Wilaya ya Serengeti inayohusu taarifa ya watu waliofukuzwa nchini tarehe 26 – 27/8/2000. **(Kielelezo Na. "C")**. Walivuka mpaka wenyewe kwenda kwao na wengine walirudi na wakakamatwa watu "33" ambao walifungwa jela miezi sita (6) na msako mkali unaendelea kuwatafuta waliorudi hadi wakamatwe na kushitakiwa kwa kuishi nchini kinyume na sheria.

Inawezekana baadhi ya wanaolalamika ndio hao wanaosakwa kwa kuishi nchini kinyume na sheria au ni watu wachache wasiopenda kuchanganyika na kabila zingine au koo zingine za Wakurya ingawa ni raia.

*Inaendelea >*

2:19 Baada ya Opereshení Hamisha Serengeti kulikuwepo na kaya "37" ambazo zilikuwa nje ya hifadhi. Wao pia walikuwa wamehesabiwa kulipwa fidia kama vile walikuwepo ndani ya Kijiji cha Nyamuma wakati huo; na kutakiwa kwenda kwenye vijiji vyao vya asili au waende kwenye vijiji walivyopangiwa kama mkataba unavyotoka. Lakini nao hawakuhama pamoja na kulipwa na kuagizwa kuondoka.

2:20 Hata hivyo, eneo hilo la kaya "37" lilikabidhiwa kijiji cha jirani cha Bonchugu ili iwe sehemu ya kijiji chao kwa sababu hakuna kijiji cha Nyamuma na hata hivyo kaya "37" hazitoshi kuwa kijiji. Hizo kaya zilikataa kuongozwa na kijiji cha Bonchugu kwa sababu sii ukoo wao.

2:21 Mwezi juni, 2001 katika Wilaya ya Tarime mapigano ya koo ya Warenchoka na Wanchali yalizuka. Watu waliuwawa huko na wauaji wakatoroka kutoka Tarime na kukimbilia Serengeti kwenye zile kaya "37"za Warenchoka wenzao.

2:22 Ndani ya mwezi mmoja wa Julai, 2001 kaya ziliongezeka kutoka kaya "37" hadi "90" kwa kujenga vibanda vya nyasi. Kwa hiyo walitorokea hapo baada ya kuua Tarime. Wakati huo huo wakaanza kuvamia vijiji vya jirani vya Rwamchanga kulima kwa nguvu, uwindaji haramu ukaongezeka sana katika eneo hilo. Wanawake kutoka vijiji vya jirani vya Bonchugu, Kebosongo wakaanza kubakwa. Kilio kikawa kikubwa toka kwa wananchi.

2:23 Taarifa ilipelekwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Kwa wakati huo mapigano ya Tarime yalikuwa yanataka kusambaa hadi Serengeti kwa kuwa watuhumiwa wa mauaji Tarime walikuwa wanajificha Serengeti, katika eneo hilo na kuanza kuchokoza.

2:24 Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa iliagiza kieneo cha Nyamuma kilichokuwa kimebaki kiondolewe

Inaendelea >

na watuhumiwa wote wakamatwe na vibanda vyote viondolewe i.e. kisiendelee kuficha wahalifu na eneo hilo likabidhiwe kijiji cha jirani.

2:25 Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya iliketi tarehe 8.8/2001 na kupita kwenye eneo hilo kuwatangazia watu wote waondoke na mali zao waende kwenye vijiji vyao vya asili au kule walikopangiwa. Watu wote waliondoka kwa muda waliopewa na tarehe 12/10/2001 ukaguzi ulifanywa na askari na wanamgambo na kabla ya ukaguzi, watuhumiwa "10" wa mauaji walikamatwa na kupelekwa Tarime kujibu tuhuma ya mauaji. Siku ya ukaguzi alikutwa mama mmoja hajamalizia kuhama na alisaidiwa kuondoa vitu vyake vilivyokuwa vimebaki na kuhamia kijiji chake cha asili baada ya kupewa kibali cha kusafirisha mifugo yake.

2:26 Uongozi wa Wilaya ulisimamia kuona kuwa haki inatendeka katika zoezi hilo ingawa hawakustahili tena kupewa muda na mali kwani waliisha fidiwa na Serikali na kuonyeshwa vijiji vya kuhamia.

2:27 Vibanda vilivyokuwa vimejengwa viliondolewa ili wahalifu wasibaki au wengine wasirudi hapo tena kama walivyofanya.

2:28 Kijiji cha Bonchugu ndicho kilichokabidhiwa eneo hilo.

2:29 Ni vema ikafahamika kwamba hakuna Kijiji cha Nyamuma. Taz. Kielelezo toka Mahakama Kuu na tangazo la Gazeti la Serikali Na. 214 la tarehe 10/6/1994. Kwa maana hiyo hakuna malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kijiji cha Nyamuma kwa sababu Nyamuma haipo.

*Inaendelea >*

## 3:0 KUKAMATWA WATAFITI KUTOKA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU TAREHE 1 – 5/1/2002 NA KUNYANG'ANYWA MIKANDA YA PICHA (VIDEO NA KAWAIDA)

3:1 Eneo lote lililokuwa la Kijiji cha Nyamuma na Gurumeti baada ya operesheni ya kuwandoa kukamilika kwa awamu zote, liliwekewa ulinzi na Idara ya Wanyamapori na vijiji vinavyopakana na eneo hilo. Hakuna mtu yeyote aliyeruhusiwa kwenda kwenye eneo hilo bila kibali. Hii ilifanyika ili kudhibiti uwindaji haramu, pia kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayerudi huko, na kwa kisehemu kilichobaki uamuzi ulitakiwa upatikane kuwa eneo hilo likabidhiwe hifadhi au kijiji. Hatua hiyo ilitokana na mapendekezo mawili yaliyotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na yaliyotolewa na Kijiji cha Bonchugu.

3:2 Kwa Wilaya za mipakani na hasa Wilaya ya Serengeti ambayo ina sifa kubwa ya ujambazi, wizi wa mifugo na matumizi ya silaha na kwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti inapata wageni wa kila aina na watalii na kwa sababu raia wa nchi ya jirani wanapenda sana kuingia ndani ya Wilaya ya Serengeti na kujishikia ardhi bila utaratibu kutokana na ukosefu wa ardhi nchini mwao, tahadhari ya kila aina imewekwa kila mahali ili kuhakikisha kuwa usalama wa raia, na mali zao usalama wa Taifa na usalama wa watalii na wanyama wetu unakuwepo masaa yote. Kwa sababu hiyo, mtu mgeni akienda kijijini bila kujitambulisha na kutambulishwa na Wilaya atakamatwa na kuhojiwa. Kwa maeneo ambayo ni ya hifadhi au yale yaliyofanyiwa operesheni, haikuruhusiwa mtu kuingia huko bila kibali. Mbali na utaratibu uliotajwa hapo juu, Watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walikamatwa huko kwa sababu hawakufahamika na wala hawakujitambulisha wilayani, tarafani, kata na kijijini. Hawakujitambulisha kwa Idara ya Wanyamapori wala usalama wa raia. Walijiiba kana kwamba kuna kitu cha siri

Inaendelea >

walichokuwa wanakitafuta au kuna maovu waliyotaka kufanya. Walikamatwa na kukabidhiwa polisi na ndipo wakakutwa wana barua inayosema kuwa wanatafiti suala la wanyama na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Kabla ya kwenda huko hawakupenda kufika kwenye ofisi ili ifahamike kuwa wapo na ikiwezekana waonyeshwe maeneo yote wanayotaka. Walikuwa na kamera na video, pia za kawaida na vifaa vingine. Idara ya Upelelezi ilifanya upelelezi wake na baada ya kutazama mkanda wa wahame, kanda na picha walizopiga, zikazuiliwa kwa sababu haikufahamika walipiga kwa sababu gani na kwa nini walijificha bila kwenda kujitambulisha kwenye ofisi za serikali. Wakati upelelezi unafanyika walikuwa wameruhusiwa kwenda wanakolala na kurudi polisi asubuhi hadi waliporuhusiwa. Baada ya upelelezi waliruhusiwa baada ya kuonywa kufuata utaratibu wanapokwenda wilayani na kuripoti kwa viongozi wa Wilaya. Kama wangefuata utaratibu huo watafiti hao wasingepata usumbufu wowote.

Uchunguzi uliofanywa na Tume umezingatia hoja zote kwa makini, na madai ya kwamba vitendo vya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti vimesababisha ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu kwa wananchi wa Kijiji cha Nyamuma. Aidha, imefahamika sasa kwamba hakuna malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kijiji cha Nyamuma kwa sababu Nyamuma haipo.

Vivyo hivyo, matatizo yaliyowapata Watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu yametolewa ufafanuzi kwa kirefu na imeshauriwa kwamba watakapokwenda tena wilayani wafuate utaratibu wa kuripoti kwa viongozi wa wilaya husika.

Kwa maelezo haya tunaamini kuwa imeeleweka.

(G. Bizuru)
kny: MWENYEKITI
**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA.**

Kituo kilipoitafakari barua hiyo kiliamua kurudi kwenye sheria kuona inasemaje pale mtu anapolalamika mbele ya Tume. Ilionekana kwa mujibu wa Sheria inayoiunda Tume baada ya malalamiko Tume inapaswa kuwasiliana na mlalamikiwa kumjulisha analalamikiwa na kumuonyesha anacholalamikiwa. Anayelalamikiwa itabidi ajibu hoja. Baada ya majibu hayo inabidi pawepo na kikao ambapo ushahidi utatolewa wa madai na mlalamikiwa ataleta mashahidi na utetezi wake hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 24 cha Sheria namba 7 ya mwaka 2001 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Hapo ilibidi tarehe 29 Mei 2003, Kituo kiandike barua kwa mwenyekiti wa Tume Jaji Robert Kisanga kumuelezea kutoridhishwa na jinsi Tume ilivyolishughulikia suala lile na majibu yake ambayo hayakuzingatia sheria. Barua hiyo ambayo itaambatanishwa mwishoni mwa kitabu iliangalia mambo makuu mawili, kwanza msingi au kiini cha madai kilivyoshughulikiwa na pili mwenendo au utaratibu uliotumika kushughulikia kiini kile. Kwenye suala la msingi au kiini cha madai, Tume ilijihusisha zaidi na kutokuwepo kwa Kijiji cha Nyamuma badala ya kuangalia hoja za watu waliopeleka malalamiko. Tume haikuzingatia kuwa Nyamuma haikuwepo kweli lakini ikajiangaliza katika vitongoji vitatu vilivyosababisha Nyamuma kutokuwepo ikaacha kuangalia kitongoji kilichokuwa kimebaki ambacho ndipo walalamikaji walipopata madhila wanayolalamikia.

Kwa upande wa utaratibu, Kituo kiliikumbusha Tume kuwa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika kifungu chake cha 7 kimeelezea uwepo wa makamishna wa Tume na kifungu cha 21(2) kinazungumzia akidi katika maamuzi ya Tume. Ile barua inaonekana iliandikwa na mtu mmoja kwa niaba ya Mwenyekiti na si wajumbe waliokuwa kwenye maamuzi wakiwa na akidi, kwani ilibidi kila kamishna awe ametia saini yake katika hayo maamuzi.

Aidha barua hiyo haionyeshi popote kuwa iliwahoji walalamikaji. Inaonekana iliwasiliana na mlalamikiwa peke yake, jambo lililokuwa

kinyume na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kifungu cha 27(1) na (2). Ilielezwa pia katika majibu hayo Tume haikuwa imezingatia kanuni na misingi ya haki asili kwa kutoitilia maanani kwani hiyo kanuni inataka watu kupewa haki ya kusikilizwa na hii ni kinyume na kifungu cha 20(1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume ilipaswa kuwasikiliza walalamikaji na kupokea ushahidi wao kabla ya kufanya maamuzi.

---

**I)** Kituo kiliiomba Tume kuangalia upya uamuzi wake na kuwapatia walalamikaji:

- **a)** Haki ya kusikilizwa na kutoa ushahidi kwa mujibu wa kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;
- **b)** Iwahoji walalamikaji na wahanga wa shauri hilo ili kukamilisha uchunguzi wake.

---

**II)** Kituo kiliiomba Tume irejee madai ya walalamikaji na kuyapatia suluhisho;

---

**III)** Tume irejee maamuzi yake kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

---

Mara baada ya Mwenyekiti wa Tume Jaji Robert Kisanga kuipokea ile barua alipiga simu kwa Mkurugenzi wa Kituo akaomba radhi kuwa barua ile ililetwa kwa makosa na hivyo isitiliwe maanani. Baada ya hapo tarehe 6 Juni 2003 Kituo kilipokea barua rasmi kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume kuwa shauri lile litaendelea kwa kusikilizwa kwa pande zote hivyo ile barua ya awali imetenguliwa .Barua ilieleza kuwa barua iliyokifikia Kituo ilikuwa ni kwa bahati mbaya kwani shauri lile ni lazima lisikilizwe kwa vile kuna mgogoro kati ya maelezo ya pande hizo zinazohusika na hivyo Tume ikikamilisha uchunguzi wake shauri litasikilizwa.

Hii ilikuwa ni habari njema sana, hivyo Kituo kilianza kujiandaa kwa ajili ya kusikilizwa kwa shauri lile. Ilibidi wateuliwe mawakili ambao

wangeweza kulisimamia shauri lile na waweze kupata muda kuwaandaa mashahidi ambao wengi walikuwa Serengeti na baadhi Tarime pamoja na maafisa wa Kituo ambao walizuiwa Serengeti na kunyang'anywa vifaa vya kazi.

Walipatikana mawakili wawili ambao ni Alex Mgongolwa na Francis Stola. Hawa mawakili ni wabobevu katika masuala ya sheria ya haki za binadamu kwani wote wawili waliwahi kufanya kazi na Kituo kwa ngazi tofauti. Wakili Mgongolwa aliwahi kuwa mwanasheria wa kujitolea wa Kituo na pia alikuwa mjumbe wa Bodi ya Kituo ambaye alishafanya mashauri mengi ya haki za binadamu. Wakili Francis Stola naye alianza kazi za haki za binadamu akiwa mwaka wa pili chuo kikuu na aliwahi kuwa mkufunzi wa haki za binadamu na baadaye mtendaji wa Kituo katika ngazi mbalimbali na hatimaye alikuwa mjumbe wa bodi ya Kituo. Mawakili hawa walishirikiana na watendaji wa Kituo katika maandalizi ya kesi na hatimaye katika usikilizwaji wa kesi hiyo.

### 4.3 Kusikilizwa kwa wazi mbele ya Tume

Tume ilitoa waraka wakuwaita walalamikaji shaurini tarehe 26, Agosti 2003. Shauri lilipangwa kusikilizwa Musoma mjini ambapo ni karibu kilomita 110 kutoka Mugumu, ambapo ni makao makuu ya wilaya ya Serengeti. Kwa umbali huo walalamikaji ambao ndio walikuwa mashahidi wasingeweza kwenda Musoma na kurudi Mugumu baada ya kutoa ushahidi wao hivyo suala la gharama za kulala angalau siku moja na kuishi Musoma ilibidi lizingatiwe. Hasa kwa vile walalamikaji hao walikuwa hawana kwao mali zao ziliteketea na hawakuwa na kipato kinachoeleweka. Tume haikuwa na fungu la kuwaleta mashahidi au kuwafuata mashahidi walipokuwepo, hivyo Kituo kikatafuta njia za kupata fedha ili mashahidi hao waweze kufika shaurini. Haki ni gharama na inakuwa ngumu sana pale mtu anapokosewa haki na hana uwezo wa kuifuatilia haki yake. Wapo watu wengi ambao haki zao zimekosekana kwa kukosa tu uwezo wakuweza kufuatilia.

Ilibidi gari la Kituo litumike kwenda Mugumu na kuwachukua walalamikaji wapatao 14 kila siku na wakapelekwa Musoma Mjini. Kwa mujibu wa Dereva wa Kituo Ally Said Mwashongo ilikuwa akifika huko Mugumu kuwachukua wanapeana taarifa na wakitimia idadi inayohusika anawachukua hadi Musoma ambapo huongea na mawakili wao na kisha hulala na asubuhi kuamkia kwenye shauri lililokuwa linafanyikia katika ukumbi katika eneo la ofisi za mkuu wa mkoa wa Mara.

Ilikuwa walalamikaji hao wakimaliza kutoa ushahidi huchukuliwa tena na kurejeshwa Mugumu kisha wengine huchukuliwa. Hili zoezi liliendelea na inaelezwa kuwa wananchi wa Mugumu walilikariri gari lililokuwa linawachukua wale wahanga na walikuwa wana wanyanyapaa kutokana na hali ya maisha yao hadi kulipa jina lile gari.

Shauri hili lilikuwa linasikilizwa kwa muda wa wiki mbili na kisha kuahirishwa na baada ya muda huo huanza tena. Shauri liliposikilizwa mara ya kwanza wananchi wa Nyamuma walifurahi sana hata kabla hawajajua watapata haki yao au la. Kilichowafurahisha ni kuwa hata mkuu wa wilaya ya Serengeti ameweza kusimamishwa kizimbani. Walidhani alikuwa juu ya sheria kwamba asingeweza kuitwa na Tume na akaenda, kwa vile alisikika akiongea kwa dharau kuwa 'hako katume hakawezi kunipa shida mimi mteule wa Rais'. Mwisho wa siku walikuwa naye mbele ya Tume.

Tume ilikaa vikao sita kabla ya kukamilisha kusikiliza walalamikaji na utetezi wa wawalamikiwa. Kila kikao kilikuwa ni wiki mbili au tatu. Katika vipindi hivyo sita kulikuwa na changamoto mbalimbali. Zilikuwepo changamoto mbalimbali nyingine za kisheria, nyingine za kiuchumi hata za kijamii. Katika changamoto ya kiuchumi kuna wakati kikao kilichopangwa kiliahirishwa kwa vile Tume haikuwa imepokea fedha kutoka serikalini na isingeweza kuendelea na kikao kilichokuwa kimepangwa. Hii ilitokea mara kadhaa na hasa kwa vile Tume ilikuwa ikipokea fedha kutoka serikali kama idara ya serikali wakati huohuo

ilikuwa na kesi dhidi ya serikali. Wakati wa uhamasishaji wa uwepo wa Tume ilipendekezwa kuwa ili Tume iwe huru ni vyema ipokee fedha zake moja kwa moja kutoka bungeni, fedha zisipitishwe kwenye wizara za serikali ili kuihakikishia Tume uhuru wake wa kiuchumi. Bahati mbaya hili halikutekelezwa na ilionekana wazi kuwa mara kadhaa Tume ilikwama kwa kutopokea fedha kwa wakati ilipokuwa inazihitaji kwa ajili ya kuendelea na shauri.

Ilifikia wakati Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu nacho kiliishiwa fedha za kuwawezesha wahanga kufika katika shauri. Hii ilitokana na kuwa Kituo cha Sheria nacho hutegemea fedha kutoka kwa wahisani. Ilitokea kuwa wahisani waliokuwa wanakipatia fedha katika eneo hilo walisitisha kutoa fedha kwa vile na wao chanzo chao cha fedha kilikuwa kimesitisha kuwapatia fedha. Hii ilikuwa changamoto kubwa kwani wahanga wangeshindwa kuendelea kufika kwenye shauri hivyo ushahidi usingetimia. Bahati nzuri sana LHRC walitoa taarifa kwa wadau mbalimbali ambao wapo walioamua kutoa msaada papo kwa papo wakiwemo ubalozi wa Uswidi ambao ni wahisani wa LHRC ambao tayari walikwisha kutoa fedha za miradi na kuendesha shirika lakini walipopata taarifa walikubali kuongezea kiasi cha fedha shilingi za kitanzania 28,220,000 ambazo ndizo zilizokuwa zinahitajika kwa wakati huo.

Vilevile wadau ambao ni mashirika wenza nao walisaidia kama shirika la Haki Elimu walitoa fedha kama asilimia 10 ya fedha zilizokuwa zinahitajika awamu ya pili kesi ilipokuwa ikiendelea ambazo ilikuwa shilingi za kitanzania milioni nne. Wapo waliowapa moyo na kufanya ufuatiliaji ambao ni pamoja na National Policy Forum na TENMET. Wadau wengine walipokea ombi kutoka LHRC na hawakujibu lakini shirika la USAID walipokea na walijibu kuwa ombi lingekubalika ila wao kesi hiyo si moja ya vipaumbele vyao hivyo wasingeweza kusaidia. Hata hivyo kwa kiasi kilichopatikana shauri liliweza kuendelea na LHRC kuwasaidia wahanga kuendelea na kesi.

Kuna wakati ambapo walalamikiwa waliitaka Tume kuhakikisha walalamikaji wanachokisema ni kweli kwa kwenda kuonyesha nyumba wanazosema wamechomewa. Hii ilikuwa changamoto kwani ilihitaji muda na fedha za kutoka huko Musoma kwenda Nyamuma Iliyobaki. Bahati nzuri serikali ilitoa fedha za mafuta ya gari ikawezekana kwenda kwenye eneo la tukio kuanzia tarehe 4 September 2003. Changamoto iliyojitokeza katika zoezi hili walalamikiwa walijaribu kuipotosha Tume kwa kutaka kuwaelekeza sehemu ambayo siyo kama ambavyo walishafanya kwa tume za uchunguzi zilizofika kufuatilia suala hilo. Ilikuwa ni bahati nzuri sana kwani walalamikaji waliweza kuieleza Tume kuwa wanajaribu kuwapeleka sehemu ambayo sipo na hivyo wakaweza kuilekeza Tume sehemu halisi na kuionyesha Tume magofu ya nyumba zao yaliyokuwa yamebaki na hata mashamba yao mengine yakiwa bado na miti ya mazao ya kudumu kama miembe, makaburi ya ndugu waliozikwa katika maeneo yao. Mfano walipofika katika eno la ndugu Eliud alipoliona kaburi la mama yake aliangua kilio akikumbuka msiba huo na kuwa ameondolewa sehemu alikomlaza mama yake n.k.

Kuna wakati walalamikiwa walikuwa wanafanya vitendo vya kuwafanya walalamikaji washindwe kufika katika shauri. Kwa mfano kulikuwa na baadhi ya walalamikaji ambao kwa makusudi walikamatwa huko Mugumu wakati shauri linaendelea na wakafunguliwa kesi za jinai ili washindwe kwenda kwenye kesi. Waliokuwa wamekamatwa tarehe 19/8/2003 ni pamoja na Jackson Mwita, Emmanuel Mwita na Imwani Pius. Ilibidi taarifa zifikishwe kwa mwenyekiti wa Tume kuhusu wahanga hao wanavyosumbuliwa hadi kufikishwa polisi bila sababu za msingi. Tume ilitoa amri kwa mkuu wa wilaya kuacha kuwabughudhi wahanga hao ambao ni mashahidi katika shauri lililokuwa linaendelea.

Changamoto nyingine kubwa ilikuwa ni jinsi shauri lilivyokuwa likiendeshwa. Kwa mujibu wa dhana ya uwepo wa Tume hii ni ili kuwasaidia na kuwawezesha watu wa kawaida kabisa kupata haki zao kwa wepesi na kwa haraka tofauti na inavyokuwa mahakamani. Dhana hii

ilikuwa haionekani sana katika uendeshwaji wa shauri hili la kwanza kwa vile kanuni za kuendesha shauri ziliandaliwa kama za kimahakama. Hii ilisumbua sana pamoja na kuwa walikuwepo mawakili. Ilifikia mahali mawakili wa walalamikaji kuieleza Tume umuhimu wa kuzingatia hiyo dhana. Kwa mfano kuna wakati walalamikaji kupitia mawakili waliiomba Tume itoe maamuzi ya awali hasa kutokana na vitendo vya vitisho walivyokuwa wanafanyiwa na mkuu wa wilaya ambaye alikuwa mlalamikiwa. Tume iliwaelekeza wakaandae nyaraka za kisheria kwa kiapo ili waweze kupatiwa nafuu hizo za awali. Mawakili waliitahadharisha Tume kuwa si kila wakati walalamikaji watakuwa na mawakili, ilibidi pale wanapoonyesha uhitaji kama huo Tume iwasikilize na kutoa maamuzi hayo. Bahati mbaya hilo halikuwezekana na hivyo pakawepo na mambo mengi ya kisheria kama mapingamizi madogomadogo katika hoja ambayo yalileta ucheleweshaji katika usikilizwaji wa shauri hilo.

Hapa ilifikia hata mawakili wa upande wa walalamikaji kuweka mapingamizi kwa kuona kuwa mawakili wa serikali walikuwa wanafanya hivyo. Mfano walipokwenda kutembelea eneo la mgogoro ipo siku moja ambapo mmoja wa makamishna hakuwepo kutokana na udhaifu wa afya hivyo akidi haikutimia ikabidi waweke pingamizi kuwa lolote litakalofanyika itakuwa ni kinyume cha taratibu za kisheria jambo lililofanya kazi hiyo kurudiwa alipopatikana mjumbe aliyekuwa hayupo. Hali kama hizi ziliendelea kuleta ucheleweshaji wa shauri.

### 4.4 Kuendelezwa kwa Mbinu za Ushawishi

Wakati shauri linaendelea LHRC ilibidi iendelee na mikakati ya kiushawishi ambayo haiathiri kesi iliyokuwa mbele ya Tume. Baadhi ya mikakati iliyokuwa ikiendelea ilihusu jinsi watu waliopo pembezoni mwa hifadhi za wanyama pori wanavyotendewa, hivyo kulikuwa na mtandao uliokuwa ukiongozwa na shirika la Lawyers' Environmental Action Team (LEAT) ulioitwa Tanzania Access Initiative [TAI] ambao Kituo kilikuwa ni

sehemu yake. Mtandao huu ulikuwa unaangaliza kanuni ya makubaliano ya Rio De Jeneiro kuhusu upatikanaji wa taarifa za kimazingira. Katika kanuni ya 10 ya makubaliano hayo Ushiriki wa watu katika maamuzi yanayohusu mazingira ulisisitizwa na pia suala la upatikanaji wa haki kama njia ya kukuza maendeleo endelevu. Katika kushiriki kwenye mitandao kama hii ilisaidia kuweka wazi masuala ya mauaji ya watu huko hifadhi ya Serengeti lakini na shauri la Nyamuma Iliyobaki kwani nalo lilihusu watu na mazingira.

Ulikuwepo pia mtandao wa wananchi uliojulikana kama TUSHIRIKISHWE, huu ulihusu kutafuta kutoka kwa wananchi wenyewe njia za kidemokrasia za kutawala mali asili nchini Tanzania. Hivyo Kituo kilishiriki katika mtandao huu.

LHRC pia ilikuwa sehemu ya kikosi kazi kilichohusu masuala ya wanyama pori. Kikosi kazi hiki nacho kiliweza kutoa taarifa ya masuala yanayoendelea katika eneo la wanyama pori kiasi kwamba LHRC wakiwa sehemu ya kikosi hiki waliandika kitabu kilichoangaliza uhifadhi na haki za watu kitabu kinajulikana kama **'Protection of Wildlife and Human Rights on a balance sheet; Case Study of Serengeti Killings'.** Kupitia kitabu hiki suala la mambo yanayoendelea kwenye hifadhi na mipakani mwake zilifika mbali kiasi cha kuvutia vyuo vikuu vya nje kutaka kujifunza zaidi na hata kuandika makala kuhusu suala la Nyamuma Iliyobaki.

Vyombo vya habari vilifanya kazi kubwa sana ya kutoa habari ya jinsi shauri linavyoendelea kuanzia siku shauri lilipofikishwa katika ofisi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora jijini Dar-es-salaam kwenye jengo la Haki barabara ya Lithuli pamoja na kila kilichokuwa kinajiri wakati shauri likiwa linaendelea huko Musoma na hata walipotembelea huko Nyamuma Iliyobaki.Vyombo vilivyohusika vilikuwa karibu vyote vya hapa nchini na hata nje ya nchi. Vyombo vilikuwa ni pamoja na magazeti, redio na runinga kama The Guardian, Mtanzania, Mwananchi, Nipashe,

Majira n.k. Pia walitoa vichwa vya habari vilivyowapa watu hamu ya kusoma hiyo habari. Mifano michache ni kama:

| KICHWA CHA HABARI | GAZETI | TAREHE |
|---|---|---|
| Mkuu wa Wilaya Matatani Serengeti kwa Kuchoma Nyumba za Wanakijiji | MTANZANIA | 7/9/2003 |
| Kesi ya Uchomaji Nyumba na Maghala: Mwenyekiti atoa ushahidi na kusema aliwekwa ndani siku nne | NIPASHE | 2/9/2003 |
| Tuhuma dhidi ya DC: Mwanamke Adai Kutolewa Mimba. | NIPASHE | 3/9/2003 |
| Tume ya Haki za Binadamu Yahamishia Makazi yake Nyamuma. | NIPASHE | 4/9/2003 |
| Tume ya Jaji Kisanga Yanyimwa Ushirikiano. | MTANZANIA | 6/9/2003 |
| DC na Mkuu wa Polisi 'Kizimbani': Wadaiwa Kuchoma Moto Nyumba 534 na Kusababisha Kaya 135 Kukosa Makazi. | NIPASHE | 27/9/2003 |
| Mashahidi Waomba Ulinzi; Wanadai Wanapewa Vitisho. | NIPASHE | 8/9/2003 |

Shauri hili lilichukua muda wa miaka miwili na zaidi katika Tume ya Haki za Binadamu kuanzia Juni 2002 hadi tarehe 13 Disemba 2004. Hatua muhimu kufikia hitimisho ilikuwa kukamilika kwa kusikilizwa kwa shauri huko Musoma ambapo mwezi Agosti 2004 ndipo Tume ilipoanza kikao cha mwisho kati ya vikao vyake sita ilivyokaa katika kusikiliza shauri hili. Baada ya kikao cha mwisho ndipo LHRC ilipowasilisha majumuisho ya mwisho kwa Tume tarehe 24 Septemba 2004 na kusikilizwa kwa mara ya mwisho 14 Oktoba 2004 katika ofisi za Tume jijini Dar-es-salaam.

### 4.5 Kusomwa kwa Mapendekezo ya Tume

Tume ilitoa wito kwa Walalamikaji ikiarifu kuwa uamuzi wake utasomwa tarehe 13/12/2004 katika ofisi za Tume Dar es Salaam. Hii ilikuwa ni

habari ya kufurahisha kwa vile wahanga walikuwa wamesubiri sana na walitamani shauri hili lifikie mwisho ili wajue hatma ya haki zao. Ikumbukwe kuwa watu hawa tangu tarehe 12, Oktoba 2001 walikuwa hawana makazi maalum, walikuwa wanaishi kwa wasiwasi na shida kama walivyoweza kuandika barua mara kwa mara kuelezea adha zinazowapata. Walipotaarifiwa kuwa shauri linafikia mwisho walipata faraja kubwa sana. LHRC waliwawezesha baadhi ya walalamikaji hao kufika katika ofisi za Tume Dar-es-salaam ili waweze kusikiliza wenyewe Tume itakavyoamua. Hiyo siku ya tarehe 13/12/2004 ukumbi wa Tume ulifurika watu wakiwemo watendaji wa LHRC, wahanga/walalamikaji kutoka Nyamuma Iliyobaki, wadau wa haki za binadamu na waandishi wa habari. Kwa muda wa zaidi ya masaa mawili mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Jaji Mstaafu Robert Kisanga (Marehemu) aliyekuwa akisaidiana na Kamishna Catherine Mbelwa Kivanda na Afisa uchunguzi Bwana Sabbas Tetti alisoma uamuzi wa Tume na Mapendekezo ya Tume kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uamuzi huo ulikuwa na sehemu mbili, ya kwanza ni uamuzi wa jumla na sehemu ya pili ni uamuzi binafsi wa Kamishna Catherine Kivanda kuhusu hoja ya watafiti wa LHRC kutokutoa taarifa walipofika wilayani Serengeti. Ufuatayo ni Uamuzi wa Tume.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

**SHAURI NA. HBUB/S/1032/2001/2002/MARA**

1. IBRAHIM KOROSSO NA WENZAKE 134.
2. KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

**DHIDI YA**

1. THOMAS LOY OLE SABAYA – MKUU WA WILAYA YA SERENGETI.
2. ALEXANDER PANTALEO LYIMO – MKUU WA POLISI WILAYA YA SERENGETI.
3. MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
S. L. P. 2643
Dar es Salaam

Simu: 2135747/8
Fax: 2111281/2111533
Barua pepe: chragg@chragg.org



Inaendelea >

## YALIYOMO

**UKURASA**

Utangulizi:

1) Mitiririko wa mambo muhimu - ........................ 2

2) Kama uondoshaji katika Kitongoji cha CCM "Centre" ulikuwa ni halali, yaani kisheria. - ........................ 14

3) Njia iliyotumika kuwaondosha walalamikaji kutokana katika eneo la mgogoro mwaka 2001 haukufuata taratibu zilizowekwa kisheria za kushughulikia migogoro ya ardhi. - ........................ 17

4) UHALIFU: - ........................ 19

Maficho ya mauaji. - ........................ 19

5) Maficho ya wauaji - ....................... 20

6) Ubakaji na Uwindaji Haramu. - ....................... 21

7) Uraia wa walalamikaji. - ...................... 21

8) Kama kulikuwa na ukiukwaji wa haki za Binadamu katika namna uondoshaji ulivyofanyika ................ 22

9) Taarifa ya kuondoka - ...................... 22

10) Uwezeshaji wa wananchi kuondoka - ...................... 24

11) Watoto kupewa nafasi ya kuendelea na Masomo yao walikohamia wazazi/walezi wao ..................... 25

12) Mapokezi ya wazazi wa Nyamuma iliyobaki - ..................... 26

13) Uvunjwaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji Wa misingi na Utawala Bora. - .................... 33

14) Unyanyasaji, udhalilishaji na ukatili - .................... 34

15) Uporaji .................... 37

16) Vitisho - ................ 38

17) Haki ya kumiliki mali - ................ 42

18) Haki ya kuishi katika mazingira na maisha bora ............ 46

Inaendelea >

| | | |
|---|---|---|
| 19) | Haki ya faragha na mtu kukaa na familia yake ................ | 48 |
| 20) | Haki ya kutendewa haki na vyombo vya dola ................. | 49 |
| 21) | Haki ya kupata elimu - ................. | 51 |
| 22) | Haki ya makazi na uraia. - ................. | 53 |
| 23) | Haki ya walalamikaji kutohamishwa kwa nguvu ............. Kutoka kwenye makazi yao ya halali (forced eviction) | 55 |
| 24) | Haki ya usawa dhidi ya ubaguzi - ................. | 56 |
| 25) | Kama ilikuwa halali kuwakamata na kuwanyang'aya Vifaa na picha watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. - ................ | 58 |
| 26) | Kama walioondolewa walikuwa ni wakazi halali Kijiji cha Nyamuma iliyobaki au CC" Centre" kama Kulikuwa na uhalali wa Kijiji cha Nyamuma iliyobaki Au kilikuwa na hadhi gani. - ............... | 62 |
| 27) | Kama kweli uongozi wa serikali ngazi ya Wilaya Na mawakala wake walitumia vibaya mamlaka Waliyopewa na sheria. - .................. | 62 |
| 28) | Vitendo vya rushwa. - ................. | 63 |
| 29) | Udhaifu wa ushahidi wa walalamikiwa. - ................. | 63 |
| 30) | Kama waalamikaji/wadai wanastahili nafuu Zilizoombwa katika hati ya malipo. - .................. | 64 |
| 31) | Angalizo - ................... | 67 |

Inaendelea >

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

**SHAURI NA. HBUB/S/1032/2001/2002/MARA**

1. **IBRAHIMU KOROSSO NA WENGINE 134**
2. **KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**

**DHIDI YA**

1. **THOMAS LOY SABAYA (MKUU WA WILAYA SERENGETI)**
2. **ALEXANDER LYIMO (MKUU WA POLISI WILAYA YA SERENGETI)**
3. **MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

**UTANGULIZI**

Hili ni lalamiko lililowasilishwa kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Tume) na Ibrahimu Korosso na wenzake 134 (Walalamikaji Na. 1) na Kituo cha Sheria na Haki za Biandamu (Kituo) (Walalamikaji Na. 2)

Ibrahimu Korosso na wenzake, kwa pamoja walnalalamikia Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Bw. Loy Thomas Ole Sabaya (Mlalamikiwa Na. 1) na Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo. Bw. Alexander Pantaleo Lyimo. (Mlalamikiwa Na. 2) kwa kuwaondosha walalamikaji kutoka kwenye makazi yao kwenye eneo la mgogoro kwa namna ambayo iliwavunjia haki zao za binadamu na kukiuka misingi ya utawala bora.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kwa upande wake, kinawalalamikia Mlalamikiwa Na. 1 na Mlalamikiwa Na. 2 kwa kuwakamata watafiti kutoka Kituo hicho, kuwaweka chini ya ulinzi na kuwanyang'anya vifaa vyao vya kazi wakati wakifuatilia tukio la uondoshwaji wa Walalamikaji Na. 1 kutoka katika eneo la mgogoro.

Kufuatia ombi la Walalamikiwa Na. 1 na Na. 2 Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliunganishwa kama Mlalamikiwa Na. 3.

Inaendelea >

**MTIRIRIKO WA MAMBO MUHIMU**

Baadhi ya Walalamikaji Na. 1 walianza kuhamia katika eneo la mgogoro mnamo mwaka 1986 wakati eneo hilo likiwa chini ya Kijiji cha Rwamchanga. Mwaka 1993 Kijiji cha Nyamuma kilisajiliwa rasmi na kupewa cheti cha usajili. Eneo la mgogoro liliangukia kwenye mipaka ya kijiji hicho.

Mnamo mwaka 1994 mipaka ya hifadhi ya Wanyamapori ya Ikorongo (Hifadhi) ilipanuliwa kutokana na Azimio la Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti la mwaka 1984. Upanuzi huo ulimega sehemu kubwa ya Kijiji cha Nyamuma na kubakiza sehemu ndogo ambayo ilijulikana kama Nyamuma iliyobaki. Hili ndilo eleo la mgogoro. Eneo la Nyamuma iliyobaki baadhi ya kijiji mama kumegwa na hifadhi, yaani eneo la mgogoro, ambalo lilikuwa na kaya 37 tu, lilikabidhiwa kijiji cha bonchugu kiutawala mwaka 2000 kwa sababu lisingeweza kuunda kijiji kutokana na uchache wa kaya hizo.

Mwaka huo huo wa 2000 baadhi ya walalamikaji walihamia eneo la mgogoro wakitokea Nyanguge (Mara Cop), baada ya kuvamiwa na watu wa Rwamchanga na kubomolewa makazi yao. Katika kundi hilo walikuwemo pia walalamikaji ambao awali walikuwa wanaishi Nyamuma iliyobaki na kasha kuhamia Nyanguge (Mara Cop). Hawa, pamoja na wengien ambao awali hawakuwa wakiishi Nyamuma iliyobaki kabla ya kuhamia Nyanguge (Mara Cop), walilazimika kurudi na kuhamia Nyamuma iliyobaki.

Tarehe 08/10/2001 mchana wakazi wa eneo hilo walitangaziwa an serikali ngazi ya Wilaya, kwa njia ya kupaza sauti, kwamba wawe wameondoka katika eneo hilo ifikapo tarehe 12/10/2001 na kuwa warudi kwenye vijiji vyao vya asili, au Kenya kwa wale ambao ni Wakenye. Ilipofika tarehe 12/10/2001 uondoshaji ulifanyika kwa njia ya uchomaji wakazi chini ay uongozi wa Serikali ya Wilaya ya Serengeti.

Inaendelea >

Tarehe 01//01/2002 watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walitembelea eneo la tukio. Siku hiyo hiyo walikamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi na kunyang'anywa vifaa vyao vya kazi.

Mhershimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, alifikisha taarifa Serikalini kwa kuwasiliana na viongozi mbalimbali kuhusu tukio la uchomaji wa makazi katika eneo la mgogoro.

Tarehe 20/06/2002 lalamiko hili lilipokelewa kwenye Tume likiwasilishwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa niaba ya wanakijiji wa iliyokuwa Nyamuma iliyobaki na kwa niaba ya Kituo chenyewe binafsi. Walalamikaji wanaiomba Tume hii mambo yafuatayo:-

(i) ILishughulikie suala hili kama suala la uharaka na Tume ichunguze vitalenga katika:-
  (a) kuwatafutia makazi.
  (b) Fidia kwa watu na mali zao zilizoharibiwa na zilizopotea chini ya mikono ya mamlaka husika.
  (c) Msaada wa kibinadamu, kama chakula, madwa, matunzo na elimu kwa watoto waliokuwa mashuleni.
  (d) Amri za kuimarisha uwazi na usalama na kukomesha kabisa unyanyasaji kwa watu kutoka Nyamuma kokote waliko.
  (e) Amri ya kutolewa mara moja kwa mikanda na filamu zote za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambayo inaonesha matukio hayo yasiyo halali, ambayvyo kwa sasa viko mikononi mwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) wa Serengeti.
  (f) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ishauri na kulipeleka suala hili mahakamani kupata nafuu ya mahakama kwa waathirika dhidi ya walalamikiwa. .
  (g) Nafuu zingine zozote ambazo Tume hii tukufu inaona haki na sawa kushauri/kutoa.

Inaendelea >

Walalamikiwa wanakanusha madai, ikiwa ni pamoja na nafuu zilizoombwa, kwa misingi kwamba wao waliondosha mahame kwa kuyachoma wakati walalamikaji walikiwa wameshaondoka na mali zao.

Baada ya walalamikiwa kukanusha madai Tume ililazimika kuendelea na uchunguzi kwa njia ya kulisikiliza shauri hili hadharani (Public Hearing). Katika kusikilizaji huo walalamikaji waliwakilishwa na Bwana Francis K. Stolla (Wakili wa Bwana Alez Mgongolwa (Wakili). Aidha walalamikiwa awali waliwakilishwa na Bwana Deus Mgengeli (Wakili wa Serikali) na Bw. Jackson Bulashi (Wakili wa Serikali). Baadaye tarehe 07/10/2003 Bw. Mgengeli aliondoka kwenda masomoni na nafasi yake kuchukuliwa na Bw. Kassim Robert (Wakili wa Serikali) ambaye naye pia, baada ya muda mfupi, aliondoka tarehe 17/10/2003 na nafasi yake kuchukuliwa na Bw. Philip Mcamanga, Wakili wa Serikali Mkuu aliyeongoza upande wa utetezi hadi mwisho wa kusikiliza shauri hili.

Mawakili wa pande zote mbili walikubaliana na Jopo likaridhia, kuwa mgogoro huu unajikita katika viini/shufaa zifuatazo:-

(a) Kama uondoshaji katika Kitongoji cha CCM "Centre" (Nyamuma iliyobaki) ulikuwa ni halali, yaani kisheria.
(b) Kama kulikuwa na ukiukaji wa haki za binadamu katika namna ya uondoshaji uliofanyika.
(c) Kama ilikuwa ni halali kuwakamata na kuwanyang'anya vifaa na picha watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.
(d) Kama walalamikaji/wadai wanastahili nafuu zilizoombwa katika hati ya malalamiko.
(e) Kama walioondolwa walikuwa ni wakazi halali wa Kijiji cha Nyamuma iliyobaki au CCM "Centre":
(f) Kama kulikuwa na uhalali wa Kijiji cha Nyamuma iliyobaki au kilikuwa na hadhi gani.

Inaendelea >

Katika majumuisho yao mawakili wa walalamikiwa waliiomba Tume iunde shufa ya nyongeza. Ombi hili halikupingwa hivyo sufaa ifuatayo, ambayo inasomeka kama ifuatavyo ilikubalika:-

g) Kama kweli uongozi wa serikali ngazi ya Wilaya, na mawakala wake, ulitumia vibaya mamlaka ukiopewa na sheria.

Katika hatua za wali za kusikiliza shauri hili, kutokana na ombi la Mawakili wa walalamikiwa, Jopo pamoja na mawakili wa pande zote mbili walitembelea eneo la mgogoro. Zoezi hili liliwajumuisha pia viongozi wa serikali ngazi ya kijiji cha Bonchugu ambacho ndicho kilikabidhiwa kiutawala eneo la iliyokuwa Nyamuma iliyobaki kabla na baada ya uondoshwaji wa walalamikaji. Zoezi hili pia lilihusisha baadhi ya walalamikaji. Katika zoezi hili mambo yafuatayo yalidhihirika na kukubalika na pande zote kwamba hayana mjadala:-

(a) Mabaki (visiki na majivu) ya nyumba, maghala, na mazizi ya mifugo ambayo yalikuwa yamechomwa siku za nyuma yalionekana.

(b) Mazao ya kudumu ya bustani, kama vile migomba, michungwa, mipapai na miti ya mbao (mikaratusi) ilionekana.

(c) Wanavijiji/walalamikaji walioondolewa kwa kuchomewa miji yao hawakurudi au kuridishwa kwenye makazi yao ya awali, isipokuwa Matiku Makuri, ambaye alikutwa akimiliki sehemu ndogo tu ndani ya lililokuwa eneo lake la awali.

(d) Wamiliki/wakazi wa sasa wa iliyokuwa Nyamuma wanadai kwamba hawajawahi kuona wala kusikia uchomaji moto wa nyumba katika maeneo hayo.

(e) Kulikuwa na kaburi ambalo Eliud Pius alidai kwamba ni la marehemu mama yake, Rahel Pius aliyezikwa tarehe 14/3/1990 na kwamba mmiliki wa sasa hana habari na kaburi hilo.

(f) Kulikuwa na mabaki ya Kanisa la (Pentecostal Evangelistic Fellowship of Africa {PEFA} lililovunjwa na kwamba Mtendaji wa Kijiji cha Bonchungu, Bwana Makena, alisema tangu 1999 alikuta limebomolewa.

(g) Tume iliona na kuelezwa juu ya jingo la Shule ya Msingi Bugumbe iliyokuwa ndani ya Hifadhi ay Ikorongo lililobomolewa na matofali yake yakatumika

Inaendelea >

kujenga ofisi za Hifadhi, na zilizokuwa nyumba za walimu wa shule hiyo zinatumika kama nyumba za kuishi wafanyakazi wa Hifadhi.

(h) Watafiti wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walionesha eneo wanalodai walisimama wakati wakipiga picha likiwa nje ya Hifadhi hiyo.

(i) Wanafamilia wa Mee Matiku Makuri, ambaye ni mlalamikaji walificha vyombo vyao vya nyumbani (vitanda, magodoro, masanduku, na vyombo vya jikoni) vichakani, na baadhi ay viongozi wa serikali ya Kijiji cha Bonchugu walionesha mahali ambapo vyombo hivyo vilijificha.

(j) Uongozi wa Kijiji cha Bonchugu ulikanusha kufanyika kwa uchomaji katika eneo hilo.

(k) Yalioneshwa makazi ya muda ya Bwana Matiku Makuri, ambapo alikuwa akiishi baada ya uchomaji wa mji wake.

Katika kuthibitisha dai hilo upande wa walalamikaji waliita jumla ya mashahidi 133. Mashahidi hao walieleza kuwa:-

(a) Baadhi ya walalamikaji walianza kuhamia katika eneo la mgogoro mnamo mwaka 1986 wakitokea sehemu mbalimbali kama vile Vijiji vya Ngarawahi na Machochwe na Wilaya ya Tarime. Watu hao waliondoka katika maeneo yao kutokana na migogoro ya kiukoo. Wakati huo eneo la mgogoro lilikuwa chini ya uongozi wa Kijiji cha Rwamchanga. Baadhi ya wahamiaji walipata maeneo kupitia uongozo wa Rwamchanga na wengine waliingia wenyewe katika maeneo ya mapori ambayo hayakuwa yanakaliwa na watu.

(b) Mwaka 18993 Kijiji cha Nyamuma kilisajiliwa rasmi na kupewa cheti cha usajili.

(c) Eneo la mgogoro liliangukia kwenye mipaka ya kijiji hicyo. Aidha kijiji hicho kiliwahi kuwa na viongozi wake kwa nyakati tofauti. Viongozi hao ni Muturi Chagucha, (Mtendaji wa kwanza), Emanuel Bwiru Mwita (Mwenyekiti wa kwanza), Joseph Makemba (Mwenyekiti), Jonas Magoge (Mtendaji wa kwanza), Emanuel Bwiru Mwita (Mwenyekiti wa Kwanza), Joseph Makemba (Mwenyekiti),

Inaendelea >

Jonas Magoge (Mtendaji), Pius Imwamu (Mwenyekiti), chacha Chonoa (Mtendaji) na Samweli Makena (Mtendaji).

(d) Mnamo mwaka 1994 mipaka ya Hifadhi ya Ikorongo ilipanuliwa. Katika upanuzi huo wanakijiji wa eneo lililomezwa na Hifadhi walitathminiwa mali zao na kulipwa fidia kabla ya kuondoka hapo Julai/Agosti mwaka 2000. Tathmini hiyo ilijumuisha pia Shula ya Msingi Bugumbe ambayo walalmikaji walichangia nguvu zao katika ujenzi wake. Baadhi ya wanakijiji waliotoka ndani ya Hifadhi walihamia katika eneo la Nyamuma iliyobaki na kupata ardhi kwa ama kununua au kumegewa na wakzi wa eneo hilo.

(e) Mwala huo wa 2000 baadhi ya walalamikaji walihamia katika eneo la mgogoro wakitokea Nyanguge (Mara Cop). Baadhi ya hawa walikuwa wamehamia Nyanguge wakitokea eneo la mgogoro lakini walilazimika kurejea eneo la mgogoro baada ya kubomolewa makazi yao huko Nyanguge wakati wa machafuko ya mwaka 2000.

(f) Tarehe 08/10/2001 Mlalamikiwa Na. 1 akiongoza msafara wa magari yaliyowaleta viongozi mbali mbali wa Serikali ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Kijiji walitangazia wakazi wa eneo la mgogoro, kupitia Katibu Tarafa wa Tarafa ya Rogoro, Bwana Paul Shanyangi, kuwa wakazi hao wawe wameondoka katika eneo hilo ifikapo tarehe 12/10/2001. Tangazo hilo lililotolewa kwa kutumia kipaza sauti.

(g) Walalamikaji hawakuweza kuhama kwa sababu walipewa muda mfupi mno wa kufanya hivyo, pia hawakujulishwa kuwa wahamie wapi.

(h) Tarehe 12/10/2001 bado walikuwepo katika makazi yao katika eneo la mgogoro.

(i) Alfajiri ya siku hiyo ya tarehe 12/10/2002:-

Inaendelea >

(j) Mlalamikiwa Na. 1 aliongoza msafara wa watu walioteuliwa kutekeleza amri ya kuwaondosha walalamikaji kwa nguvu kutoka katika makazi yao. Msafara huo ulijumuisha Mlalamikiwa Na. 2, askari polisi, askari magereza, askari wanyamapori, viongozi na wanavijiji wa vijiji vya karibu vikiwemo vijiji vya Rwamchanga, Bonchugu, Miseke na Kebisongo.

(ii) Washiriki wa msafara huu walichoma makazi, mazizi na mgahala ya walalamikaji yaliyokuwa na vyakula.

(iii) Wahiriki wa msafara huu walipora baadhi ya vymbo vya nyumbani, vyakula vilivyokuwa kwenye maghala pamoja na mifugo.

(iv) Baadhi ya walalamikaji walifanyiwa vitendo viovu ikiwa ni pamoja na kupigwa, kuteswa, kunyanyaswa na vilema kuachwa bila msaada wowote.

(j) Zahanati iliyokuwa CCM "Centre" ilitumiwa na msafara wa wanaondosha kama kituo cha kukutania na kupokea taarifa ya utekelezaji wa zoezi la uondoshaji, na kuwa baadhi ya walalamikaji waliokuwa wanawekwa ndani ya magari ya msafara walikuwa wanapelekwa sehemu hiyo.

(k) Jioni ya tarehe 12/10/2001 walalamikaji walikimbilia Mugumu mjini kutafuta hifadhi, lakini watu wa huko walisita kuwapa msaada kwa madai kuwa Mlalamikiwa Na. 1 alikuwa ametishia kumchukulia hatua mtu yeyote atakayewapa msaada watu kutoka Nyamuma.

(l) Walalamikaji hawakuweza kusalimisha au kuchukua kitu chochote. Mali zao zote ama ziliteketezwa au kuporwa wakati wa zoezi la uchomaji. Aidha waliacha mazao mashambani. Mlalamikaji pekee aliyekiri kusalimisha baadhi ya mali zake ni Emmanuel Pius (SMJ. 14) ambaye alisafirisha mifugo yake usiku moja kabla ya siku ya opereshení.

Inaendelea >

(m) Katika tafrani hiyo watu wa familia walipotezana na ilichukua muda watu hao kukutana tena, na wengine walikuwa hawajaonana na jamaa zao hadi tarehe 25/10/2004 usikilizaji wa shauri hili ulipomalizika.

(n) Kuanzia tarehe 12/10/2001 walalamikaji walipoondoshwa kwenye makazi yao maisha yao yamekuwa ya dhiki, na kuwa:-

(i) Hawana makazi ya kuaminika, wanatangatanga na kulazimika kuishi kwenye mazingira duni yanayodhalilisha utu wa binadamu, kama vile familia yenye mume na mke na watoto wa jinsia tofauti kulazimika kuishi kwenye chumba kimoja.

(ii) Hawana kipato cha kuaminika,

(iii) Hawana chakula,

(iv) Watoto wao hapatai elimu,

(v) Baadhi wanatishiwa maisha yao.

(o) Walalamikaji walitafuta msaada kutoka sehemu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwa Mbunge wao Dr. James M. Wanyancha (SMJ. 6) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

(i) Kutokana na ombi hilo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilipeleka watafiti wake katika eneo la tukio. Watafiti hao, Kaleb Lameck Gamaya (SMJ 11) na Clement Julius Mashamba (SMJ 12) walitembelea eneo la tukio wakiongozwa na walalamikaji wawili, Ibrahimu Korosso (SMJ 4) na Eliud Pius (SMJ 13). Wakati wanatembelea eneo hilo watafiti hao walikamatwa na askari wa wanyamapori, wakawekwa chini ya ulinzi, wakakabidhiwa polisi, wakanyang'anywa vifaa vyao vya kazi na kisha wakapelekwa kwa mlalamikiwa Na. 1 kwa kuhojiwa. Waliendelea kuwa chini ya ulinzi hadi tarehe 4/1/2002 huko Tarime kwa amri ay Mkuu wa Wilaya hiyo ya Tarime Bwana Paschal mabiti, bila kufunguliwa shitaka lolote hadi sasa. Kabla ya kuondoka Tarime walikabidhiwa vifaa vyao vyote isipokuwa mkanda mmoja wa 'video' na mikanda miwili (2) ya picha za

Inaendelea >

kawaida ambayo walielezwa kuwa vimebaki Polisi Muhumu ili viendelee kufanyiwa kazi.

(ii) Kutokana na ombi hilo hilo la walalamikaji Mbunge wa Silaya ya Serengeti, Mheshimiwa James M. Wanyancha (SMJ. 6) aliwasilisha suala hili serikalini kwa kuwasiliana na viongozi mbalimbali. Kufuatia taarifa hiyo, na kwa nyakati tofauti, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib (Mbunge) aliyekuwa Waziri wa Mambo ay Ndani ya nchi kwa wakati huo, na Mkuu wa Mkowa wa Mara, Mhershimiwa Balozi Nimrod Lugoe, walitembelea eneo husika. Katika maelezo yake Mheshimwia Waziri alikanusha kuwepo kwa uchomaji katika eneo hilo.

Walalamikaji waliochomewa makazi yao waliorodhesha mali zao katika vielelezo walivyowasilisha kwenye Tume kama sehemu ya ushahidi wao. Orodha ya mali hizo, na thamani yake, vimeainishwa katika jedwali lililoambatishwa kwenye maamuzi haya.

Katika utetezi wao walalamikiwa waliita mashahidi thelathini na watatu (33). Kimsingi walalamikiwa na mashahidi wao wamekanusha madai ya walalamikaji kwa kusema kuwa:-

(a) Walalamikaji, kuanzia mwaka 1986, walivamia eneo la mgogoro ambalo lilikuwa ni sehemu ya Kijiji cha Rwamchanga.

(b) Kutokana na uvamizi huo kumekuwepo na mgogoro wa muda mrefu kati ya wakazi wa eneo husika na wanakijiji wa Rwamchanga, yakiwemo matukio ya mauaji, na kuwa taarifa za mgogoro huu zimewahi kuwasilishwa katika ngazo zote za serikali kwa nyakati tofauti. Serikali, kwa upande wake, ilitoa maelekezo kuwa wavamizi hao waondolewe kwa sababu hawakufuata taratibu za kujiunga na kijiji.

(c) Mwaka 1984 Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ilipitisha azimio la kupanua mipaka ya hifadhi ya wanayamapori ya Ikorongo.

(d) Mwaka 1993 Kijiji cha Nyamuma kilisajiliwa kikiwa ndani ya Hifadhi na kuwa kwa msingi huo usajili huo ulikuwa ni batili, hivyo hapajawahi kuwa na kijiji cha Nyamuma kisheria.

Inaendelea >

(e) Mwaka 1994 mipaka ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Ikorongo ilitangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali kwa GN. Na. 214 ya mwaka 1994.

(f) Katika upanuzi huo kijiji chote cha Nyamuma, ambacho kwa maoni yao kilikuwa ni batili, kilimezwa na Hifadhi.

(g) Watu waliokuwa wanaishi ndani ya Hifadhi walitathminiwa mali zao na kulipwa fidia na kutakiwa kuhamia katika vijiji walivyokuwa wampangiwa.

(h) Baada ya watu hao kulipwa fidia ilichukua jumla ya siku sabini (70) kuweza kukamilisha zoezi la kuwahamasisha.

(i) Baadhi yao walihamia katika sehemu ya mgogoro. Matokeo yake ni kuongezeka kwa vitendo vya uvamizi wa ardhi, uwindaji haramu, ubakaji wa wanawake wa Kijiji cha Rwamchanga, wizi wa mifugo, eneo hilo kugeuka kuwa maficho ya majangili, wauaji na amani ilianza kutoweka.

(j) Matukio haya yaliongeza msukumo wa Serikali ya Wilaya kutekeleza maelekezo ya awali ya kuwaondosha wakazi wa eneo la mgogoro. Mikakati ya operesheni ya uondoshaji ilipangwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Serengeti na kupata ridhaa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mara.

(k) TArehe 08/10/2001 mchana wakazi wa eneo la mgogoro walitangaziwa na serikali ngazi ya Wilaya, kwa njia ya kipaza sauti, kwamba wawe wameondoka katika eneo hilo ifikapo tarehe 12/10/2006 na kuwa warudi kwenye vijiji vyao vya asili, au Kenye kwa wale ambao ni Wakenya.

(l) Tarehe 11/10/2001 viongozi hao hao walitembelea eneo husika na kubaini kuwa wakazi wote walishaondoka, na kuwa wliondoka na mali zao zote.

(m) Alfajiri ya tarehe 12/10/2001, viongozi hao hao, wakiwa na askari polis, askari magereza na askari wa wanyamapori wenye silaha na viongozi na wananchi wa vijiji vya jirani vya Rwamchanga, Bonchugu, Miseke na Kebosongo walifika katika eneo la tukio na kufanya kazi ya uondoshaji kwa kuchoma mahame yasiyokuwa na watu au mali, na kuwa hakukuwa na mtu/watu waliokutwa kwenye eneo la tukio siku hiyo.

(n) Katika zoezi hili mahame yote yalichomwa isipokuwa jengo la Kanisa la PEFA.

(o) Eneo la zahanati ya Kijiji cha Nyamuma lilitumika kama sehemu ya kukutania na kutoa taarifa ya utekelezaji wa zoezi la siku hiyo.

*Inaendelea >*

(p) Tarhe 01/01/2002 watafiti wawili wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walikamatwa kwa sababu ya kuingia kwenye eneo la Hifadhi ya Wanyamapori bila kibali. Baadhi ya vifaa vyao vya kazi vilizuiwa na vinaendela kuzuiwa kwa ajili ya kuendelea kufanyiwa kazi.

Kutokana na hayo ni hoja ya walalamikiwa kwamba:-

(a) Walalamikaji hawakuwa wakazi halali wa Kijiji cha Nyamuma iliyobaki kwa sababu kuwepo kwa kijiji hich hakukuwa halali.

(b) Uongoshaji wa watu kutoka katika Kitongoji cha Nyamuma iliyobaki ulikuwa halali.

(c) Hawakuwafanyia walalamikaji vitendo vinavyovunja haki za binadamu kwa sababu hawakuwepo kwenye eneo la tukio.

(d) Ilikuwa halali kuwakamata watafiti wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na kuzuiwa vifaa vyao.

Kama sehemu ya utetezi wao walalamikiwa, kupita Mawakili wao waliiomba Tume ikakague eneo la mgogoro. na kutaka kila mlalamikaji akaonesha eneo alilokuwa anamiliki kabla ay uondoshwaji. Tume iliridhia ombi hilo na ukaguzi wa eneo ulifanyika.

Huu ndo muhtasari wa ushahidi wa pande zote mbili. Hatua inayofuata ni tafakuri ya viini vya shauri lililowasilishwa mbele ya Tume kwa kuzingatia ushahidi uliopokelewa.

(a) Kama uondoshaji katika Kitongoji cha CCM "Centre" (Nyamuma iliyobaki) ulikuwa ni halali, yaani kisheria.

Jambo la kwanza la kutafakari ni kama kulikuwepo na watu na mali zao katika eneo la mgogoro tarehe ya tukio.

Walalamikaji, katika ushahidi wao, wanasema kwamba siku ile ya tukio walikuwepo wao pamoja na mali zao, isipokuwa Emanuel Pius SML 14 ambaye alisafirisha mifugo yake siku moja kabla ya siku ya operesheni, ingawa yeye alibaki na mali zake nyingine

Inaendelea >

katika eno lake. Walalamikiwa kwa upande wao, wanashikilia kwamba siku hiyo ya operesheni wakazi wa eneo hilo walishaondoka na mali zao. Mawakili wa waalamikiwa wameleta rai kwamba Tume iukabili ushahidi huu, hoja ambayo inapingwa na mawakili wa walalamikaji.

Ushahidi wa pande zote mbili unashabihiana katika mambo yafuatayo, kwamba:-

(a) Operesheni ilianza saa 12:00 asubuhi siku ya tukio.

(b) Mlalamikiwa Na. 1 na 2 walikuwapo kwenye operesheni hiyo

(c) Magari yalitumika kuwaleta viongozi wa operesheni na kuwa walalamikiwa Na. 1 na Na. 2 walikuwa kwenye gari moja.

(d) Katika operesheni hiyo viongozi wa Wilaya waliongoza askari polisi, magereza, wanyamapori na viongozi wa wanavijiji wa Vijiji vya Rwamchanga, Bonchugu, Miseke na Kebosongo.

(e) Eneo la Zahanati ya kilichokuwa Kijiji cha Nyamuma lilitumika kama kituo cha kukutania na kutoa taarifa za operesheni.

Isitoshe Ibrahim Korosso (SMJ. 4) katika ushahidi wake aliwataja watu watano (5) ambao anadai kuwa aliwaona katika eno la mgogoro siku ya tukio, mmoja wao akiwa ni Waisero Nyamhanga (SMW.10) na kuwa walishiriki katik azoezi la uondoshaji la tarehe 12/10./2001. Waisero Nyamhanga (SMW. 10) katika ushahidi wake alithibitisha kushiriki katika zoezi hilo.

Swali la kujiuliza ni kwamba, iwapo walalamikaji hawakuwepo kwenye eneo la tukio siku ya operesheni wangewezaje kuwa na ufahamu wa mambo/matukio haya? Kushabihiana huku kunaonesha kwamba walalamikaji walikuwepo kwenye eneo la mgogoro siku ya operesheni. Pili, mnamo mwaka 2000 watu walihamishwa kutoka hifadhi ya Ikorongo. Wakati huo watu hao walipewa notisi ya siku thelathini (30) lakini baada ya notisi hiyo kumalizika hawakuwa wameweza kuhama, wakaongezewa siku zingine thelathini (30) za ziada lakini hata hivyo hawakuweza kuhama, wakaongezewa tena siku kumi (10) zaidi ndipo wakaweza kuhama. Iweje watu kutoka ndani ya hifadhi walihitaji siku sabini (70) za kuhama lakini walalamikaji waweze kuwa wamehama ndani ya siku tatu (3) tu?

Inaendelea >

Mawakili wa upande wa walalamikiwa walitoa hoja kwamba walalamikaji walikuwa wamepewa notisi ndefu tangu mwaka 2000 ambayo ilitosheleza kuwawezesha kuhama. Hoja hii haina nguvu kwa kuwa notisi waliyopewa watu waliokuwa hifadhini haikuwahusu watu walikokuwa katika eneo la mgogoro.

Ushahidi unaonesha kwamba baada ya operesheni ya kuwaondoa watu ndani ya hifadhi, wakazi wa eneo la mgogoro walikabidhiwa kijiji cha Bonchugu kiutawala. Kama notisi hiyo ingewahusu walalmikaji, wao pia wangekuwa wamelipwa au kuondoka kama wale wa ndani ya hifahdi, hivyo suala la wao kukabidhwia kijiji cha Bonchugu kiutawala halingekuwepo. Katika hali hiyo Tume ina maoni kwamba ushahidi wa walalamikaji kuhusu suala hili una uzito na ni wa kuaminika. Ushahidi wa walalamikaji, ambao tunaukubali, unaunga mkono hoja ya mawakili wa walalamikaji kwamba walalamikaji walikuwepo kwenye eneo la mgogoro siku ya operesheni. Tume inaafiki hoja hiyo.

Utetezi wa walalamikiwa ni kwamba kuondoshwa kwa walalamikaji kulikuwa halali kwa kuwa walikuwa ni wavamizi, wahalifu na pia ni raia wa Kenya. Kuhusu uvamizi walalamikiwa wameorodhesha majina ya walamaikaji wafuatao wanoadaiwa kuwa ni wavamizi wa mashamba ya wanakijiji wa Rwamchanga. Walalamikaji hao ni:-

| | | |
|---|---|---|
| 1) Pius Imwamu | - | SMJ. 40 |
| 2) Mugere Mwita | - | SMJ. 120 |
| 3) Daniel Bwiru | - | SMJ. 19 |
| 4) Jackson Mwita | - | SMJ. 5 |
| 5) Matiku Makuri | - | SMJ. 2 |
| 6) Mwita Kalaki | - | SMJ. 61 |
| 7) Emmanuel Bwiru | - | SMJ. 1 |

Ushahidi uliopo, na ambao haukupingwa, ni kwamba walalamikaji/wavamizi wameingia kwenye eneo la mgogoro kati ya mwaka 1986 na 1988. Mwaka 1992 Jackson Mwiga (SMJ. 5) ambaye ni mmojawapo wa watu wanaodaiwa kuvamia ardhi ya Rwamchanga, alifikishwa mahakamani akiwa na wenzake kumi na watano (15) kwa kudaiwa kuvamia

Inaendelea >

ardhi ya Rwamchanga. Shitaka hili lilitupiliwa mbali kwa misingi kwamba hakukuwa na uvamizi wa ardhi. Tangu wakati huo hadi wakati wa operesheni hakuna mgogoro wowote wa ardhi uliowahi kufikishwa mahakamani au kwenye chombo kingine chochote chenye mamlaka. Aidha wakati walalamikaji wakitoa ushahidi mbele ya Tume mawakili wa walalamikiwa hawakuwahi kuwahoji walalamikaji kuhusu uvamizi wa ardhi ya mashahidi wa walalamikiwa. Isitoshe kuna ushahidi kwamba mwaka 2000 wakazi wa Nyamuma waliodaiwa kuvamia eneo la Nyanguge, ambalo ni sehemu ya Rwamchanga, waliondolewa kwa nguvu kutoka katika eno hilo. Wakati huo waondoshaji hawakuingia eneo la mgogoro. Suala la kujiuliza ni kwamba kama wakazi wa eneo la mgogoro walikuwa ni wavamizi kwa nini wakati wa uondoshaji huo wa Nyanguge watu wa Rwamchanga hawakuvuka na kuingia eneo la mgogoro na kuwaondolsha walalamikaji wote katika shauri hili, ikiwa ni pamoja na hao waliotajwa hapo juu?

Njia iliyotumika kuwaondosha walalamikaji kutoka katika eneo la mgogoro mwaka 2001 haikufuata taratibu zilizowekwa kisheria za kushughulikia migogoro ya ardhi.

Kifungu 167(1) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kinabainisha kwamba (kama kinavyosomeka kwa lugha ya kiingereza), tunanukuu:-

> "167-(1) The following couts are hereby vested with exclusive jurisdiction, subject to the provisions of this part, to hear and determine all manner of despute, auctions and proceedings concerning land, that is say:-
>
> a) The Court of Appeal;
> b) The Land Division of the High Court established in accordance with law for the time being in force stablishing court divisions.
> c) District Land and Housing Tribunals.
> d) Ward Tribunals.
> e) Village Land Council.

Kifungu 62(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999 kinasema (kama kinavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza), tunamkuu.

Inaendelea >

*"The following courts are hereby vested with exclusive jurisdiction, subject to the provisions of Part XII of the Land Act 1999, to hear and determine all manner of disputes, actions and proceedings concerning land, that is to say:-*

*(a) The Court of Appeal.*

*(b) The Land Division of the High Court.*

*(c) District Land and Housing Tribunals.*

*(d) Ward Tribunals.*

*(e) Village Land councils.*

Chini ya sheria hii mamlaka pekee zilizopewa uwezo kisheria wa kutatua migogoro ya ardhi katika vijiji ni:-

(a) Mahakama ya Rufaa,

(b) Kitengo cha Ardhi cha Mahakama Kuu,

(c) Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

(d) Baraza la Kata,

(e) Baraza la Ardhi la Kijiji.

Aidha kifungu 181 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kinaweka bayana suala hili kwa kusisitiza kwamba migogoro ya ardhi isishughulikiwe na chombo chochote isipokuwa mamlaka zilizoainishwa. Chini ya Sheria hizi mamlaka iliyoendesha zoezi la kuwaondosha walalamikaji kutoka katika eneo la mgogoro sio mojawapo ya mamlaka zilizoainishwa katika sheria hizi. Katika kujadili hoja hii mawakili wa walalamikwia walidai kwamba mgogoro huu ulikuwa wa kijinai na kwamba serikali isingeweza kusubiri mgogoro huo utatuliwe kwa taratibu za kisheria. Tume inashindwa kukubaliana na hoja hiyo kwa kuwa mgogoro wenyewe ulikuwa wa siku nyingi na haukuchukua sura yoyote ya udharura. Kwa kuwa nchi hii inaendeshwa kwa msingi ya ya utawala wa sheria (The rule of law) ingetazamiwa mamlaka iliyohusika na operesheni husika ingezingatia misingi hiyo.

Tume yenyewe, kwa upande wake inatambua kwamba sio mojawapo ya mamlaka zilizoorodheshwa chini ya zile sheria zilizotajwa na kupewa mamlaka ya kutatua migogoro ya ardhi. Hivyo katika kuchunguza shauri hili Tume haitashughulikia suala la mgogoro wa

*Inaendelea >*

ardhi baina ya wanakijiji wa Rwamchanga na walalamikaji. Tume itajishughulisha tu na madai ya uvunjwaji wa haki za binadamu za walalamikaji na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Tume imepewa mamlaka haya chini ya Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na. 7 ya 2001, jinsi ilivyorekebishwa, (kama kinavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza), kinachosomeka:-

*"15-(1) The Commission shall have powers to investigate any human rights abuses or mal administration:-*

*(a) On its own initiative or*

*(b) On receipt of complaint or allegation under this act by:-*

*(i) An aggrieved person acting in such persons own interests;*

*(ii) An association actin in the interest of the members; or*

*(iii)A person acting in the interest of a group or class of persons".*

Chini ya utaratibu huu Tume sasa itaendelea na uchunguzi wake wa madai ya walalamikaji ya uvunjwaji wa haki zao za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika utetezi wa walalamikiwa wamedai kuwa uondoshaji ulikuwa halali kwa sababu walalmikaji walikuwa wamefanya itendo mbali mbali vya uhalifu.

UHALIFU

***Matukio ya mauaji***

Walalmikiwa waliorodhesha watu waliouawa kati ya mwaka 1986 na 2000 kama ifuatavyo:-

1986 – Mahiti Nyantacho
Kinyege Satima,

1992 - Ochieg Francis

1994 - Ninai Machonchori
Mwita Muhume.

2000 - Surona Matambaricha
Makenye Nyamraba

Inaendelea >

Hoja ya walalamikiwa ni kwamba mauaji ya wanakijiji waliotajwa hapo juu yalifanywa na walalamikaji, na kwamba hili ni sababu mojawapo ya kuwaondosha walalamikaji kwa nguvu. Mauaji haya yamefanyika ndani ya kipindi kirefu cha miaka kumi na mine (14). Waliodaiwa kuuawa ni wanakijiji saba (7) tu na sio mauaji ya halaiki. Isitoshe baadhi ya wahushika wa mauaji walitambuliwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Baadhi yao waliwekwa ndani na baadaye kuachiwa na mahakama. Aidha hadi wakati wa kusikiliza shauri hili mashauri ya baadhi ya watuhumiwa yalikuwa yanaendelea mahakamani. Vile vile kitendo cha kuiadhibu jamii nzima kwa kuwaondoa kwenye eneo la mgogoro kwa ajili ya watuhumiwa wachache ni jambo lisilokubalika na ni kinyume kabisa na misingi ya utawala bora.

**Maficho ya mauaji**

Ilidaiwa kwamba watu waliokuwa wanafanya mauaji kule Rwamchanga walikuwa wanajificha katika eneo hili la mgogoro, na kwamba hali hii ilizidi kuwa mbaya baada ya mapigano ya koo za Warenchoka na Waanchari huko Tarime, ambapo Warenchoka, baada ya kufanya mauaji huko, walikimbilia eneo hili la mgogoro na kuungana na ndugu zao. Ili kuzima mauaji ya Tarime yasihamie katika Wilaya ya Serengeti ilibidi kuchukuliwa hatua ya kuwaondosha wakazi wa eneo la mgogoro.

Upo ushahidi unaonesha kwamba baadhi ya walalamikaji waliwahi kukamatwa na kupelekwa Tarime kujibu mashtaka ya mauaji lakini wakaachiwa baada ya kukosekana ushahidi. Kama ilifahamika kwamba kuna wahalifu kutoka Tarime ambao wamehamia katika eneo la mgogoro wangekamatwa na sheria ingechukua mkondo wake kama ilivyofanya katika walalamikaji wale waliofikishwa mahakamani na baadaye watu hao wakaachiwa au kutiwa hatiani kama utakuwepo ushahidi wa kutosha.

**Ubakaji wa uwindaji haramu**

Watuhumiwa katika makosa ya ubakaji na uwindaji haramu walistahili kukamatwa na kupelekwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Tume ina maoni kwamba vitendo vya uhalifu vya kuficha mauaji, wabakaji na wawindaji haramu, ama vikichukuliwa kimoja kimoja au katika ujumla wake, havitoshelezi kuwa sababu za kuchukua hatua kama

Inaendelea >

zilizochukuliwa hapa. Hivi vilikuwa ni vitendo ambavyo vilistahili kudhibitiwa na vyombo husika kama vile polisi na mahakama, kwa mujibu wa sheria za nchi.

**Uraia wa walalamikaji**

Walalamikiwa wanadai kwamba walioondosha walalamikaji kwa sababu ni raia wa Kenya na sio raia wa Tanzania. Huu ni utetezi dhidi ya walalamikaji walioeleza kwamba wao ni raia wa Tanzania kwa mfano:-

> Zablon Chahe (SMJ.44) ambaye alisema awali kutuhumiwa kuwa ni raia wa Kenya, lakini mamlaka za uhamiaji za Tanzania na Kenya zilibaini kuwa alikuwa ni raia wa Tanzania.
>
> Bhoke Mwita Chahe (SMJ. 49), aliieleza Tume kwamba wakati wa zoezi la kupeleka Kenya baadhi ya walalamikaji kwa nguvu, mwanawe mchanga alifariki dunia na kwamba alilazimika kumzika mwanawe huyu kwa kumfunika matawi ya miti kenye kichaka katika eneo la Nyamwanga, Wilayani Tarime, akiwa safarini kurejea Serengeti baada ya Mamlaka ya Uhamiaji ya Kenya kumkana yeye na walalamikaji wengine kuwa walikuwa Wakenya.

Ushahidi wa walalamikaji kuwa walikuwa ni raia wa Tanzania haukupingwa. Mawakili wa walalamikiwa walidai kwamba baadhi ya walalamikaji waliwahi kukabidhiwa notisi ya mtu asiyetakiwa nchini "Prohibited immigrant" (P1.) Wakati wa kusikiliza shauri hili hakuna afisa yeyote wa uhamiaji aliyeitwa kutoa ushahidi kwamba notisi ya namna hiyo iliwahi kutumwa kwa malalamikaji yeyote. Aidha walalamikaji wanaosemakana kwamba walipewa notisi hizo hawajachukuliwa hatua zozote kuwasafirisha kwenda kwao.

**b) Kama kulikuwa an ukiukaji wa haki za binadamu katika namna uondoshaji ulivyofanyika.**

Hoja ya walalamikiwa ni kwamba uondoshaji wa walalamikaji kutoka katika eneo la mgogoro ulikuwa halali kwa maana kwamba ulifanyika kwa kuzingatia haki za binadamu, kwamba:-

Inaendelea >

kuvunja majengo yaliyojengwa bila kibali cha ujenzi hutoa notisi ya mwezi mmoja kuvunja majengo hayo. Aidha notisi hii iliyotolewa kwa njia ya kipaza sauti tarehe 08/10/2001 katika eneo la mgogoro ilikuwa ni kinyume na taratibu. Notisi kama hii inatakiwa kutolewa kwa maandishi na kuwekwa bayana sehemu mbalimbali za wazi ili kuwezesha taarifa hiyo kuwafikia wanakijiji wote, hata wale ambao hawakuwa kijijini siku ya tangazo. Kuna ushahidi kwamba, kwa mfano, siku hiyo ya tangazo mlalamikaji mmoja, Maria Mwita (SMJ. 85) hakuwepo kijijini siku ya tangazo na siku ya operesheni pia hakuwepo, kwa hiyo familia yake iliondoshwa yeye akiwa hayupo. Katika ushahidi wake alisema, tunanukuu:-

> ***"Tarehe 13/10/2001 nilikuwa mjini Musoma nikaambiwa kuwa huko Nyamuma Mkuu wa Wilaya amechoma nyumba na hakuna kilichobaki, na kwamba anatangaza kuwa Warenchoka hawatakiwi. Nilifunga safari kwenda kuwatafuta watoto wangu ambao niliwakuta watoto wawili wao wamekaa kwenye kichaka. Na mimi nilikaa nao kwenye kichaka kwa muda wa siku tatu. Kila nikienda kwenye mji mwingine niweke ze wale watoto ili niendelee kumtafuta mtoto wa kiume, watu walikuwa wanakataa kuwapokea kwa kuogopa kukamatwa. Mpaka leo hii mtoto huyo aitwaye Christopher Mwita hajaonekekana. Nilikwenda kwa OCD nikasema namtafuta mtoto Christopher Mwita, akaniambia "wewe si Mrechoka"? Nenda kwenu Kenya kwa Moi".***

Njia nyingine ambayo ilipaswa kutumiwa ni kuwaambia viongozi ili watoe taarifa kwa watu hao.

Kutokana na ushahidi uliopo, Tume inaafiki hoja ya walalamikaji kwamba notisi iliyotolewa katika zoezi hili haikuwa ya kutosheleza na ilikuwa kinyume na taratibu.

**ii) Uwezeshaji wa wananchi kuondoka.**

Walalamikiwa wamewasilisha hoja kwamba walalamikaji walipewa misaada mbalimbali, pale walipohitaji/walipoomba, ya kuwawezesha kuondoka. Walalamikiwa, katika kuleta hoja hii, waliwataja Pius Imwamu (SMJ. 40) na Emanuel Pius (SMJ. 14) kama walalamikaji waliowezeshwa kuondoka. Ushahidi

*Inaendelea >*

unaonesha kuwa Pius Imwamu alipewa kibali cha kuhamia kijiji cha Nyinchoka kwa barua ya tarehe 01/09/2000. Pius alieleza kuwa wakati huo hakuhama kwa sababu barua hiyo ya kibali cha kuhamia Nyinchoka ilikuwa ni shinikizo la Mlalamikwia Na. 1. Barua hiyo haina uhusiano na ombi la kibali cha kusafirisha mali kuhusiana na operesheni ya tarehe 12/10/2001, hivyo Pius Imwamu hakupata msaada wowote kumwezesha kusafirisha mali zake kwa minajili ya opereshini hii.

Kuhusu Emanuel Pius, ushahidi unaonesha kwamba ni kweli alipewa kibali cha kusafirisha mifugo ambayo ilikuwa ni ng'ombe 10, mbuzi na kondoo. Kibali hiki kilitolewa tarehe 11/10/2001 naye alikiri kusafirisha mifugo yake tarehe hiyo hiyo ya kibali ingawa yeye alibaki na mali zake nyingine kwenye eneo lake. Emanuel Pius ni mmoja tu kati ya walalamikaji, takribani mia moja na thelathini (130), ambao waliondoshwa katika eneo la mgogoro siku ya operesheni.

Tume ina maoni kwamba ushahidi kama huu hautoshi kuunga mkono hoja kwamba walalamikaji walipewa misaada mbalimbali kuwawezesha kuondoka. Kwa maana hiyo tunakubaliana na ushahidi wa walalamikaji kwamba waliondoshwa bila kupatiwa msaada wa kuwawezesha kuchukua mali zao, hivyo mali hizo zilibaki kwenye eneo la mgogoro.

**Watoto kupewa nafasi ya kuendelea na masomo yao walikohamia wazazi/wazeli wao.**

Ni hoja ya walalamikiwa kwamba baada ya Shule ya Msingi Bugumbe, iliyokuwa ndani ya Hifadhi, kuondoshwa, utaratibu uliwekwa ili watoto waliokuwa wakisoma kwenye shule hiyo, wakiwemo watoto wa walalamikaji, waweze kuendelea na masomo kwenye maeneo wanayohamia wazazi/walezi wao. Baada ya hapo hakuna malalamiko yoyote yaliyopokelewa kwamba kuna mwanafunzi yeyote kutoka eneo la mgogoro aliyewahi kukataliwa kusoma katika shule yeyote Wilayani Serengeti.

Inaendelea >

Upo ushahidi kwamba Shule ya Msingi Bugume iliondoshwa mwaka 2000, na kwamba wakati huo taratibu zilifanyika za kuwahamishia watoto waliokuwa wanasome shuleni hapo katika shule mbalimbali. Upo ushahidi pia kwamba watoto wa baadhi ya wakazi wa eneo la mgogoro walihamishiwa katika Shule ya Msingi ya Bonchungu mwaka huo huo wa 2000, ingawaje inadaiwa kwamba baadhi ya watoto hao hawakukubaliwa kujiunga na shule hiyo kwa madai kwamba Mlalamikiwa Na. 1 alitoa amri kuwa wasipokelewe. Hakuna ushahidi kwamba utaratibu kama huu ulifanyika wakati wa operesheni ya kuwaondoa walalamikaji mwaka 2001. Walalamikaji waliondoshwa baada ya notisi ya siku tatu (3) tu ambazo hazingewatosha kufanya utaratibu wa uhamisho wa watoto. Hata kama wangepata nafasi katika shule mbali mbali wazazi wao wasingeweza kuwapatia mahitaji ya shule kutokana na hali duni ya maisha yao baada ya kupoteza vyanzo vyao vya mapato kama vile mashamba, mifugo, biashara na ajira.

**iv) Mapokezi ya wakazi wa Nyamuma iliyobaki.**

Walalamikiwa walitoa hoja kwamba uondoshaji wa walalamikaji kutoka eneo la mogoro ulizingatia haki za binadamu kwa kuweka utaratibu uliowawezesha walalamikaji kupokelewa katika maeneo waliyokuwa wamepangiwa kuhamia. Katika kutetea hoja hiyo walalamikiwa waliengemea katika ushahidi wa Maafisa Watendaji sita (6) ambao walieleza kwamba waliwapokea walalamikaji ishirini na manne (24) katika maeneo yao kufuatia agizo la Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya. Orodha ya Maafisa Watendaji hao, vijiji vyao na majina ya watu wanaosemekana waliwapokea ni kama ifuatavyo:

| Jina la Afisa Mtendaji | Kijiji | Mamlaka aliyopokelewa |
|---|---|---|
| Jackob Mbota (SMW. 23) | Itununu | - Mwikwabe Mabeche (SMJ. 42) |
| Hamisi Muchandi (SMW. 24) | Nyakitono | - Jackson Mwita (SMJ. 5) |
| Joseph Maka Masongore (SMW. 25) | Burunga | - Meng'anyi Chahe (SMJ. 68) |
| Peter Chacha (SMW. 26) | Mosongo | - Ndumbe Nchama (SMJ. 74) |

Inaendelea >

| | | |
|---|---|---|
| | - Zablon Chahe (SMJ. 44)<br>- Chacha Magweiga (SMJ. 56)<br>- Mwita Mosoba (SMJ. 56) | |
| Philemon Mniko (SMW. 27) | Merenga | - Gisiori Magebo (SMJ. 109)<br>- Mahemba Kerongo (SMJ. 43)<br>- Ntunyo Range Mugosi (SMJ. 90)<br>- Samweli Marko (SMJ. 54)<br>- Chacha Machange (SMJ. 71)<br>- Juma Kasim @ Mwita Nyamhanga (SMJ. 106) |
| Wilson Tomas (SMJ. 30) | Kyambai | - Nokwe Mwita (Bubu) aliyetolewa ushahidi na mkewe Chacha Nokwe (SMJ. 30).<br>- Francis Mwita (SMJ. 46)<br>- Samson Nyamhanga (SMJ. 86)<br>- Kiringo Makere (SMJ. 45)<br>- Chacha Makere (SMJ. 78)<br>- Bhoke M. Chacha (SMJ. 126)<br>- Mwita Nokwi (SMJ. 47)<br>- Wankuru Nehama (SMJ. 101)<br>- Ibrahim Makere (SMJ. 87). |

Ushahidi wa Maafisa Watendaji hawa unaonesha kwamba utaratibu walioueleza ulihusika na zoezi la kuwahamisha watu kutoka ndani ya Hifadhi mwaka 2000 kwa kuwa waliitwa kwenye mikutano ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya Mwaka 2000. Aidha upo ushahidi kwamba walalamikaji waliotajwa hapo juu, wanaodaiwa kuhamia katika vijiji vilivyotajwa, walifanya hivyo kati ya mwaka 2000 na mwanzoni mwa 2001, kwa mfano.

Inaendelea >

inadaiwa kuwa walalamikaji waliodaiwa kuhamia Vijiji vya Itununu, Nyakitono, Burunga na Mosongo walifanya hivyo mwaka 2000, na kwamba wale waliohamia Kijiji cha Kyambai walifanya hivyo kati ya mwezi Januari na Aprili 2001. Kutokana na ushahidi huo Tume ina maoni kwamba zoezi hili halikuwa na uhusiano na operesheni ya tarehe 12/10/2001 iliyoanzishwa na tangazo la tarehe 08/10/2001 lililotaka wakazi wa eneo la mgogoro kuhama mara moja.

Ushahidi wa Maafisa Watendaji kwamba waliwapokea walalamikaji ishirini na wanne (24) katika vijiji mbali mali unatia wasi wasi kwa sababu haiwezekani kuwapo kwa walalamikaji hao katika vijiji hivyo kati ya mwaka 2000 na April, 2001 kabla ya kutolewa ile amri ya tarehe 08/10/2001 ya kuwaondosha walalamikaji kutoka katika eno la mgogoro. Ushahidi wa walalamikaji, ambao unaungwa mkono na ushahidi wa walalamikiwa, ni kwamba amri ya kuwaondosha walalamikaji ilieleza kwamba waende kwenye vijiji vyao vya asili. Kama maafisa hawa watendaji walikuwa wameandaliwa kuwapokea hawa walalamikaji katika vijiji vyao kama wanavyodai, kwa nini amri ya tarehe 08/10/2001 iwaelekeze walalamikaji kwwenda kwenye vijiji vyao vya asili na sio kwenda kweney vijiji vinavyodaiwa kuandaliwa kwa ajili yao?

Aidha hoja ya walalamikiwa kuhusu suala hili ina dosari kutokana na ukweli kwamba wakati walalamikaji wanatoa ushahidi mbele ya Tume hawakuhojiwa kama walipokelewa au hawakupokelewa au mafias watendaji hawa katika vijiji mbali mbali kama invyodaiwa. Kama wangeulizwa wakati huo, wangeweza kukanusah au kukubali na kutoa maelezo, kwa mfano, kuna ushahidi kwamba katika mila na desturi za wenyeji wa Wilaya ya Serengeti, inayojumuisha eneo la mgogoro, ni kawaida kwa watu kuwa na zaidi ya mji mmoja katika kijiji kimoja au katika vijiji tofauti. Kama walalamikaji wangekuwa wamepokelewa kama inavyodaiwa wangeweza kueleza kama walikuwa au hawakuwa na miji katika eneo la mgogoro. Lakini hawakuulizwa. Isitoshe wakati Tume ilipotembelea eneo la mgogoro kufuatia ombi la walalamikiwa kuwa walalamikaji waonesha maeneo wanayodai kuwa walikuwa wanayakalia wakati wa uondoshwaji walalamikaji hawa, pamoja na wengine, waliweza kuonesha Tume maeneo yao bila kusita. Si hivyo tu, walalamikaji wote ishirini na wane (24), isipokuwa watatu wana jirani au majirani waliyoyaonesha. Ifuatayo ni

Inaendelea >

orodha ya walalamikaji ishirini na moja (21) na watu wanaowatunga mkono kuwa ni majirani zao:-

| S/NA | JINA LA MLALAMIKAJI | JINA LA MTU/WATU WALIOMTAMBUA |
|---|---|---|
| 1. | Mwikwabe Mabeche (SMJ. 43 | 1. Joseph Keroko (SMJ. 41)<br>2. Magere Mwita (SMJ. 102)<br>3. Marwa Chacha (SMJ. 37)<br>4. Thomas G. Chacha (SMJ. 15) |
| 2. | Jackson Mwita (SMJ. 5) | 1. Mwakwabe Mabeche (SMJ. 42)<br>2. Chacha Gisima (SMJ. 79)<br>3. Mwita Kalaki (SMJ. 69)<br>4. Mwenge Mwikwabe (SMJ. 69)<br>5. Samwel Rubirya (SMJ. 75)<br>6. Marwa Kehai (SMJ. 22)<br>7. Chacha Mwita (SMJ. 2) |
| 3. | Meng'anyi Chahe (SMJ. 65) | 1. Nchama Marwa (SMJ. 60)<br>2. Nyamhanga Muriaga (SMJ. 74)<br>3. Ndumbe Nchama (SMJ. 74) |
| 4. | Simson Omare (SMJ. 29) | 1. Samson Kohe (SMJ. 66)<br>2. Nyamhanga Mwqita (SMJ. 81) |
| 5. | Ndumbe Nchama (SMJ. 74) | 1. Kahama Laban Makuri (SMJ. 16)<br>2. Meng'anyi cahe (SMJ. 68)<br>3. Nyamhanga Muriaga (SMJ. 98) |
| 6. | Zablon Chahe (SMJ. 44) | 1. Thomas Chacha ( SMJ. 115)<br>2. Bhoke Mwita Chacha (SMJ. 49) |
| 7. | Mwita Mosoba (SMJ 56) | 1. Emanuel Pius (SMJ. 14) |
| 8. | Mahemba Kerongo (SMJ. 33) | 1. Thomas Chacha (SMJ. 115)<br>2. Samwel Marko (SMJ. 54). |
| 9. | Ntunyo Range (SMJ. 90) | 1. Mtundi Mwita (SMJ. 26). |
| 10. | Samweli Marko Nyambibo | 1. Mtundi Mwita (SMJ. 26) |

Inaendelea >

| | | |
|---|---|---|
| | (SJM. 54) | |
| 11. | Chacha Machage (SMJ. 71) | 1. Chacha Nyamhanga (SMJ. 91).<br>2. Chacha Mesagawe (SMJ. 50)<br>3. Patrisi Marwa (SMJ. 94).<br>4. Rahel Simon W/O Nyangi Nyangi (SMJ. 119). |
| 12. | Juma Kasimu @ Mwita Nyamhanga (SMJ. 106) | 1. Kahama Laban Makuri (SMJ. 16).<br>2. Samweli Mwita (SMJ. 128). |
| 13. | Nokwe Mwita (SMJ. 30) | 1. Kirindo Makere (SMJ. 45)<br>2. Mendo Marwa (SMJ. 110) |
| 14. | Francis Mwita (SMJ. 46) | 1. Sospeter Mugosi Wantora (SMJ. 39) |
| 15. | Kirinddo Makere (SMJ. 86) | 1. Mendo Marwa (SMJ. 110)<br>2. Chacha Makere (SMJ. 78) |
| 16. | Samson Nyamhanga (SMJ. 86) | 1. Imwamu Pius (SMJ. 35)<br>2. Nyangige Mataro (SMJ. 57)<br>3. James Chacha Gentanyi (SMJ. 18) |
| 17. | Chacha Makere (SMJ. 78) | 1. Kirindo Ibrahimu Makere (SMJ. 87) |
| 18. | Bhoke Mwita Chacha (SMJ. 47) | 1. Rahel Range (SMJ. 70)<br>2. Helen Ramadhani (SMJ. 32)<br>3. Thomas Chacha (SMJ. 115) |
| 19. | Mwita Nokwi (SMJ. 47) | 4. Alipewa eneo na baba yake Nokwi Mwita ambaye ametambuliwa na majirani kama mkazi wa eno la mgogoro. |
| 20. | Wankuru Nchama (SMJ. 101) | 1. Imwamu Pius (SMJ. 35)<br>2. Samson Nyamhanga (SMJ. 86)<br>3. Rhobi Mrumbwa (SMJ. 83). |
| 21. | Ibrahim Makere (SMJ. 87) | 1. Kirindo Makere (SMJ. 45) ambaye ametambuliwa kama mkazi wa eneo la mgogoro, ndiye aliyemkaribisha kwenye eneo hilo. |

*Inaendelea >*

- Rhobi Mrumbwa - (SMJ. 83)
- Samweli Mwita - (SMJ. 128)
- Susana Nyanokwi - (SMJ. 93)
- Francis Mwita - (SMJ. 46)
- Wilson Korosso - (SMJ. 28)
- Helen Ramadhani - (SMJ. 32)

Walalamikaji hawa, katika ushahidi wao walikanusha kupokea malipo hayo. Tume ilieleza uchunguzi wa Kitaalamu kufanyika kuhusu jambo hili kwa kulinganisha alama za vidole gumba vya walalamikaji na alama za vidole gumba zilizopo katika hati ya malipo iliyotumika kufanya malipo hayo. Uchunguzi umebainisha kuwa walalamikaji watano (5) hawakuhusika na malipo hayo. Kuhusu mlalamikaji wa sita uchunguzi wa kitaalamu hakuweza kufanyika kwa sababu alama zake za vidole zilizochukuliwa kwa ajili ya zoezi hilo hazikutosheleza (insufficient for comparison).

Ni maoni ya Tume kuwa kufuatana na ushahidi uliochambuliwa hadi sasa hoja ya walalamikiwa kwamba baadhi ya walalamikaji si wakazi wa eneo la mgogoro haina msingi, hasa ikizingatiwa kuwa walalamikaji wote waliionesha Tume maeneo wanayodai kuyakalia kabla ya operesheni ya tarehe 12/10/2001. Mawakili wa walalamikiwa, wakiendeleza hoja hii, walidai kwamba wakati ukaguzi wa eneo la mgogoro baadhi ya walalamikaji waliionesha Tume maeneo waliyodai kuyakalia kabla ya operesheni, lakini hapakuwa na alama zozote za kukaliwa maeneo hayo kama vile mabaki ya nguzo za kuta za nyumba. Hoja hii haina uzito kwa sababu si rahisi kubaki kama hayo kuonekana baada ya mengi ya maeneo hayo kuwa yamekuwa yanalimwa kwa takribani miaka mitatu (3) tangu siku ya operesheni. Aidha hakuna ushahidi unaounga mkono hoja ya walalamikiwa kwamba walalamikaji waliopoondoshwa kutoka katika eneo la mgogoro taratibu ziliwekwa kuwawezesha kupokelewa katika vijiji mbali mbali walikohamishiwa. Kinyume na hayo ushahidi ulioko unaonesha kwamba walalamikaji, baada ya kuhamishwa kutoka katika eneo la mgogoro, hawakuwa na mahala pa kwenda bali walibakia kutangatanga. Hii inathibitishwa na Mlalamikiwa Na. 1 katika barua yake Kumbu. Na. U. 10/35/87 ya tarehe 26/03/2003 aliyomwandikia Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti. Katika

Inaendelea >

barua yake hiyo alikiri kuwepo kwa walalamikaji tisini na wanne (94) baadhi yao wakiwa wanatangatanga mjini Mugumu, na kwamba ili kutekeleza maamuzi ya mkutano wa Kamati ya Siasa ya Mkutano sasa anawapangia walalamikaji hawa maeneo katika vijiji mbalimbali Wilayani Serengeti. Kwa kuzingatia ushahidi uliopokelekwa, Tume inaona kwamba walalamikaji waliondoshwa kutoka eneo la mgogoro kimabavu na bila kuzingatia taratibu za kisheria na kwamba zoezi hili lilivunja haki za binadamu za walalamikaji na kukiuka misingi ya utawala bora.

## UVUNJWAJI WA HAKI ZA BINADAMU NA UKIUKWAJI WA MISINGI YA UTAWALA BORA

1. **Notisi ya kuondoshwa ya Tarehe 08/10/2001.**

   Kama ilivyoelezwa awali katika maamuzi haya, notisi hii ya siku tatu iliyotolewa katika taratibu za kushughulikia mgogoro wenye chimbuko lake kwenye masuala ya ardhi haikutolewa na chombo chenye mamlaka kisheria kushughulikia masuala ya migogoro ya ardhi, hivyo notisi hiyo haikuwa halali kisheria. Aidha ilikuwa fupi mno, hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya walalamikaji walikuwa wamekalia maeneo hayo kwa muda mrefu wa zaidi ya miaka kumi na miwili (12) na walikuwa na mali nyingi zinazohamishika napia zisizohamishika, kama vile nyumba na mazao ya kudumu. Ni wazi kwamba notisi hii ilikiuka misingi ya utawala bora, ambayo pamoja na mambo mengine, inahitaji kwamba katika zoezi kama hili walalamikaji walistahii notisi ndefu kuwawezesha kuondoka pamoja na mali zao na kuvuna mazo yao ya muda mfupi yaliyokuwa bado mashambani, kama vile mihogo na viazi. Mawakili wa walalamikiwa walidai kwama walalamikaji hawakustahili kupewa muda wa kuondosha mazao yaliyokuwa mashambani kwa sababu walalamikaji walipovamia mashamba hayo kulikuwa na mazao. Tume haikubaliani na hoja hiyo. Tume ina maoni kuwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, na kama zoezi lingefanyika kisheria, walalamikaji walipaswa kwanza kufidiwa mali zao zote ikiwa ni pamoja na mazao yaliyokuwa mashambani kabla ya kuondoshwa kama ilivyofanyika kwa watu walioondoshwa kutoka Hifadhini.

*Inaendelea >*

**2. Unyanyasaji, udhalilishaji na ukatili**

Walalamikaji wanadai kwamba wamefanyiwa vitendo vya unyanyasaji, udhalilishwaji na ukatili vikiwemo kuigwa, kujeruhiwa, kuteswa na hata kulazimishwa kuchoma nyumba zao wenyewe. Walalamikaji kadhaa walitoa maelezo kuhusu vitendo viovu walivyofanyiwa kwa mfano:-

Kabla tu na mara baada ya uondoshwaji walinyanyaswa, kukamatwa na kuwekwa ndani bila sababu za msingi na bila kufunguliwa mashitaka, kwa mfano:-

Rahel Range (SMJ. 70) alidai kuwa yeye na wenzake waliwekwa 'lock up' ndani ya stoo huko Rwamchanga kwa muda wa siku nne (4) kuanzia tarehe 12/10/2001.

Bugere Mwita (SMJ. 102) kilema wa miguu alisema kwamba alipigwa begani na Mlalamikiwa Na. 1 kwa kutumia kiboko, (aliionesha Tume kovu la kiboko) aliteswa, na magongo yake kuvunjwa na kuchomwa moto. Pia alieleza kuwa Mlalamikiwa Na. 1, baada ya kuchoma moto magogo yake alisema, tunanukuu:-

*"Wewe si unapenda kuishi hapa? Basi ishi hapa!"*

Ester Jackson (SMJ. 9) alieleza kwamba alipigwa na Walalamikiwa Na. 1 na Na. 2, na pia Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Benchugu. Katika tafrani hiyo aliangukia tumbo, akaburuzwa, akapigwa makofi, akapigwa mateke tumboni na kukanyagwa mgongoni. Shambulio hili lilimsababishia kupoteza ujauzito wa miezi sita (6) kesho yake tarehe 13/10/2001.

Bibi Nyamhanga Marwa (SMJ. 82), alieleza kwamba baada ya kukataa amri ya mlalamikiwa Na. 1 kumtaka achome nyumba yake mwenyewe, mlalamikiwa huyo alimpiga mpaka akazirai na kutokwa na haja ndogo.

Bhoke Mwita, (SMJ. 126) alieleza kwamba baada ya kukataa amri ya Mlalamikiwa Na. 1 ya kumtaka achome nyumba yake mwenyewe alipigwa na malalamikiwa huyo

Inaendelea >

mgongoni na sehemu nyingine za mwili kwa kutumia kiboko, na kuwa alizirai hadi saa 6:00 mchana. Aliendelea kueleza kwamba siku hiyo hakuweza kuondoka eneo hilo na kuwa yeye na mke wenzie aliyekuwa anamsaidia walilala kichakani hadi asubuhi ya kesho yake tarehe 13/10/2001 walipoondoka kwenda Mugumu.

Nchanga Magonera (SMJ. 125) alieleza kuwa siku ya tukio, baada ya yeye kuchomewa nyumba yake, aliamriwa na polisi kuingia ndani ya gari na akapelekwa Mugumu mjini na kukataliwa kumpa msaada mtoto wake kilema ambaye alikuwa anatembelea magoti na kulazimika kumuacha pale pale kwenye eneo la mgogoro. Mtoto huyo kilema aliokotwa porini baada ya siku tatu (3), na yeye mama kumpokea mtoto huyo siku ya nne (4).

Mwita Nsato (SMJ. 122) alieleza kwamba alipigwa na Mlalamikiwa Na. 2 kwa kutumia kiboko. Alieleza pia kuwa alipigwa teke karibu na kiuno na kuwa hadi siku ya kutoa ushahidi wake mbele ya Tume alikuwa bado anasikia maumivu. Alieleza kuwa alipigwa kwa sababu alikuwa anajaribu kuokoa maharage ili ayafiche kichakani. Baada ya hapo aliwekwa ndani ya gari na kupelekwa Mugumu ambako aliwekwa rumande, kwa siku hizo kumi na nane (18), hakuwahi kuoga, kupiga mswaki wala kubadili nguo.

Charles Nyamhanga, (SMJ. 31) alieleza kuwa kama saa 9 usiku mke wake mdogo alianza kuumwa na uchungu wa uzazi. Kama saa 11:30 walipotaka kumuweka kwenye baiskeli wampeleke hospitali wakasikia ngurumo za magari. Akamuona Mlalamikiwa Na. 1 na watu wengine. Shahidi na watu aliokuwa nao wakajificha kichakani kwenye kilima. Saa 4:00 asubuhi mkewe akajifungua. Saa 3:00 usiku wakateremka toka mlimani na wakatembea na kufika Mugumu mjini saa 8:00 usiku. Shahidi aliendelea kueleza kuwa wakati wote huo mkewe alikuwa hajapata chakula wala mtoto hakuweza kunyonya, pia mama huyo pamoja na mtoto hawakupata maji ya kuoga. Alieleza kuwa walipofika Mugumu iliwachukua muda mrefu kupata msaada kwa sababu watu walikuwa wanahofu kuchukuliwa hatua na Mlalamikiwa Na. 1 iwapo watawapa msaada watu wa Nyamuma. Mwishowe waliweza kupata maji ya moto na mzazi akaoga. Wakati huo mdomo wa mtoto ulikuwa umeshikamana ikabidi kumdondoshea

Inaendelea >

matone ya maji ya uvuguvugu mdomo na kuanza kuulainisha mdomo huo kufunguka kwa kutumia mikono yao. Hatimaye mtoto akaweza kutoa sauti ya kulia, na baadaye, baada ya juhudi za kumdondoshea maji ya uvuguvugu mdomoni kuendelea, na kumuogesha, akaweza kunyonya.

Wilson Korosso (SMJ 98) alieleza kuwa Mlalamikiwa Na. 1 alijulishwa kuwa yeye Wilson alikuwa mmojawapo wa wale waliofanya maasi Tarime na kuwa sasa anaanza tena kuichokonoa serikali. Aliendelea kueleza kuwa Mlalamikiwa Na. 1 alimwambia yeye mlalamikaji kuwa akileta tena chokochoko atamfanyia kama vile Iddi Amini alivyokuwa anawafanyia watu.

Mwita Mosoba, (SMJ, 56) alieleza kuwa amepata ulemavu wa vidole kwa kukata na mkuku na Mlalamikiwa Na. 1. Alieleza kuwa hakwenda kutibiwa hospitali kwa sababu alikwua amejificha msituni yeye na wenzake, na kwamba walipata habari baadaye kuwa Warenchoka hawatakiwi Mugumu mjini. Alieleza pia kuwa alishonwa kidonda na Ayubu Zablon kwa kutumia sindano ya kushonea nguo na nyuzi za chumvichumvi, na kwamba nyuzi zilichukua siku tisa (9) na ndipo akamuelekeza mkewe kuzitoa kwa kutumia (pliers).

**Uporaji**

Ibrahimu Korosso alieleza kuwa waligawana vitu vya nyumbani kwake, ng'ombe, kondoo, mbuzi na kuku, pia walichukua redio, baiskeli, vitanda, magodoro na vitu vingine vyote vya ndani. Aliendelea kueleza kuwa baada ya muda Mlalamikiwa Na. 1 alifika na kuwaambia askari wafanye haraka kuchukua vitu maana wao viongozi wanataka zoezi limalizike haraka.

Ryoba Ghati (SMJ, 33) alieleza kuwa Askari Lollet wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Ikorongo alifungulia ng'ombe na raia wengine wakafungulia mbuzi na kuwa mifugo hiyo iliswagwa kuelekea kwenye Zahanati CCM "Centre".

*Inaendelea >*

Marwa Chacha, (SMJ. 37) alieleza kuwa Paul Shanyangi alichoma nyumba, watu wengine walikuwa wanapora vitu vya nyumbani na kuwa viongozi waliokuwepo hawakuwakataza.

Chacha Nokwe, (SMJ. 37) alieleza kuwa Mlalamikiwa na. 1 aliwaambia watu wagawane vitu. Askari wakatoa paa na kugawana vitu ndani ya nyumba, na kuwa Mlalamikiwa Na. 1 akawauliza kama wamemaliza kuchukua vitu vyote ili wasichelewe kufanya kazi, wasije wakaunguzwa humo.

Juma Marwa, (SMJ. 29) alieleza kuwa walimleta ng'ombe wa Eliud Pius kwenye Zahanati CCM "Center" wakamchinja na kuwa Eliud alipouliza kwa nini wananchinja ng'ombe wake alinyamazishwa kwa kupigwa kiboko na polisi ili asipige kelele.

Eliud Pius, (SMJ. 8) alieleza kuwa alifungwa mikono kwa kamba na kupelekwa kwenye Kituo walalamikiwa walichokuwa wametenga kwenye zahanati. Aliendelea kueleza kuwa aliona makundi ya ng'ombe yakipita na kuwa mmoja alikuwa ni wa kwake, ambaye alichinjwa na nyama yake kugawiwa wananchi.

Walalamikaji wanasema kuwa kitendo cha kuwastusha na kuwakurupusha asubuhi na mapema tarehe 12/10/2001 kwa mingurumo ya magari, milio ya risasi na wingi wa waondoshaji kiliwatisha na kuwatia hofu kubwa.

Jonas Machage (SMJ. 8) amedai kuwekwa ndani kuanzia tarehe 4/10/2001 hadi tarehe 12/10/2001 saa kumi jioni bila kufunguliwa mashtaka.

Jackson Mwita (SMJ. 5) na Zablon Chabe (SMJ. 44) wamedai kuwa wamekuwa wakikamatwa, kuwekwa ndani na kuachiliwa mara kwa mara bila sababu za msingi na bila kufunguliwa mashitaka mahakamani.

Baada ya walalamikaji kuwasilisha lalamiko hili kwenye Tume Mlalamikiwa Na. 1, akihutubia mikutano ya hadhara kwa nyakati tofauti katika vijiji mbali mvali,

*Inaendelea >*

aliwatishia walalmikaji kwa kusema kwamba endapo walalamikaji hawatashinda katika shauri hili basi watafute kwa kwenda au wajichimbie. Taarifa ya vitisho ilifikishwa mbele ya Tume na walalamikaji wakiomba Tume ichukuwa hatua. Baada ya Tume kuridhika kwamba, kutokana na ushahidi wa pande zote mbili, vitisho hivyo vimethibitika, Tume katika maamuzi yake yaliyotolewa tarehe 31/01/2004 ilitoa amri kumkataza Mlalamikiwa Na. 1 kuendela na vitisho hivyo.

Walalamikiwa walikanusha kuwatendea walalamikaji vitendo kama vilivyotajwa kwa madai kwamba hawakuwepo watu katika eneo la mgogoro siku ya opereshi. Wanadai pia kwamba walichofanya siku hiyo ni kuondosha mahame katika sehemu hiyo kwa kuyachoma moto.

Mapema katika maamuzi haya Tume ilishatoa maoni kwamba walalamikaji walikuwepo katika eneo la tukio siku ya operesheni. Suala la kujiuliza sasa hivi ni kama walalamikaji walitendewa vitendo mbalimbali kama wanavyodai au hapana. Utetezi wa walalamikiwa ni kwamba hawakutenda vitendo hivyo kwa vile hapakuwa na watu katika eneo la mgogoro siku hiyo ya operesheni.

Kama ilivyooneshwa hapo awali katika maamuzi haya, walalamikiwa waliita Maafisa Watendaji wa vijiji sita (6) ambao walidai kuwapokea baadhi ya walalamikaji katika vijiji mali mbali. Hili ilikuwa ni kama jitihada za walalamikiwa kuonesha kwamba siku hiyo ya uondoshaji, watu wote, wakiwemo walalamikaji waliodaiwa kupokelewa, walikwishaondoka kutoka katika eneo la mgogoro. Walalamikiwa wametumia ushahidi wa maafisa watendaji hao kujaribu kuonesha kwamba baadhi ya walalamikaji na mali zao, ikiwemo mifugo, walipokelewa katika vijiji mbali mbali, hivyo kuimarisha hoja yao ya msingi kwamba siku ya hiyo ya operesheni mali za walalamikaji pia zilikuwa hazipo tena kwenye eneo la mgogoro, kwani zilikwishahamishwa.

Baada ya kuchambua ushahidi wa Maafisa watendaji hao sita Tume ilisema kuwa ushahidi huo ulikuwa na mapungufu kiasi cha kuifanya Tume ishindwe kuuamini na kuuegemea, hususan kulikuwa na udhaifu mkubwa pale maafisa hao walipodai

Inaendelea >

kuwapokea baadhi ya walalamikaji na mali zao hata kabla ya operesheni yenyewe kuanza. Kwa sababu zile zile zilizotolewa awali, na ambazo sio lazima kuzirudia, Tume inashindwa pia kuukubali ushahidi wa maafisa hao kuhusu suala hili.

Kuna ushahidi wa Mwita Rhobi (SMW. 18) ambaye sio Afisa Mtendaji bali ni mwanakijiji wa kawaida. Juyu alieleza kuwa wakati wa uchomaji alikuwa ameshikilia nafasi ya Mwenyekiti wa Kitongoji cha Komeka, Kijiji cha Bonchugu, kilichopakana na eneo la mgogoro. Alidai kuwa yeye alikuwa ni jirani wa Matiku Makuri (SMJ. 2) ambaye siku mbili kabla ya uchomaji alipeleka mifugo yake kwa shahidi kwa ajili ya kupatiwa hifadhi, ikiwa ni ng'ombe thelathini na wawili (32), mbuzi arobaini na sita (46) na kondoo ishirini (20). Aidha shahidi alisema kuwa alipata taarifa kwamba Matiku aliwekeza ng'ombe wengine kumi na wawili (12) kwa Joseph Kichambati (SMW.12) ambaye aliunga mkono ushahidi huu, na kwamba kwa usemi wa Mwita Rhobi, siku ya operesheni hapakuwa na mifugo yoyote iliyobaki kwenye mji wa Matiku.

Ni maoni ya Tume kwamba ushahidi huu pia sio wa kuaminika. Wakati Matiku akitoa ushahidi mbele ya Tume hakuulizwa ili aweza kukubali au kukanusha kuwekeza mifugo kwa Mwita Rhobi na Joseph Kichambati. Ushahidi kama huu wa Mwita Rhobi na Joseph Kichambati, ambao ni wa kushtukiza huwa hauna nguvu.

Isitoshe ushahidi wa Mwita Rhobi kwama siku ya operesheni hapakuwa na mifugo yoyote kwenye mji wa Matiku ulikuwa ni ushahidi wa kuambiwa tu, sio wa kuona. Cha zaidi ni kwamba Mwita Rhobi na Joseph Kichambati walikiri kuwa hawajui idadi ya mifugo aliyokuwa nayo Matiku. Kutokana na hilo hata kama ingekubalika kuwa Matiku amewekeza ng'ombe thelathini na wawili (32), mbuzi arobaini na sita (46) na kondoo ishirini (20) kwa Mwita Rhobi, na ng'ombe kumi na wawili (12) kwa Joseph Kichambati, haitoshi kuonesha kwamba Matiku hakubakiza mifugo na mali nyingine katika mji wake. Hizi ni dosari kubwa zinazodhoofisha ushahidi wa Mwita Rhobi na Joseph Kichambati kiasi kwamba Tume inashindwa kuukubali.

Inaendelea >

Msisitizo wa walalamikiwa ni kwamba siku hiyo ya operesheni hapakuwa na mali yoyote katika eneo la mgogoro ambayo ingeweza kutekelezwa au kuporwa. Tume imetafakari kwa makini ushahidi wa pande zote mbili kuhusu suala hilo. Katika kufanya hivyo Tume imekuwa na fursa ya kuwaona na kuwasikia mashahidi wa pande zote mbili wakitoa ushahidi wao. Katika tathmini yake Tume ina maoni kuwa kwa kiasi kikubwa walalamikiwa na mashahidi wao wamekuwa sio wa kweli, na kwamba ushahidi wa upande wa walalamikaji una uzito kuliko wa upande wa walalamikiwa. Na mashahidi wao wamekuwa sio wakweli, na kwamba ushahidi wa upande wa walalamikaji una uzito kuliko ule wa upande wa walalamikiwa. Kutokana na sababu hiyo Tume inaridhika kwamba walalamikaji, pamoja na mali zao, walikuwepo katika eneo la mgogoro siku ya operesheni, na kuwa walifanyiwa na walalamikiwa vitendo vya unyanyasaji, udhalilishaji, ukatili, uporaji, vitisho na pia kupewa notisi fupi ya uondoshwaji kinyume na sheia na taratibu zilizowekwa.

Vitendo hivi vinakiuka, pamoja na vipengele vingine, Ibara ya 12 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara), inayosema:-

> **" 12(2) Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake"**

Aidha vitendo hivi vinakiuka Ibara ya 5 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948), na Ibara ya 7 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ya mwaka 1966 zinazoweka masharti kama yaliyomo kwenye Katiba yetu.

**4. Haki ya Kumiliki mali.**

Walalamikaji katika ushahidi wao wanadai kwamba walalamikiwa na washirika wao walichoma nyumba, mgahala na mazizi. Baadhi ya vifaa vya ndani villibwa na vingine viliteketezwa. Baadhi ya vyakula vilivyokuwa kwenye maghala viliporwa na vingine kuteketezwa, na mifugo iliporwa. Aidha, vitu vingine vya thamani kama vile mashine ya kukoboa na kusagisha nafaka, majembe ya kukokotwa na wanayama, baiskeli na redio viliporwa na mabati yaliezuliwa, na mengine yalikuwa yamehifadhiwa pia

Inaendelea >

yaliporwa. Mazao yote ya muda mfupi, na yale ya kudumu yaliachwa mashambani. Kwa ujumla walalamikaji wanadai kwamba katika kuondoshwa kwao hawakuwahi kusalimisha mali zozote.

Walalamikiwa katika kukanusha madai haya walishikilia kwamba siku ya operesheni hakukuwa na ama watu, au mali yoyote kwenye eneo la tukio na kwamba walichochoma ni mahame tu. Katika kutilia mkazo hoja hii walidai kwamba tarehe 11/10/2001 viongozi wa ngazi ya Wilaya walitembelea eneo husika na kubaini kuwa wakazi wote walishaondoka na kuwa waliondoka na mali zao. Waliendelea kudai kwamb akwa misingi hiyo hakukuwa na mali yoyote ambayo ingeweza kuporwa au kuchomwa.

Mapemba katika maamuzi haya Tume imeeleza kuhusu kuridhika kwake kwamba walalamikaji walikuwa kwenye eneo la mgogoro mpaka siku ile ya operesheni. Hoja ya walalamikiwa kwamba siku hiyo ya operesheni hakukuwepo na mali zozote ambazo zingewez kuchomwa au kuporwa hain msingi. Hii ni kutokana na hoja kwamba kwa kuwa siku hiyo ya operesheni walalamikaji walikuwepo, na wazi kwamba walikuwa na mali zao pale, na hasa ikizingatiwa kwamba baadhi yao walikuwa wameshi katika eneo hili kwa kipindi kirefu.

Ni maoni ya Tume kwamba upande wa walalamikiwa hawasemi ukweli kuhusu suala hili. Kumekuwepo na jitihada za kutaka kuficha ukweli wa mambo, kwa mfano, kama ilivyoshaoneshwa mapama katika maamuzi haya, Mhe. Muhamed Seif Khatib (Mbunge), aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati huo, alitembelea eneo la tukio. Katika taarifa yake ya ziara hiyo alikanusha kuwepo kwa uchomaji katika eneo hilo. Akijibu barua ya Mhe. Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, Mhe. Waziri katika barua yake Kumbu. Na. HAC. 112/09/B/20 ya tarehe 15/2/2002 alisema, tunanukuu:-

> ***"Tuhuma kwamba, katika Kijiji cha Bonchugu nyumba 250 zilichomwa moto na watu 500 hawana chakula wala makazi, imebainika kuwa siyo ya kweli.***

*Inaendelea >*

***Uchunguzi unaonesha katika kijiji hicho hakuna nyumba zilizochomwa wala hakuna watu wanaokabiliwa na njaa wala kukosa makazi.***

***Aidha uchunguzi umeonesha kuwa katika kijiji jirani cha Nyamuma, nyumba zilivunjwa mwaka juzi (2000) kwa kuwa nyumba hizo zilikuwa ndani ya eneo la Hifadhi ya Taifa kinyume cha sheria".***

Hii inashangaza kwa sababu Mlalamikiwa Na. 1 katika ushahidi wake mbele ya Tume alisema kwamba alimuonesha Mheshimiwa Waziri wa eneo lililohusika na uchomaji, ambalo ndilo eneo la mgogoro. Alipoulizwa ni kwa nini ushahidi wake unapingana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye jambo hili, alijibu, "Aulizwe yeye". Jibu hili linashangaza hasa ikizingatiwa kwamba Mlalamikaji Na. 1 ndiye aliyeongoza msafara wakati Mhe. Waziri alipotembelea eneo lililochomwa. Suala la kujiuliza ni kwamba kama Mlalamikiwa Na. 1 alimuonesha Mhe. Waziri eneo lililohusika na uchomaji, iweje Mhe. Waziri aseme kwamba hakukuwepo na uchomaji katika eneo hilo, hasa ikizingatiwa kwamba Jopo pamojana wakili wa pande zote mbili walipokagua eneo hili tarehe 04/09/2003 waliona kuwa kulikuwa na uchomaji uliokuwa umefanyika!

Isitoshe Tume na mawakili wa pande zote mbili walipotembelea eneo hilo tarehe iliyotajwa, uongozi wa serikali ngazi ay kijiji, ukiongozwa na Bw. Samweli makena (SMJ. 8), Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Bonchugu, ulikanusha kuwepo uchomaji katika eneo hilo. Kiongozi huyu wakati akiuongoza msafara huo kwenye ukaguzi wake, alidiriki kuuelekeza kwenye maeneo ambayo hayakuhusika na uchomaji. Jitihada hizi ziligonga mwamba baada ya baadhi ya walalamikaji waliokuwa wameongozana na Tume kuingilia kati na kuiambia Tume kwamba Afisa huyo alikuwa antaka kuielekeza Tuem kwenye maeneo yasiyohusika. Baada ya kustuliwa huko ndipo Afisa Mtenaji huyo, kwa shingo upande, akaanza kuiongoza Tume kuelekea kweney maeneo sahihi. Hata hivyo katika kutekeleza zoezi hilo ushirikano wake ulikwua hafifu sana. Hata watu ambao Tume iliwakuta kwenye eneo hilo, ambao waligawiwa eneo hio baada ya walaalmikaji kuondolewa, walikanusha kuwepo kwa uchomaji katika eneo hilo japokuwa uchomaji ulifanyika kabla ya wao kuhamai katika eneo husika. Ni maoni ya

Inaendelea >

Tume kwamba hizi zilikuwa ni jitihada endelevu za kutaka kuficha ukweli wa mambo zilizopeleka walalamikwia kukanusha kuwepo kwa mali zozote katika eneo la mgogoro wakati wa operesheni, pia kuficha ukweli wa matukio yaliyojiri tarehe 12/10/2001.

Baada ya kuwaona na kuwasikiliza mashahidi wa pande zote mbili wakitoa maelezo yao mbele ya Tume, Tume inaamini ushahidi wa upande wa walalamikaji na kuona kwamba siku ya operesheni mali za walalamikaji zilikuwepo kwenye eneo hilo na kuwa zilichomwa na nyingine kuporwa. Pamoja na mali zilizochomwa au kuporwa wlalamikaji walilazimika kuacha mali zao zisizohamishika kama vile mazao yaliyokuwa mashamani yakijumuisha mihogo, viazi, miti ya matund ana ya biashara katika eneo la tukio.

Kitendo cha kuwakosesha walalamikaji mali zao, kama ushahidi unavyoonesha, ni kukiuka haki ya walalmaikaji ya kumiliki mali bila kunyang'anywa mali hiyo na mtu yeyote kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 24(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara), tunanukuu:-

> ***"24(1) Bila ya kuathiri masharti ya sheria za nchi zinazohusika, kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi kwa mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria.***
>
> ***(2) Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1) ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisah au madhumuni mengineyo bila idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili".***

Aidha kitendo hicho kinakiuka Ibara ya 17(1) & (2) ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948) (kama kinavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza) inasema:-

> ***"17-(1) Everyone has the right to own property alone as well as with others.***
>
> ***(2) No one shall be arbitrarily deprived of his property".***

*Inaendelea >*

Vipengele hivi vya Katiba na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la (1948) linaweka sharti la kulipa fidia kwa watu ambao mali zao zimetwaliwa. Kuhusu masuala ya ardhi, Sheria ya kutwaa ardhi ya mwaka 1967, kifungu cha 11, kinaweka sharti la kulipa fidia inayostahili pale serikali inapotwaa ardhi kwa manufaa ya umma.

Kwa kuwa Tume hii sio miongoni mwa vyombo vilivyopewa mamlaka ya kushughulikia masuala yanayohusu migogoro ya ardhi, Tume haitaendelea kushughulikia suala la walalamikaji kunyimwa haki ya kumiliki ardhi. Kitendo cha kuwakosesha wananchi ardhi ni suala la mgogoro wa ardhi ambalo, kama lilivyooneshwa awali, linastahili kushughulikiwa na mamlaka husika. Kuhusu zile mali nyingine za walalamikaji, Tume inaridhika kwamba walikuwa na haki ya kumiliki mali hizo na kwamba kwa kukoseshwa haki yao hiyo wamenyimwa haki yao ya binadamu.

5. Haki ya kuishi katika mazingira na maisha bora.
6. Walalamikaji, katika ushahidi wao, wameeleza kwamba baada ya kuondoshwa kutoka kwenye eneo la mgogoro wamekuwa wakiishi maisha duni. Hawana makazi maalum, hivyo wanaishi kwa kutangatanga na kubabaisha. Hawana shughuli maalum ya kuwaingizia kipato, hivyo hawana uwezo wa kujenga ama kupata nyumb zenye kukidhi mahitaji yao, ikiwa ni pamoja nakupata lishe bora. Baadhi ya waliohamia Mugumu ambako wachache kati yao walibahatika kupata hifadhi kutoka kwa ndugu na jamaa, wakati wengine walihangaika bila ya kupata makazi kwa ajili ya familia zao au waliishi kwa msongamano katika vyumba vidogo vya kupanga. Wengine hawakuwa na uwezo wa kupanga nyumba au kujipatia chakula kwa urahisi, kwa mfano; Mtongoji Nenga (SM.J. 52) ambaye aliieleza Tume kuhusu ugumu unaomkabili, alisema:-

   " ***Maisha yangu kwa sasa ni ya shida sana. Ninaishi kwa kufanya vibarua tu ambayo vinapatikana kwa shida. Nikikosa vibarua nauza mwili wangu ili niweze kulisha watoto. Sasa hivi sina uhakika na mwili wangu, inawezekana nina virusi vya ukimwi, jambo ambalo linanipa wasi wasi kwa afya ya mwili wangu***".

Inaendelea >

Tatizo la ugumu wa maisha linakuzwa zaidi na ukweli kwamba jamii ya walalamikaji ina desturi ya kuwa na familia yenye mke zaidi ya mmoja na watoto wengi kwa mfano:-

Gati Range Mwita (SMJ. 124) alieleza kuwa yeye na wake zake wawili na watoto saba (7) huishi na kulala chumba kimoja.

Gisire Magoro (SMJ. 111) alieleza kuwa yeye na wake zake wawili na watoto wanane (8) huishi katika chumba kimoja.

Mwita Nsato (SMJ. 122) alieleza kuwa yeye na wake zake watatu na watoto wanane (8) huishi katika chumba kimoja.

Marasi Mendo (SMJ. 92) alieleza kuwa yeye na watoto wake tisa (9) huishi katika chumba kimoja.

Patrisi Marwa (SMJ. 94) alieleza kuwa yeye na wake zake watatu na watoto wanane (8) huishi katika chumba kimoja.

Hali hii inawasononesha sana walalamikaji hasa ikizingatiwa kuwa awali, kabla ya kuondoshwa na kulazimika kwenda Mugumu mjini, walikuwa na nyumba zilizokuwa zinatosheleza mahitaji ya familia zao.

Kitendo cha kuwaondosha walalamikaji kwa nguvu kutoka kwenye makazi yao na kuwatumbukiza katika mazingira ya maisha duni ya kuishi kwa kutangatanga na familia zao, na bila uwezo wa kujipatia mahitaji yao ya msingi, ilikuwa ni kuwanyima haki yao ya binadamu ya kuishi maisha bora, haki ya kupata makazi bora na haki ya kupata lishe bora.

*Inaendelea >*

**Haki ya faragha na mtu kukaa na familia yake.**

Ushahidi uliotolewa mbele ya Tume unaonesha kwamba operesheni ay kuwaondosha walalamikaji na familia zao ilisababisha familia nying kusambaratika, kwa mfano:-

Wilson Korosso (SMJ. 28) aliieleza Tume kwamba wakati zoezi hilo linaendelea familia yake ilitawanyika na kusababisha yeye kupotelewa na mke ajulikanaye kama Eshter Wilson pamoja na motto mmoja aliyekuwa akinyonya, ambao mpaka siku ya mwisho ya kusikilizwa shauri hili tarehe 25/10/2004 walikuwa hwajapatikana.

Simon Omare (SMJ. 29) aliieleza Tume kwamba baada ya zoezi hilo kufanyika familia yake ilitawanyika na kumsababishia kupotelewa na mkewe na watoto wadogo, ambao pia walikuwa hawajapatikana hadi siku ya mwisho ya kusikilizwa shauri hili.

Aidha operesheni hiyo ilifanyika kwa namna ambayo iliingilia faragha ya walalamikaji na familia zao. Ushahidi wa upande wa walalamikaji uliotolewa mbele ya Tume umedhihirisha kwamba walalamikaji wengi, pamoja na familia zao, waliamshwa na kukurupushwa alfajiri na mapema wakati wakiwa bado wamelala.

Tatizo hili waliendelea nalo hata huku waliokwenda, kwa mfano Mugumu mjini. Kama ilivyokwishaoneshwa, baadhi ya walalamikaji, ambao kila mmoja ana zaidi ya mke mmoja, wanaishi kwenye chumba kimoja kimoja pamoja na watoto wao wa jinsia tofauti na wa umri tofauti. Ushahidi ambao Tume inaukubali unaonesha kwamba walalamikaji wamevunjiwa haki yao ya faragha na ya kujumuika na familia zao, na pia haki ya unyumba, kama ilivyowekwa na Ibara ya 16 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara), inayosema:-

*Inaendelea >*

*"16 (1) Kila mtu anastahili kusheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, Maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi".*

Aidha vitendo vya walalamikiwa viliwakosesha walalamikaji haki hii vilikiuka Ibara ya 16(3) ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la (1948) na Ibara ya 17(1) & (2) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966 zinazoweka masharti kama yale ya ibara ya 16 ya Katiba ya nchi yetu.

7. Haki ya kutendewa haki na vyombo vya dola

Vitendo vya walalamikiwa vinakiuka haki ya msingi ya walalamikaji kama ilivyoainishwa chini ya Ibara 13(6)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kikifafanuliwa na Vifungu vya 32 na 23 vya Sheria ya Menendo wa Jinai ya mwaka 1985. Ibara a 13(6)(a) ya Katiba hiyo inasema:-

"13-(16) Kwa madhumuni ya kuhakikisha uswaa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba:-

(a) ……………………………………

(b) ……………………………………

(c) ……………………………………

(d) Kwa ajili ya kuhifadhi haki ya uswa wa binadamu, heshima ya mtu itakuzwa katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshajui wa mambo ya jinai na katika shughuli nyinginezo ambazo mtu anakuwa chini ya ulinzi bila uhuru, au katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu;

(e) Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhamu zinazomtweza au kumdhalikusha:

Kifungu 32 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai katika ufafanuzi wa sheria hii kinawataka polisi kumfungulia mashtaka mtuhumiwa katika mahakama yenye mamlaka kabla

Inaendelea >

haujapita muda wa saa ishirini na nne (24) tangu kukamatwa, hasa katika makosa madogo. Nacho kifungu Na. 23(1) cha sheria hiyo hiyo kinamlazimisha Afisa wa Polisi au mtu yeyote anayemkamata mtuhumiwa kumweleza mtuhumiwa huyo kosa alilotuhumiwa kutenda na sababu za kukamatwa kwake kwa mujibu wa kipengele hiki. Kuna maeneo machache ambayo mtu anayemkamata mtuhumiwa halazimiki kumweleza sababu za kumkamata, lakini walalamikaji waliokamatwa katika shauri hili hawakuangukia katika maeneo hayo.

Aidha vitendo walivyofanyiwa walalamikaji vinakiuka baadhi ya mikataba ya kimataifa kuhusu haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia, kwa mfano, Ibara ya 9 ya tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 inapiga marufuki mtu yeyote kukamatwa bila kuwepo sababu za msingi. Ibara hiyo inafafanua kwamba ni marufuku mtu yeyote kutiwa nguvuni au kuhamishwa nchini kimabavu au bila kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa. Ibara hiyo (kama inavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza), inasema:-

*"9 – no one shall be subjected to arbitrary arrest, detention or exile"*.

Ibara ya 9 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa nayo inaweka masharti yanayofanana na haya, (akama inavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza), kwa kusema:-

" 1) Everyone has the right to liberty and security of person. No one shall be subjected to arbitrary arrest or detention. No one shall be deprived of his liberty except on such grounds and in accordance with such procedures as are established by law.

2) Everyone who is arrested shall be informed, at the time of arrest, of the reasons for his arrest and shall be promptly informed of any charges against him.

3) Any one arrested or detained on a criminal charge shall be brought promptly before a judge or other officer authorized by law to exercise judicial power and shall be entitled to trial within a reasonable time or to realize. ………..."

Inaendelea >

**8. Haki ya kupata elimu**

Baadhi ya walalamikaji walidai kwamba watoto wao walishindwa kuendelea na masomo ay elimu ay msingi kutokana na amri ay Mlalamikiwa Na. 1 kwa walimu wakuu wa shule zote za msingi Wilayani Serengeti ya kuwakataza kuwapokea watoto hao katika shule zao.

Dai hili lilipingwa na Mlalamikiwa Na. 1 Tume kwa upande wake inashindwa kupokea ushahidi huu kwa sababu haukuungwa mkono. Hakuna mwalimu mkuu hata mmoja aliyeitwa mbele ya Tume kueleza kuwa alipewa amri kama hiyo na mlalamikiwa na. 1. Hata hivyo awali katika maamuzi haya, Tume imeona kwamba wakati wa kuwaondosha walalamikaji hakuna taratibu zilizowekwa za kuwahamisha watoto wao kutoka kwenye shule walizokuwa wanasoma. Walalamikaji na watoto wao walikurupushwa tu na hwakuelezwa kwamb anahamia wapi, hivyo hakukuwa na uwezekano wa wazazi kushughulikia suala al uhamisho wa watoto wao. Katika hali hii ni vigumu kuona jinsi gani ambavyo watoto wangeweza kupokelewa kwenye shule mpya wakati wakiwa hawana nyaraka za uhamisho.

Aidha ushahidi wa walalamikaji unaonesha kwamba hata kama watoto wao wangekuwa na nyaraka za uhamisho wasingeweza kuwahudumia watoto hao kimasomo katika hizo shule mpya, kama vile kuwanunulia vitabu, daftari na sare za shule kutokana na hali zao kuwa duni kimapato. Tume ina maoni kwamba kutokana na hali hii baadhi ya watoto wameathirika kielimu. Huu ni ukiukwaji wa Ibara ya 28 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto inayosema:-

***" 28.1 Nchi zilizosaini Mkataba huu zinatambua haki ya mtoto kupata elimu na kwa lengo la kufanikisha haki hii hatua kama hatua kwa msingi wa haki sawa kwa sawa, hasa zinazotekeleza yafuatayo:-***

***(a) Kufanya elimu ya msingi kuwa ni ya lazima na itatolewa bure kwa wote.***

***(b) Kuhimiza uanzishaji wa mafunzo mbali mbali ya elimu ya sekondari ikiwa ni pamoja na elimu ya jumla na mafunzo ya ujuzi, ili kila mtoto aweza kujiunga na kuchukua hatua zinazofaa kama vile uanzishaji wa elimu ya bure na kutoa msaada wa fedha pale unapohitajika".***

Inaendelea >

Sharti la ibara hii limefafanuliwa na Kifungu Na. 57 cha Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 ambaheo kinasisitiza, miongoni mwa mambo mengine, kwamba kila mtoto ana haki ya elimu. Sharti hili limezidi kutiliwa mkazo na Kanuni Na. 4(2) ya Kanuni za Shule za Msingi (Uandikishwaji na Mahudhurio ya Lazima) za mwaka 2002 zilizotungwa chini ya kifungo Na. 35(4) cha Sheria ya Elimu ya mwaka 1978. (Kama inavyosemeka kwa lugha ya Kiingereza), Kanuni hiyo inasema:-

> ***" 4. –(1) Any parent to whom these Rules apply, who falls to enroll his child commits an offence and is liable on conviction, in the case of a first offence to a fine not less than thirty thousand shillings and not exceeding fifty thousand shillings or for a second offence, to a fine not less than fifty thousand shillings but not exceeding one hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding six months or to both such fine and imprisonment.***
>
> ***(2) Any parent or any other person in any circumstance who causes a child not to attend school regularly until the completion of primary education commits an offence and is liable on conviction to a fine of not less than thirty thousand shillings but not exceeding fifty thousand shillins or a term of imprisonment not exceeding six months or to both such fine and imprisonment".***

Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) ni marufuku kwa mzazi au mtu yeyote na ni kosa la jinai kwa mzazi au mtu yeyote kumzuia kwenda au kusababisha mtoto kutokwenda shule kwa sababu yoyote kable ya kumaliza elimu ya msingi. Kanuni hiyo pia inatoa adhabu ya kifungo au faini au vyote kwa pamoja kwa mtu anaypatikana na hatia ya kukiuka kanuni hii.

Mlalamikiwa Na. 1 kwa kuondosha au kusimamia uondoshwaji wa walalamikaji kutoka katika eneo la mgogoro alisababisha, na amekuwa akisababisha watoto kadhaa wa walalamikaji kutohudhuria masomo yao ya shule ya msingi kama ilivyoelezwa hapo awali. Kitendo hiki kinakiuka kanuni Na. 4(2) kama ilivyonukuliwa.

Inaendelea >

**9. Haki ya makazi na uraia**

Kama iliyoeneshwa hapo awali katika maamuzi haya ushahidi uliotolewa mbele ya Tume, na ambao haukupingwa, unaonesha kwamba walalamikaji ohi raia wa Tanzania, hivyo madai ya walalamikiwa kwamba baadhi ya walalamikaji walikuwa ni raia wa Kenya, na kwamba waliondolea kutoka kwenye eneo la mgogoro kwa sababu hiyo ilikuwa ni ukiukwaji wa haki yao ya msingi ya uraia.

Ibara ya 17(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema:-

> ***"Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kwenda, kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhruri ya Muungano."***

Haki hii inatambulika pia chini ya Iara ya 15 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 (kama inavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza) inayosema:-

"No one shall be arbitrary deprived fo his nationality no denied the right to change his nationality".

Kwa upande mwingine Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 inasema kwamba, mtu anayeweza kunyang'anywa uraia wa Tanzania ni yule ambaye alipewa uraia kwa kuomba, baada ya kuwa amekiuka masharti mbalimbali yaliyotajwa na sheria hiyo.

Kifungu cha 14 cha Sheria hiyo (kama kinavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza) kinasema:-

***" 14. The Minister 9responsible for Home Affairs) may by order deprive any person, other than a person who is a citizen by birth, of his citizenship of the United Republic if the Minister is satisfifed that that person has at any time while a citizen of the United Republic and of full age and capacity voluntarily claimed and exercised, in a foregn country, any right available to him under the law of that country, being a right accorded exclusively to its own citizens, and that it is not conducive to the public good that he should continue to be a citizen of the United Republic".***

Inaendelea >

Walalamikaji sio raia waliopewa uraia kwa kuomba na wameeleza kwamba wao ni raia wa kuzaliwa kwa maana kwamba mama na baba zao wamezaliwa Tanzania na wazazi wa wazazi hawa vile vile walizaliwa Tanzania kabla ya uhuru 1961. Chini ya kifungu hiki hata Waziri hana uwezo wa kuwanyang'anya uraia walalamikaji, uraia amboa ni wa kuzaliwa.

Ni maoni ya Tume kuwa hata kama wangekuwa ni raia wa Kenya utaratibu uliotumika kuwaondosha na kuwatelekea bila mali zao wala huduma za kibinadamu, kama vile chakula na maji na huduma za kiafya (medical and sanitary facilities) ulikuwa ni uvunjaji wa haki zao za binadamu.

**10. Haki ya walalamikaji kutohamishwa kwa nguvu kutoka kwenye makazi yao halali (forced eviction)**

Kutokana na ushahidi ulioko mbele ya Tume, Tume imetosheka kwamba walalamikiwa na washiriki wao waliowaondosha walalamikaji kutoka kwenye eneo la mgogoro na kwamba uondoshaji huo ulitekelezwa kikatili na kwa nguvu kubwa. Baadhi ya walalamikaji walikuwa wamekalia maeneo haya kwa muda mrefu na walikuwa na mali zao za kutosha kukdhi mahitaji yao, lakini waliondoshwa bila kupewa fursa ya kuchukua mali zao. Waliondoka wakiwa fukara. Waliondoshwa bila kujulishwa waende wapi. Walijikuta ni wakimbizi nchini mwao. Kitendo cha kuwaondosha na kuwasababishia hali hii ni kinyume na Ibara ya 15 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema:-

*"15 – (1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru.*

*(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu:-*

*(a) Katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, au*

*(b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai".*

Inaendelea >

**11. Haki ya usawa dhidi ya ubaguzi.**

Ushahidi uliotolewa mbele ya Tume na mashahidi wa upande wa walalamikaji unadhihirisha kwamba vitendo vilivyofanywa na Walalamikiwa Na. 1 na 2 na washiriki wao dhidi ya walaalmikaji vilikuwa vya kibaguzi. Ushahidi huo, amboa Tuem imeukubali, unaonesha kwamba ubaguzi huo ulitokana na sababu kwamba walalamikaji wanatoka katika koo za Warenchoka wakati wakazi wa maeneo ya vijiji vya Rwamchanga na Bonchugu wanatoka katika koo za Wanaybasi na waikoma.

Kihistoria koo za Arenchoka na Zile za Waikoma zina uhasama na ugomvi wa mara kwa mara. Ushahidi unaonesha kwamba walalamikiwa, kama viongozi wa Serikali ngazi ay Wilaya, walikuwa na upendeleo kwa Waikoma dhidi ya Warenchoka, kwa mfano, wakati wa tukio la kuwaondosha wakazi wa kitongoji cha Nyangube (Mara Cop) mnamo mwanzoni mwa mwaka 2000 kwa madai kwamba walivamia ardhi ya Rwamchanga, Mlalamikiwa Na. 1 aliwaamuru wananchi wenye asili ya Waikoma kutoka Rwamchanga kubomoa nyumba za Warenchoka waliokuwa wakiishi katika kitongoji hicho. Hali hii ilichochea uhasama na ndiyo ilikuwa chimbuko la mgogoro wa baadaye katika eneo la mgogoro. Aidha karibu na mwishoni mwa mwaka huo huo wa 2000 Mlalamikiwa Na. 1 aliamuru baadhi ya warenchoka kukusanywa na kupelekwa mpakani mwa Kenya na Tanzania kwa madai kwamba wao sio raia wa Tanzania. Watu hao walirejeshwa nchini baada ya Serikali ya Kency kuona kwamba hawakuwa raia wa Kenya.

Akiunga mkono ushahidi huo wa upande wa walalamikaji, Paul Shanyangi, (SMW. 3) akiwa pia Muikoma, ambaye ni Katibu Tarafa wa Tarefa ya Rogoro, aliieleza Tume kwamba wakati anahamia katika Kata ya Ikoma, wakati huo akiwa Katibu Kata mwaka 1992, alikuta mgogoro katika eneo hilo kati ya wakazi wa kijiji cha Rwamchanga na baadhi ya watu walioeleweka waliokuwa wamevamia eneo hilo, (yaani Warenchoka). Alipotakiwa na Tume aeleze ni hatua gani alichukua baada ya kuona kuwa kuna mgogoro, alisema:-

Inaendelea >

"Tuliwaarifu wanakijiji wa Rwamchanga waende wakawahamishe hawa wavamizi (walalamikaji) kwa nguvu kwa sababu walikuwa wamejenga kwenye mashamba ya watu wa Rwanchanga, na waliwahamisha kwa kubomoa vibanda vyao mwaka 1992".

Japokuwa Paul Shanyangi (SMW. 3) alikuwa akielezea mgogoro wa mwaka 1992, huu ulikuwa ni mgogoro uliohusu suala lile lile na watu wale wale, ambao baada ya kufukuzwa eneo la Nyanguge (Mara Cop), baadhi yao walihamia Nyamuma, ambalo ndilo eneo la mgogoro. Baada ya baadhi ya walalamikaji kuhamia Nyamuma, mgogoro huo uliendelea na ulikuja kufikia kilele chake katika matukio ya tarehe 12/10/2001, wakati huo mgogoro ukimhusisha Mlalamikiwa Na. 1 na viongozi wengine wa ngazi ya Wilaya, Tarafa na Kata.

Ubaguzi huu uliendelezwa na Mlalamikiwa Na. 1 hata baada ya tukio la uondoshaji, kwa mfano, Edward Ryoba (SMJ 76) katika ushahidi wake alisema kwamba tarehe 6/10/2003 katika Kata ya Nyaisho Wilaya ya serengeti, mlalamikiwa na. 1 alidiriki kutamka hadharani kuwa "Wale Warenchoka nitaendelea kuwatesa mmoja mmoja mpaka waishe". Aliendela kusema, "Kesi yenu mnayojidanganya mnaendesha, mkishindwa mjichimbie".

Aidha, shahidi mwingine, Mwita Nyamhanga (SMJ. 106), alisema kuwa wakati Mlalamikiwa Na. 1 alipokuwa anahutubia wananchi wa Machochwe alisema, "Watu wanaojidai kunishtaki kwenye Katume ka Haki za Binadamu, mimi sitasimama kizimbani hata siku moja. Na kale Katume hakana uwezo wa kunifanya lolote kwa sababu mimi mtu aliyeniletea hapa ni Rais tu na ndiye anayejua kazi ninayoifanya kwa hakika. Nikishinda kesi Warenchoka nitawahamisha katika Wilaya hii kwa sababu wao ni Wakenya.

C. Kama ilikuwa halali kuwakamata na kuwanyang'anya vifaa na picha watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

Inaendelea >

Katika suala hili ushahidi wa upande wa walalamikaji ulitolewa na Kaleb Gamaya (SMJ. 11) na Clement Mashamba (SMJ. 12) wote wakiwa watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Dar es Salaam. Wameeleza kwamba taarifa ya uchomaji ilipowasilishwa Kituon kwao walisafiri kwend Wilaya ya Serengeti ili kujionea hali halisi. Walipofika Mugumu Wilayani Serengeti waliongozwa kwenda kwenye eneo la tukio na baadhi ay walalamikaji. Wakati wakikagua eneo lililochombw aalikamatwa na askari wa wanayamapori wakapelekwa Kituo cha Polisi Mugumu. Askari wa wanaymapori waliwaeleza kwamba kukamatwa kwao kulitokana na amri ya Mlalamikiwa Na. 1 kwamba ni marufuku kwa mtu kutembelea eneo lililochomwa bila idhini yake. Aidha walipofikishwa Polisi waliambiwa kwamba kukamatwa kwao kunatokana na amri ay Mlalamikiwa Na. 1 na kwamba kutokana na amri hiyo watapelekwa wkake kwa kuhojiwa. Kabla ya kupelekwa kwa Mlalamikiwa n. 1 walipekuliwa na vifaa vyao vya kazi vilishikiliwa. Vifaa hivyo ni 'still camera" na mkanda wake, "video camera' na mikana miwili ya picha za kawaida.

Walipofikishwa kwa Mlalamikiwa na. 1 walihojiwa kuhusu ujio wao katika maeneo hayo na walijibi kwamba wao ni watafiti kutoka Kituo cah Sheria na Haki za Binadamu na kuwa wamekwenda kufuatilia tukio hili lililoripotiwa kituoni kwao na walalamikaji. Baada ya kuhojiwa kwa kirefu kwa siku mbili au tatu kuhusu suala hili, Mlalamikiwa Na. 1 alielekeza Polisi kuwapeleka kwa Mkuu wa Wilaya ya Tarime kuhojiwa zaidi kwa sababu walipita huko kufanya utafiti kabla ya kuingia wilaya ya Serengeti. Huko Tarime, baada ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Bwana Pachal Mabiti kuangalia picha zilizoko kwenye mikanda yao na kuona kuwa hakukuwa na madhara yoyote alieleza waachiliwe. Walalamikaji waliachiliwa na kurejeshewa vifaa vyao isipokuwa mkanda wa "video" na mikanda miwili ya picha za kawaida ambavyo vilibaki mikononi mwa Polisi Mugumu hadi leo hii. Walalamikaji hawa walikuwa chini ya ulinzi wa Polisi kwa muda wa siku tano (5) na kuachiliwa siku ya sita (6).

Utetezi wa walalamikia ni kwamba walalamikaji hawa walikamatwa, na vifaa vyao kuzuiliwa kwa sababu waliingia ndani ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Ikorongo bila kibali. Waliendelea kueleza kwamba vifaa vya walalamikaji vinaendelea kuzuiwa kwa

*Inaendelea >*

sababu suala hili liko kwa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa (Reginal Crime Officer – RCO) na kuwa upelelezi unaendelea.

Utetezi huu wa walalamikiwa una udhaifu katika maeneo makuu mawili. Kwanza uteteizhuu unaegemea ushahidi wa kuambiwa. Walalamikaji wote wawili wameeleza katika ushahidi wao kwamba walifahamishwa na askari wa Wanyamapori waliowakamata, na pia askari polisi ambao walikabidhiwa walalamikaji hao baada ya kukamatwa, kwamba walalamikaji walikamatwa wakiwa ndani ya eneo la Hifadhi. Hakuna askari wa wanyamapori wala askari polisi aliyehusika na tukio hili aliyeitwa kutoa ushahidi mbele ya Tume kudhibitisha usemi huu. Hivyo ushahidi wao ni wa kusikia tu "hear say evidence" ambao unakatazwa chini ya Vifungu 61 na 62 vya Sheria ya Ushahidi Na. 6 ya mwaka 1967. Hiyo pekee ni sababu tosha kuukataa ushahidi wa walalamikiwa, lakini kuna sababu ya ziada, nayo ni kwamba ushahidi wa Mlalamikiwa Na. 1 umejikanganya.

Maelezo yake mbele ya Tume kwamba walamikaji walikamatwa eneo la Hifadhi unapingana na maelezo yake ya awali aliyotuma kwenye Tume kwamba walalamikaji walikamatwa kwa kuwa hawakujitambulisha kwa watendaji ngazi ya Wilaya, Tarafa Kata au Kijiji. Maelezo haya yako kwenye barua yake kwa Tume yenye Kumbu. Na. CA.20/7/161 ya tarehe 12/01/2003. Katika barua hiyo mlalamikiwa hakusema lolote kuhusu walalamikaji kukutwa ndani ya hifadhi. Iwapo sababu hii ingekuwa ni ya kweli ingejitokeza mapema iwezekanavyo wakati mlalamikiwa alipokuwa anaandika barua hii. Kuleta maelezo haya wakati huu kunaibua hisia kwamba ushahidi huu ni wa kutunga. Kwa sababu hizi mbili Tume inaukataa utetezi wa walalamikiwa kwamba walalamikaji walikamatwa ndani ya hifadhi.

Hata yale maelezo ya awali ya Mlalamikiwa Na. 1 kwamba watafiti walalamikaji hawakujitambulisha kwa watendaji ngazi ya Wilaya, Tarafa, kata au Kijiji sio sababu ya kuwakamata kwa sababu kutokujitambuisha huko si kosa chini ya sheria yoyote ya nchi.

*Inaendelea >*

Mjumbe mmoja wa Jopo, Kamishna Catherine Harrieth Mbelwa Kivanda ana maoni tofauti (Dissenting opinion) ambayo tayasoma. Maoni yake ni kwamba haikuwa sahihi kwa watafiti hawa kuingia wilayani Serengeti kufanya kazi ayo bila kujitambulisha kwa watendaji, kinyume na taratibu za serikali. Maoni ya wajumbe wawili waliobaki ni kwamba Tume hakikuwa inasikiiza shitaka dhidi ya watafiti kuingia Serengeti kinyume na taratibu za serikali kwa sababu walalamikaji hawakushitakwia kwa tuhuma hiyo. Aidha Tume haikupokea ushahidi kuhusu taratibu hizo za serikali zinazosemekana zilikiukwa. Hata kama watafiti walikiuka taratibu za serikali kuna njia za kushughulikia ukiukwaji huo kama vile kuwachukulia hatua za kinidhamu, lakini haikuwa ni sababu ya kuwav unjia haki zao za binadamu chini ya Katiba kwa kuwakamata na kuwaweka chini ya ulinzi wa polisi wka siku tano (5) na kuwanyang'anya vifaa vyao vya kazi, ambalo ndilo suala lililoko mbele ya Tume.

Kama Malalamikiwa Na. 1 mwenyewe alivyosema suala la walalamikaji kujitambulisha ilikuwa ni kwa manufaa yao wenyewe, kwa mfano kama wangepatikana na mkasa au jambo lolote lile serikali iwe in ahabari zao na ikibidi kuwatolea taarifa, lakini alikiri kwamba kujitambulisha huko ilikiwa sio lazima. Kwa missing hiyo hapakuwa na sababu yeyote kisheria ya kuwaweka walalamikaji chini ya ulinzi wa polisi kwa siku tano (5) na kuzuia vifaa vyo vya kazi kwa sababu wahakuwa wamevunja sheria yoyote ya nchi. Kuwazuia walalamikaji na kuchukua vifaa vyao kulivunja haki ya msingi ya uhuru wa mtu kwenda atakako kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 15 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia ambyo inasema:-

"15 – (1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru. Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamtwa, kufungwa, kuwekwa kuzuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo isipokuwa:-

(a) Katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, au

(b) Katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai".

Inaendelea >

Aidha vitendo hivyo vya walalamikiwa vilikiuka ibara ya 9(1) na (2) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa 1966 (kama inavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza), inasema:-

***"Article 9 – 1) Every one has the right to liberty and scurity of person. No one shall be subjected to artibrary arrest or detention. No one shall be deprived of his liberty except on such grounds and in accordance with such procedures as are established by law.***

***2) Every one who is arrested shall be informed, at the time of arrest of the reasons for his arrest and shall be promptly informed of any charges against him".***

Walalamikiwa katika utetezi wao wamedai kwamba kwa sasa luala la walalamikaji liko mikononi mwa Polisi ambapo upelelezi unaendelea. Ni muda mrefu sana, takribani miaka mitatu (3), tangu walalamikaji walipotiwa msukosuko. Mpaka leo hawajafiksihwa mbele ya mahakama wala kufunguliwa shitaka lolote, na hadi sasa vifaa vyao vya kazi vimeshikiliwa. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa ibara ndogo ya (3) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (kama inavyosomeka kwa lugha ya Kiingereza), inayosema:-

***3) " Any one arrested or detained on a criminal change shall be brought promptly before a judge or other officer authorized by law to exercise judicial power and shall be entitled to trial within a reasonable time or to realize ………………………."***

***(e&f) Kama walioondolewa walikuwa ni wakazi halali wa Kijiji cha Nyamuma iliyobaki au CCM "Centre"/Kama kulikuwa na uhalali wa Kijiji cha Nyamuma iliyobaki au kilikuwa na hadhi gani.***

Ushahidi uliopo mbele ya Tume unaonesha kwamba walalamikaji walianza kuhamia eneo la mgogoro kuanzia mwaka 1986 na kuendelea. Walilikalia eneo hili likiwa ni sehemu ya Kijiji cha Rwamchanga mpaka mwaka 1993. Mwaka huo kijiji cha Nyamuma kilisajiliwa rasmi na kupewa namba ya usajili. Usajili huu ulihalalisha kuwepo kwa Kijiji cha Nyamuma. Mwaka 1994 mpaka wa Hifadhi ya Wanyamapori ya Ikorongo ulipanuliwa au

*Inaendelea >*

kumega sehemu kubwa ay kijiji cha Nyamuma na kubakiza hili eneo la mgogoro lililokuwa na kaya 37. Kutokana na idadi ndogo ya kaya, ambazo hazikutosheleza kuunda kijiji, eneo hili ambalo ni sehemu ya kilichokuwa kijiji halali cha Nyamuma, lilikabidhiwa kijiji cha Bonchugu kiutawala mwaka 2000 na likaendelea kuwa chini ya Bonchugu mpaka siku ya tukio, kwa maana hiyo kuwepo kwa eneo hili kulikiwa ni halali. Kutokana na uhalali huo wakazi wa eneo hili la mgogoro walikuwa ni wakazi halali.

**vii. Kama kweli uongozi wa serikali ngazi ya Wilaya na mawakala wake walitumia vibaya mamlaka waliyopewa na sheria.**

Hiki ni kiini cha ziada ambacho hakikuorodheshwa hapo awali, lakini ambacho walalamikaji wamependekeza Tume ikishughulikie kwa sababu kimejitokeza wakati shauri linasikilizwa.

Tume imetafakari kwa makini kiini hiki na kubaini kwamba hoja zake, kama zilivyoainishwa, isipokuwa hoja ya vitendo vya rushwa zimekwisha zingatiwa wakati tume ikitafakari vile viini ilivyoainishwa awali. Kujadili kiini hiki sasa itakuwa ni marudio.

**Vitendo vya rushwa**

Kutokana na ushahidi uliopokelewa na Tume kuna madai kwamba baadhi ya watendaji wa Serikali wamejihusisha na vitendo vya rushwa. Kwa kuwa suala hili linahitaji uchunguzi wa kina wa kujitegemea Tume italielekeza kwenye Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU), ambayo ndiyo yenye mamlaka kisheria kuchunguza masuala haya, ambako Tuem inaamini itashughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

**Udhaifu wa ushahidi wa walalamikiwa**

Walalamikaji wametoa hoja kwamba mashahidi wa walalamikiwa sio wa kuaminika, na kwamba kutoaminika huko kunadhihirika wazi wazi katika mtiririko wa utetezi wao tangu mwanzo wa shauri hili mpaka mwingo, na kuwa unapingana, hivyo unastahili kutotiliwa maanani na kutupiliwa mbali.

Inaendelea >

kumega sehemu kubwa ay kijiji cha Nyamuma na kubakiza hili eneo la mgogoro lililokuwa na kaya 37. Kutokana na idadi ndogo ya kaya, ambazo hazikutosheleza kuunda kijiji, eneo hili ambalo ni sehemu ya kilichokuwa kijiji halali cha Nyamuma, lilikabidhiwa kijiji cha Bonchugu kiutawala mwaka 2000 na likaendelea kuwa chini ya Bonchugu mpaka siku ya tukio, kwa maana hiyo kuwepo kwa eneo hili kulikiwa ni halali. Kutokana na uhalali huo wakazi wa eneo hili la mgogoro walikuwa ni wakazi halali.

**vii. Kama kweli uongozi wa serikali ngazi ya Wilaya na mawakala wake walitumia vibaya mamlaka waliyopewa na sheria.**

Hiki ni kiini cha ziada ambacho hakikuorodheshwa hapo awali, lakini ambacho walalamikaji wamependekeza Tume ikishughulikie kwa sababu kimejitokeza wakati shauri linasikilizwa.

Tume imetafakari kwa makini kiini hiki na kubaini kwamba hoja zake, kama zilivyoainishwa, isipokuwa hoja ya vitendo vya rushwa zimekwisha zingatiwa wakati tume ikitafakari vile viini ilivyoainishwa awali. Kujadili kiini hiki sasa itakuwa ni marudio.

**Vitendo vya rushwa**

Kutokana na ushahidi uliopokelewa na Tume kuna madai kwamba baadhi ya watendaji wa Serikali wamejihusisha na vitendo vya rushwa. Kwa kuwa suala hili linahitaji uchunguzi wa kina wa kujitegemea Tume italielekeza kwenye Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU), ambayo ndiyo yenye mamlaka kisheria kuchunguza masuala haya, ambako Tuem inaamini itashughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

**Udhaifu wa ushahidi wa walalamikiwa**

Walalamikaji wametoa hoja kwamba mashahidi wa walalamikiwa sio wa kuaminika, na kwamba kutoaminika huko kunadhihirika wazi wazi katika mtiririko wa utetezi wao tangu mwanzo wa shauri hili mpaka mwisho, na kuwa unapingana, hivyo unastahili kutotiliwa maanani na kutupiliwa mbali.

*Inaendelea >*

mgogoro, ni maoni ya Tume kwamba kutokana na mapendekezo kwenye (a) (ii) hapo juu, suala hili sasa limepitwa na wakati. Suala hili hapo awali liliwasilishwa serikalini kwa barua ya Tume yenye Kumbu. Na. HBUB/S/1032/2001/2002/MARA/65 ya tarehe 28/10/2003 ambayo haikujibiwa. Kinachotakiwa sasa ni utatuzi wa kudumu wa suala hili.

c) Kwa kuwa imethibitika kwamba wakati wa uondoshwaji walalamikaji waliokuwepo, pamoja na malai zao ambazo ziliteketezwa au kuporwa, walalamikaji wana haki ya msingi ya kulipwa fidia ya mali zoa hizo, kama walioomba, hasa ikizingatiwa kwamba walalamikiwa hawakuleta ushahidi kupinga thamani ya mali hizo. Mali hizo walizoainisha katika vielelezo walivyowasilisha mbele ya Tume kama sehemu ya ushahidi wao, na Tume imevitumia kuyatayarisha jedwali lililoambatishwa na maamuzi haya.

d) Kwa kuwa imethibitika kwamba kutokana na vitendo vya walalamikiwa, walalamikaji wametumbukizwa katika lindi la uduni wa maisha, walalamikaji wanastahili misaada ya kibinadamu na ya dharura kabla hawajaweza kurejea kwenye hali ya kawaida ya maisha yao. Tume inapendekeza kwamba Serikali itoe misaada ya kibinadamu kama vile chakula, madwa na elimu kwa watoto kama ilivyoaninishwa katika barua ya Tume kwa Serikali yenye Kumbu. Na. HBUB/S/1032/2001/2002/MARA ya tarehe 28/10/2003 hadi hapo walalamikaji watakaporejea katika hali ya kawaida ay maisha yao.

e). Kwa kuwa imethibitika kwamba kumekuwepo na vitendo vilivyokuwa vinakiuka haki za binadamu dhidi ya walalamikaji kama vile unyanyasaji, udhalilishaji, ubaguzi, mateso na vitisho, Tume inatoa amri kukomesha kabisa vitendo hivi.

f) Kwa kuwa imethibitika kuwa walalamikaji Kaleb Gamaya (SMJ. 11) na Clement Mashamba (SM.J. 12) walishikiliwa na Polisi na kunyang'anywa mikanda ya picha, lakini wakaachiliwa bila kufunguliwa shitaka lolote, na kuwa vifaa vyao hivyo vinaendelea kushikiliwa na Polisi kwa madi kwamba upelelezi unaoendelea, Tume inaelekeza kwamba Polisi waharakishe upelelezi wao ili hatma ya suala hili ifahamike.

*Inaendelea >*

g) Kwa kuwa Tume hii haina mamlaka ya kuchunguza suala la ardhi, Tume inashauri kuwa walalamikaji watafute msaada mahala pengine ili waweze kupeleka suala hili mahakamani kwa ajili ya kuomba nafuu wanazoona wanastahili.

h) Tume inapendekeza kwamba walaalmikaji wafuatao walipwe kifuta machozi kutokana na vipigo walivyopata ambavyo vilikuwa vikali sana au ambavyo viiwasababishia majeraha:-

- Ester Jackson (SMJ. 9) aliepata vipigo vilivyomsababishia kupoteza ujauzito wa miezi sita (6). Mlalamikaji huyu pia arejeshewe shilingi elfu saba na mia nne (7,400/=) zikiwa ni gharama zake za matibabu.
- Bugere Mwita (SM. J. 102) kilema wa miguu aliyepigwa kiboko begani na kumsababishia jeraha, pia afidiwe magongo yake ya kutembelea yaliyochomwa.
- Bibi Nyamhanga Marwa (SM. J. 82) aliyepigwa kiboko mpaka akazirai na kutokwa haja ndogo.
- Bhoke Mwita (SM. 126) aliyepigwa kiboko akazirai toka asubuhi hadi saa 6:00 mchana.
- Mwita Nsato (SM. J. 122) aliyepigwa kiunoni na kusababishiwa maumizi aliyokuwa nao mpaka wakati wa kutoa ushahidi mbele ya Tume.
- Mwita Masoha (SMJ. 56) aliyepata ulemavu wa vidole kwa kukatwa na mkuki na mlalakikiwa Na. 1.

Kwa mujibu wa kivungu 28 –(2) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Serikali katika ngazi zote inapewa muda wa miezi mitatu (3) kuanzia leo tarehe 13/12/2004 kuleta taarifa kwenye Tume kuhusu utekelezaji wa maamuzi haya.

**ANGALIZO:**
Walalamikaji Wilson Korosso (SMJ. 28) na Simon Omare (SMJ. 29) walieleza kwenye ushahidi wao kwamba walipotelewa na jamaa zao na kwamba hadi tarehe 25/10/2004 wakati usikilizaji wa shauri hili ulipomalizika, jamaa hao walikuwa hawajapatikana. Endapo watu hao hadi sasa hawajapatikana, Tume inaelekeza kwamba Polisi iendelee na

*Inaendelea >*

juhudi za kuwatafuta. Wakati huo huo mawasiliano kati ya Tume, Polisi na waliopotelewa na ndugu hao yaendelea kuhusu suala hili.

……………………………………………………………

Mh. Robert H. Kisanga (Jaji Mstaafu) – Mwenyekiti

……………………………………………………………

Mhe. Catherine Harrieth Mbelwa Kivanda – Kamishna

……………………………………………………………

Bw. Sabbas Basil Tetti – Afisa Uchunguzi Mkuu 1

Dar es Salaam

13/12/2004

Inaendelea >

## MAONI BINAFSI YA KUTOKUBALIANA NA HOJA KUWA ILIKUWA NI SAHIHI KWA WATAFITI KUTOKA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU, DAR ES SALAAM, KUTOTOA TAARIFA KWA UONGOZI WALIPOINGIA KIKAZI WILAYANI SERENGETI – (DISSENTING OPINION)

Mimi Catherine Harrieth Mbelwa Kivanda, Kamishna na mjumbe wa jopo la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Tume) lililosikiliza hadharani (public hearing) shauri Na. HBUB/S/1032/03/Mara ambalo ni lalamiko lililowasilishwa Tume na Ibrahim Korosso na wenzake 134, (Walalamikaji Na. 1) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, (Walalamikaji Na. 2), dhidi ya Thomas Loy Sahaya, Mkuu wa Wilaya ya Serengeti (Mlalamikiwa Na. 1), Alexander Pantaleo Lyimo, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti, (Mlalamikiwa Na. 2), na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Mlalamikiwa Na. 3), nina maoni binafsi (dissenting opinion) kuhusu suala la kama ilikuwa ni sahihi au si sahihi kwa Kaleb Lameck Gamaya (SMJ. 11) Clement Julius Mashamba (SMJ 13), watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kuingia Wilayani Serengeti na kufanya kazi ya kufuatilia tukio la uchomaji nyumba za wakazi wa lililokuwa eneo la Nyamuma iliyobaki hapo tarehe 12/10/2001 bila kutoa taarifa Wilayani humo kwa uongozi ngazi ya wilaya, au Tarafa, au Kata, au Kijiji.

Maoni yangu mimi binafsi ni kwamba watafiti hao, pamoja na kwamba kisheria hawakutenda kosa la jinai, lakini haikuwa sahihi kwao kuingia Wilayani Serengeti (au katika Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata au Kijiji chochote nchini, kwa hilo, (for that matter), na kuanza kufanya kazi ya uchunguzi au kazi nyingine yoyote ile iliyo rasmi, (official), bila kutoa taarifa kwa kiongozi wa ngazi yoyote ile. Maoni yangu pia ni kuwa pamoja na kwamba Tume haikuwa inasikiliza shitaka dhidi ya watafiti kuingia Wilaya ya Serengeti kinyume cha taratibu za Serikali, na kwamba hawakushitakiwa kwa tuhuma hiyo, lakini ni muhimu kuzungumzia dosari (anomally) iliyojitokeza kuhusu jinsi walivyoingia Wilaya ya Serengeti. Hoja hii siyo ngeni kwao kwa sababu hata wakati wa kusikiliza shauri lililokuwa mbele ya Tume waliuliza kuhusu dosari hii na wakaitolea maelezo.

*Inaendelea >*

Wakati wa kusikiliza shauri hili watafiti hao, walipohojiwa na jopo, walieleza kuwa walikuwa na hati ya utambulisho kutoka ofisini kwao iliyokuwa imeandikwa "KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA" ikieleza kuwa wao ni watafiti kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Dar es Salam waliokuwa wanafanya utafiti kuhusu mbuga za wanyama na hali ya mazingira ya vijiji/maeneo yanayozunguka mbuga hizo. Katika maelezo yao watafiti hao hawakueleza kuwa hati hiyo ya utambulisho ilieleza pia kuwa walitakiwa kufanya uchunguzi kuhusu uchomaji nyumba katika lililokuwa eneo la Nyamuma iliyobaki. Hati hiyo ya utambulisho haikutolewa kama kielelezo mbele ya jopo. Waliendelea kueleza kuwa utafiti wao uliamzia Wilaya ya Tarime na kuwa huko walitoa taarifa kwa viongozi wa ngazi toafauti katika maeneo waliyokuwa wanafanyia utafiti katika maeneo ya vijijini.

Katika mahojiano kuhusu kuingia kwao Wilaya ya Serengeti walieleza kuwa hawakuweza kutoa taarifa kwa uongozi wa ngazi yeyote ile kwa sababu walifika huko majira ya siku za mapumziko za sikukuu ya Krismasi. Walieleza pia kuwa walikwenda huko kufuatilia/kufanya uchunguzi kuhusiana na lalam, iko lililokuwa limewasilishwa Kituo cha Sheria an Haki za Binadamu na Iberahim Korosso na wenzake 134 (Walalamikaji Na. 1), la kuchomewa nyumba zao katika eneo la Nyamuma iliyobaki, Wilaya ya Serengeti. Uchunguzi huu, kwa maoni yangu ulikuwa kinyume nay ale waliyoeleza kuwa yaliandikwa katika hati ya utambulisho, "KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA" waliyokuwa wametayarishiwa ofisini kwao ambayo haikuzunguma lolote kuhusu kufuatilia suala la eneo la Nyamuma iliyobaki. Ni vigumu pia kwangu kukubali maelezo kuwa hawakutoa taarifa kweney uongozi ngazi yoyote kwa madai kwamba ilikuwa wakti wa mapumziko ya sikukuu ya Krismasi, hasa ikizingatiwa kuwa walitiwa msukosuko kuanzia tarehe 01/01/2002 ikiwa ni siku ya sita (6) baada ya mapumziko ya Krismasi kumalizika hapo tarehe 26/12/2001. Hii ina maana kuwa walikuwa na muda mrefu wa kuweza kutoa taarifa kwa uongozi ngazi mbalimbali kabla ya kuanza ufuatiliaji wao.

Katika majadiliano wakati shauri linasikilizwa na wakati wa kutayarisha maamuzi ya jopo, wajumbe wenzangu walikuwa na hoja zifuatazo wakati nikitofautiana nao katika suala hili, ambazo ni vema nizieleze, kwamba:-

Inaendelea >

- Ilikuwa sahihi kwa watafiti kutotoa taarifa kwa sababu Wilaya ya Serengeti siyo nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya na kwamba hata yeye Mkuu wa Wilaya, katika utetezi wake mbele ya jopo, alisema kuwa haikuwa lazima watafiti kutoa taarifa kwa uongozi walipoingia wilayani humo.

- Wangetoa taarifa wangekataliwa kwenda kufanya uchunguzi, hivyo Tume isingepata taarifa ya yale yaliyokuwa yamejiri kule Nyamuma iliyobaki.

- Hawakuvunja sheria yoyote ya nchi na kwamba hata kama upo utaratibu wa kumtaka mtu atoe taarifa kwa uongozi anapoingia Wilayani utaratibu huo siyo sheria.

Kwa maoni yangu hoja hizo siziafiki kwa sababu zifuatazo:-

- Wilaya ya Serengeti ni "Nyumbani" kwa Mkuu wa Wilaya (kama vile ambavyo katika wilaya nyingine zote Wakuu wa Wilaya ni "majumbani" kwao, hali kadhalika kwa Wakuu wa Mikoa kwa mikoa yao au kiongozi wa nchi kwa nchi yake). Kiongozi yoyote anapopewa eneo la nchi kusimamia kiutawala inakuwa ni "nyumbani" kwake kwa maana kwamba linakuwa chini ya mamlaka yake, hivyo mtu yeyote anapoingia huko kikazi utaratibu, heshima na maadili ya kazi yanamhitajia " abishe hodi" kama vile ilivyo muhimu kiutaratibu, kiheshima na kimaadili kubisha hodi mtu anapoingia nyumbani kwa mtu mwingine. Kutoa taarifa/kujitambulisha kwa uongozi katika ngazi tofauti za ngazi ya Serikali inayohusika wakati mtu anapoingia katika eneo husika kikazi ni moja ya misingi ya uendeshaji/usimamiaji bora wa shughuli za serikali, (best practices fo the government administrative machinery).

Katika kuzingatia umuhimu huu hata jopo la Tume lilitoa taarifa na kwenda kujitambulisha ofisini kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, pia ofisini kwa Mkuu wa Wialya ya Serengeti wakati wa kufanya uchunguzi wa suala la eneo la iliyokuwa Nyamuma iliyobaki pamoja na kwamba jopo lilikuwa linamchunguza Mkuu huyo wa Wilaya. Suala la kuwa hata yeye Mkuu wa Wilaya alisema, wakati akitoa utetezi wake mbele ya jopo la Tume, kuwa

*Inaendelea >*

haikuwa lazima kwa watafiti husika kutoa taarifa, izingtiwe kuwa katika maelezo yake kwa Tume, katika barua yake yenye Kumbu. Na. CA. 20/7/161 ya tarehe 12/01/2003 alieleza kuwa watafiti husika walikamatwa kwa sababu hawakuwa wametoa taaria ya kuwepo kwao kwa uongozi ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata au Kijiji. Maelezo yake haya yanapingana na yale aliyotoa kwa mdodo mbele ya jopo. Katika hali kama hii ni maoni yangu kuwa maelezo aliyotoa kimaandishi yana nguvu zaidi kwa sababu bila shaka aliyapata kutokana na ushauri wa wataalamu wake wanaojua taratibu za mienendo ya shughuli za Serikali.

- Wangetoa taarifa kwa uongozi na kukataliwa kwenda kufanya uchunguzi ingelipa uzito zaidi lalamiko la kuchomwa nyumba huko Nyamuma iliyobaki maana umma wa Tanzania, na ulimwengu kwa ujumla, ungelizipata habarihizo na kujiuliza, "kulikuoni? Mbona Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, alishatoa taarifa ya tukio la uchomaji nyumbani serikalini, lingetoa msukumo zaidi kwa Tume, na labda vyombo vingine pia, kuchukua hatua za haraka kulichunguza suala hili. Watafiti kutotoa taarifa ni kuingia kinyemela katika eneo la mamlaka ya utawala wa Wilaya husika. Suala la kujiuliza ni kuwa, katika zama hizi za uwazi na ukweli, ni kwa nini waingiea kinyemelanyemela, kimafichomaficho? Jibu la harakaharaka ni kwamba ilifanywa hivyo kwa makusudi Fulani mahsusi na kwa nia mbaya, (by intention and in bad faith).

- Inawezekana kwamba hawakuvunja sheria yeyote ya nchi, lakini, kama nilivyoeleza wali, ni taratibu kisheria kwa mgeni yeyote anapoingia nchini, mkoani, wilayani, tarafani, katika Kata au kijiji kikazi kutoa taarifa kwa uongozi wa sehemu husika. Watafiti husika walitumwa kufanya kazi na Shirika lisilokuwa la Kiserikali lililosajiliwa na Serikali ambalo linapaswa kujua taratibu za Serikali, kuziheshimu, kuzifuata an kuwaelimisha wale wanaowatuma kufanya kazi zao kuhusu umuhimu wa kufuata taratibu hizo. Jambo la kuheshimu na kufuata utaratibu ni mojawapo ya misingi na taratibu zinazosimamia utawala bora ambao Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ina wajibu wa kuzisimamia, kuzitetea na kuuelimisha umma kuhusiana nazo. Ni wazi kwamba Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinajua haya na ndiyo maana kikawatayarishia watafiti wake hati ya huko kuchunguza matukio ya uchomaji moto nyumba katika eneo la Nyamuma iliyobaki ilikuwa

Inaendelea >

kinyume na taratibu, maadili na heshima kwa uongozi, kinyume na kanuni za utawala bora na kinyume na misingi ya utawala bora.

Catherine Harrieth Mbelwa Kivanda

**KAMISHNA NA MJUMBE WA JOPO**

**TUME HA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Inaendelea >

**JEDWALI LA WALALAMIKAJI NA JUMLA YA FEDHA/MALI INAYODAIWA KUCHOMWA/KUPORWA/KUBAKI MASHAMANI WAKATI WA OPERESHENI TAREHE 12/10/2001 – SEHEMU YA NYAMUMA ILIYOBAKI**

| SMJ NA | JINA LA MLALAMIKAJI | KIELELEZO LJ NA. | JUMLA YA MADAI |
|---|---|---|---|
| 1. | Emmanuel B. Mwita | 1A | 45,763,000.00 |
| 2. | Matiku Makuri | 4 | 60,609,100.00 |
| 3. | (Angalia SMJ. 30) | - | |
| 4. | Ibrahim C. Korosso | 5A | 34,358,800.00 |
| 5. | Jackson Mwita | 13(1) | 45,079,960.00 |
| 7. | Paulo Joseph Sogita | 20 | 9,507,000.00 |
| 8. | Jonas Machage | - | - |
| 9. | Esther Jackson (Angalia SMJ. 5) | - | - |
| 13. | Eliud Pius Imwamu | 31 | 14.455,000.00 |
| 14. | Emmanuel G. Pius | 36 | 27,034,000.00 |
| | " " (Kanisa) | 37 | 12,131,000.00 |
| 15. | Thomas Gati Chacha | 41 | 16,410,500.00 |
| 16. | Kahama Laban Makuri | 38 | 10,781,500.00 |
| 17. | Chacha Itara | 38A | 9,211,000.00 |
| 18. | James Chacha Gentanyi | 39 | 36,563,000.00 |
| 19. | Daniel Marwa Mwita | 40 | 4,485,000.00 |
| 20. | Werema Itara | 44 | 3,939,400.00 |
| 21. | Chacha Mwita | 42 | 8,416,600.00 |
| 22. | Marwa Kehai | 43 | 3,698,000.00 |
| 23. | Weikama Mahende | 45 | 1,423,000.00 |
| 24. | Mwikwale Chacha (Ghati Gichele) | 46 | 3,556,500.00 |
| 25. | Bugando Mwita | 47 | 4,478,000.00 |
| 26. | Mutundi Mwita | 48 | 5,656,500.00 |
| 27 | Nsato Marwa | 49 | 987,000.00 |
| 28 | Wilson Korosso | 50 | 14,634,600.00 |
| 29. | Saimon Omare | 51 | 4,143,500.00 |

*Inaendelea >*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30. | Sofia Chacha Nokwe (Nokwe Mwita) | 52 | 9,021,400.00 |
| 31. | Charles Nyamhanga | 54 | 8,730,000.00 |
| 32. | Helena Ramadhani | 55 | 1,986,700.00 |
| 33. | Ryoba Gati Kogecha | 56 | 5,772,000.00 |
| 34. | Robert Bhoke | 57 | 2,595,999.00 |
| 35. | Imwamu Pius | 58 | 4,323,000.00 |
| 36. | Bhoke Itara | 59 | 11,098,000.00 |
| 37. | Marwa Chacha Makemba | 60 | 17,659,400.00 |
| 38. | Joseph Gentanyi | 61 | 7,428,800.00 |
| 39. | Sospeter M. Wantora | 62 | 2,180,000.00 |
| 40. | Pius Imwamu | 63 | 3,355,500.00 |
| 41. | Joseph Keroko | 64 | 7,020,000.00 |
| 42. | Mwikwabe Mabeche | 65 | 3,846,200.00 |
| 43. | Mahemba Kerongo | 66 | 4,739,000.00 |
| 44. | Zabron Chahe Kengare | 67 | 11,940,550.00 |
| 45. | Kirindo Makere Mudogo | 70 | 8,685,100.00 |
| 46. | Francis Mwita | 71 | 16,593,700.00 |
| 47. | Mwita Nokwe | 72 | 2,488,500.00 |
| 48. | Ryoba Nyanokwe | 73 | 3,755,000.00 |
| 49 | Bhoke Mwita Chacha | 74 | 3,734,500.00 |
| 50. | Chacha G. Masengwe | 75 | 2,716,500.00 |
| 51. | Mgosi Kemano | 76 | 1,197,100.00 |
| 52. | Mtongori Mnenga | 77 | 2,778,999.00 |
| 53. | Juma Marwa | 78 | 4,281,000.00 |
| 54. | Samwel Marko Marwa | 79 | 41,063,050.00 |
| 55. | Johanes Makenye | 80 | 5,959,000.00 |
| 56. | Mwita Musoba | 81 | 6,904,000.00 |
| 131. | Ryoba Mwita Ikungu | 160 | 2,947,500.00 |
| 132. | Monika Joseph (Angalia SMJ. 38) | | |
| **JUMLA** | | | **890,523,950.00** |

### 4.6 Mapendekezo ya Tume

Tume kama uamuzi wake unavyoonyesha hapo juu ilishughulikia malalamiko kwa misingi ya haki za binadamu na haki zilizovunjwa na kukiukwa. Iliangalia;

i). Haki ya makazi na uraia;
ii). Haki ya elimu;
iii). Haki ya kumiliki mali;
iv). Haki ya kuishi katika mazingira na maisha bora;
v). Haki ya kutohamishwa kwa nguvu toka maeneo yao;
vi). Haki ya faragha na mtu kukaa na familia yake;
vii.) Haki ya kutendewa haki na vyombo vya dola; na
viii). Haki ya usawa dhidi ya ubaguzi.

Baada ya kuzichambua haki hizo, Tume ilijielekeza katika malalamiko na kutoa uamuzi iwapo walalamikaji wanastahili nafuu walizoziomba na kisha kutoa mapendekezo kwa serikali.

1) Tume ilibaini kuwa Nyamuma Iliyobaki ni sehemu ya kijiji halali cha Nyamuma kilichosajiliwa na msajili wa vijiji mwaka 1993 na kwamba walalamikaji walikuwa ni wakazi halali wa maeneo hayo. Aidha Tume iliridhika kuwa operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu walalamikaji na kuwachomea nyumba zao katika eneo hilo la Nyamuma Iliyobaki ilifanyika kinyume cha sheria na kinyume cha haki za binadamu na ilikiuka misingi na kanuni za utawala bora. Hivyo Tume ilikubaliana na walalamikaji kuwa walikuwa wakazi halali wa eneo hilo la mgogoro lililokuwa awali sehemu ya kijiji cha Nyamuma na baadaye kukabidhiwa Kijiji cha Bonchugu. Kwa mantiki hiyo walalamikaji wana haki ya msingi ya kurejeshwa katika maeneo yao kama walivyoomba. Tume ilipendekeza kuwa Serikali ya Kijiji cha Bonchugu na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti iwarudishe walalamikaji kwenye maeneo yao haraka iwezekanavyo.

2) Tume ilithibitisha kuwa walalamikaji walikuwepo wakati wa uondoshwaji katika eneo lao na mali zao ziliteketezwa au kuporwa hivyo walalamikaji wana haki ya msingi kulipwa fidia ya mali zao hizo kama walivyoomba.

3) Tume ilithibitisha kuwa walalamikaji wametumbukizwa katika lindi la uduni wa maisha hivyo walistahili misaada ya kibinadamu na ya dharura kabla hawajarejea kwenye hali ya kawaida ya maisha yao. Tume Ilipendekeza kwa serikali kutoa misaada ya kibinadamu kama vile chakula, madawa na elimu kwa watoto hadi hapo walalamikaji watakaporejea katika hali ya kawaida ya maisha yao.

4) Tume ilithibitisha uwepo wa vitendo vilivyokiuka haki za binadamu kama vile unyanyasaji, udhalilishaji, ubaguzi, mateso na vitisho. Tume ikatoa amri ya kukomesha kabisa vitendo kama hivyo.

5) Tume ilithibitisha kuwa walalamikaji Kaleb Gamaya na Clement Mashamba (waliokuwa maafisa wa LHRC) walishikiliwa na Polisi na kunyang'anywa mikanda ya picha, na kuachiliwa bila kufunguliwa mashtaka na vifaa vyao vinaendelea kushikiliwa na polisi, Tume ilielekeza polisi waharakishe upelelezi wao ili kuhitimisha suala hilo.

6) Tume ilipendekeza walalamikaji kadhaa wapate kifuta machozi kutokana na vipigo walivyopata ambavyo vilikuwa vikali sana au viliwasababishia majeraha, hawa ni wafuatao:

   a) Ester Jackson aliyepata vipigo hadi kupeteza uja uzito wake wa miezi sita.
   Huyu alitakiwa arejeshewe shilingi 7,400 ambazo zilikuwa gharama za matibabu;

   b) Bugere Mwita ambaye ni mlemavu wa mguu alipigwa kiboko begani na kusababishiwa jeraha. Huyu afidiwe magongo yale yaliyochomwa moto;

c) Bibi Nyamhanga Marwa aliyepigwa kiboko mpaka akazirai na kutokwa na haja ndogo;

d) Bhoke Mwita aliyepigwa akazirai kuanzia asubuhi hadi saa sita mchana;

e) Mwita Nsato aliyepigwa kiunoni na kusababishiwa maumivu aliyokuwa nayo hadi wakati wa kutoa ushahidi mbele ya Tume;

f) Tume ilitoa Angalizo la watu waliopoteana na ndugu zao ambao hadi tarehe 25/10/2004 walikuwa hawajapatikana. Tume ilielekeza polisi iendelee na juhudi za kuwatafuta huku mawasiliano yakiendelea kati ya Tume, polisi na ndugu waliopotelewa na ndugu zao.

7) Tume ilipendekeza mamlaka zinazohusika ziwachukulie hatua wale wote waliosababisha vitendo vile vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mapendekezo ya Tume yalipokelewa kwa shangwe na wote wapenda haki. Tume ilijijengea heshima kubwa kwa jamii kuwa imeweza kusimamia haki na wananchi waliokosewa haki walipata matumaini makuu kuwa hatimaye haki yao itapatikana pamoja na mateso mengi waliyoyapata. Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga alisifiwa sana kuwa ameweka msingi mzuri sana wa utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hasa kwa kuwa hili ndilo lilikuwa shauri la kwanza ambalo Tume ililishughulikia tangu ilipoanza kufanya kazi baada ya kuundwa. Hii imedhihirika hata miaka mingi baadaye kwa kauli ya aliyemrithi Jaji Kisanga Mheshimiwa Tom Nyanduga alivyozungumza baada ya kifo cha Jaji Kisanga. Akinukuliwa na gazeti la The Citizen la tarehe 25 Januari 2018 alisema Jaji Kisanga ndiye aliyefanya Tume iwe illivyo kwa wakati huo. Alisema Jaji Kisanga alifanya kazi kubwa sana ya msingi ya kuifanya Tume kuwa chombo imara kilichokuja kuheshimiwa. Aliweka kanuni na akahakikisha zinafuatwa. Aliitaja Kesi ya Nyamuma kama mfano wa jinsi Jaji Kisanga alivyokuza heshima ya Tume na kuifanya iweze kuwa chombo chenye nguvu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilipokea pongezi kwa kuweza kulisimamia suala hilo hadi pale lilipofikia. Kati ya simu na barua walizopokea moja ni kutoka kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Haki za Binadamu ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam ikitoa pongezi kwa ushindi uliopatikana kwa wananchi wa Nyamuma Iliyobaki.

Vyombo vya habari navyo vikawa mstari wa mbele kutangaza uamuzi wa Tume. Gazeti la The Guardian la tarehe 14 Disemba 2004 liliandika kwa kichwa kikubwa cha habari 'Victory for Nyamuma Villagers', yaani 'Ushindi kwa wanakijiji wa Nyamuma'. Gazeti la Majira liliweka kichwa cha habari kilichosema 'Serikali yapewa Masharti' wakati Mtanzania lilitoa kichwa cha habari 'Uongozi Serengeti Ulikiuka Haki za Binadamu'. Mwananchi lenyewe liliandika kwa kichwa kilichosema 'Heko Tume ya Jaji Kisanga'. Hii ikiwa ni tahariri wakati ikiwa na habari yenye kichwa cha habari 'Serikali yatiwa hatiani kilio cha Wananchi Mkoa wa Mara'. Haya ni baadhi ya magazeti siku ya pili baada ya Tume kukamilisha kazi yake. Aidha redio na runinga zilitoa hiyo habari kwa kuonyesha ushindi wa wananchi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

Kikubwa kilichoonekana ni nafasi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika kusimamia haki za binadamu nchini. Wale waliokuwa wamepigania uwepo wa Tume waliona hatimaye matunda mazuri yametokea ambayo ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa haki za binadamu nchini.

### 4.7 Serikali Ilivyopokea Mapendekezo ya Tume

Baada ya maamuzi hayo ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora serikali ilipelekewa rasmi na kutakiwa kutekeleza katika kipindi cha miezi mitatu tangu uamuzi huo upatikane kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora namba 7 ya mwaka 2001 kifungu cha 28(2). Hata hivyo katika kipindi chote cha miezi mitatu, serikali ilikuwa kimya, bila dalili zozote za utekelezaji hadi muda ule wa miezi mitatu ukapita.

Ilibidi Kituo kiandike barua tarehe 21 Machi 2005 kwenda kwa Tume kutaka kufahamu lini hasa serikali itatekeleza mapendekezo yake. Barua hiyo ilifuatiwa na mkutano na waandishi wa habari tarehe 22 Machi 2005 kuelezea masikitiko ya kutotekelezwa kwa mapendekezo yale kwa muda uliotakiwa ilihali wale wananchi wanazidi kuumia na hali zao zikizidi kuwa duni kila iitwapo leo. Wananchi wa Nyamuma nao waliandika barua kwa Tume wakinakili kwa Kituo nao wakielezea adha zao na kuwa bado hawajaona dalili za mapendekezo yale kutekelezwa hata yale yaliyosemekana kuwa ni ya dharura.

Tarehe 24 Machi 2005 baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kumpigia simu Mwenyekiti wa Tume, ndipo Kituo kilipopokea barua rasmi toka kwa mwenyekiti wa Tume kuwa serikali ilikuwa imeomba muda zaidi kuandaa utekelezaji. Ilikuja kufahamika kuwa ilipobakia siku tatu kabla ya tarehe ya mwisho kwa serikali kutekeleza mapendekezo ya Tume, Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati huo Andrew Chenge aliandika barua kwa Tume ikiwa ni tarehe 10/3/2005 akiijibu Tume kuwa serikali inahitaji muda zaidi ili waweze kutekeleza mapendekezo ya Tume. Tume ilikubaliana na serikali pamoja na kuwa haikuwapa muda maalum wa kukamilisha utekelezaji huo.

Hapo ilibidi watu waendelee kuwa na subira wakijua kuwa serikali inajipanga na itafanya utekelezaji wa yale Mapendekezo ya Tume kama yalivyoainishwa. Hiyo ni Tume iliyoanzishwa kikatiba na kwa mujibu wa sheria hivyo hapakuwa na shaka kabisa kuwa serikali itaweza kushindwa kutekeleza mapendekezo ya Tume hiyo.

Ilipofika Mwezi Mei ilipokelewa barua iliyokuwa imepelekwa kwa Mwenyekiti wa Tume ambayo iliandikwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Andrew Chenge Tarehe 18 Mei 2005 kwa Mwenyekiti wa Tume Jaji Robert Kisanga, ikiwa na kichwa cha habari Mapendekezo ya Tume Kuhusu Kesi ya Serengeti CHRAGG/1032/2001/2002/MARA. Barua hii iko kwa lugha ya Kiingereza kama ilivyoambatanishwa hapa chini na kutolewa tafsiri kwa Kiswahili chini yake.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF JUSTICE AND CONSTITUTIONAL AFFAIRS

P. O. Box 9050
Dar es Salaam

18 May 2005

Hon. Robert H. Kisanga
The Chairman
The Commission for Human Rights and
Good Governance
P. O. Box 2643
**DAR ES SALAAM**

**SUB: THE COMMISSION RECOMMENDATIONS REGARDING SERENGETI CASE CHRAGG/1032/2001/2002/MARA**

1. As you may be aware, pursuant to Section 28 of the Commission for Human Rights and Good Governance Act No. 7 of 2001 the Commission presented to the Government the Recommendations regarding the allegations against the Serengeti District commissioner one Thomas Ole Sabaya and the District Police Commander one Pantaleo Lyimo.

2. First and foremost I would like to commend the Commission for being very instrumental in the Serengeti case. Taking into account that this is the first case to be engineered by the Commission from the initial stage to the final stage, it is undoubted that the Commission has gained an experience as regard the application of the law and probably it has spotted some short comings in the said law which need review or amendments. The government promises to collaborate with the Commission to enable it to meet the needs of the Tanzanians.

3. As one may remember, the Commission recommended that the Government should take disciplinary actions against the irresponsible Officials in the Serengeti cases and also pay compensation to the victims/complainants.

*Inaendelea >*

4. **Hon. Chairman,**

The Government of Tanzania is aware that the Commission Recommendations should be adhered to purposely to enable the Commission to accomplish its objectives and also to enhance the dignity of the Commission. In that regard the Government endeavered to execute the Commission recommendations in accordance with the laws of the land. Upon executing the Commission recommendations specifically the disciplinary ones the Government has to abide with the laws pertaining to evidence and Criminal Procedures. In that regard the Government conducted investigations in the said areas in order to capture the persons recommended by the Commission that they should be prosecuted.

The purpose of the investigation was to gather evidence before taking any criminal charges. The evidence shows that should the Commission conducted the same, the recommendations could have changed or in other words the Commission could have come up with different opinions. For example the witnesses who testified on the allegations on the burnt houses in the Village of "remaining Nyamuma" (Nyamuma iliyobaki) revealed that:

(a) The interviewed persons who thoroughly know the Complainants (some of them being their relatives) testified to the effect that there had been no humiliation, threats intimidation, discrimination, brutality, house burning, destruction of stores or any damage of properties whatsoever. This is contrary to what was testified to the Commission.

(b) Statements from the traditional leaders are to the effect that the houses alleged to have been burnt were just some deserted places which were burnt by the neighbouring villages of Bonchungu, Rwamchanga, Kebosongo and Miseke and during the operation the said Traditional leaders/elders were absent/not in the scene.

*Inaendelea >*

(c) Investigation has shown that fourteen (14) complainants out of 135 were Kenyan citizens. The Commission has recommended for compensation of these fourteen people also.

Further the Commission commented that the nationality/citizenship of the said 14 people could not be justified since the Court had earlier founded them prohibited immigrants - after their Case had been adjudicated by the District Court of Tarime.

After the said order which was not challenged by the complainants which is also honoured by the Government, - the Government found itself at the cross road in that it is supposed to either abide to the Court Order or by the recommendation of the Commission which rests on the statement that the nationality of the 14 people is not yet justified. The Government found itself somehow confused regarding the execution of the recommendation of the Commission because the evidence in record greatly contradicts the one presented before the Commission.

5. The Government has discovered that most of recommendations made by the Commission rest on cooked stories that is:

- The list of the Complainants includes the names of Complainants whose properties were not destroyed at all but in turn it recommended to be compensated by the Government.
- The list of the Complainants includes the names of persons who had no properties or at all during the occurrence of the event but they are now recommended to be compensated.
- The list includes the name of ghost complainant or the name of persons who cannot be found or at all.

Traditional leaders/elders were absent/not in the scene.

Inaendelea >

- The list also comprised of people from Nyamuma and Gummeli villages who had previously prosecuted the Government (in 1997) challenging the order to remove/evict them from the Villages.

  In that Case through consent judgement the Complainants were paid TShs 114,885,000/- and in addition of TShs. 1,500,000/- being the costs of prosecuting the Case. At the end of the day the Complainants were transferred to other places. This group is also included in the list of the ones to be compensated for the second time. Surprisingly, some Complainants in this group have nicknamed themselves for the purposes of anonymity so much so that no one can discover that they had previously been compensated.

6. In this surrounding/circumstances where the complainants have deceited or cheated the Government, the Government has found itself in doldrums as regard to executing the Commission recommendations.

   As stated above a criminal charge can be effected against any complaint whenever there is a prima-facie evidence/case. Worst still in this case some of the complainants have objected/denied their own statements before the Police Officers. The said complainants alleged that the Police should use the statement averred before the Commission. This is indeed against the principle of Criminal Procedure.

   As I stated above the statements given by complainants before the Police contradict the ones given to the Commission. This cannot justify prosecutions in Court. The Government has failed to abide by the recommendations regarding the dismissal of its employees because of the circumstances given herein above. The Government has discovered that the evidence given by the complainants is very much exaggerated:- and therefore to dismiss or take any action against the said employees under such circumstances is a total humiliation.

*Inaendelea >*

Pursuant to S.28(2) of the Commission for Human Rights and Good Governance Act – Act No. 7 of 2001 and after conducting a thorough investigation, the Government is satisfied that:

(a) No human right violation has been done against any person nor was there any action against good governance in the purported area.

(b) Neither District Commissioner nor the Police Commander of Serengeti did misuse power/abused their power and the two have acted in accordance with the law of the land.

(c) In view of the foregoing the Government hesitates to execute the recommendations of the Commission which directed to the effect that the Complainants should be reinstated to the disputed area. The Government evicted the Complainant from the disputed area for security purposes taking into account that there emerged tribal (civil) wars in the said area that precipitated into animal theft and also hindered the securing the wildlife at IRONGO

After incurring such big expenses that included paying compensation to the complainants and transferring them to new places the Government is not ready to bring them back to the dispute land. The Government still believes that should the complainants testified in good faith before the Commission as regards the procedures taken by the Government at the time of transferring them from the dispute land to the new land the Commission should have been satisfied that the exercise was done in accordance with the laws of the land and humanity.

Thank you in advance.

(Signed)
**Andrew J. Chenge (MP)**
**ATTORNEY GENERAL**

**Cc:** Hon. The President of United Republic of Tanzania
White House,

*Inaendelea >*

**Dar es Salaam**

Hon. Prime Minister
P. O. Box 3021
**Dar es Salaam**

Hon. Regional Commissioner
Mara Region
P. O. Box 299
**Musoma**

Hii barua kama inavyoonekana ina kurasa sita. Aya ya kwanza inanukuu kifungu cha 28 cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sheria Namba 7 ya mwaka 2001, kuwa Tume ndiyo ilitumia kifungu hicho kupeleka mapendekezo yake kwa serikali ikihusu malalamiko dhidi ya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti aitwaye Thomas Ole Sabaya na Kamanda wa Polisi wilaya aitwaye Alexander Pantaleo Lyimo.

Aya inayofuata Mwanasheria Mkuu ameanza kwa kuipongeza Tume kwa kuwa makini katika kesi hiyo ya Serengeti hasa ikitiliwa maanani kuwa hii ndiyo kesi ya kwanza iliyofanyiwa kazi na Tume kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ameelezea kuwa bila shaka Tume imepata uzoefu kuhusu matumizi ya sheria na kwa vyovyote huenda imeona mapungufu katika sheria husika inayoweza kuhitaji mabadiliko au marekebisho. Alielezea kuwa serikali inaahidi kushirikiana na Tume katika kufikia mahitaji yake.
Aya iliyofuata katika barua hii imeanza kwa kueleza kuwa kama itakavyokumbukwa Tume ilipendekeza Serikali ichukue hatua za kinidhamu dhidi ya maafisa wa serikali waliohusika katika kesi ya Serengeti na kuwalipa fidia wahanga au walalamikaji. Aya inayofuata imeeleza kuwa Serikali inafahamu kuwa mapendekezo ya Tume ni lazima yazingatiwe ili Tume iweze kutekeleza madhumuni yake na kukuza heshima ya Tume. Na kwa sababu hiyo Serikali ilikusudia kutekeleza mapendekezo hayo ya Tume kwa mujibu wa sheria za nchi.

Katika kutaka kutekeleza mapendekezo hayo na hasa kuwaadhibu watendaji wa serikali, ilibidi Serikali ifuate sheria za ushahidi na mwenendo wa makosa ya jinai. Hapo ndipo ilibidi serikali ifanye uchunguzi wake katika maeneo yale ili iwapate wale watu walioguswa na Tume ili waweze kushtakiwa. Alieleza katika aya hiyo kuwa sababu za uchunguzi ilikuwa ni kupata ushahidi kabla ya kufungua kesi za jinai. Ushahidi wao ulionyesha iwapo Tume ingefanya kama walivyofanya wao mapendekezo yao yangekuwa tofauti. Kwa mfano mashahidi waliotoa Ushahidi kuhusu nyumba zilizochomwa katika Kijiji cha Nyamuma Iliyobaki walieleza kuwa hapakuwa na unyanyasaji, ubaguzi, ukatili au

nyumba kuchomwa au uharibifu wa maghala ya chakula wala uharibifu wa mali. Hiki ni kinyume na yaliyoshuhudiwa kwenye Tume barua hiyo imekazia.

Maelezo ya viongozi wa jadi barua hiyo imeeleza yanaonyesha nyumba zilizochomwa zilikuwa mahame, hazikuwa na watu na zilichomwa na wanakijiji jirani cha Bonchugu na Rwanchanga, Kebosongo na Miseke, na hao viongozi wa jadi hawakuwepo wakati Kijiji hicho kinachomwa. Barua hiyo ilizidi kusisitiza kuwa uchunguzi walioufanya unaonyesha walalamikaji 14 kati ya 135 walikuwa wa Kenya. Tume imetoa mapendekezo hata hawa 14 nao walipwe fidia. Serikali ikaeleza iko katika njia panda kwani watu hao inaonekana walikuwa wahamiaji haramu kwa mujibu wa kesi iliyoamuliwa na Mahakama ya Tarime hivyo Serikali haijui iwapo ifuate maamuzi ya Tume au ya Mahakama.

Serikali katika aya yake ya tano ilisema kuwa imegundua mapendekezo mengi yaliyotolewa na Tume yanatokana na hadithi za kutungwa kama vile orodha ya walalamikaji ambayo ina majina ya watu ambao mali zao hazikuharibiwa kabisa lakini Tume ikaamua nao walipwe. Orodha ilikuwa na majina ya walalamikaji waliokuwa hawana mali hata kidogo wakati wa tukio lakini wanatakiwa walipwe na kuwa orodha ina majina hewa ya watu ambao hawawezi kupatikana. Aidha orodha ina majina ya watu waliokuwa wanaishi vijiji vya Nyamuma na Gummeli ambao walishaishitaki serikali huko nyuma mwaka 1997 wakipinga kuondolewa kijijini kwao. Kwa hali hiyo hao watu kwa maafikiano walilipwa milioni mia moja kumi na nne laki nane na themanini na tano pamoja na gharama za kesi milioni moja na laki tano na mwishowe walihamishiwa sehemu nyingine, nao wapo kwenye kundi la kulipwa, barua inauliza. Kwa mshangao kuna walalamikaji waliojipa majina ya utani ili wasijulikane kuwa walishalipwa.

Katika aya ya sita barua ya Mwanasheria Mkuu inaeleza kuwa kwa hayo yaliyoandikwa ambayo yanaonyesha walalamikaji kuwa wadanganyifu Serikali imejikuta katika hali ngumu kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Tume. Serikali imeshindwa kukubali mapendekezo ya Tume

kuwaachisha kazi watendaji wake kutokana na hali halisi iliyoeleza hapo juu. Serikali imeona ushahidi umetiwa chumvi sana kwa hiyo kuwafukuza kazi au kuchukua hatua dhidi ya wafanya kazi wake itakuwa ni kuwadhalilisha.

Serikali ikaendelea kujibu kwa kusema kwa mujibu wa kifungu cha 28(2) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Namba 7 ya 2001 na kwa uchunguzi iliyofanya Serikali imejiridhisha kuwa:

a) Hakuna haki ya binadamu iliyovunjwa dhidi ya mtu yeyote wala hapakuwa na tendo lolote dhidi ya utawala bora katika eneo husika;
b) Si Mkuu wa Wilaya wala Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Serengeti aliyetumia madaraka yake vibaya bali hao wawili walifanya kama sheria inavyowataka kufanya;
c) Kutokana na hayo yaliyoelezwa Serikali inasita kutekeleza mapendekezo ya Tume yaliyotaka walalamikaji warejeshwe katika ardhi yenye mgogoro. Serikali iliwaondoa kwa sababu za kiusalama ikizingatia kulitokea vita vya kikabila katika eneo hilo iliyosababisha wizi wa mifugo na kukosesha usalama wa wanyama pori huko Ikorongo.

Baada ya Serikali kuingia gharama ya kuwahamisha na kuwalipa fidia haikuwa tayari kuwarudisha tena kwenye ile ardhi. Serikali bado inaamini kama walalamikaji wangetoa ushahidi kwa nia njema mbele ya Tume kulingana na taratibu zilizochuliwa wakati ikiwahamisha kwenda makazi mapya, Tume ingeridhika kuwa ilifanywa kwa mujibu wa sheria na kiutu.

Huo ndio mwisho wa hiyo barua na imesainiwa na Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Na nakala zikapelekwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Mkuu na Mkuu wa Mkoa wa Mara.

Yaani kwa kifupi ni kuwa serikali ilieleza kuwa haitatekeleza mapendekezo ya Tume kwa vile imefanya uchunguzi wake ikagundua kuwa Tume ilidanganywa.

Hili lilikuwa ni jambo la ajabu sana na la kusikitisha sana. Iwapo Serikali ilikuwa haikuridhika ilitakiwa ichukue hatua za kisheria kupinga mapendekezo hayo mahakamani ili iweze kusikilizwa na kutoa ushahidi wake mpya na si kuijibu Tume kama ilivyofanya. Mambo kadhaa yalionyesha jinsi serikali ilivyoshindwa kuiheshimu Tume. Kwa mfano, Tume ilidanganywa vipi wakati Tume iliendesha shauri wakiwepo na wa wakilishi wa serikali ambao waliwahoji mashahidi na hata kufanya utetezi wao. Tume ilipotembelea eneo la mgogoro ilikuwa na mawakili wa walalamikaji na mawakili wa serikali ambao wote waliona magofu ya nyumba zilizokuwa zimechomwa moto. Iweje serikali iondoke katika mfumo usiofuata taratibu na sheria ukafanye uchunguzi wake kimyakimya na kubatilisha kazi yote Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora chini ya mwenyekiti wake jaji mstaafu Robert Kisanga iliyofanywa kwa zaidi ya miaka miwili ? Katika majibu hayo pia kuna kujikanganya kwani serikali inasema hakuna watu waliovunjiwa haki lakini hapohapo inasema orodha ya walalamikaji imejumlisha watu ambao hawakuwa na mali kwa maana kuwa walikuwepo waliokuwa na mali. Pili inasema orodha imejumuisha watu ambao mali zao hazikuharibiwa kwa maana kuwa wapo ambao mali zao zilizoharibiwa. Serikali imetumia mifano ya mashauri ya nyuma waliyoshitakiwa na kuifanya kama ni ya suala lililokuwa mbele ya Tume. Serikali inasema ushahidi umetiwa chumvi kwa hiyo ni kweli hilo yapo malalamiko ila yameelezewa kwa undani zaidi. Kisha serikali inawakinga watendaji wake waliofanya vibaya sana kinyume cha sheria, uvunjifu wa haki za binadamu na kutozingatia utawala wa sheria.

Jibu hili lilizua taharuki na hata Jaji Robert Kisanga, mwenyekiti wa Tume, alipohojiwa na waandishi wa habari aliishia kujibu kuwa anamuachia Mungu. Kwa kweli ilikuwa ni jambo la kukatisha tamaa sana kwani Tume iliifanya hiyo kazi kwa weledi mkubwa kiasi hata cha kulalamikiwa na mawakili wa walalamikaji kuwa inaegemea sana taratibu za kisheria wakati Tume ilitakiwa ilegeze taratibu hizo ili iwe nafuu kwa wananchi wa kawaida.  Tume ilifanya kazi kwa kuzingatia sheria na ikasimamia kanuni zilizowekwa ambazo zilikuwa ni za kisheria sana.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kiliitisha mkutano na waandishi wa habari na kutoa tamko lililokuwa na kichwa cha habari 'Impunity in Tanzania' ikimaanisha kuwa Tanzania kuna hali ya serikali kutojali baada ya kukosa na kuwa watu wanaweza kukosa bila kuadhibiwa. Ukweli ukiwa ni kuwa ilikuwa wazi watu walichomewa nyumba zao, wakafukuzwa katika ardhi yao kinyume na sheria na Tume ilithibitisha bila shaka yoyote. Hivyo kwa wale waliotenda, kwao imekuwa ni sawa na wameachwa huru na waliotendewa wamedhulumiwa, hapo hakuna uwajibikaji wala hakuna nafuu waliyoipata wale waliokiukiwa haki zao. Katika tamko hilo ilioneshwa jinsi Mwanasheria Mkuu alivyovunja sheria kwa kukiuka utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume kwani alichotakiwa ni kutekeleza sio na yeye ambaye alikuwa mmoja wa walalamikiwa kwenda kufanya uchunguzi kinyemela akiegemea upande mmoja.

Kituo pia kilitaka Watazania waelewe zaidi kilichotokea hivyo kiliandaa kipindi cha runinga siku ya tarehe mosi Juni mwaka huo wa 2005 kikiwa ni kipindi cha moja kwa moja kupitia runinga ya 'Channel Ten' ambapo kwa saa nzima ikiwa mubashara Profesa Chris Maina Peter, Wakili Francis Stola na Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu wakati huo Helen Kijo-Bisimba walielezea uvunjifu wa sheria uliofanywa na serikali na madhara yake kwa haki za binadamu na hasa kwa utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo ilikuwa imetoa Mapendekezo yake kwa mara ya kwanza. Huu ulikuwa ni mfano mbaya sana kwa serikali kufanya bila kujali watu waliodhulumiwa haki zao. Wananchi walipiga simu katika kipindi hicho wengi wakiilaumu serikali kwa kile ilichofanya na hasa wakimnyoshea kidole Mwanasheria Mkuu wa Serikali Andrew Chenge ambaye alitakiwa kuishauri serikali vizuri akiwa ndiye mshauri mkuu wa kisheria kwa serikali.

Hapa ndipo wale wananchi waliodhani wameipata haki yao ya kurudi kwao, kuwa na kwao, waliyoona haki imewafikia, haki imetendeka, wakarejea tena kwenye giza nene. Mwanasheria mkuu huyu alikuwa anaonyesha ana kejeli na kuikebehi Tume iliyofanya kazi yake kwa zaidi

ya miaka miwili. Ilibidi kutafuta suluhisho. Pamoja na Jaji Kisanga 'kumuachia Mungu' ilibidi sheria iangaliwe tena kuona ni nini kinachoweza kufanyika bila kukata tamaa.

Iwapo watu walikwisha subiri tangu mwaka 2001, mwaka huo 2005 bado wangeweza kusubiri kuitafuta na kuifukuzia haki yao. Kama inavyofahamika kuwa haki huwa inatafutwa kwa gharama yoyote ile, si rahisi haki iliyopokwa mtu aletewe kwenye sahani ya fedha. Wanasheria wa Kituo waliingia kazini kutafuta suluhisho la Kisheria na wahanga walielekezwa na wakawa tayari kuendelea na safari hiyo ngumu ya kuitafuta haki yao

SURA YA TANO

05

# WANANCHI WA NYAMUMA ILIYOBAKI WAFUATILIA HAKI YAO YA KUWA NA KWAO

## 5.1 Uamuzi wa Mahakama ipi ya Kuiendea

Baada ya kutafakari kwa kina Kituo kiliwasiliana na Tume ya Haki za Binadamu kuhusu Serikali ilivyokataa kutekeleza mapendekezo ya Tume. Kwa kuzingatia kifungu cha 28 (3) cha sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora namba 7 ya 2001, ambayo imeweka bayana kuwa, iwapo Tume itaona hakuna kilichofanyika kadiri Tume ilivyopendekeza kwenye taarifa yake katika kipindi kilichowekwa kisheria , basi Tume itaweza kupeleka shauri mahakamani au kuitaka mamlaka nyingine yenye uwezo kisheria kupeleka shauri mahakamani kudai utekelezaji wa mapendekezo ya Tume.

Katika mjadala wa ipi Mahakama ya kuiendea Tume iliamua kutoa kibali/ruhusa kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kupeleka shauri mahakamani ili kuitaka serikali itekeleze mapendekezo ya Tume. Ilionekana kuwa pamoja na Tume kuwa na mamlaka ya kuipeleka serikali mahakamani ingeweza kuwa na ugumu na ingeleta mgongano wa kimaslahi hasa kwa vile Tume bado ni tegemezi kifedha katika serikali.

Baada ya Kituo kupata kibali hicho cha kuweza kupeleka madai mahakamani, jopo la mawakili wake lilikaa na kujipanga kuona watakavyoweza kufanya hilo jukumu. Pia ilibidi kuwataarifu wahanga ambao ndio walikuwa walalamikaji ili wajiandae kwa hatua mpya ya kuitafuta haki yao. Serikali ilikuwa imerudisha nyuma mchakato wa kuwapatia haki wakazi wa Nyamuma kwa kuwa shauri hili lingeweza kuwa limefunguliwa mahakamani lakini iliamuliwa lipelekwe Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kutegemea kuwa kutakuwa na urahisi na pia muda utakaotumika hautakuwa mwingi. Kwa kukataa kwa serikali, ilibidi shauri lipelekwe mahakamani kwa ajili ya kukazia mapendekezo ya Tume jambo ambalo ilikuwa ni kama kuanza upya.

Katika mambo yaliyofanyiwa kazi na mawakili ni kuamua shauri hilo lipelekwe mahakama ipi. Kwenye kila shauri ipo mahakama yenye uwezo kisheria kulingana na kiasi cha fedha kinachohusika aina ya shtaka na eneo mgogoro ulikozukia. Katika shauri hili Mahakama iliyoonekana kuwa na Mamlaka ya Kisheria ya Kukazia shauri hili ni Mahakama Kuu ya Tanzania. Kwa vile Mahakama Kuu inavyo vitengo mbalimbali, kwa shauri lililohusu Ardhi yaani kurejeshwa katika Ardhi yao ilibidi kupeleka shauri katika Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi. Kwa upande wa madai ya fidia ilibidi shauri lipelekwe Mahakama Kuu, Masijala Kuu. Ni kwa muktadha huo yaliandaliwa maombi mawili tofauti ili kuwezesha kufunguliwa kwa mashauri ya kukazia mapendekezo katika Mahakama Kuu sehemu hizo mbili.

### 5.2 Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilipeleka shauri la Ardhi kwenye Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi tarehe 30 mwezi Mei mwaka 2005 ambayo iliandikishwa/kusajiliwa kama 'Misc. Land Case namba 22 ya 2005 mdai akiwa ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) dhidi ya Thomas Loy ole Sabaya Mkuu wa Wilaya ya Serengeti akiwa Mdaiwa wa kwanza, Alexander Lyimo Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Serengeti akiwa mdaiwa namba mbili na Mwanasheria Mkuu wa serikali akiwa mdaiwa namba tatu, Halmashauri ya wilaya ya Serengeti akiwa Mdaiwa namba nne na Halmashauri ya kijiji cha Bonchugu akiwa mdaiwa namba tano.

Maombi yaliyopelekwa mbele ya Mahakama Kuu na mdai kwa ajili ya kufanyiwa uamuzi yalikuwa mawili:

i. Mahakama iweke bayana na kutambua kuwa Ibrahim Koroso na wengine 134 walikuwa walalamikaji wa kwanza katika lalamiko namba HBUB/S/1032/203/MARA mbele ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na kwamba walikuwa wanaishi na kutumia Ardhi ya mgogoro inayojulikana kama Nyamuma katika Kijiji cha Bonchugu Wilayani Serengeti Mkoa wa Mara;

ii. Mahakama itoe amri kwamba kwa mujibu wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume mlalamikaji wa kwanza arudishwe katika Ardhi ya mgogoro ijulikanayo kama Nyamuma huko Kijiji cha Bonchugu.

Maombi haya hayakuweza kuendelea kusikilizwa kutokana na mapingamizi ya awali yaliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyekuwa akiwawakilisha walalamikiwa. Mapingamizi hayo ya awali yalikuwa matano:

1. Kwamba maombi yalikuwa na kasoro kwa vile mleta maombi hana uwezo kisheria kuleta maombi haya kwa mujibu wa sheria ambayo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa mapendekezo;

2. Kwamba maombi yalikuwa ni mabovu kisheria kwa vile yaliwasilishwa Kinyume na kifungu cha 28(3) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora namba 7 ya mwaka 2001;

3. Kwamba waleta maombi wanachezea mchakato wa Mahakama kwa vile shauri kama hili na kwa wahusika hao hao lipo kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania, Masijala Kuu;

4. Maombi hayakubaliki kwa mujibu wa sheria kwa kufuata kanuni ya Res Judicata; na

5. Kwamba Mahakami hii haina uwezo kisheria kulisikiliza shauri hilo.

Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi kupitia Jaji mstaafu Projestus Rugazia (marehemu) ilisikiliza maelezo ya waliopeleka mapingamizi, kuwa pingamizi la kwanza lilihitaji waleta maombi ambao ni shirika, ilihitajika kuwa maombi yaletwe na wadhamini waliosajiliwa. Pamoja na kuwa waleta maombi walieleza kuwa wao ni kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria ya makampuni na kuwa haina bodi ya wadhamini bali bodi ya wakurugenzi, bado waleta pingamizi walisisitiza palihitajika kibali cha Bodi ya Wakurugenzi na wakatoa kielelezo cha mashauri yalikwisha amuliwa mwaka 1999 na mwaka 1970 kuwa kampuni ikiwa ni kiumbe cha sheria inaweza tu kufanya kazi kupitia wakurugenzi wake.

Waleta maombi nao walipinga hoja ya mleta pingamizi kwa kuiangaliza mahakama kesi ya Solomon dhidi ya Solomon ya mwaka 1897 kama ilivyonukuliwa katika kitabu kilichoandikwa na L.B.C Gower kiitwacho Principles of Modern Company Law. Kwa mujibu wa kitabu hicho walieleza kampuni ni mtu kisheria tofauti na walioianzisha na inaweza kushtaki na kushtakiwa kwa jina lake. Hata wakurugenzi hawawezi kushtaki kwa niaba ya kampuni.

Baada ya hoja hizo kutoka kwa waleta maombi na watoa pingamizi, Jaji Rugazia alitoa uamuzi wake akisema kuwa hakuna ubishi kisheria kuwa mleta maombi ni Kampuni iliyoanzishwa chini ya sheria ya makampuni.

Baada ya utambuzi huu ulio bayana kilichofuata ni kuangalia iwapo kampuni hii itaweza kupeleka mashtaka ili kutafuta haki yake ya kisheria na iwapo inaweza pia kushtakiwa. Jaji Rugazia alieleza kuwa hafahamu sheria inayohitaji Ushahidi wa kiali kutoka kwenye azimio la Bodi ya Wakurugenzi ili kampuni iweze kufungua shauri. Alisema pia hana ufahamu wa sheria yoyote ya utekelezaji inayoweka utaratibu au uhitaji wa hilo. Inafahamika kuwa kampuni inafanya kazi kupitia wakurugenzi wake lakini bado kampuni ni mtu kisheria kwa mujibu wa sheria na iko tofauti na wanachama na wakurugenzi wake.

Kwa sababu hizo na kwa kiwango cha maelezo hayo Jaji Rugazia aliamua bila shaka kuwa mleta maombi ana uwezo kisheria kufungua shauri katika mahakama Kuu ya Tanzania.

Kwenye pingamizi la pili walalamikiwa walikuwa na maoni kuwa mleta maombi hakuwa na mamlaka kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 28(3) cha sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora namba 7 ya mwaka 2001. Kwa pingamizi hili walidai kuwa Tume ilikosea kwa kuwapendekeza/kuwaruhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kuleta madai mbele ya mahakama hiyo. Walidai kuwa taasisi inayoruhusiwa kuleta maombi au madai ni Tume yenyewe au mamlaka nyingine yenye uwezo lakini sio Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwani sio moja ya mamlaka zilizokusudiwa na Sheria. Walidai kuwa mamlaka yenye uwezo huo ni serikali. Walizidi kufafanua kuwa Bunge lilipokuwa linapitisha Sheria hiyo halikutoa uwezo kwenye Taasisi nyingine yoyote zaidi ya serikali na Tume, kwa hiyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinakosa mamlaka ya kuendeleza shauri hili.

Waleta maombi ambao ndio Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu nao walitoa majibu kuwa wanaweza kupata mamlaka kupitia kifungu cha 15 cha sheria iliyoanzisha Tume kinachoipa uwezo Tume kumpendekeza mtu au mamlaka itakayofaa au kuitaka mamlaka hiyo kuchukua hatua ambazo inaweza kuleta nafuu.

Jaji Rugazia alisema kwa uwazi kabisa kuwa kifungu cha 15 hakikutumiwa sawa na waleta maombi. Hata hivyo Jaji alizidi kuangalia iwapo Kituo kina mamlaka au uwezo kisheria na akasema ni wazi kuwa neno mamlaka halikupewa tafsiri chini ya Sheria husika wala katika sheria ya tafsiri ya Sura Namba 1 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002. Lakini Jaji aliona kuwa walalamikiwa waliona Kituo cha Sheria ana Haki za Binadamu kama kampuni ni mtu Kisheria lakini hana uwezo au sio mamlaka yenye uwezo kuleta maombi wakati Kituo cha Sheria ana Haki za Binadamu kilijibu kuwa kwa kuwa chenyewe ni mtu kisheria na kinasimama kwa niaba ya walalamikaji 135 basi ni mamlaka yenye uwezo kisheria.

Jaji akakiri kuwa anavutwa kukubaliana na hoja za mleta maombi kwa vile haoni ni kwa vipi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora katika hekima yake ingependekeza serikali ijipeleke yenyewe mahakamani. Hiyo ilikuwa ni hoja ya ajabu sana kwa mujibu wa Jaji Rugazia na kuwa haileti maana. Jaji alihoji kuwa hiyo Serikali ndiyo iliyokataa kutekeleza mapendekezo ya Tume na hiyo Tume ikaamua shauri lipelekwe mahakamani, itakuwa ni jambo lisilofikirika kwa Tume tena kuitaka serikali ijishtaki yenyewe. Kwa hiyo ndio maana ilibidi iwe na njia mbadala ambayo ilikuwa ni kupendekeza hii taasisi ya haki za binadamu kupeleka shauri mahakamani. Kwa sababu hizo Mahakama iliona pingamizi hilo la pili nao lilikosa nguvu kisheria na akalitupilia mbali kama lile la kwanza.

Katika pingamizi la tatu ambalo lilidai kuwa shauri jingine linalofanana na shauri hili liko mbele ya mahakama nyingine waleta maombi walieleza shauri lililopo mbele ya mahakama hii linahusu Ardhi wakati lile jingine lilihusu malipo ya fedha ya fidia kwa hiyo kanuni ya res-subjudice haihusiki.

Walalamikiwa walioleta pingamizi hawakubisha madai hayo, hivyo mahakama iliamini kuwa mashauri hayo mawili hayafanani na hivyo hapakuwa na hoja katika hilo pingamizi hivyo pingamizi hilo nalo likatupiliwa mbali.

Kwenye pingamizi la nne lililodai kuwa shauri lililoko mbele ya mahakama hii ni sawa kabisa na lililoamuliwa na jaji Nchala kwa makubaliano kwenye shauri namba 24 la mwaka 1997 lililoamuliwa tarehe 8 Mei 2000, ilielezwa kuwa shauri hilo lilihusu fidia kwa watu waliokuwa wakiishi Kijiji cha Nyamuma ambacho kilichukuliwa kuwa sehemu ya hifadhi ya Ikongoro mwaka 1994 kupitia GN 214 ya mwaka 1994 na hiyo ndiyo iliyoleta hukumu ya makubaliano. Shauri lililokuwa mbele ya Tume lilihusu kuchomewa na kuhamishwa kwa nguvu kwa walalamikaji kutoka eneo lao bila kulipwa fidia. Hivyo basi hakuna shauri lolote au mgogoro wowote kuhusu Nyamuma Iliyobaki ambao umeshahitimishwa na mahakama yoyote. Kwa kuwa hapakutokea ubishi kwenye maelezo hayo Jaji aliamua kuwa pingamizi hili nalo lilikuwa halina mashiko na hivyo akalitupilia mbali.

Pingamizi la awali lililokuwa la mwisho Jaji aliliona kuwa la muhimu sana. Waleta pingamizi walisema mahakama haina uwezo kisheria kusikiliza hilo shauri kwa vile Tume ilisema kwenye kifungu (g) ukurasa wa 7 wa ripoti yake kuwa haina mamlaka kushughulikia mashauri ya ardhi. Na Tume iliwashauri walalamikaji wafungue shauri mahakamani. Na kwa sababu hiyo sheria haikutoa uwezo kwa mahakama kutekeleza mapendekezo ya Tume bila kufunguliwa kwa kesi mpya ya Madai ya Ardhi. Walalamikaji walijaribu kutoa ufafanuzi kwa kukiangalia kifungu 28(3) ambapo Tume ilitoa mapendekezo kuwa walalamikaji warejeshwe kwenye ardhi yao kama walivyoomba na kwa kuwa hilo ni suala la ardhi ambalo mahakama hii ina uwezo kamili wakulishughulikia inapaswa kutekeleza mapendekezo ya Tume kuhusiana na ardhi kwa kuwa walalamikiwa wamekataa kufuata mapendekezo ya kuwarejesha walalamikaji katika ardhi yao, basi mahakama hii kwa kiwango cha kurejeshwa kwenye ardhi yao inatakiwa kutekeleza na iwapo kuna mtu atakayeumizwa na kurejea kwa walalamikaji katika ardhi inayolalamikiwa atakuwa na haki yakupeleka shauri mahakama ya ardhi yenye mamlaka.

Jaji Rugazia alijiuliza iwapo ni rahisi kiasi hicho na iwapo hiyo ndiyo tafsiri sahihi kisheria kama ilivyoelezwa na waleta maombi. Walalamikiwa

waliikataa hii tafsiri na Jaji akakubaliana na hoja zao nao kuwa wana sababu nzuri za kukataa. Jaji aliona zipo sehemu nyingi ambapo mleta maombi alikosea. Kusema kuwa mapendekezo ya Tume ni sawa na maamuzi/amri ya mahakama kama walivyojieleza wakinukuu kifungu cha 17(1) cha sheria iliyoanzisha Tume si sawa. Jaji alisema kwa tafsiri yoyote ile mapendekezo hayawezi kulinganishwa na maamuzi ya mahakama ambayo yanaweza kutekelezwa na mahakama.

Jaji alisisitiza kwamba kwa manufaa ya mleta maombi na kama ilivyoelezwa na mlalamikiwa, mapendekezo ya Tume sio maamuzi ya kimahakama ambayo yanaweza kutekelezwa na mahakama. Kwa tafsiri hiyo Jaji Rugazia akakubaliana na hoja kuwa kilichomaanishwa kupitia mapendekezo ya TUME ni shauri kusikilizwa upya na si vinginevyo. Jaji hakudhani kuwa watunga sheria walikuwa na mawazo tofauti na ingekuwa hivyo basi wasingekuwa na sababu ya kutokuweka wazi jambo hilo kwenye sheria. Jaji Rugazia alikazia maamuzi yake kwa kusema kuwa, ukiangalia baadhi ya vifungu kama kifungu 6(2) na 15(3) cha sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora namba 7 ya mwaka 2001 vinatamka bayana kuwa Tume inaweza kwenda mahakamani jambo ambalo lingekuwa halihitajiki iwapo Tume ina nguvu za kimahakama. Baada ya maelezo hayo Jaji alieleza kuwa mahakama hiyo kama walalamikiwa walivyoomba, hauna uwezo kisheria kutekeleza maombi ya walalamikaji kama waliyoomba na kwa hiyo alikubaliana na pingamizi hilo la awali. Matokeo yake alifutilia mbali maombi yaliyopolewa mbele ya mahakama hiyo. Alihitimisha kwa kusema kila upande utajigharimia kwenye shauri hilo hadi lilipofikia. Hiyo ndiyo ilikuwa amri ya mahakama.

Pamoja na kuwa hoja zote za pingamizi zilijibiwa vyema na Mawakili wa LHRC, ikiwemo hoja ya kuwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu hakina uwezo wa kisheria kufungua shauri hilo Mahakama Kuu ya Tanzania, hoja hiyo ya pingamizi ilikubaliwa na Mahakama hivyo shauri hilo likatupiliwa mbali/kuondolewa Mahakamani

### 5.1.1 Uamuzi wa Mahakama Kuu Kitengo Cha Ardhi, Jaji Rugazia

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**

**(LAND DIVISION)**

**AT DAR ES SALAAM**

**MISCELLANEOUS LAND APPLICATION NO. 22 OF 2005**

**LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE....................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**THE ATTORNEY GENERAL & 4 OTHERS..........RESPONDENTS**

**RULING**

**Rugazia, J.**

The applicants in this matter filed an application for the enforcement of recommendations of the Commission for Human Rights and Good Governance. The said recommendations were made by the Commission, it will be so referred in this ruling, after an inquiry which was conducted on complaints which were lodged before it by one Ibrahim Korosso and 134 others as first complainants and the Legal and Human Rights Centre. The respondents were Thomas Ole Sabaya, District Commissioner Serengeti; Alexander Pantaleo Lyimo, the Officer Commanding District and the Hon. Attorney General.

The applicant is praying for the orders as contained in the chamber application that:

*Inaendelea >*

(a) The Honourable Court be pleased to declare that Ibrahim Korosso and 134 others as first complainants in the complaint No. HBUB/S/1032/2003/MARA before the Commission for Human Rights and Good Governance, were living in and occupying and using the disputed land commonly known as Nyamuma area in Bonchugu village within the District of Serengeti in Mara Region.

(b) The court be pleased to grant an order that, for the purpose of enforcement of the Commission's recommendations, the first complainants be resettled back to the disputed land commonly known as Nyamuma area in Bonchugu Village.

The application could not proceed to hearing due to a number of preliminary objections raised by the Hon. Attorney General who is also appearing for all respondents. In total, five preliminary objections were raised and they are as follows:

1. That this application is incompetent as the Applicants do not have **locus standi** under the law under which the Commission's recommendations were made.
2. That this application is misconceived and bad in law as it has been filed contrary to the provisions of section 28(3) of the **Commission for Human Rights and Good Governance Act**, No. 7 of 2001

*Inaendelea >*

3. The applicants are abusing the court process as the same matter in issue between the same parties is pending in the High Court of Tanzania, Dar es Salaam Main Registry as Misc. Civil Cause No. 49 of 2005
4. That the application is untenable in law under the doctrine of **res judicata**
5. That this Honourable Court lacks jurisdiction to adjudicate this matter.

The Respondents' submissions in respect of the first preliminary objection were quickly watered down by the applicants in rebuttal in that, as it is, the respondents had taken the applicant to be a body corporate with trustees. This being the case, it was asserted that the application could only be brought through the names of registered trustees which renders this application incompetent. In rebuttal, it was submitted that the applicant is a company limited by guarantee established under the **Companies Ordinance Cap. 212.** It was thus submitted that the applicant has no Board of Trustees but has the Board of Directors.

Nevertheless, even after this clarification, the respondents still maintained their stand that there has to be evidence of authorization by the board of directors to institute this matter. Fortifying their argument, the respondents made reference to the case of **E. R. Investments Ltd. vs The Tanzania Development Finance Co.**

*Inaendelea >*

**Ltd and Another** Civil Case No. 66 of 1999 HC-DSM (unreported). The High Court in this case was following the holding in **Bugerere Coffee Growers Ltd vs Ssebaduka and Another** (1970) E. A. 147 in which it was held that a company being a creature of statute can only operate through its directors.

The applicant countered this assertion by revisiting the landmark case of **Solomon vs Solomon** (1897) AC 22 as it appeared in one of the learned author's (L. C. B. Gower) books titled **Gower's Principles of Modern Company Law,** Fourth Edn, Steven & sons, London, 1979. What is said in this book is an everyday song to many if not all lawyers, of the legal personality of the company quite separate from its subscribers and also that it can sue or be sued in its own name. The applicant submitted further that directors cannot sue for the company.

My own view regarding this argument is that it is not controverted that the applicant is a Company established under the Companies Ordinance. Once this is established, it follows that it can either sue to enforce its legal rights or it can be sued. I know of no law which requires evidence in the form of board resolution to authorized the company to take legal action. I am not even aware of any procedural law laying down such a requirement. Obviously we all know that the company can only operate through its directors but

*Inaendelea >*

still, a company is a legal person in the eyes of the law quite distinct from its members and directors.

Thus, to that extent, I can hold unhesitatingly that the applicant has the capacity to sue in a court of law. However, the respondents in their second preliminary objection were of the view that the applicant is not a competent authority within the meaning of section 28(3) of the **Commission for Human Rights and Good Governance Act**, No. 7 of 2001 hereinafter referred to as the Act. It was their submission that the Commission erred by recommending the Legal and Human Rights Centre to bring an action before this court. According to them, institutions allowed to bring any action to court is the Commission itself and any competent authority but, certainly, the Legal and Human Rights Centre is not such an authority. They contended that a competent authority in this regard is the Government. It was argued with unwavering certainty that Parliament did not confer these powers upon any other institution apart from the Government and the Commission so the Legal and Human Rights Centre lacks the mandate to pursue this matter.

On its part, the applicant replied that it can as well derive its mandate from Section 15 of the Act. This is what the said section provides:

**"15 (2) After conducting an investigation under this Act, the Commission shall have power to:**

Inaendelea >

(a) ..............

(b) .............

(c) **recommending to the relevant person or authority such measures, or requiring that authority to take such measures, as will provide an effective settlement, remedy or redress.**

Here I have to say it straight away that the applicant is wrong. I do not think whether this is a proper interpretation of the section. In my view, I think what is meant here by relevant person has to be found from the whole section to avoid the dangers of misinterpretation. If you look at sub-section 2(b) it is provided that the Commission shall have power to causing the complaint and the findings of the Commission to be reported to the appropriate authority or person having control over the person in respect of whose act or conduct an investigation has been carried out. By the same token, I encounter no difficulty in interpreting the relevant person referred to in sub-section 2(c) of the Act to mean the same person in 2(b). The only difference between these two clauses is that while in 2(b) the complaint and findings are reported, in sub-section 2(c) the Commission recommends on the measures to be taken. What this means, therefore, is that the Legal and Human Rights Centre could not have got its mandate from that section and, in fact, the Commission is not given any powers to recommend to any competent authority to bring an action before the court

*Inaendelea >*

otherwise the Commission would not have been given an option of going to court under S. 15(3) of the Act.

On whether the Legal and Human Rights Centre is a competent authority it is conceded by the contending parties that the word "authority" is not defined in either the Act or the **Interpretation of Laws Act, 2002.** However, while respondents submitted that while the Legal and Human Rights Centre as a company is a legal person but certainly not a competent authority, the Legal and Human Rights Centre countered that since it is a person in law and it is acting in the interest of 135 complainants then it is a competent authority.

Admittedly, I am tempted to subscribe to the argument by the applicant. I find it highly incomprehensible how the Commission could have, in its wisdom, recommended to the Government to take the Government (itself) to court!! This is a very strange argument and at all odds with common sense. An old adage says a monkey cannot arbitrate in forestry affairs the Kiswahili equivalent of a monkey and baboon case. Just imagine – it is this same government which found it impossible to act on the Commission's recommendations which prompted the Commission to opt for court action. It would be preposterous to imagine the Commission asking the government to sue itself. Which is why, I think, and it is a viable option, it had to recommend this renowned human rights body to take this course of action.

*Inaendelea >*

In the circumstances and eliminating all other possibilities, there was nothing the Commission could do other than picking on the applicant for this task. Having thus found, it is evident that the first and second preliminary objections have no merit and, accordingly dismissed.

On whether this matter is **res subjudice** as the matter in issue is also directly and substantially in issue in the pending case in the High Court main registry, it was submitted that this is a contravention of section 8 of the Civil Procedure Code. It was therefore prayed that this matter be stayed to avoid multiplicity of trials on the same subject matter.

Responding to this, the applicant submitted that while this is a land matter the pending suit in the Dar es Salaam district registry of the High Court is in respect of compensation of Tshs. 850,523,950/= so the doctrine of **res subjudice** cannot apply.

It did not escape my attention that the rejoinder by the respondents never responded to this rebuttal which makes me believe that what the applicants contended is the true state of affairs. I can therefore hold with confidence that this mater is not **subjudice** which effectively means that the preliminary objection has no merit and it is also dismissed.

*Inaendelea >*

Another preliminary objection is that this application is untenable in law as the issue before this court is directly and substantially the same with the one that was decided through consent judgment by Nchalla J. in Civil Case No. 24 of 1997 of the 8th day of May, 2000

In response which is elaborate by the look of it, I suppose, because the respondents did not respond to it, the applicant had this to say. It was submitted that the said matter was about compensation to the people who were living in **Nyamuma** Village area which was taken as part of Ikorongo Game Reserve in the year 1994 by virtue of GN 214 of 1994 thus giving rise to that consent judgment. In contrast, the complaint before the Commission was about the burning and forceful eviction of the complainants without compensation from the area outside the game reserve in October, 2001. As such it was asserted, there is no suit or any dispute on **"Nyamuma Iliyobaki"** which has been finally and conclusively determined by any competent court. There being no rebuttal to this submission and having no reason to doubt the applicant, I take it that the preliminary objection was raised without grounds and it is accordingly dismissed.

On the last preliminary objection which I find to be very crucial, the respondents asserted that this court lacks jurisdiction to

*Inaendelea >*

adjudicate this matter because even the Commission ruled under item (g) at page 66 of the report that it had no jurisdiction to adjudicate on land matters. The Commission, it was submitted, went further to advise the complaints to lodge a case in court. The respondent went on to submit that the Act does not give powers to courts to enforce recommendations of the Commission without a properly filed case.

The applicant had totally contrasting views regarding the interpretation of section 28(3) of the Act. It provides as under:

> ***"28(3) If within the prescribed time after the report is made no action is taken which seems to the Commission to be adequate and appropriate, the Commission may, after considering the comments, if any, made on behalf of the department, authority or person against whom the complaint was made either, bring an action before any court or recommend to any competent authority to bring an action and seek such remedy as may be appropriate for the enforcement of the recommendations of the Commission"***

The applicant opined that since the Commission recommended that the complainants have to be resettled back to their land as they

prayed, this is a land issue which this court has exclusive jurisdiction to adjudicate; in this case, to enforce the recommendation by the Commission based on land. Given the fact that the respondents have refused to comply with the recommendation to resettle the complainants, the applicant submitted that this court is simply invited to give an order to the extent of resettling the complainants so that if any person is aggrieved by the complainants' stay at the disputed land, shall have the right to take the dispute to the competent land court.

Is it that simple and is this a correct interpretation of the law as the applicant would like to put it? The respondents fault this reasoning and I personally think with good reasons. There are many areas where the applicant goes wrong. In what I consider to be a wrong view for instance, the applicant submitted that it is wrong to say that recommendations of the Commission are not decisions when that is what the law says. The law i.e. Section 17 (1) says that such decisions shall have the status of a recommendation to the appropriate authority. By any definition a recommendation cannot be equated to a decree to be enforced in a court of law. The respondents gave an example of the **Security of Employment Act** under section 28 (1) (c) where an order of the Labour Officer **(sic)** is enforceable by courts of law as a decree of court. I may wish to make a correction that it is not the Labour Officer but the Minister's decision on a reference to him under section 27 of that Act.

*Inaendelea >*

It has to be said for the benefit of the applicant that as submitted by the respondents, recommendations by the Commission are not judicial decisions to be enforced by a court of law. I endorse the view that what is meant by court action for enforcement of Commission recommendation is not simply execution but a trial. I do not think that this was what the legislature had in mind otherwise there was no impediment to say so in clear words. If you look at some sections of the Act i. e. Sections 6(e) and 15 (3) it is provided that the Commission may go to court a requirement which would have been unnecessary if it had judicial powers.

All in all, it has to be said that this court as prayed by the respondents, has no jurisdiction to do what the applicant is praying for and, having said that, the preliminary objection is upheld. Consequently, the application stands dismissed. Each party to bear own costs due to the way the preliminary objections have been disposed of.

Order accordingly.

**P. A. Rugazia**
**JUDGE**
**5/10/2005**

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Wanasheria na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na wale wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora walikaa pamoja na kuangalia njia ya kuifikia haki pasipo kukubali kirahisi kwamba hapo ndipo mwisho wa shauri hilo. Uamuzi uliofuata ilikuwa ni kukata Rufaa katika Mahakama ya Rufaa Tanzania ambayo ndiyo mahakama ya juu kabisa nchini na ndiyo mahakama ya mwisho. Aidha Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kiliamua kuangalia uamuzi wa Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi kwa uchanya zaidi kuwa pamoja na hoja hii moja kufanya shauri litupwe zile hoja nne zilizokataliwa na mahakama zilikuwa za muhimu sana katika ulingo wa sheria na zinafaa sana kufahamika na watu kama sehemu ya ushindi hata kama ni wa nadharia zaidi. Safari ilianza upya kuelekea Mahakama ya Rufaa Tanzania.

### 5.2 Rufaa katika Mahakama ya Rufaa Tanzania

Baada ya kutolewa kwa hukumu ya Jaji Rugazia na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kutokukubaliana nayo, ilibidi wanasheria kuandaa nyaraka kwa ajili ya rufaa dhidi ya maamuzi ya Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi na kuyafikisha Mahakama ya Rufaa Tanzania. Mnamo tarehe 7/10/2005 wanasheria wa Kituo waliwasilisha kusudio/nia ya kukata rufaa ilipelekwe Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Nia hasa ya kukata rufaa ilikuwa ni kupata ufafanuzi wa kisheria kuhusu kifungu cha 28(3) cha Sheria ya Tume ya Hali za Binadamu na Utawala Bora, Sheria namba 7 ya 2001 kutoka kwenye mahakama ya juu ya nchi kwani ilivyotafsiriwa na Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi na Jaji Rugazia haikukidhi tafsiri ya kisheria. Kifungu hicho kinasomeka kwa kiingereza hivi:

> 28 (3). if within the prescribed time after the report is made no action is taken Which seems to the Commission to be adequate and appropriate, the Commission, may after considering the comments, if any, made by or on behalf of the department, authority or person against whom the complaint was made either, bring an action before any court or recommend to any competent authority to bring an action

and seek such remedy as may be appropriate for the enforcement of the recommendations of the Commission.

Kifungu hiki kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili kinasomeka; ***'Iwapo muda uliotolewa kisheria kushughulikia mapendekezo ya Tume utapita na pasiwepo na kilichofanyika na Tume ikaona hakuna sababu za msingi au za kutosha kutofanya hivyo itabidi baada yakuangalia maelezo yoyote yaliyotolewa na mamlaka husika, idara au mtu anayelalamikiwa, ama kupeleka mahakamani au kuteua mamlaka yoyote yenye sifa kupeleka shauri mahakamani ili kutafuta nafuu itakayofaa kutekeleza mapendekezo ya Tume'.***

Baada ya kuwasilishwa kwa kusudio/nia ya kukata rufaa hatimaye ziliandaliwa nyaraka za rufaa nakuwasilishwa mahakama ya Rufaa ambapo zilisajiliwa na kupewa namba 88 ya 2006 na shauri hilo lilianza na kuendelea katika mahakama hiyo ya rufaa likisikilizwa na aliyekuwa Jaji Mkuu Agustino Ramadhani, Jaji Damian Lubuva na Jaji Harod Nsekela. Ilichukua tena zaidi ya miaka mitatu ndipo shauri hili lilipofikia hitimisho katika Mahakama hiyo ya rufaa. Tarehe 11/10/ 2008, Mahakama ya Rufaa ilitoa maamuzi yake na kuelekeza kuwa Mapendekezo ya Tume yanapaswa kupewa nguvu kisheria katika Mahakama za nchi. Hapa chini ni hukumu hiyo kama ilivyotolewa kwa lugha ya Kiingereza na itatolewa maelezo yake kwa Kiswahili chini yake.

**THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA**
**AT DAR ES SALAAM**
**(RAMADHANI, C. J.; LUBUVA, J. A.; And NSEKELA, J. A.)**
**CIVIL APPEAL NO. 88 OF 2006**
**BETWEEN**
**LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE ... APPELLANT**
**AND**
**THOMAS OLE SABAYA AND 4 OTHERS ... RESPONDENTS**
**(Appeal from the Ruling of the High Court of Tanzania, Land Division at Dar es Salaam)**
**'(Lugazia, J.)**
Mahakama ilipokamilisha kazi yake kwa kutoa amri ya walalamikaji kurudishwa katika eneo lao kilichobakia ilikuwa ni utekelezaji wa amri hiyo. Ili amri hiyo itekelezwe ilibidi pawepo na amri ya mahakama ya utekelezaji. Ilibidi kurudi tena mahakamani kutafuta amri ya kutekeleza hiyo hukumu au maamuzi ya Mahakama. Tarehe 9/9/2013 ndipo L.A. Mlacha, Msajili wa Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi alipotoa amri ya kumteua dalali wa mahakama atakayesimamia zoezi la utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama Kuu yaliyotolewa na Jaji Richard Mziray. Amri hiyo ilimteua Bwana Enock Mwakasala wa **GEMACO AUCTION MART AND COURT BROKER** akapewa jukumu la kwenda Kijiji cha Nyamuma wilaya

ya Serengeti ili akafanye tathimini ya awali wa njia zitakazofaa kutekeleza Mapendekezo ya Tume. Aliamriwa afanye mambo yafuatayo:

1. Aende Kijiji cha Nyamuma na kuitambua mipaka ya Kijiji hicho;
2. Awatambue watu wanaopaswa kurejeshwa katika hilo eneo na orodha yao aiwakilishe Mahakamani;
3. Azijulishe mamlaka za Wilaya, Kata na Kijiji uwepo wa amri hiyo na atafute usaidizi wa mamlaka hizo wakuwarejesha watu hao kwa tarehe zitakazopangwa.
4. Hatimaye amri ilieleza kuwa gharama za utekelezaji wa zoezi hilo zitalipwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambacho kitawajibika pia kuchagua maofisa watakaoongozana na huyo Dalali wa Mahakama.

Nadhani itakumbukwa kuwa amri hii inapotolewa tayari ni miaka miwili tangu amri ya Jaji Mziray ilipotolewa kuthibitisha kuwa Mapendekezo ya Tume yanapaswa kutekelezwa. Amri hiyo ilikuwa ya mwezi wa 9 mwaka 2011. Na pia ni takriban miaka 18 tangu wananchi hao wa Nyamuma Iliyobaki waondolewe kinguvu toka makazi yao. Wananchi hao kila wakati wamekuwa wakipiga simu na kuandika barua kuulizia kulikoni na wakati huo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kikijibidisha kutafuta kila njia ili watu hawa waweze hatimaye kurudishwa katika eneo lao na waweze kuendelea na Maisha yao baada ya miaka yote waliokaa nje ya makazi yao.

### 6.2 Jinamizi la utekelezaji wa Maamuzi

Baada ya dalali kupatikana aliwasiliana na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na mipango ikapangwa ya jinsi watakavyosafiri kwenda Serengeti na kuweza kutekeleza amri aliyopewa. Wakati wote huo wananchi waliokuwa wahanga walieleza kuwa Ardhi yao ilikwisha gawiwa watu wengine ambao Mkuu wa Wilaya aliwauzia mara tu wao walipoondolewa. Jambo hili lilikuwa limewahuzunisha sana kuwa Ardhi yao ilipewa watu wengine kwa kuuziwa na wao hawakuona sababu ya kuondolewa kwao. Ukweli huo ulithibitika kwani hata mmoja wa wahanga yeye aliweza kununua Ardhi yake na hivyo alirejea nakuendelea na maisha.

Ukweli huu ndio ulikuwa changamoto katika kutekeleza amri ya mahakama kwani wale watu waliokuwa wameuziwa hapo 'kihalali' wangezua mgogoro iwapo wangetakiwa kuondoka kuwapisha. Dalali alipofika huko Nyamuma alikabiliana na wananchi waliokuwa tayari wanaishi hapo kwa zaidi ya miaka kumi na walipomuona mtu wasiye mjua walizusha taharuki hadi ilibidi dalali afyatue risasi hewani ndipo hali ilipotulia na akaweza kuwaelezea kazi iliyompeleka na akafanikiwa kulitambua eneo.

Hapa ilibidi kufanya tafakari kubwa ingawa dalali aliona ni jambo linalowezekana kisheria kwa vile wakati hao watu wakipewa hiyo Ardhi kulikuwa na mgogoro uliokuwa ukiendelea kwenye Tume ya Haki za Binadamu na hatimaye mahakamani. Lakini pia miaka 12 ilikuwa haijaisha tangu watu hao wawepo hapo kwa mujibu wa sheria ya Ardhi. Dalali alitaka kutumia nguvu kwa mujibu wa sheria na mamlaka aliyopewa ili kuwaondoa waliopo na kuwarejesha waliopewa haki na mahakama.

Dalali alipokamilisha kazi aliandaa taarifa yake na gharama alizohitaji ili kufanikisha kazi hiyo. Jambo lililokuja kusumbua kabisa ni gharama za kufanya hilo zoezi ambazo dalali alizitoa kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Gharama zilikuwa ni kubwa sana na pia mamlaka yakushirikiana na dalali haikuwa tayari. Kutokana na gharama kuwa kubwa Kituo kiliomba mahakama iamuru serikali igharamie maana ndio waliosababisha watu kuondolewa. Serikali ilijibu kuwa haihitaji dalali kwani yenyewe ina uwezo wakutekeleza bila kumhusisha dalali. Serikali iliomba muda kuwasiliana na Halmshauri ya Wilaya ya Serengeti na wangeleta taarifa mahakamani kuhusu utaratibu wa utekelezaji.

### 6.3 Msimamo wa Mamlaka ya Wilaya ya Serengeti

Mamlaka ya Wilaya ya Serengeti kwa kutambua ilichokuwa imekifanya katika mgogoro ule iliandika barua kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ikieleza kuwa utekelezaji kwa kuwarejesha wale walalamikaji utakuwa mgumu kwa vile tayari wapo watu wanaishi eneo hilo ambao walipatiwa hiyo ardhi kwa taratibu za kisheria. Wao

walishauri badala ya watu hao kurejeshwa pale wapatiwe fedha kama fidia kwa ardhi yao ili watafute eneo jingine na kuwaacha hao watu waliopo hapo wakati huo.

Tume ya Haki za Binadamu wakati huo ikiongozwa na Mwenyekiti Jaji mstaafu Amiri Manento ilikubaliana na Wilaya ila ilishauri kuwa watu hawa wapewe maeneo mengine ya ardhi na si fidia kama mamlaka ya wilaya ilivyotaka. Wakati haya yanaendelea ipo amri halali ya mahakama inayotaka watu hawa warejeshwe katika ardhi yao. Vyombo hivi viwili vikijibishana kwa barua jambo ambalo ni nje ya amri ya mahakama wakati walalamikaji ambao ni wahanga bado wanahangaika nje ya eneo lao la ardhi. Suala la utawala wa sheria hapa limewekwa kando na kinachoendelea ni masuala ya kiutawala ambayo ukiyaangalia yanapingana na amri ya Mahakama.

Upande mwingine pia kama Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilivyokuwa kinajiangaliza ni suala la kiutu na kijamii kuwa wale watu ambao waliuziwa lile eneo iwapo wataondolewa hawatakuwa na makazi hivyo litajirudia tena suala la kuwakosesha watu makazi ili kuwapatia watu waliodhulumiwa makazi yao. Hapa lilionekana kuwa ni tatizo juu ya tatizo. Hata hivyo wazo la kuwapatia Ardhi mbadala lilionekana kuwa lingefaa zaidi iwapo watu hao watakuwa radhi.

## 6.4 Wizara ya Ardhi na Vyombo vingine vya Serikali

Kila mara wahanga hawa wamekuwa wakilalamika kwenye mikutano na popote pale walipoweza kulalamika kwani tayari walikwisha shinda kesi mahakamani na kilichosalia ilikuwa ni utekelezaji tu. Ilifikia mahali mawakili wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walifika kwenye mamlaka ya wilaya ya Serengeti, ili kuzungumzia suala hilo na ndipo mamlaka hiyo ilipoonesha utayari wakutoa ardhi nyingine katika ardhi iliyopo hapo wilayani. Ilitokea bahati kuwa ipo ardhi iliyokuwa inamilikwa na mtu mmoja aliyekuwa muwekezaji ila alikuwa hajaliendeleza hivyo Kamishna wa ardhi alimshauri Rais kuitwaa ardhi ile ili itumiwe na

wananchi wasiokua na ardhi. Ardhi ile ilitwaliwa na Rais na naibu Waziri wa Ardhi Mh. Anjelina Mabula akiwa huko mkoa wa Mara aliagiza sehemu ya ardhi hiyo wapatiwe hao wahanga wa Nyamuma Iliyobaki.

Hili lilionekana kuwa suluhisho na ilibidi serikali kupitia ofisi 'Solicitor General' kufuatilia utekelezaji wa amri ya mahakama kwa kuwapatia wananchi hao ardhi hiyo. Haikuwa ni rahisi kiasi hicho kwani kwanza wapo watu kati ya wale wahanga waliokuwa hawako tayari kupewa ardhi mbadala walitaka wapatiwe ardhi yao ileile kwani ni ardhi yenye historia kwao, ni kwao na kuwa kwao kunaambatana na mambo mengi ikiwemo sehemu zao za ibada makaburi ya wazee wao na kadhalika.

Serikali ilijitahidi kuwaelewesha watu wale, kisha wakaonekana wote kukubaliana kupewa ardhi mbadala na waliongozana kwenda kuiona ardhi ile. Walipofika huko ilionekana tayari sehemu ya ardhi hiyo imevamiwa na watu waliokuwa hawana ardhi. Ikaonekana ili watu hao waliokuwa wahanga wasije wakapata shida tena, ile ardhi iliyosalia ipimwe na ikishakupimwa wafahamike wale wote walio na haki ya kuipata hiyo ardhi ndipo wagawiwe. Pia ilikubaliwa kuwa ugawaji hautafuata kiasi cha ardhi mtu alichokuwa nacho bali ardhi itakayoweza kupatikana kwa kila mtu.

Ile ardhi baada ya kutwaliwa na Rais ilirudi kuwa radhi ya wilaya hivyo lilikuwa ni jukumu la wilaya kupima ile ardhi. Jambo la kusikitisha ni kuwa mamlaka ya halmashauri ya wilaya ilikiri kutokuwa na fedha zakuweza kulipima hilo eneo. Kiasi cha fedha kilichokuwa kinahitajika ni shilingi za kitanzania milioni tano tu. Hapa ilibidi juhudi zifanyike ili fedha hizo zipatikane ardhi ipimwe na hawa watu waweze kugawiwa hiyo ardhi. Upande wa fidia hilo lilikuwa halijazungumzwa kabisa ila msemaji wa serikali alisisitiza kuwa kwanza wajulikane wahanga wote kisha wapatiwe ardhi ndipo suala la fidia liendelee.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeweza kukusanya fedha za upimaji wa eneo hilo.

SURA YA SABA

07

# MADHARA YA KUIKOSA HAKI YA KUWA NA KWAO NA UGUMU KUIFIKIA HAKI

## 7.1 Jinamizi la Kujikuta Huna Kwako

> Siku hiyo kwangu ni kama kiama. Nilikuwa mkimbizi katika nchi yangu niliyozaliwa, nilikosa faragha, lishe ikawa duni, kupoteza mali yangu[mifugo] na hata kupoteza mazao yangu yote, hata pakufanyia ibada ya Mungu wangu palikosekana.

**Samwel Chunes Masese**
Mhanga wa Nyamuma iliyobaki



Katika kuangalia hali iliyowakuta hawa wananchi wa Nyamuma Iliyobaki inabidi kuwaangalia kama binadamu na kwa vile waliishi mahali pamoja yaani katika kitongoji cha CCM Senta Nyamuma Iliyobaki na wengi wao walikuwa na asili moja hivyo walielewana katika lugha yao. Mamlaka ya Serikali ilipoamua kuwaondoa kwa nguvu kwenye ardhi na makazi yao iliwaangalia katika umoja wao na si mtu mmojammoja ndio maana wote walichomewa nyumba zao, wote walifukuzwa bila kujali watoto wadogo, watu wenye ulemavu au wazee, wanawake waja wazito au wagonjwa.

Hali hii inaonyesha kuwa wakazi wa Nyamuma iliyobaki kwa pamoja wamekosewa haki zao. Zipo haki zinazowagusa watu kwa pamoja na zipo haki walizonazo katika ubinafsi wao. Katika mikataba ya kimataifa kuna watu wanaoangaliwa na haki zao kulindwa ambao husemekana ni watu wenye asili, mahali na ni wa mbari/kabila moja. Wakazi wa Nyamuma Iliyobaki walistahili kulindwa na kupewa hifadhi ya kuwekwa katika kundi hili kwa jinsi walivyotendewa na kitendo walichotendewa nacho kinaweza kufananishwa na uwekaji wa masharti muhali kuishi/au uangamizwaji wa kabila ; Mkataba wa Kuzuia na Kutoa Adhabu ya Makosa ya Uangamizaji wa Kabila au Uwekaji wa Masharti Muhali wa mwaka 1951 unatafsiri hali hiyo kuwa ni kitendo chenye nia ya kuharibu kwa kiasi au kabisa nchi, kabila, watu wa asili moja au dini kwa kuwaua, kuwaumiza vibaya kimwili au kiakili au kuwatendea vitendo vinavyoweza kuwasababishia kutokupata watoto au kwa nguvu kuwahamisha watoto wao.

Ifahamike kuwa kauli za Mkuu wa wilaya ya Serengeti kwa wakati huo, Ndugu Thomas ole Sabaya kuwa wakazi wa Nyamuma ni raia wa Kenya na kuwataka warudi Kenya haikuwa sahihi na alichokifanya mbele ya watu hao ni kutaka wasiwepo katika kile Kijiji na pia watokomee pamoja na ukweli kuwa hawa hawakuwa wakenya bali kwa sababu alizozijua yeye aliamua kuwafuta katika hilo eneo.

Wahanga wa Nyamuma iliyobaki wanapaswa kutazamwa kwa sura hizi mbili; mosi, watu wenye asili ambao wanatafutwa kuondolewa asili yao; Pili, uteketezaji wa makazi na mali zao ambao umechukua sura ya

maangamizi juu yao. Watu hawa wana haki ya uwepo wao na haki ya kuishi na kumudu maisha yao na ardhi yao. Kilichowatokea ghafla ni kujikuta wameondolewa katika ardhi yao na haki ya uwepo wao kuwa mashakani. Ukiangalia mtu aliyekuwa na ekari 20 au 30 za ardhi mara anajikuta akiambiwa hana chochote, kwani wapo waliochomewa nyumba na waliotakiwa kuzichoma nyumba zao na waliochomewa maghala ya chakula wakakimbia wakiwa watupu kabisa. Haki yao ya uwepo ilikuwa mashakani.  Wapo waliopoteza ndugu kama ndugu Wilson Korosso ambaye walipotezana na mke na mtoto na hakuwahi kuwaona tena.

Mama Ester Jackson huyu haki yake ya uzazi iliingiliwa kwani alipopigwa mateke tumboni mimba yake iliyokuwa ya miezi sita, iliharibika na alipobahatika kutibiwa hakuwa na pakurudi kwenda kujiuguza aliishia kutafuta msaada kwa majirani na wasamaria wema.

Hawa watu walikuwa na haki ya kuwa na usawa katika utu wao. Ghafla utu wao ulikuwa mashakani kwani hata mtu mwenye ulemavu alidhalilishwa kwa magongo yake kuchomwa moto. Kama mwenyewe Mugele Mwita alivyojieleza, alinyang'anywa miguu yake ya ziada.




**Jackson Mwita Chacha**
Mhanga Nyamuma Iliyobaki

Wahanga wa Nyamuma Iliyobaki kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa na kwa mujibu wa haki zao kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haki yao ya kuwa raia wa Tanzania ilitiliwa mashaka ikabidi wapate shida ya kujitambulisha kuwa ni raia wa Tanzania. Baadhi yao walishtakiwa kuwa si raia na wakafungwa miezi sita wakati wao ni raia na ndio maana hata baada ya kifungo waliendelea kuwepo nchini Tanzania kwani hawana nchi nyingine.

Wahanga hawa endapo walikuwa wamekosa kama aliyekuwa mkuu wa wilaya ya Serengeti alivyosema, walikuwa na haki ya usawa mbele ya sheria bila ubaguzi kama inavyoainishwa kwenye ibara ya 13[1] ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Badala ya watu hawa kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria walifanyiwa vitendo vilivyowavunjia utu wao na haki zao.

Wahanga wa Nyamuma Iliyobaki walijikuta haki zao za kiuchumi zikiwa zimevunjwa kwani hawakuweza kuendeleza maisha yao kiuchumi; kwa waliokuwa wanalima hawakuwa tena na mahali pa kulima, waliokuwa wafugaji hawakuwa na mifugo tena, waliokuwa wanafanya biashara zao kijijini haikuwezekana tena hivyo haki zao za kiuchumi ziliiingiliwa kabisa na kwa miaka yote wamekuwa wakihangaika bila kupata unafuu katika eneo hilo.



Watoto waliokuwa katika kitongoji cha Nyamuma na wazazi wao walipoondolewa kinguvu walisitishwa kupata elimu na wengine elimu iliishia palepale wakati wengine wakichukua muda kabla ya wazazi kutulia na wao kupatiwa mahali pengine pakuendelea na elimu yao. Uchumi wa wazazi ulipoyumba watoto wasingeweza kuendelea na masomo yao kwani fedha zilihitajika kuwezesha mtoto kuendelea na shule.

> Kwa sasa tunaishi kishidashida tu anajua tu Mungu. Nina watoto wana akili wamefaulu kwenda sekondari lakini uwezo wakuwasomesha sina, ningekuwa na ardhi ningelima niuze mazao niweze kupata fedha niwasomeshe wanangu.

**Bhoke Sospeter Wantola**
Mhanga Nyamuma Iliyobaki

> Maisha ni magumu sana. Nina watoto waliofaulu kwenda Sekondari lakini nimeshindwa kuwapeleka, Naomba msaada ili watoto waweze kuendelea na Elimu.

**Nyangige Mataro**
Mhanga Nyamuma Iliyobaki

### 7.2 Ukweli wa Maisha katika Hali Halisi

Wahanga wa Nyamuma Iliyobaki walijikuta wakipatwa na mkasa ambao hawakuutarajia maishani. Kila mmoja alijaribu kuikabili hiyo hali kwa kadri alivyoweza. Kama wasemavyo wahenga anayezama maji hata akiona unyasi huushika akidhani utamuokoa. Baada ya kupona vipigo na kufukuzwa wahanga hao walitafuta njia za kujikimu. Wale walioweza kukimbilia Mugumu Mjini walitafuta ndugu na marafiki wakuwahifadhi. Kama mmoja wa wahanga mama Bhoke Sospeter alivyojieleza, alichoweza kufanya wakati wa kukimbia ni kuwanyakua watoto yeye na mume wakaondoka wakikimbia kupitia maporini kwani kwenye njia walijaa askari. Walipofika Mugumu mjini walijikuta yeye akiwa na gagulo

tu na mume akiwa na bukta wakati watoto hawakuwa na nguo kabisa. Walipokelewa na msamaria mwema kwa jina Elias Mang'era ambaye aliwapa chumba akawanunulia watoto nguo za mitumba na kuwapa debe la mahindi. Na baada ya hapo walianza kufanya vibarua ili waweze kujikimu.

Wale waliopelekwa mpakani na Kenya walipoonekana kuwa si wa Kenya walijaribu kurejea Mugumu kwa njia ya mabasi kutoka Tarime kuelekea Mugumu. Mkuu wa wilaya ya Serengeti alipopata taarifa aliwatuma askari kanzu ambao waliwakamata watu hao wakiwa ndani ya magari na kuwashusha kwenda kuwafungulia mashtaka. Watu ishirini na nane walikamatwa kwa njia hii na wakapelekwa polisi na hatimaye mahakamani ambapo wengine walipatikana na hatia kwa vile tu hawakuwa na njia ya kujitetea kwa kukosa vielelezo kama vitambulisho, vyeti mbalimbali ambavyo kwa wakati ule vilikuwa ama vimechomwa moto au kupotea wakati wa kufukuzwa kinguvu, na wengine hawakuwa navyo tu kwa vile vijijini si kila mtu ana vyeti hivyo. Wahanga wengine waliweza kuhukumiwa vifungo kwa kuwa walikosa msaada wa haraka wa kisheria na haikuwa rahisi kupata watu wakuwashuhudia kwa kumuogopa mkuu wa wilaya.

Wahanga wa Nyamuma Iliyobaki hatimaye walianza maisha mapya ya ukimbizi ndani ya nchi yao ambao kitaalam hufahamika kama 'internally displaced people'. Watu walio nje ya makao yao lakini ndani ya nchi yao. Wahanga wanavyosimulia ni kuwa waliopata watu wakuwakaribisha mjini Mugumu walikuwa wakiishi kwa kujifichaficha, walikuwa hawana kazi. Walijaribu kutafuta vibarua ndivyo vilivyowasaidia kujikimu. Wakati mwingine wanaotoa vibarua kama vya kulima, kuchota maji, kuchanja kuni, walikuwa nao na hofu kwani ilikuwa imekatazwa kushirikiana na wahanga hao kwa hali yoyote ile. Wapo waliohamia wilaya nyingine ambako huko ilibidi wakaanze upya kutafuta nyumba za kupanga kufanya kazi za vibarua.

Wapo waliopoteza maisha kwa mfano Jackson Chacha kwa muda mfupi alimpoteza bibi yake na baba yake ambao alisema walikosa mahitaji muhimu kama chakula, malazi na matibabu. Kuna kipindi watu kadhaa walikufa kutokana na kudhoofu na hivyo ugonjwa kidogo tu ukipita wanapoteza maisha. Wapo Wananchi waliofiwa na watoto na hasa watoto wadogo kwa kukosa lishe bora.

Wahanga wa Nyamuma Iliyobaki walipohojiwa kipindi fulani walieleza kuwa maisha yao yalikuwa ni yakutangatanga mjini, kufanya vibarua kama kusukuma mikokoteni, kuzibua vyoo vilivyojaa, kupanga nyumba, jambo hilo kwao lilikuwa geni kwani kijijini kwao kila mtu aliishi kwake au kwao. Wengine walifanya vibarua vya ulinzi majumbani mwa watu.

Mmoja wa wahanga alisimulia jinsi alivyokoswakoswa na wanyama pori wakati akikimbia baada yakufukuzwa. Lugha za maelezo ya maisha hayo zinasikitisha. Wapo walioona maisha yameyumba kwa kukosa sehemu maalum yakuendesha maisha. Wengine walisema wameishi maisha ya 'sintofahamu'. Maisha bila uhuru kwenye nchi huru.

> Mimi kama Mzee wa familia naishi kwa kujihami, kufanya kibarua chochote ili mradi nipate Kibaba kwa ajili ya familia waende choo
>
> **Chacha Gisima**
> Mhanga Nyamuma iliyobaki



Katika kipindi chote hicho wahanga waliungana kwa maana yakufahamu kila mmoja yupo wapi na anapokuwa na shida kuweza kusaidiana. Walimteua mmoja kuwa kiongozi na msemaji wao. Waliweza kujaribu

kuandika barua kuomba misaada ya hali na mali lakini bahati mbaya hakuna aliyekuwa tayari kuwasaidia. Wengi walipohojiwa walitambua misaada binafsi walioipata kwa siri kwa ndugu na baadhi ya marafiki ingawaje yupo mmoja aliyekiri kuwa hakusaidiwa chochote na yeyote. Hapa ni kuwa anaongelea misaada ya kijamii ya kujikimu kwani msaada wa kisheria walioupata haukuwa karibu kwake kwa matatizo ya kijamii yaliyomfika ikiwemo ada za shule za watoto kiasi kwamba watoto wengine ilibidi waache shule.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilipokea barua za wahanga mara kadhaa.

Kituo hakikuwa na fedha za kuweza kuwasaidia kimaisha zaidi ya msaada wa kisheria. Ifahamike kuwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu huwa hakina bajeti ya huduma za kijamii, hivyo ilikuwa rahisi kuomba fedha za kusaidia kuendesha kesi lakini si fedha za kujikimu wahanga hawa. Kwa mfano Kituo kilipopokea maombi ya misaada ya kijamii kutoka kwa wahanga na kwa kuwa hapakuwepo na bajeti ya misaada ya aina hiyo, Kituo kiliandika kwa mashirika yaliyodhaniwa yangeweza kutoa msaada kama ***Norwegian Church Aid na Tanzania Christian Refugees Services***. Bahati mbaya taasisi zote hizo hazikuweza kusaidia hata kidogo.

Ilifika mahali wahanga hawa waliamua kujiunda kuwa chama ambacho kingeweza kufanya kazi za kuwaingizia kipato. Walijiunda na wakaamua kufanya kazi ya kutengeneza matofali ili waweze kuyauza wapate fedha, tatizo lilikuja kuwa ni mtaji ambapo walihitaji shilingi milioni tatu na laki tano. Hawakuwa na kimbilio zaidi ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ambapo napo walishindwa kusaidiwa kwa sababu zilezile na wakaelekezwa Foundation for Civil Society ambapo napo hawakuweza kukidhi matakwa yake kwani walihitajika wawe na andiko na pia wawe na hati ya hesabu zilizokaguliwa wakati wao hawana fedha hata kidogo.

Wapo waliopata bahati ya kupata misaada toka makanisa waliokuwa

wanaabudu. Huko kuna waliosaidiwa kulipa kodi ya wakati fulani, wapo waliosaidiwa ada za shule na kuna wakati walipatiwa vyakula.

Kwa ujumla wahanga waliachwa na umaskini wa hali ya juu, watoto wengi hawakuweza kusoma, maisha yamekuwa magumu, kama mmoja wao alivyojieleza 'maisha yamekuwa ni ya kubahatisha, bila kibarua huwezi kuishi, tumekuwa watu wa kuombaomba misaada'.

### 7.3 Kesho Itakuwaje

Jambo ambalo liko wazi ni jinsi wahanga walivyokuwa wavumilivu. Hata walipokutana na kuwasiliana hawakumbuki kujaribu kufanya uovu wowote ili kuonyesha maumivu yao. Jambo kubwa lililowapa uvumilivu, ni pale walipoona wanapatiwa msaada wa kisheria. Kila wanapoona hali haendi walikuwa wanapiga simu kwa mawakili wao au Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Mkurugenzi huyo anakumbuka sana kuwa angalau mara moja kwa mwezi aliweza kupokea simu kutoka kwa mmoja wa wahanga hao akiulizia kinachoendelea, anakumbuka simu kutoka kwa Wilson Korosso aliyekuwa Tarime na Ibrahim Koroso.

Wahanga walipopokea vitisho na kunyanyaswa walitoa taarifa Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu ambapo kuna wakati Mkurugenzi wake ilibidi ampigie simu kamanda wa polisi wa wilaya ama Kamanda wa Polisi wa mkoa kuhusu kuacha kuwanyanyasa wahanga hao. Walijitahidi sana kuwa na matumaini hasa kesi ilipoanza kusikilizwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume ilipotoa ripoti yake walipata nguvu mpya na tumaini jipya kiasi kwamba kusubiri serikali itekeleze haikuwa shida. Hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati huo, Ndugu Andrew Chenge alipokataa kutekeleza mapendekezo ya Tume watu hawa hawakufa moyo kwani mawakili wao na watendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walifika Mugumu ambapo waliwakutanisha na kuwaeleza kitakachofanyika baada ya hapo. Hilo nalo liliwapa moyo kuwa lipo litakalowezekana kama la mwanzo lilivyowezekana.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilihakikisha kuwa shauri linapokwisha Mahakamani kiliweza kuwatembelea na kuwapa maendeleo na njia inayofuata. Waliamini waliyoambiwa na mawakili kuwa haki wanayo hivyo waifuatilie bila kukata tamaa kwani inaweza kucheleweshwa lakini hatimaye itapatikana. Haikuwa rahisi sana kupokea ujumbe kama huo katikati ya dhiki walizokuwa nazo lakini baada ya mwanga wakurejeshewa ardhi yao, wengi walisema 'haki haipotei, ni bora kufuata sheria', Wapo ambao walisaidiwa na imani zao kwa kumuomba Mungu huku wakiendelea kuwa wavumilivu, wakiingoja kesho bora kuliko jana mbovu.

Kila aliyesikia kisa hiki aliwaona hawa watu kuwa walikuwa wavumilivu sana, hata watu wanaoishi katika wilaya hiyo waliosikia au kushuhudia yaliyowatokea watu hawa na jinsi walivyoendelea kufuatilia huku wakihangaika wamewasifia kuwa wamekuwa wavumilivu sana kwani wengine wanasema huenda kwa wingi wao mji usingekalika kwa jinsi ambavyo wangeweza kuungana kufanya uhalifu na uvunjaji wa amani. Pia wapo ambao bado wamekuwa na imani na serikali kwa mfano mzee James Chacha Matiko ambaye aliondolewa Nyamuma akiambiwa kuwa ni mkenya akarudishwa nchini kwa vile si mkenya ni mtanzania. Huyu ana miaka 73 mwaka 2019 ana Watoto 12, bado ana imani na serikali kwani anasema 'tumeomba misaada kila mahali hatujapata, tunaiomba serikali ya awamu ya tano itusaidie tutoke katika hali hii mbaya.'

### 7.4 Kumbukumbu Isiyosahaulika Maishani

Wengi wa Wahanga waliohojiwa wanakumbuka sana ile tarehe ambayo Mkuu wa wilaya alifika na kuchoma nyumba zao. Hiyo tarehe iko moyoni, mmoja alisema 'si tarehe yakusahaulika tarehe 12/10/2001'. Kuna ambaye alisema kila akikaa anamuona Mkuu wa Wilaya alivyowasha moto ile nyumba ya kwanza kwani hakuamini kitu kama kile kingeweza kutokea. Huwa anaona kama ni senema, maana baada ya ule moto wa kwanza mara nyumba nyingine zikaanza kuungua na kila akitafakari hapati jibu kuwa inakuwaje katika nchi hii huru inayosemekana nchi ya

amani kitu kama hicho kiliweza kutokea na aliyetenda hivyo yupo tu na anaendelea na maisha yake vizuri kabisa.

Kuna wanaokumbuka jinsi walivyopoteana na watoto na mke/mume na jamaa ambao wengine hadi leo hawajaweza kuonana. Wengine wanakumbuka walipokutana na watoto wao baada ya miezi na jinsi watoto walivyokuwa wamedhoofu. Yupo anayekumbuka jinsi jengo la kanisa lilivyobomolewa. Hakuamini wala kutegemea jambo kama hilo litokee akiwa anaona. Hayo alikuwa akiyasikia nchi nyingine si hii nchi ya amani. Yuko aliyeumizwa sana kwa kutoweza kula kwa pamoja na familia yake jambo alilokuwa amelizoea, sasa familia iligawanyika kwa kukosa makazi.

Kuna anayekumbuka jinsi ilivyobidi kumuandikia Jaji Kisanga, aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kumshukuru na kumpongeza hata kabla shauri halijafikia mwisho. Hasa ni kwa jinsi walivyoshangaa kuwa hata Mkuu wa Wilaya ya Serengeti aliweza kuitii mamlaka ya Tume nakufika kuhojiwa. Hiyo siku kwao ilikuwa ni ushindi hata kama wasingeshinda hiyo kesi.

Kumbukumbu isiyomtoka kichwani mmoja wa wahanga ni pale alipofika Dar-es-Salaam kusikiliza hukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Anakumbuka ukumbi ule ulivyokuwa na watu na jinsi Jaji alivyosoma na mwisho akasikia walitakiwa warejeshwe katika ardhi yao na pia walipwe fidia. Hiyo ilikuwa siku nzuri sana aliogopa kutembea peke yake kwani kiwewe kilichompata angeweza kugongwa na gari.

Mama mmoja anakumbuka jinsi ilipobidi wakimbie na akakumbuka haoni watoto akidai walikuwa wamelala akawavuta akakimbia nao maporini, hadi walipofika mjini, watu wakiwashangaa kwani walikuwa hawajavaa ipasavyo na Watoto hawakuwa na nguo.

### 7.5 Rejea Yaliyopita na Iwapo Mwisho ni Ushindi

Upo msemo unaosema haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyokoseshwa au iliyonyimwa. Shauri la Nyamuma Iliyobaki upo mtego mkubwa katika kuangalia iwapo baada ya mkasa huo na yote yaliyojiri hatimaye hawa wahanga ni washindi au huo ulikuwa ushindi au la. Watu hawa walikuwa wanataka nini baada ya kupatwa na mkasa huo? Haki yao hasa ilikuwa ni nini? Walikuwa wanashindana na nani ili wawe wao ndiyo washindi au walioshindwa?

Wananchi wa Nyamuma Iliyobaki ni watanzania ambao kama watanzania wengine wana haki ambazo zinatambuliwa na Katiba ya nchi na hata mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Haki walizonazo hazipaswi kuondolewa kiholela na bila wao kupata nafuu baada ya hali hiyo.

Wapo waliopoteza haki yao ya kuishi. Watu waliokufa wakiwa katika kuhangaika wengi walikufa kutokana na kukosa haki ya maisha bora, haki ya afya na hata haki ya malezi. Kwa hao hata kama ardhi yao itarejeshwa na fidia ikapatikana huwezi kusema wameshinda pamoja na kuwa kwa ujumla wameweza kupatiwa walichokuwa wanadai. Kuna kitu huwezi kukirejesha kikiondoka ambacho ni uhai. Waliokufa wamekufa pamoja na kuwa dunia imetambua kuwa walikuwa na haki na walipaswa kurejeshewa haki yao. Bahati mbaya uhai hauwezi kurejeshwa.

Jambo jingine ambalo likitoweka haliwezi kurejeshwa ni muda. Kwa muda wa miaka kumi na minane watu hawa wamekuwa wakiifuatilia haki yao, haki hii ikipatikana baada ya muda huu ushindi ni kile walichokipata na si muda walioupoteza. Kwani iwapo haki hiyo wangeipata mapema kama ni ardhi ambayo wangeamua kuweka mazao wangeshavuna mara nyingi au kama ni mazao ya muda mrefu napo yangeshakua. Kwa kuipata haki miaka 18 baadaye watakuwa wamepoteza vingi vilivyokuwa vipatikane kwa wakati huo.

Kwa wale waliokuwa watoto waliotegemewa kuendelea na shule nakupata elimu kwa haki hii kucheleweshwa wamepoteza muda na elimu wameikosa kwa muda uliohitajika.

Kwa watu wanaotetea haki ushindi ni pale haki ile inapopatikana. Kwa vile haki inapominywa mminyaji hana mpango wakuirejesha hivyo mtafuta haki anapoweza kuisimamia na kuhakikisha haki hiyo inapatikana huo ni ushindi. Ndiyo maana wapo waliohesabu ushindi pale mkuu wa wilaya alipofikishwa kizimbani. Wengine waliona ushindi Tume ilipotambua haki yao na kuwa walikosewa. Wegine waliona ushindi pale mahakama ya Rufaa ilipotamka kuwa mapendekezo ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora yanapaswa kupewa nguvu kisheria. Kwenye lugha ya kiingereza kuna maneno ya 'war' na 'battle'. War ni vita kubwa. Battle ni vita ndani ya vita yaani vita ndongo. Kuna wakati ushindi hutokea katika vita ndogo kuelekea ushindi wa vita kubwa. Kwa hiyo katika kufuatilia haki ya wahanga wa Nyamuma Iliyobaki, kulikuwa na ushindi wa vita ndogo ndogo kuelekea ushindi wa vita yenyewe kubwa.

Kwa watetezi wa haki za binadamu upo ushindi katika kisa hiki kwa vile haki zilizovunjwa zilitambuliwa na ikajulikana kuwa kweli walivunjiwa haki na hivyo basi haki zao zipatikane kwa kurejeshwa makwao na kulipwa fidia.

**"Ila naomba serikali yangu initendee haki na kunijali na ikiwezekana inirudishe eneo langu ili niendelee kulima kama wengine nisiendelee kuwa mkimbizi katika nchi yangu"**

**Chacha Gisima**
Mhanga Nyamuma iliyobaki



Kama Bhoke anavyojieleza kurudishwa katika eneo lake sio kupewa ardhi ni ardhi tu. Tulipoongelea haki yakuwa na kwao maana yake ni pale mahali pa asili pa mtu. Kwa wengi hiyo ndiyo ingekuwa haki. Pia kupata uhakika wakulindwa hiyo haki ili isijirudie tena kuondolewa kwa njia zisizofaa na zisizofuata taratibu wala sheria au hata utu.

Wengine watapenda kuona baada ya kurejeshwa makwao na kulipwa fidia ili kukomesha matendo kama haya basi waliyoyatenda haya nao wachukuliwe hatua za kisheria. Yale matendo yalitendwa na watu waliokuwa na akili timamu na kwa makusudi kabisa na ni matendo jinai. Watu hawa walikuwa watendaji wa serikali na walifanya yale kinyume kabisa na kazi walizokuwa wamepewa na kwa hali hiyo wameiingiza serikali katika gharama ya kuendesha kesi na pia kulipa fidia na kutoa ardhi kwa watu waliokuwa na ardhi yao. Watu hawa walitakiwa na hata sasa inawezekana wachukuliwe hatua za kisheria kwa kosa la jinai na pia kwa kwenda nje ya mamlaka yao au kutumia mamlaka yao vibaya.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ndivyo ilivyoelekeza na ili ushindi huu uwe kamili hilo nalo inabidi litendeke. Wengi wa wahanga na hata watu waliolifahamu jambo hili, waliohojiwa baada ya shauri hili kuonekana kufikia mwisho, walisema, itolewe adhabu kali kwa wale viongozi waliohusika kuvunja sheria. Bahati mbaya sana watu hawa pamoja na nafasi walizokuwa nazo na hata elimu yao hawakuonekana kabisa kujutia walichokifanya walionekana kutaka kuficha ukweli na hata kuendeleza mateso na manyanyaso kwa wahanga wakati kesi ikiwa inaendelea. Wapo waliosisitiza kuwa ili kweli haki iwe imetendeka kwa kuzingatia utendaji wa serikali ya awamu ya tano, inabidi serikali hii ndiyo ichukue hatua ili watu wale wakamatwe, wapewe adhabu kwa vile wameitia serikali hasara kubwa sana kwa kuwaumiza watu na kuharibu mali zao.

Kwa barua ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakati huo Ndugu Andrew Chenge ya Mei 18 2005, serikali ilionyesha kuwa haikuwa tayari kuwachukulia hatua watendaji wake, lakini mapendekezo ya Tume yako

dhahiri nakuthibitishwa na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Iwapo serikali itakuwa haiko tayari kuchukua hatua basi inawezekana watu binafsi wakaiomba mahakama wafanye kesi binafsi yaani 'private prosecution' dhidi ya Thomas ole Sabaya na Alexander Pantaleo Lyimo na wale wote walioshiriki kuchoma nyumba zile na wakajulikana kwa majina. Hapa huenda ushindi ukawa kweli ni ushindi bayana.

SURA YA NANE

08

# HITIMISHO

## 8.1 Ukweli wa Maisha; Umuhimu wa Kuwa na Uhakika wa Haki ya Kuwa na Kwenu

Kwa kuangalia kisa hiki cha kweli kilichowakuta watanzania katika nchi yao kuna mambo mengi yakuangalia na pia yakufanyiwa kazi ili hali kama hii isitokee tena na ikitokea kisa hiki kiwe ni fundisho ya jinsi ya kushughulikia mambo kama haya. Kituo na Sheria na Haki za Binadamu pamoja na kuwa kimeshughulikia kesi nyingi na nyingine zenye uelekeo kama huu lakini katika kutimiza miaka 25 tangu kianzishwe kimeona kiweze kuweka kumbukumbu ya kesi hii. Katika miaka 25 ya kituo miaka 18 kimekuwa kikipambana na kesi hii. Yapo kilichoweza kujifunza na hivyo ni somo kwa watu na mashirika mengine nchini na hata nje ya nchi.

### 8.1.1 Haki ya Kuwa na Kwenu

Hii ni haki ambayo watu wanaoishi sehemu kwa umoja wao wakiwa na ardhi yao na maisha yao inabidi wawe na uhakika wa maisha yao. Bado upo mjadala mkubwa kuhusu watu wa aina yao hasa kwenye nchi kama yetu ambapo ukoloni ulikwisha na tukajaribu kuunda utaifa na kuona kuwa kila mtu aliyepo kwenye mipaka yetu ambaye ni mzaliwa au kwa kuandikishwa basi ni Mtanzania na hivyo haki zake ni zile zilizoainishwa kikatiba. Ukitazama Katiba sehemu ya haki ya kuishi inajumuisha hali nzima inayoelekeza haki hii ya mtu kuwa na kwao kwani ibara ya 14 inasema kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake. Kilichowakuta wananchi hawa wa Nyamuma pamoja na kuwa waliendelea kuishi yaani wengi wao kuwa hai, hifadhi ya maisha yao ilikuwa mashakani na hadi wengine walipoteza maisha hivyo haki hii hawakuweza kuifaidi.

Ibara inayofuata ya kumi na tano inazungumzia haki ya kila mtu ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru. Visa vilivyoelezewa katika sakata hili ni wazi kabisa haki hii haikulindwa kwani watu hawa walipoondolewa kinguvu katika miji yao yaani kwao, walianza kuwindwa na kutendewa mambo yasiyo linda uhuru wao na hata watu waliojaribu kuwasaidia nao walikuwa mashakani. Pia walikuwa wananyanyapaliwa kwa kuitwa majina ya kibaguzi. Hapa hiyo haki ya mtu kuwa na kwao haipo kwani unapokuwa kwenu unakuwa na uhuru na unaishi kama mtu huru. Kifungu kidogo cha pili cha Ibara ya 15 ya Katiba kinaweka msisitizo wa njia za kuuhifadhi uhuru wa mtu kinapoweka marufuku ya mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu kama walivyotendewa wananchi wa Nyamuma Iliyobaki. Hawa waliondolewa kwa nguvu na kufanyiwa ukatili kutoka katika ardhi yao waliokuwa wakiimiliki kihalali wakijua ndio kwao na ndipo palipokuwa kwao.

Katiba katika kulinda haki hii ya mtu kuwa na kwao katika ibara ya 16 inatoa ulinzi wa haki ya faragha. Lakini tumeona jinsi ambavyo watu walitimuliwa, wengine wakaondoka bila nguo wakati ibara hii

inazungumzia hifadhi ya nafsi, maisha binafsi na familia yake, heshima na maskani yake. Iwapo palikuwa na sababu yoyote yakuingilia maskani ya watu kifungu cha pili cha Ibara hii ya 16 kinazitaka mamlaka kuweka utaratibu unaofaa. Hapa tumeona jinsi watu walivyovamiwa alfajiri wengine wakiwa wamelala na kuanza kufukuzwa na nyumba zao kuchomwa moto na mali kuteketezwa na nyingine zikiimbwa. Mtu anahitaji kuhifadhiwa anapokuwa kwake si kutimuliwa kama ilivyoonekana. Ibara ya kumi na saba ya Katiba inazuia mtu kushurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka Jamhuri ya Muungano. Kisa hiki kinaweka bayana jinsi watu walivyofukuzwa kutoka kijijini kwao na kufukuzwa kutoka nchini kwa kuitwa wa Kenya hadi kupelewa mpaka wa Kenya. Hata kama wangekuwa wa Kenya kitu ambacho hawakuwa bado sheria inatoa muongozo namna ya kuwachukulia hatua wahamiaji haramu.

Mtu huwa na kwao pale pia anapoweza kumiliki mali, kama ilivyowekwa vizuri katika ibara ya 24 ya Katiba kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo. Wananchi wa Nyamuma Iliyobaki, wanaelezea walivyokuwa kwenye ardhi yao ambayo ni mali kuu, wengine wakiwa na ekari 20 hadi 30 na mali nyingine kama mifugo na vyakula kama nafaka na mazao. Vyote hivi walivikosa kwa siku moja na ndio maana Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi katika hukumu yake kwa kesi hii ya Nyamuma mbele ya Jaji Mziray ilikubali kuwa watu hawa walikosewa haki yao hii na inabidi warejeshwe katika ardhi yao kama Tume ilivyopendekeza. Na Tume ya Haki za Binadamu iliamuru walipwe fidia ya mali walizopoteza.

Haki hii ni msingi wa haki ya kuishi kwani mtu akiwa hana uhakika na alipo kuwa ni kwake na kuwa haki yake hii italindwa basi hata kuishi kwake kutakuwa ni kwa mashaka na wasiwasi. Haki hii inabidi iwekwe bayana kabisa ikiambatana na haki ya uraia kwani si sahihi kwa raia wa nchi kutakiwa yeye ndio athibitishe uraia wake kwani taratibu zikiwekwa sawa kila aliye raia atajulikana iwapo ataandikishwa na kupewa jina tangu anapozaliwa na baadaye kupewa hati ya uraia anapofikisha umri

unaostahili kufanya hivyo. Ilikuwa ni shida sana kwa wananchi wa Nyamuma walioambiwa si raia na wao ndio wakatakiwa kuthibitisha kuwa wao ni raia watanzania. Hapa haki ya kuwa na kwao ilikiukwa kwani hata walipelekwa mahakamani na kufungwa walipotoka walibaki nchini kwani ndipo kwao na hawana kwao kwingine. Haki hii inapaswa ilindwe kwa kila raia wa Tanzania.

### 8.1.2 Wakimbizi wa Ndani

Wananchi wa Nyamuma katika kisa hiki walijikuta kuwa ni wakimbizi wa ndani ya nchi yao kwani wote walioondolewa kwa nguvu kuacha yule aliyeweza kuinunua tena ardhi yake waliondoka kwao wakaanza kuhangaika nje ya makao yao huku wakisakwa.

Katika himaya ya kimataifa wakimbizi wa ndani pamoja na kuwa wanatambulika lakini hawana chombo maalum cha kuwashughulikia. Mwaka 1998 ziliundwa Kanuni za Kimataifa za kuongoza hali ya ukimbizi wa ndani ambazo zilitokana na uwepo wa wakimbizi wengi wa ndani duniani kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe na uvunjifu wa haki za binadamu. Kanuni hizo zina vifungu 30 ambavyo vinaelekeza jinsi ya kuzuia ukimbizi wa ndani, jinsi yakuwasaidia waliyojikuta kuwa wakimbizi wa ndani na jinsi ya kutoa msaada kwa wakimbizi wa ndani na pia jinsi yakuwasaidia wanaporejea kwao au mahali pengine walipopapata baada ya kukimbia. Kanuni hizi si sheria ambazo nchi zinalazimika kuzifuata pamoja na kuwa nchi kama Kenya imeweka sheria kwa kuzifuata kanuni hizo ili kuwasaidia wale watakaojikuta wamekuwa wakimbizi wa ndani. Hapa nchini hakuna sheria inayoangalia hali kama hiyo ya ukimbizi wa ndani pamoja na kuwa hali za wakimbizi hawa wa ndani hujitokeza hata kama si kwa wingi.

Hata hivyo mwaka 2012 yaani miaka 11 tangu wananchi wa Nyamuma wawe wakimbizi wa ndani, Umoja wa Nchi za Afrika ulipitisha Mkataba wa Kiafrika kwa Ulinzi na Usaidizi wa wakimbizi wa ndani Afrika. Mkataba huu unaungana na zile kanuni za kimataifa na utafaa sana kuwasaidia

wahanga wanaojikuta wamekuwa wakimbizi ndani ya nchi yao. Kwa vile wahanga hawa wa Nyamuma Iliyobaki wako katika kurejeshwa katika eneo mbadala ni vyema serikali ikaweza kutumia kanuni na mkataba huu wa Afrika kuona jinsi wahanga hawa wanavyoweza kuanza maisha yao kwa upya wakiwa watu huru katika nchi yao.

United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR) katika mpango kazi wake unaelezea jinsi watu hawa wanaokimbia wakiwa ndani ya nchi yao walivyo na taabu kuliko wale wanaokimbia na kuvuka mipaka. UNHCR inasema kuwa kuna ugumu wa kuwafikia watu hawa ambao mara nyingi wako katika hatari ya kufa zaidi kama tulivyoona kwa hawa wahanga wa Nyamuma, wako katika hatari ya kudhurika, kudhalilishwa na kukosa huduma, yote haya yamedhihirishwa na kisa hiki cha Nyamuma. Pamoja na kuwa imesemekana kuwa UNHCR inasaidiana na mashirika mengine kutoa misaada ya kiutu kama vyakula, mahema na kadhalika tumeona kuwa wahanga hawa hawakuweza kupokea msaada wowote kutoka kwenye mashirika hayo pamoja na kujaribu kuomba misaada kwa baadhi ya hao. Wahanga hawa hawakuikabili UNHCR kwa vile ipo mifano hai pale baadhi ya wahanga wengine wa aina hii walivyojaribu kutafuta msaada huko bila mafanikio kama wale waliobomolewa nyumba kule Kimara Dar-es-salaam.

Kutokana na haya yaliyotokea Nyamuma Iliyobaki ni kweli kuwa hapakuwa na usaidizi au hata ulinzi wao pamoja na kuwa hili ni fundisho hasa pale wanaokuwa wamesababisha hali hiyo ni hao hao watendaji wa serikali ambao walitegemewa kuwa walinzi wa usalama wa watu ndani ya nchi. Kwa mashirika ya haki za binadamu ni vyema kufuatilia haki za watu hawa waliojikuta kuwa wakimbizi wa ndani. Kwa upande wa kisheria inabidi kutafuta haki ya kurejeshwa makwao lakini pia kutafuta njia za kuweza kuhakikisha wanapata nafuu za kibinadamu kama vile vyakula, malazi na mengineyo ya muhimu. Kwa hawa wahanga wa Nyamuma Iliyobaki hawakuonekana bayana kwa vile hawakukimbilia sehemu moja na kuweza kuonekana kwa wingi wao bali kila mtu alikimbia kivyake na waliishi sehemu tofautitofauti kwa vile pia walikuwa bado wanawindwa.

Hata hivyo waliweza kutunza mawasiliano na ushirikiano kwamba mtu akiwahitaji angeweza kuwapata mara moja.

### 8.1.3 Haki ya Kupata Nafuu ya Kisheria kwa Muda Unaofaa

Kama Katiba inavyoelekeza katika Ibara ya 13 kifungu kidogo (3) kuwa usawa mbele ya sheria ni pamoja na haki za raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu kulindwa na kuamuliwa na Mahakama na vyombo vinginevyo vya mamlaka ya nchi vilivyowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria. Ni kweli kuwa wananchi wa Nyamuma walivifikia vyombo vya sheria, lakini kutokana na hali iliyowakuta ilichukua muda mwingi sana kwa wananchi hawa kuweza kuvifikia vyombo sahihi vya sheria baada ya tukio lenyewe. Waliondolewa kwao tarehe 12/10/ 2001 lakini waliweza kukifikia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu mwezi wa Desemba mwaka huo. Yaani miezi miwili yote walihangaika wakienda kwa Mwanasheria Mkuu, na Polisi ambao wote walikuwa upande wa aliyewatendea hayo. Hatimaye walipofika Kituo watendaji wa Kituo nao wakapatwa na adha walipozuiwa kwa siku sita huko wilayani Serengeti na huyo huyo mkuu wa wilaya aliyekuwa anajaribu kuficha ukweli wa tukio hilo. Kuanzia Mei 2002 baada ya kupeleka shauri mbele ya Tume ya Haki za Binadamu mapendekezo yalipatikana mwaka 2004 mwezi Desemba tarehe 13 ikiwa ni miaka mitatu baadaye. Ilitegemewa baada ya miezi mitatu serikali itekeleze mapendekezo tumeona haikuwa hivyo na ikabidi tena kurudi Mahakamani.

Watu hawa walikuwa wanaendelea na dhiki nyingi hadi kesi ikapelekwa Mahakamani kwa utekelezaji na ilipomaliza mlolongo wa mahakama ilikuwa tayari miaka kumi tangu waondolewe kwao. Kuanzia hapo utekelezaji nao ukawa ni shida kwa ajili ya taratibu zake na pia suala la ukiritimba hadi wakati huu tunapoandika. Jambo zuri ni kuwa watu hawa hawakukata tamaa na wameweza kufuatilia haki yao hadi ikafikia mwisho. Ila ni vyema masuala kama haya yanayogusa maisha ya watu kwa ukaribu kiasi hiki yakaweza kuhitimishwa kwa haraka kwani watu hawa wamepoteza si mali tu bali wamepoteza na muda na wengine maisha kabisa. Haki ikicheleweshwa inakuwa kama imepotea.

### 8.2 Waliotenda Haya Wako Wapi?

Hili nalo limekuwa swali la msingi kwani si vyema kabisa mtu atende kosa kubwa kama hili awaache watu kama hawa wapate shida walizopata na yeye aendelee tu na maisha kama vile hakuna kitu kilichotokea. Katika utetezi wa haki za binadamu inasisitizwa kuwa ili utawala wa sheria ufanye kazi, kila mtu anayekiuka haki za binadamu inabidi awajibike au awajibishwe. Kitendo cha mtu au watu kukiuka haki na ikathibitika amefanya hivyo kisha akaachwa tu bila kuwajibishwa ni hali isiyokubalika kabisa katika nchi inayofuata utawala wa sheria. Katika kisa hiki ni wazi kuwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti wakati huo ndugu Thomas Loy Ole Sabaya na Mkuu wa Jeshi la Polisi wilaya afande Alexander Pantaleo Lyimo ndio walioongoza kufanyika uvunjifu huo wa haki na walitambulika kabisa ushiriki wao pamoja na watendaji wengine waliojulikana wakitokea katika serikali za vijiji jirani. Walifika mbele ya Tume na hawakuweza kukanusha uhusika wao bali walijaribu kuutetea bila hofu wala aibu. Ili haki itendeke na pasiwepo na hiyo hali ya kutojali haki inapovunjwa, watu hawa inapaswa wachukuliwe hatua za kisheria kama Tume ilivyoagiza. Waliyoyafanya pamoja na kuwa ni uvujifu wa haki za binadamu lakini pia ni makosa ya jinai, hivyo kosa la jinai huweza kushughulikiwa wakati wowote kwani halina ukomo wa muda.

Ni vyema kuwa palikuwepo na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kuwashika mkono kwa kuwatetea wahanga hao. Pia ilikuwa ni vizuri kuwa ilikuwepo Tume ya Haki za Binadamu tena ikiwa mpya tu na bahati sana ikawa na mwenyekiti mahiri aliyeweza kujali na kufuatilia suala hili hadi kutoa mapendekezo. Pamoja na ujeuri wa serikali wakati huo imekuwa vizuri kuwa sheria iko wazi kuwa wasipotekeleza upo uwezekano wakwenda mahakamani. Jambo zuri zaidi ni kuwa palikuwa na uwezekano wa rufaa pale mahakama iliyoanza kusikiliza shauri hilo ilipokubali pingamizi la awali kutoka kwa walalamikiwa na ilikuwa vizuri zaidi Mahakama ya Rufaa ilipoweza kulirudisha shauri Mahakama Kuu na lisikilizwe na jaji mwingine ilikuweza kutoa haki. Baada ya njia zote hizo kufukuzia haki imekuwa faraja kwa wahanga kuwa hatimaye haki yao

haikupotea kabisa. Na kwa muda watakaosalia duniani wataweza kufaidi matunda ya kufuatilia haki yao.

Na hapa tunahitimisha kwa kuwapa moyo wote wanaovunjiwa haki kuwa HAKI hufuatwa na kufukuziwa popote hadi ipatikane, si rahisi kupokea haki kwenye sahani ya shaba.

Yote haya ni katika kuhakikisha tunaifikia hali ya kuwa na Jamii yenye Haki na Usawa.